**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Sita - Tarehe 16 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Zilizowasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA PAMOJA NA MAHUSIANO NA URATIBU:**

Randama za Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

16 APRILI, 2013

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 43

**Kazi za Maafisa wa Mifugo wa Kata**

**MHE. NEEMA H. MGAYA** aliuliza:-

Je, Maafisa wa Mifugo wa Kata wana kazi gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa waraka wa Maendeleo ya Utumishi Namba 5 wa mwaka 2002, Nyongeza II inayohusu Muundo wa Utumishi wa Mafisa Mifugo Wasaidizi *(Livestock Field Officers),* kazi za Maafisa Mifugo katika ngazi ya Kata ni kama zifutazo:-

1. Atafanya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kwa wafugaji wa eneo lake.

2. Kwa kushirikiana na wakaguzi wa afya atakagua nyama na usafi wa machinjio mara kwa mara.

3. Atakusanya takwimu za nyama na mazao yatokanayo na mifugo kama ngozi na kuandika ripoti.

4. Atatibu magonjwa ya mifugo chini ya usimamizi wa Daktari wa mifugo na kushauri wafugaji jinsi ya kukinga mifugo dhidi ya magonjwa.

5. Atatembelea wafugaji mara kwa mara na kuwapa ushauri fasaha wa kifedha katika eneo lake la kazi.

6. Atashauri na kusimamia ujenzi wa majosho, machinjio, vibanio na Miumdo mbinu inayohusiana na ufugaji bora.

7. Atasimamia uchanganyaji wa dawa ya josho.

8. Atahusika na uhamilishaji (*Artificial Insemination)* na uzalishaji *(Breeding)* wa mifugo kwa ujumla.

9. Atawashauri wafugaji kuhusu mbinu bora za kuzalisha maziwa na utunzaji wa ndama.

10. Atashauri wafugaji umuhimu wa kufuga mifugo yao kulingana na maeneo/malisho.

11. Atasimamia na kuhakikisha utaratibu wa karantini uliowekwa unatekelezwa ipasavyo.

12. Atahamasisha uundwaji wa vikundi vya wafugaji mbalimbali kwa ajili ya ufugaji masoko na kadhalika.

13. Ataandaa mipango ya ufugaji ya mwaka katika eneo lake.

14. Atafanya kazi nyingine za fani yake kama atakavyo agizwa na Mkuu wake wa kazi. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA H. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, lakini nilikuwa nina maswali mawili madogo ya nyongeza, Serikali ina mpango gani katika kuwapitia vitendea kazi hawa Maafisa Mifugo wa Kata kwa sababu mifugo inapatikana mbali hivyo Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha kuwa wanapatiwa usafiri wa kuweza kuwafikia hawa watu wa mifugo. Kwa sababu Afisa Mifugo wa Kata anakuwa anaenda sehemu mbalimbali kwa umbali mrefu lakini vile vile vitendea kazi kama dawa.

Swali la pili, kuna baadhi ya Kata nyingi hapa nchini huko vijijini hizi kazi za Maafisa Mifugo zinafanywa na Maafisa Kilimo.

Je, ni uhaba wa Maafisa Mifugo au ni nini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nishukuru kuwa maswali ya nyongeza sasa yameulizwa kwa sababu tulijiuliza Mheshimiwa Neema anataka nini lakini sasa tumeelewa anachotaka. Hawa Maafisa wanaozungumzwa hapa wako pale katika *Ward Development Committee* na wako katika Halmashauri na hizi shughuli zinazofanyika hapa ni shughuli kubwa. Ukienda kwenye machinjio ukipeleka mbuzi mmoja pale unatozwa ushuru na Halmashauri. Ukipeleka ng'ombe pale unatozwa ushuru na Halmashauri. Kwa hiyo, yako mapato yanayotokana na shughuli zinazofanyika katika machinjio na hata wale ambao wanapata huduma ambayo hawapitii katika machinjio kwa kufuatana na kazi zile nilizozieleza.

Kwa hiyo, ikitokea kuwa wanakwenda kufanya kazi, vifaa na kadhalika, hii ni kazi ya Halmashauri kuhakikisha kuwa hawa Watumishi ambao wanafanya kazi hizi ambazo nimezieleza hapa Halmashauri inawapatia hivyo vitendea kazi. Ninataka nikiri hapa kuwa anazungumzia pia masuala ya usafiri. Ni kweli kabisa kuwa hawa Watumishi tunaowazungumzia hapa wengi wao katika kada hii hawajapata usafiri. Kwa sababu sasa hivi tunawahudumia wale Maafisa wa Kata pamoja na Maafisa Tarafa. Kwa hiyo, kidogo kidogo utaona tunajaribu lakini kunapokuwa na matukio makubwa Halmashauri inatoa gari au pikipiki ili kwenda ku- *arrest* hiyo *situation* kufuatana na tatizo ambalo litakuwa limejitokeza pale.

Pili, ameuliza hapa na tumemwelewa anasema kwamba inakuwaje unamkuta huyu wakati mwingine anatumika anakwenda kufanya kazi za Afisa Kata kule na kadhalika. Ile ya mwisho tulipoisoma tulisema pia kuwa na maagizo mengine atakayopewa na Mkuu wake wa kazi.

Katika *Ward Development Committee* mkuu wake wa kazi ni mtu anayeitwa Afisa Mtendaji. Ninajua kuwa hapa tusingependa kusikia kwamba mtu anayehusika na mifugo anakwenda kuwa Kaimu Mtendaji wa Kata tena kwa mwaka mzima wakati anapokuwa ameondoka au amefariki dunia unasema hebu shilikilia mara moja lakini tuna *replace* mara moja na kurudisha tunafanya haraka tunafanya haraka na hatutaki kusikia.

Mheshimiwa Spika, ninataka kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nitoe maelekezo hapa kuwa hatutaki kusikia mtendaji anahusika na mambo ya mifugo anakaa kwenye kituo tunaambiwa kuwa ni Afisa Mtendaji.

Mwisho, hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Mama Kombani jana alisema hapa na katika eneo hili pia wanafanya kazi hiyo hawa Maafisa wanaohusika hapa wa Kilimo na Mifugo 2500 wanaandaliwa kwa ajili ya kazi hiyo, ili kuondokana na tatizo hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge anazungumzia.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Maafisa hawa wa Kata ni wachache katika maeneo mengi na waliopo hawawajibiki na huwatoza wananchi kwa huduma hiyo ambayo Mheshimiwa Waziri kasema kuwa huduma hiyo ni bure.

Je, ni nini tamko la Serikali kwa hao Maafisa wanapowatoza wananchi wakati wanatakiwa kupata huduma hii bure?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sikusikia swali.

**SPIKA:** Anasema kuwa wanawatoza gharama wakati wa kutoa huduma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Sijasikia swali swali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, hebu rudia swali lako kwa kifupi.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nimeuliza hivi, kwa kuwa Maafisa Kata wa Mifugo ni wachache katika maeneo mengi na waliopo walio wengi wanatumia taaluma yao kuwatoza wananchi, na katika jibu lako la msingi umetueleza kuwa kazi nyingi za Maafisa Kata lakini Maafisa Kata huwatoza wananchi wakati wananchi hawa wanatakiwa kupata huduma hii bure ni nini tamko la Serikali kuhusiana na Maafisa wanaowatoza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Nimesikia sasa nimesikia, hawa anaowaleza hawa wala hatuwatambui hawa watu wanaofanya kazi hiyo hawezi kutoka hapa Afisa wa Mifugo anazungukazunguka anakwenda kumsaidia mama mmoja ng'ombe wake,anatoka hapa na kuingia pale anasaidia halafu anatoza na dawa anapeleka pale. Mimi ninaelewa kitu ambacho kinajitokeza hapa hii shughuli ya mifugo na ninaelewa Mheshimiwa Lekule Laizer na wenzake wananisikiliza na mimi ninataka ku- *declare interest* hapa kuwa 50% ya wapiga kura wangu mimi ni wafugaji.

Kwa hiyo, ninaelewa kinachozungumzwa hapa ni kwamba tumekubaliana na *private sector* kuwa nayo itakuwa inachangia katika suala hili la madawa na matibabu na vitu vingine, linaweza likaleta matatizo kama mganga amejiingiza pale au mtumishi amejiingiza pale tukashindwa kupambanua sasa kuwa ni wakati gani hii shughuli inayofanyika hapa ni ya Serikali kwa maana ya Halmashauri na inapofanyika hapa ni mtu binafsi. Mimi ninamwomba Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ana watu anawafahamu wanazunguka zunguka huko wanachukua hela ya mtu anakwenda kwenye machinjio pale hatozwi kitu chochote anachotakiwa kutozwa atuambie.

Mheshimiwa Spika, sisi tunachojua ni kwamba tunapotoza tunatoza kwa maana ya kuingiza katika mfuko wa Halmashauri. Kwa hiyo, ninamwomba sana kama ana watu wa namna hiyo atuambie. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Maafisa Kilimo kwenye Kata yetu wamepewa mlolongo wa majukumu na majukumu mengine ni yale ambayo yanapelekea hizo ofisi zao za Kata ziwe na vyombo maalum vya kisayansi ikiwa ni pamoja na maabara; na kwa kuwa amemtaja kwa kazi namba moja ni afisa mchunguzi wa magonjwa yote katika Kata.

Mheshimiwa Waziri anaweza kututajia angalau Kata moja tu katika nchi yetu ambayo ina maabara ya kiuchunguzi kwenye Kata juu ya magonjwa ya mifugo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, Maofisa wa Mifugo wa Kata wanapoona kuna hali ya ugonjwa ama dalili yoyote kutokana na walivyofundishwa, wanatoa taarifa katika ofisi za Kanda na kuna ofisi zetu za Kanda zinaitwa *Veterinary Investigation Centers* ambazo ziko saba Tanzania.

Kwa maana hiyo wao hawatakiwi kwasababu hakuna maabara kwenye Kata lakini wanatakiwa kutoa taarifa katika vituo vyetu vya Kanda na ndivyo wanavyofanya. *(Makofi)*

Na. 44

**Madhara yatokanayo na Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Uharibifu wa Mazingira nchini umeleta athari kubwa ya mabadiliko ya misimu ya kilimo, uhaba mkubwa wa maji na kukauka kwa vyanzo vya maji kama ilivyotokea Wilayani Lushoto.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kudhibiti uharibifu wa mazingira hasa ukataji ovyo wa miti?

(b) Ili kuzuia ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa, Serikali inachukua hatua gani kupata nishati mbadala ili misitu isitumike?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya kupanda miti katika mashamba ya Serikali yaliyovunwa na mpaka sasa hajayajapandwa miti mingine kwenye mashamba ya magamba na msitu wa Kandelepaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a)Katika kukabiliana na uharibifu wa Mazingira utokanao na ukataji miti, Serikali iliandaa na kupitisha Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya Maji wa mwaka 2006.

Mkakati unaelekeza watumiaji wa kuni na mkaa kuandaa mashamba ya miti; kudhibiti uchomaji wa misitu na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa, kuhamasisha upandaji miti kwa watumiaji , kuzitaka Halmashauri za Vijiji kuwa na mashamba ya miti kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa.

Aidha, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kupitia *program* ya usimamizi Shirikishi wa misitu inahimiza jamii kupanda miti katika mashamba na kutenga hifadhi za misitu ya jamii.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina hamasisha mkakati nilioutaja. Hii ikiwa ni pamoja na kuendeleza matumizi na utafiti kuhusu nishati mbadala na Teknolojia sahihi ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Serikali kwa ushirikiano na wadau inahimiza matumizi ya mabaki ya mazao na karatasi *(briquettes),*umeme wa jua, upepo, gesi asilia, bayogesi, mkaa wa mawe na matumizi ya majiko bunifu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga maeneo ya mashamba ya miti ikiwemo eneo la shamba la miti la Magamba. Shamba hili lipo kwenye mpango wa miaka mitano (5)unaoweka bayana utaratibu wa kuvuna na kupanda miti.

Aidha, msitu wa Kandelepaa ambao uliungua mwaka 1997/1998, ulihifadhiwa, ili kuruhusu uoto wa asili *(natural regeneration)* hata hivyo sehemu ya aeneo lililoungua limepandwa miti *(enrichment planting),* ingawa ukuaji wa miti unakabiliwa na changamoto ya kuzidiwa na mimea mingine aina ya *ferns*. Juhudi zinafanywa za kupunguza mimea hiyo ili miti ya asili istawi.

**MHE. HENRY D SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, ninafurahi kwa majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Waziri amekiri kuwa eneo la Kandelepaa liliungua na kwa bahati mbaya hili ndilo eneo tunategemea maji kutoka eneo la Kibohelo na eneo hili kwa kuungua kwake maji yameanza kupungua sana.

Je, miti hii ya Mikaratusi Serikali inatamka nini na kwa nini Serikali isikubali *TANAPA* kulinda eneo hili?

Mikaratusi Serikali inatamka nini na kwa nini Serikali isikubali *TANAPA* kulinda eneo hili?

Swali la pili, la kitaifa; kuna ukataji wa miti kwa jeuri kabisa kwa mfano eneo la Kiteto kwa bahati nzuri nilipokuwa Mkuu Mkoa kuna eneo wanakata miti kwa hasira wanatumia dizeli, Serikali inachukua hatua gani kupunguza hili la kukata miti kwa jeuri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza tuchuku ushauri wa Mheshimiwa Shekifu ambao anasema kuwa *TANAPA* ndiyo ipewe jukumu la kulinda misitu hii.

Lakini hili linahitaji ushirikiano kati ya Wizara yetu na Wizara ya Maliasili na Utalii tutaona ni kwa namna gani tunaweza kuiweka *TANAPA* kuweza kulinda miti hii kwa kuwa kuna issue za kiutawala na issues za kimkakati ambazo inabidi tuzifanye kanza. Nimuombe Mheshimiwa Shekifu niuchukue ushauri wake ili Serikali iweze kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukataji wa miti; Serikali kupitia taasisi yake ya uhifadhi misitu imejiwekea mkakati ambao kwa kweli ni wa kupanda miti pamoja na Wizara yetu tunashirikiana nao ambapo, kwa kushirikiana na TAMISEMI tumeweka mkakati kuwa kwa kila Wilaya kila mwaka angalau miti milioni 1.5 iweze kupandwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna hiyo tunaweza kuhakikisha kuwa miti hii inapandwa katika maeneo yote ambayo yameharibiwa.

Na. 45

**Utatuzi wa Kero za Muungano**

**MHE. ALI KHATIBU KAI** aliuliza:-

Pamoja na kuundwa kwa Tume zaidi ya 20 kwa ajili ya kutatua kero za Muungano, lakini hadi sasa upande mmoja wa Muungano bado unalalamika kuhusu kero hizo.

Je, ni kweli kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano haina nia thabiti ya kutatua kero hizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Napenda kumkakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, nia ya Serikali zetu zote mbili ni thabiti katika kutatua mambo yote yanaleta vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano.

Hoja zote za Muungano zinatakiwa zipate mashauriano ya kina ili kufikia uamuzi kwa faida ya pande zote za Muungano.

Katika kuthibitisha hili mwaka 2004 Serikali ya Awamu ya Tatu iliunda Kamati zilizoweka Utaratibu wa kushughulikia kero za hizo.

Aidha, mwaka 2006 Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ilianza kusimamia kero hizo. Kati ya hoja 13 zilizowasilishwa, hoja 9 zimekamilika na ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja hizo ni :-

Utekelezaji wa sheria ya haki za binadamu Zanzibar, utelekezaji wa *Merchant Shipping Act* katika Jamuhuri ya Muungano na uwezo wa Zanzibar katika kujiunga na *International Maritime Organization (IMO),* Ushiriki wa Znzibar katika Jumuia ya Afrika Mashariki, uwepo wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, uvuvi kwenye Ukanda wa uchumi wa Bahari kuu, ongezeko la gharama za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO,* Mfuko wa Maendeleo ya jimbo ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na kodi nyinginezo *(PAYE).*

Mheshimiwa Spika, hoja 4 ziko katika hatua nzuri za kukamilika, nazo ni Mgawanyo wa mapato, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asili, ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za nje na usajili wa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Spika, tunatoa wito kwa wananchi wote wavute subira kwani Serikali iko makini kushughulikia changamoto zote za Muungano. *(Makofi)*

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba suala la wafanyabaishara wa Zanzibar limepatiwa ufumbuzi.

Je, Serikali inatoa kauli gani?

(b) Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi la Waziri amesema kero iliyopatiwa ufumbuzi ni uwezo wa Zanzibar kukopa nje ya nchi, Waziri unaweza kutupa mifano mitatu ya Zanzibar kukopa nje ya nchi bila kushirikisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?(*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, masuala ya wafanyabiashara sikuweka katika orodha ya mambo yaliyokwishakufanyiwa kazi, yamefanyiwa kazi lakini bado yana utata.

Katika wakati huu Wizara za Fedha mbili SMT na SMZ wameweka Makamishna wao na wasaidizi katika sera za kodi kulifanyia kazi suala hili na jawabu watatuletea katika kikao cha tarehe 28 Aprili, 2013 kitakachofanyika Dar es Salaam. Kwa hiyo, bado suala hili tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la uwezo wa Zanzibar kukopa nje ya nchi, ni kwamba kabla suala hili kufanyiwa kazi Zanzibar walikuwa hawawezi ku-*negotiate* mkopo wenyewe nje ya Tanzania na kwa hivyo walikuwa wanaweka mahitaji yao Hazina ya Dar es Salaam, Hazina ina-*negotiate* halafu ndiyo wanapata.

Kinachotokea sasa hivi ni kwmaba Zanzibar wanakwenda *straight* ku-*negotiate* wenyewe, wame-*negotiate* na Exim Bank ya China, wame-*negotiate* na *World Bank*, wame-*negotiate* na mashirika mbalimbali.

Kinachotokea ni kwamba kama *United Republic of Tanzania* lazima ombi lile la mkopo lipite Hazina ya Dar es Salaam halafu linyooshwe.

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba bado Zanzibar wanalalamika na urasimu uliopo ndani ya Hazina, lakini suala la urasimu siyo kwa Zanzibar peke yake, hata huku Tanzania Bara bado wanalia na urasimu kwenye mikopo uliyopo Hazina.(*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, Muungano wetu huu sasa hivi una takribani umri wa miaka 49 toka uanzishwe, lakini mara zote ukiwasikiliza wenzetu Wazanzibar wamekuwa wakilalamikia Muungano huu kwa kipindi kirefu. Serikali inasita nini kujaribu mfumo wa Mungano ambao wenzetu Wazanzibar wamekuwa wakiulilia ili tuone kama malalamiko haya yataendelea angalau kwa miaka miwili halafu baadaye tukiona kwamba mfumo huo unafaa basi tuendelee nao na tukiona kama haufai tukarudie kwenye mfumo ule ambao tunao sasa hivi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa hiyo umesema tujaribu kwa miaka miwili, Waziri wa nchi majibu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, suala la kujaribu mfumo mwingine ni masuala ambayo yataamuliwa katika Katiba ijayo, maoni ya wananchi yametolewa na Tume itaangalia mfumo upi kulingana na maoni ya wananchi unafaa kwa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba Serikali haiendeshwi kwa *'try and error'* kwamba tujaribu haikufaa turudi, tujaribu turudi, Serikali haiendeshwi hivyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ingekuwa hivyo ingekuwa ajabu sana. Mheshimiwa Mtinda.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kila mara tumekuwa tukisikia upande mmoja ukilalamika kwamba una kero nyingi na kero zao hazitatuliwi.

Je, upande wa Zanzibar hauoni kwamba umepewa upendeleo wa muhimu hasa hapa Bungeni, kwa sababu kuna wawakilishi wengi kutoka Zanzibar mfano, kuna wawakilishi kutoka Baraza la Wawakilishi, kuna Wabunge wa Majimbo, kuna Wabunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar lakini hakuna hata mmoja huku anayehudhuria Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Je, hiyo haioneshi kwamba Tanzania Bara haiwakilishwi vizuri hasa katika kutetea mambo yao kule Zanzibar kuliko wao wanavyowakilisha hapa Bungeni?(*Makofi*)

**SPIKA:** Waziri wa nchi majibu, naona maswali magumu na majibu magumu pia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Wazanzibar ndani ya Bunge siyo upendeleo bali ni matakwa ya Katiba, lakini Katiba hiyo hiyo haikueleza kwamba kuwe na uwakilishi kutoka Bungeni kwenda Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, ningemwomba Mbunge tutakapojadili hapa katika Bunge la Katiba penyeza na hilo, ahsante.*(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Itakuwa imejaa mambo kweli, tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Blandes atauliza swali hilo kwa niaba yake Mheshimiwa Chacha Nyangwine.

Na. 46

**Ugawaji wa Vitalu Ranchi ya Kitengule**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES )** aliuliza:-

Ugawaji wa vitalu vya ufugaji vya Ranchi ya Kitengule umeonyesha upungufu mkubwa mkubwa ikiwa ni pamoja

na kuvinyima Vijiji vya Katanda, Kihanga, Kibwera, Kishoju, Mlamba, na Mushabaiguru na baadhi ya maeneo kugawiwa wageni toka nje, na vingine viligawiwa kwa watu wasio na mifugo huku baadhi yao wakishindwa kutimiza masharti ya kuwekeza katika vitalu hivyo:-

(a) Je, ni Wawekezaji wangapi wageni kutoka nje walipata vitalu?

(b) Je, ni wawekezaji wangapi wameshindwa kuendeleza vitalu hivyo?

(c) Je, ki-utaalamu, vijiji vya Mushabaiguru, Kibwera, Katanda, Kihanga, Kishuru na Mlamba vinahitaji eneo kiasi gani kwa ajili ya ufugaji?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

(d) Mheshimiwa Spika, wawekezaji wote waliogawiwa vitalu katika ranchi ya Kitengule ni wazalendo na hakuna mwekezaji kutoka nje ya nchi.

(e) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ni kimoja tu kitalu Na. 288/14 ambacho uwekezaji haujaanza kutokana na mgogoro wa waombaji toka vijiji vya jirani. Hivi sasa mgogoro huo umekwisha.

(f) Mheshimiwa Spika, kitaalamu kulingana na hali ya malisho katika vijiji tajwa, hekta mbili na nusu (2.5) zinahitajika kumtunza ng’ombe mmoja mkubwa *(livestock unit)* kwa mwaka. Hivyo, Kijiji cha Kibwera chenye ng’ombe 3,015 kinahitaji hekta 6,332; Kijiji cha Katanda hekta 2,625; Kijiji cha Kahanga 6,966 na Kijiji cha Kishoju hekta 882. Hivyo, vijiji vyote alivyotaja Mheshimiwa Mbunge vina jumla ya ng’ombe 8,002 na vinahitaji jumla ya hekta 16,255 kwa idadi hiyo ya mifugo.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika ahsante, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza; Je, wananchi wa Karagwe hasa wa vijiji vya Mushabaiguru, Kibwera, Kishoju, Kihanga na Mlamba, watanufaikaje na uwekezaji huo?

Pili; kama mgogoro umekwisha ni lini uwekezaji utaanza katika vijiji vilivyotajwa.(*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kufaidika wanafaidika kwa sababu uwekezaji na moja ya masharti ya uwekezaji ni pamoja na kufuga kisasa, kufuga kitalaamu na kuwekeza vilivyo na kuachana na kuchunga bali ni kufuga kisasa. Kwa hiyo watajifunza kutokana na ufugaji ule wa kisasa unaoendeshwa katika uwekezaji ule.

Mheshimiwa Spika, Lakini la pili; baada ya mgogoro huo kuisha sasa hivi tunaandaa kumpatia mwekezaji huyo *sub lease* ili aweze kuanza shughuli hii ya ufugaji wa kisasa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Hivi karibuni tumepitisha mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana wanaojihusisha na sekta ya kilimo na maeneo mengine, ningependa kujua ni nini mpango wa Wizara wa kuwawezesha vijana wanaojishughulisha na masuala ya kiufugaji kwa kuwagawia vitalu vya ufugaji ili waweze kufuga kisasa na pia waweze kujikomboa na ajira.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, mpango wa kuwawezesha vijana kwa kuwapatia vitalu huwa haupo, lakini wanachoweza kufanya ni kukopa kwenye benki zetu *TIB* na sasa tupo kwenye mchakato wa kuanzisha benki ya kilimo ili kusudi waweze kupata mtaji wa kuweza kuomba vitalu rasmi na kupatiwa ili waweze kuwekeza kitaalamu.

Na. 47

**Deni Kubwa la Taifa**

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED** aliuliza:-

Deni la Taifa linaonekana kuwa ni kubwa kiasi cha kuwafanya Watanzania kuwa na wasiwasi nalo hasa kwa sababu halilipiki na bado Serikali inaendelea kukopa:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje Watanzania wapate kuelewa fedha hiyo iliyokopwa imetumika katika maeneo gani?

(b) Je, Serikali ina uhakika upi kwamba fedha hiyo imefanya kazi iliyokusudiwa na si vinginevyo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhammed Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa fedha zinazokopwa zimekuwa zikitumika kugharamia miradi ya maendeleo hususan miundombinu ya nishati, barabara, maji, afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, Fedha zilizokopwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/12 zilielekezwa katika miradi ya ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW60 Jijini Mwanza tulikopa (Euro Milioni 61, kutoka *HSBC*), ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 100 Ubungo – Dar es Salaam (dola milioni 1.3.728 kutoka *HSBC*) Miradi mbalimbali ya barabara nchini (dola milioni 103.728 kutoka *Credit Suisse*).

Aidha, Serikali ilikopa dola za Marekani milioni 178.125 kutoka *Exim Bank* ya India kugharamia miradi mbalimbali ya maji, pia Dola za Marekani bilioni 1.2 kutoka *Exim Bank* ya China kugharamia ujenzi wa bomba la kusafirishia gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na Dola za Marekani 230 kutoka *Standard Bank* kugharamia miradi mbalimbali ambayo ilikuwa imeainishwa katika bajeti ya maendeleo kwa mwaka husika Kitabu *Vol. IV,* upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar, Serikali ilikopa Dola milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kutoka Serikali ya Korea Kusini, Dola 70 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Zanzibar kutoka Serikali ya watu wa China, dola milioni 42 kwa ajili kwa ajili ya uimarishaji wa sekta ya elimu kutoka Benki ya Dunia, dola milioni 21 kwa ajili ya mradi wa Serikali mtandao (*E-Government*) na miradi mingine mingi inayotekelezwa kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza kuwa ukopaji wa Serikali inazingatia mkakati wa kitaifa wa (*National Debt Borrowing Strategy)* unaoainisha maeneo ya msingi kabla ya kukopa. Aidha, Serikali kupitia sheria na mifumo yake ya ufuatiliaji na tathmini *Monitoring and Evaluation* (*ME*) imekuwa ikisimamia matumizi ya fedha ikiwemo mikopo ili kubaini kwamba fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa kuwa, kutokana na uwiano wa pato la Taifa na Deni la Taifa linazidi kwa asilimia 40, na kwa kuwa riba ya deni inazidi kupaa kila leo.

Je, Waziri unaweza kuliambia Bunge hili kwamba ni jumla ya madeni ya kiasi gani ambayo mpaka sasa hivi hayajalipwa, au miaka mingapi mtaweza kulipa madeni hayo.

Swali la pili; hivi kuna madeni mangapi mpaka sasa hivi ya nje ambayo mmekwishayalipa au bado tu sisi tungali tunakopa na kupunguza kwa kila mwaka?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwanza maswali yake yame-*base* katika takwimu halisi, kwa hivyo naomba nipate muda ili niweze kumletea takwimu halisi hasa za madeni mangapi ambayo hayajalipwa na mengine ambayo tunaendelea kulipa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kumfahamisha kwamba madeni ambayo tunalipa sasa hivi mengine yalichukuliwa miaka ya nyuma pengine yanawezakuwa ni madeni ya miaka mingi kuliko umri wangu mimi hapa niliyesimama. Kwa hiyo naomba tu nipate hizi takwimu sahihi ili niweze kumpatia na yeye atafahamu kiasi halisi.

Mheshimiwa Spika, riba tunayolipa vile vile nyingine inatokana na madeni ambayo bado hatuja-*negotiate group* ambalo linaitwa *Non Paris Club*, bado tunaendelea ku-*negotiate* nao lakini riba ile kwa sababu hatulipi mpaka tumalize *negotiation* zetu ndiyo maana zinakaa. Kwa hiyo ninaomba tu kwamba nikupatie takwimu sahihi na nitakuletea kwa ajili ya *reference* yako.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi. Moja ya sababu kubwa ambayo inasababisha deni la Taifa kukua kila mwaka na kila siku ni pamoja na matumizi ya ndani kuwa makubwa zaidi hata kuliko uwezo wa fedha zetu za ndani tunazokusanya kila mwaka.

Kwa mfano mwaka wa fedha 2011/2012 tulikuwa na uwezo wa kukusanya trilioni 7.3 lakini Serikali katika matumizi yake ya kawaida ilitumia trilioni 8.6, *gap* la trilioni 1.3 maana yake zile tulikopa. Mwaka 2012/13 Serikali ilikusanya trilioni 9 lakini matumizi yetu ya kawaida yalikuwa trilioni 10.6 *gap* la trilioni 1.6.

**SPIKA:** Hilo ni swali la nyongeza au hotuba? maana yake hatuna muda sasa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika namaliza, ni lini sasa Serikali itakuwa na uwezo wa kuhakikisha kuwa inakuwa na mapato yake ya ndani ya kutosheleza ku-*fund* matumizi ya kawaida, na kuhakikisha kwmaba matumizi ya kawaida yanakuwa kidogo ili kuweza kuleta maendeleo kwa wananchi?

**SPIKA:** Swali refu sana la nyongeza Waziri naomba ujibu kifupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli swali lilikuwa refu lakini sikuweza kumpata hasa kitu anachokitaka kiundani kabisa, lakini naomba nimhakikishie kwamba kuwa takwimu zake azifanye sahihi. Serikali matumizi yake ya ndani hayatumii fedha za mkopo za nje kwa ajili ya kugharamia matumizi ya ndani.

Fedha zetu za ndani zinagharamia matumizi yetu ya kawaida ya ndani na kama jibu langu la msingi lilivyosema kwamba fedha ambazo tunakopa nje tunatumia kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa sababu ya kuleta tija na kuweza kuu-*service* huo mkopo pamoja na riba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia kwamba fedha yetu ya ndani ndiyo ambayo tunatumia kwa ajili ya matumizi ya ndani tu.

Na. 48

**Uratibu wa Kutoza Kodi Bidhaa Zinazoingizwa Nchini**

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS** aliuliza:-

Kuna tatizo kubwa la urasimu katika Idara ya Ushuru wa Bidhaa na Forodha *(Import Duty)* ya *TRA* unaoashiria rushwa na kupelekea kupungua kwa mapato.

Je, ni utaratibu gani unatumika kutoza kodi bidhaa zinazoingizwa nchini hasa magari?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja ya nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazotumia Sheria moja yaani *East African Community Customs Management Act 2004* katika kutoza ushuru wa forodha.

Aidha, nchi hizi kwa pamoja zinatoza ushuru wa viwango vinavyofanana kwa bidhaa zote zinazoingia nchini mwao kutoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tathmini ya bei ya magari hufanyika na kuhakiki bei iliyosemwa na mwingizaji kabla ya kutoza kodi kwa kiwango stahili.

Ili kufanikisha hilo, Idara ya Forodha na ushuru wa bidhaa inao mfumo wa kielectroniki unaotunza bei mbalimbali za bidhaa (magari) tofauti *(transactional price data base)* na hutumika kuhakiki bei zinazosemwa na

waingizaji mali kwa nia ya kuondoa udanganyifu unaoweza kusababisha kulipa kodi kidogo kuliko ilivyostahili.

Mheshimiwa Spika, vituo vyote vikubwa vya kuingizia magari nchini, isipokuwa Zanzibar, vimeunganishwa kielektroniki na kituo cha huduma za forodha kilichoko Dar es Salaam, ambapo uthamini na utozaji kodi bila kujali gari ilikoingilia hufanyika kwa kutumia...

**SPIKA:** Unahitajika utulivu ndani ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): ...***transactional price Data* au *import Export Commodity DATA Base (IECDB).* Utaratibu huu wa uthamini na utozaji kodi mahali pamoja nchini ulioanza Juni, 2011 umeleta uwiano ulio sawa kwa vituo vyote nchini na kuondoa tofauti ya kodi kwa bidhaa moja inapoingizwa nchini kupitia bandari au mipaka tofauti.

Mheshimiwa Spika, kupitia utaratibu huu, mwagizaji anaweza kukokotoa kodi za gari analokusudia kuagiza hata kabla ya kuliagiza ili mradi anafahamu aina ya gari, *model*, mwaka lilipotengenezwa na nchi linakotoka. Utaratibu huu umewawezesha waagizaji kufahamu kiasi cha kodi kabla ya kuagiza na hivyo kufanya maandalizi ya kutoa magari yao forodhani yanapofika na kwa kiasi kikubwa umepunguza malalamiko.

Mheshimiwa Spika, hapo awali uthamini wa magari ya aina hii ulitoa changamoto kwa *TRA* kutokana na baadhi ya waagizaji kutotoa bei halisi kwa kuwasilisha Ankara *(Invoice)* sahihi walizopewa wakati wa kununua magari.

Kwa kuliona tatizo hilo *TRA* ilianzisha ukadiriaji kodi kwa kutumia *calculator* ambayo imewekwa katika tovuti yake *www.tra.go.tz.* Utaratibu huu unajulikana kama '*Used Motor Vehicle Valuation System'* na upo kwenye tovuti ya *TRA*. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mhshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kodi inavyolipishwa ni *Cost Insurance and Freight (CIF).* Sasa inakuwaje *TRA* ya nchi hii waweke bei ambazo wamezitoa katika vichwa vyao na si bei halisi za bidhaa zenyewe zinavyouzwa katika soko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kama mfumo huu upo kweli, ni kwa nini basi usiwekwe wazi? Wafanyabisahara ku-*access* kuuona na kujua uhalisia wa bei gani watalipa ushuru, ili kuondosha ubabaishaji na rushwa iliyokithiri *TRA? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Haroub, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tozo inayotozwa pale siyo tu ya *CIF,* lakini vilevile ina-*consolidate* bei ya gari ambayo umenunulia pale. Kwa hiyo, ukienda kwenye tovuti pale list za magari pamoja na *model* zilizoko pale na mwaka kwa hivyo, kinachokokotolewa pale ni *taxes* ambazo zipo, *depreciation* ipo na kila kitu kinafanyika pale.

Kwa hivyo, hakuna bei ambayo inatolewa na mtu wa *TRA* kichwani, isipokuwa bei ipo katika *DATA Base* na mnunuaji anaona kabisa popote alipo kwa sababu, ni *web site* ambayo inakuwa *accessed around the world* kwa hivyo, popote ulipo kabla hujanunua gari lako ama umeshanunua gari lako, ukienda katika tovuti ya *TRA* katika *IECDB,* utaona bei halisi ya gari, mwaka na utajua bei halisi ambayo ipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hilo nalo linajibu swali lako la pili. Mfumo huo upo kweli na pengine tukipata muda ninaweza nikakuonesha. Nina *access* na *internet* humu ndani, ninaweza nikakuonesha.

Tuko katika tovuti ya *www.tra.go.tz,* tukienda pale tutaona *web site* wote. Kwa hivyo, ninatoa wito kwa wafanyabiashara kwamba, wanaponunua magari yao wahakikishe kwamba, wamekwenda katika *web site* wameona *DATA Base* ilivyo na watapata uhalisia wa bei ambayo wataweza kutumia.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu nihakikishe kwamba, bado kumekuwa kuna wafanyabiashara ambayo siyo waaminifu, wanaleta *invoice ambazo siyo* zile halisi walizonunulia gari. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba tushirikiane kwa hili kuhakikisha kwamba, mfumo huu unafanya kazi kwa ajili, ya kukidhi matakwa ya maendeleo nchini. *(Makofi)*

Na. 49

**Kukomesha Mauaji ya Raia Yanayofanywa na Polisi**

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA** aliuliza:-

Hivi karibuni kumekuwa na matukio ya mauaji ya wananchi wasio na hatia yanayofanywa na Jeshi la Polisi katika Mikutano ya Siasa:-

(a) Je, Serikali, imechukua hatua gani kukomesha na kudhibiti mauaji hayo ya kinyama kwa raia?

(b) Je, Serikali, ipo tayari kukiri kwamba, imeshindwa kuwalinda raia wake kwa kuwa, vyombo vyake ndivyo vinavyofanya matukio hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naomi Amy Mwakyoma Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu *(a)* na *(b)* kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 29 (1) & (2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura 322 na Kifungu 21 (1) & (2) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya JInai Sura ya 20, sambamba na Kanuni za Kudumu za jeshi la Polisi, *(PGO 274)* vinampa Askari Polisi uwezo wa Kisheria wa kutumia silaha anapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Askari Polisi haruhusiwi kutumia silaha hiyo kinyume cha Sheria na kusababisha vifo au madhara mengineyo kwa raia mwema. Pamoja na elimu na mafunzo Serikali, imekuwa ichukua na itaendelea kuwachukulia hatua za Kisheria, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi na kufikishwa Mahakamani Askari wote watakaobainika kutumia vibaya silaha wanazokabidhiwa wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya IV ya *CCM,* haijashindwa kutoa ulinzi madhubuti kwa raia wake. Utulivu na amani iliyopo hapa nchini ni ishara kwamba, hali ya ulinzi kwa raia na mali zao ni ya kuridhisha.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ambayo hayajazingatia hali halisi, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba; ikiwa Sheria ndivyo isemavyo, basi inakuwaje kwamba, matukio ya watu kuuwawa na Polisi kwa risasi au kuumizwa yanazidi kuongezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, Serikali, iko tayari kuunda Tume ya Mahakama *Judicial inquiring,* ili kuchunguza haya matukio kwa ajili, ya kunusuru nchi yetu kuingia katika ghasia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu maswali mawali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza kuongezeka kwa mauaji. Polisi ni wasimamizi wa usalama wa raia. Usimamizi wao unategemea mazingira ambayo yana-*prevail.* Iwapo teknolojia zinabadilika mfano, ikiwa *attitudes* za watu zinabadilika mfano, ni lazima Polisi *approach* yao na matukio yawe tofauti na ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu la sasa ni uamuzi wa kutokutii Sheria kwa makusudi. Matukio ambayo yalitokea yote, Polisi *pro-actively* walisema kwamba, maandamano au mikusanyiko hii isifanyike kwa sababu, ya hatari ya kutokea madhara na bado tukaendelea kufanya; tutaendelea kuyapunguza haya matukio iwapo tu, tutatii Sheria bila shuruti yoyote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali iko tayari kuunda Tume; utaratibu wa kuunda Tume, mara nyingi unakuwa pale mauaji yana mashaka, hatujui nini kilitokea, hatujui mwuwaji ni nani na mazingira yake yote ni ya mashaka. Mauaji ambayo, yametokea kwa bahati au kwa sababu, hizo ambazo nimezisema ni mambo ambayo tunajua ame-*shoot* nani na kapiga risasi ngapi. Kwa hiyo hapa hatuhitaji uchunguzi kwa vyo vyote vile.

Na. 50

**Uchimbaji wa Makaa ya Mawe Kijiji cha Ntundawaro**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Kampuni ya *TANCOAL* imeanza uchimbaji wa makaa ya mawe katika Kijiji cha Ntundawaro, Kata ya Ruanda, Wilayani Mbinga:-

(a) Je, Serikali, haioni umuhimu wa kufua umeme kwa kutumia makaa hayo?

(b) Je, Serikali, haioni umuhimu wa kuyashirikisha mashirika kama *PPF* na *TANESCO* katika kununua mitambo ya kufua umeme huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, lenye sehemu *(a)* na *(b)* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia Shrika la Umeme *(TANESCO),* iko kwenye majadiliano ya kuingia mkataba wa ubia na mwekezaji, Kampuni ya *Intra Energy Tanzania Ltd.,* ili kuweka mitambo ya kufua umeme wa *Megawatt* 200 huko Mbinga kwa kutumia makaa ya mawe ya Ngaka.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia *NDC,* imeingia ubia na kampuni ya *Intra Energy Tanzania Ltd.* kuunda kampuni ya *TANCOAL.* Katika ubia huo *NDC* ina hisa 30% na hiyo *Intra Energy Tanzania Ltd.* ina hisa 70%. Aidha, Serikali, ina mpango wa kuwa na hisa zaidi kupitia mashirika yake kama *TANESCO* na *NDC* katika ufuaji wa umeme huo wa *Megawatt* 200 huko Ngaka, Wilayani Mbinga.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, lakini kabla sijauliza maswali yangu ya nyongeza mawili, ningependa kuiomba Serikali, irekebishe jibu lake la (a). Usahihi ni kwamba, *TANESCO* ndio kwanza sasa wanajadiliana juu ya kuuzianau meme huo na majadiliano yao yanahusu ubia.

**SPIKA:** Kwa hiyo, swali la pili, uliza?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Aah haa, sijauliza swali.

**SPIKA:** La kwanza si ndio hilo?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nimemwambia arekebishe jibu lake.

**SPIKA:** Atarekebisha, maana yake hivyo hivyo; haya, uliza la pili.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, sio swali. Sikutaka kusema tu jibu sio sahihi, ilikuwa ni uungwana.

**SPIKA:** Uliza la pili bwana.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, *TANESCO* sasa hivi wanatumia bilioni 5 kila siku kwa ajili ya kuendesha yale majenereta. Umeme huu wa makaa ya mawe ungeweza kuuzwa pengine kwa senti 10 au 15 ya *USD;* majadiliano haya sasa yamechukua miaka minne, yataisha lini?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa, la kwanza nalo jibu na la pili jibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kayombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kwamba, katika utaratibu wa uwekezaji katika masuala ya umeme kwa namna yoyote ile ni lazima *TANESCO* waweze kuhusika, ndio biashara ya umeme iweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ni kwamba, ni kweli kwamba, tunatumia fedha hizo katika kuzalisha umeme. Ni kweli kwamba, tunayo makaa ya m awe ambayo yanaweza kuzalisha umeme wa bei rahisi zaidi, lakini masuala haya ni mchakato.

Kwa hivyo, wakati wowote mchakato huu utakapokamilika, mradi huu utatekelezwa kwa sababu, ni miongoni mwa miradi ambayo Serikali, imeiweka kuwa miradi ya kipaumbele.

Na. 51

**Umeme Hafifu - Kanda ya Kaskazini**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI K.n.y. MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO** aliuliza:-

Katika Kanda ya Kaskazini, hasa Mkoa wa Kilimanjaro, kuna mtandao mkubwa wa umeme wa gridi ya Taifa, lakini umeme unaopatikana ni hafifu sana ambao haufai kusomea wala kuwasha hata taa ya mshumaa *(tube light)*:-

Je, Serikali, ina mkakati gani wa kurekebisha umeme huo, ili uwe umeme wa kweli?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, matatizo mbalimbali ya umeme katika Kanda ya Kaskazini, hasa Mkoani Kilimanjaro, yanatokana na ukweli kwamba, mtandao wa umeme katika Mkoa huo ni mkubwa na wa muda mrefu sana. Hali hiyo imesababisha kuzidiwa kwa gridi kwa upande mmoja na kuzidiwa kwa vituo vyetu vya kupoozea umeme na hivyo husababisha kukatika kwa umeme mara kwa mara na kuwa na umeme hafifu kwenye mfumo.

Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia *TANESCO,* inatekeleza mradi mkubwa wa *TEDAP* katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, ili kutatua matatizo ya umeme hafifu. Miradi hii ya kuimarisha umeme katika Mikoa hiyo, inahusisha:-

(i) Ujenzi wa njia kubwa ya kupoozea umeme wa msongo wa *KV 66* kutoka Kiyungi hadi Makuyuni.

(ii) Upanuzi wa vituo vya Kiyungi *(20 MVA), YMCA (17MVA)* na Lawate *(10MVA)*

(iii) vituo vipya viwili vimejengwa ambavyo ni Makuyuni *(20MVA)* na *KCMC (10MVA)* na miradi hii imekamilika na kukabidhiwa tarehe 18 Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi mingine inayotekelezwa chini ya *TEDAP,* inayohusisha:-

(i) Kituo cha *KIA,* kitakachokuwa na ukubwa wa *40MVA* na kitahudumia baadhi ya maeneo ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara – Mererani.

(ii) Ujenzi na uboreshaji wa njia za msongo wa *KV33* ya kusambaza umeme kutoka kwenye Kituo kipya. Ujenzi wa kituo hiki utakamilika mwezi Juni mwaka huu wa 2013.

Aidha, miradi mingine ya *TEDAP* itakayokamilika mwaka 2014 itahusisha upanuzi wa kituo cha Kiyungi, kwa kuweka transfoma kubwa ya *50MVA* na kubadili miundombinu ya Kituo kutoka mfumo wa zamani na kuwa wa kisasa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, ili kusaidiana na Serikali kutatua tatizo la umeme katika Kanda hii, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai, pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Hai, wametafuta na kupata Mfadhili, ambaye yupo tayari kufufua mitambo ya kufua umeme iliyoko kule Kikuletwa – Rundugai, kwa thamani ya Dola milioni 18.

Je, ni kwanini, Serikali, inaona kigugumizi kukabidhi mitambo hii kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, ili kuweza kuifufua na kusaidia kutatua tatizo la umeme katika eneo hili?

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo *TANESCO* wameweka nguzo za umeme tangu mwaka 2004, kwa mfano eneo kutoka kwa Luka – Mchomba hadi Nduweni – Tarakea katika Wilaya ya Rombo. Mpaka sasa hivi nguzo zile zimesimama na hakuna kinachoendelea.

Je, ni lini Serikali, itapeleka umeme kwenye maeneo kama haya ambayo nguzo zimewekwa muda mrefu na hakuna lolote linaloendelea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeaza ya Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na chanzo cha *hydro* ndogo ya Kikuletwa, kule Hai, sina taarifa zozote kwamba, Mheshimiwa Mbowe, amewahi kutafuta mfadhili na sijawahi kuona *document* yoyote katika Wizara yetu. Kwenye kile Kituo, baada ya maombi ya Chuo Cha Ufundi – Arusha *(Arusha Technical College)* kuomba kukitumia kituo kile, kwanza kufufua ule mradi ili uweze kutumika kuzalisha umeme, lakini pili wanataka kutumia kwa ajili ya kufanya *training* kwa wanafunzi. Kwa hiyo, kitakuwa ni kituo ambacho kitafanya mafunzo kwa vijana wanaojifunza umeme kutoka Chuo cha Ufundi - Arusha. Kazi imeshaanza na wanafunzi kwa kutengeneza vipuri vyao wenyewe vya Watanzania hapa hapa, sio kuagiza kutoka nje. *(Makofi)*

Kuna maeneo ambayo kama ya kwa Luka Mchomba, ambako kuna nguzo zimesimikwa. Naomba hili tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge, tuone namna gani zinaweza zikawekwa nguzo zikakaa muda wote huo hakujawekwa umeme, tujue tatizo ni nini.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na kama tulivyoona saa imefika kwa hiyo, tunaendelea.

Katibu tuendelee!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtaona kwamba majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu leo ndiyo siku ya mwisho. Kwa hiyo, Wabunge mtachangia asubuhi hii wachangiaji kumi na tano halafu tutaita baadhi ya Manaibu Waziri wajibu halafu tutaingia jioni tutaingia kwenye mjadala.

Kwa hiyo watu ambao tulitegemea wachangie katika hotuba hii ni 103 na kwa sababu ya nidhamu tuliyokuwa nayo, hiyo namba imefikiwa. Lakini Waheshimiwa Wabunge sijui jana mlipagawa na kitu gani badala ya kujadili hotuba mkajadili matusi mimi naomba kuwashangaeni kabisa mmevaa suti vizuri kabisa mnatoa matusi midomoni mwenu mbona havifanani. Unajua mtu ukivaa rasmi namna hii halafu unatoa matusi yasiyofanana na wewe inakuwa aibu kabisa. *(Makofi)*

Basi nina ujumbe mmoja ulioletwa kwenye simu yangu nimepokea *message* inasema hivi:

Hilo Bunge lenu sasa limezidi mpaka mnaitana..........hata mimi naogopa hata kutaja maneno hayo mdomoni mwangu. Sitaji vitu vya namna hii. Anasema huyo mtu kuanzia sasa sitathubutu kukaa na watoto sebuleni kusikiliza tena maana ni aibu inabidi niwe nawasikilizeni ninyi chumbani.

Hilo neno alilotaja mimi siwezi kutamka mdomo mwangu haupaswi kutamka matusi. Jamani tafadhali mjiheshimu hata kama mnashindana kwa vyama hivi kweli mliunda vyama kushindana kwa matusi jamani. Vitu vingine muwe mnaona aibu umevaa suti vizuri sijui halafu mnatoa matusi jamani ni aibu kabisa aibu aibu.

Sasa tutakubaliana mimi nina mamlaka kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, mtu yoyote anatumia matusi namwita polisi anachukuliwa humu ndani anakwenda, kwa pande zote atachukuliwa na Polisi kama utakata rufaa ukate baadaye. Maana kuna watu wanasema mimi sifanyi jambo lolote jamani tunafikiri watu wazima tukielewana tunaelewana.

Wananchi hawakutatuma mtukane jamani na haiwasaidii kitu. Sasa mjadili vizuri kama mlivyoanza kujadili tuendelee namna hiyo kwa heshima kama mnataka kutukana basi tuwatengenezee ukumbi maalum muwe mnatukanana peke yenu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kutokana na muda uliopo tatizo ni muda Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, leo kama ulivyotuambia ndiyo tuna jadili Bajeti hii. Kwa kawaida tunaingia kwa vifungu lakini zana nzima ya kugeuza utaratibu wetu ilikuwa ni kwamba tuwape Wizara, tuipe Serikali muda wa kuweza kuchukua mawazo yetu na kuona wapi ambapo wanaweza wakarekebisha mahesabu yao au takwimu ambazo wametuletea kwa sababu kuna sehemu zingine tungependa kuona hela nyingi zaidi zinaenda kwa umwagiliaji au kwa maji.

Baadhi ya mikoa ambayo tuliyo nayo wala hatujui fedha gani ambayo tumepewa zaidi katika Wilaya kama vile Wilaya ya Ikirima sijui ulikuwa unaonaje wewe Mheshimiwa Spika, tukiingia kwa vifungu leo tukapitisha si tutakuwa tu tumerudia makosa yale yale kama yale ambayo tumefanya muda wa miaka hamsini.

Mheshimiwa Spika, isingekuwa vizuri labda tungewapa muda sasa wakaenda wakatafakari halafu waone ni vitu gani wanaweza wakarekebisha katika voti hii naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Cheyo nashukuru kwa kusema hivyo ndiyo ukweli utaratibu tuliokubaliana unapasa kufanya mawasiliano kabla. Lakini tulipoangalia kwa sababu ya muda uliokuwepo Dar es Salaam na hoja nyingi zilizotoka kwenye Kamati.

Kwa hiyo, kamati ya Bajeti imeendelea kukaa na nafikiri watakaa baada tu ya hotuba ya Waziri Mkuu watakaa maana yake zile sekta Waziri Mkuu hakuna sekta ya maana sana na hata Kamati yao waliridhiana wakati wanapitisha matokeo katika mambo ya TAMISEMI waliridhiana lakini sekta zingine watakaa siku ya Alhamisi yale mengine tunaangalia upya.

Maana yake kuna maeneo yale ya kisekta ndiyo maana walielewana na Kamati yao hatuna hoja za msingi katika ofisi ndiyo maana tukaona tuanze, lakini tutoe muda kwa Bajeti *Committee* kupitia yale waliyoleta wenyeviti kutoka kwenye Kamati zao ndiyo Bajeti *Committee* toka tumefika hapa wanaendelea na kufanya kazi hiyo na itakamilika alhamisi. Tutakaa Bajeti *Committee* na zile sekta na Serikali tuweze kusema hayo unayosema.

Kwa hiyo, ni sahihi lakini kwa maana hii Ofisi ya Waziri Mkuu kulikuwa hakuna hoja maalum na Ofisi yenyewe ni jumla mno ndiyo sababu. Kwa hiyo namwita Mheshimiwa Catherine Magige atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Nchambi na Mheshimiwa Rose Kamili ajiandaye, tusitumie muda bila sababu. Nani anasema mwongozo.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya fedha anajibu swali Namba 48 la Mheshimiwa Haroub lililokuwa linahusiana na *TRA* kutoza kodi kwa kutofuata zile bei ambazo ni za wale wanaotuuzia magari ambayo tunaona hata kwenye *website* bei zao.

Mheshimiwa Naibu Waziri yeye akawaambia Watanzania kwamba ukifungua tovuti ya *TRA* ndiyo utaona pale kuna bei na *model* na mwaka sasa nataka kujua kama ni sahihi kwamba *TRA* siku hizi nao wanauza magari ili tuweze kujua kwamba tukitaka kununua gari tunafuata bei za *TRA* kwa sababu Watanzania eneo hili la kununua magari wamekuwa wakipata matatizo. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako kama ni gari kwa kuangalia tovuti na bei za *TRA.*

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea Mheshimiwa Catherine Magige, atafuata Mheshimiwa Masoud Chambi.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Naomba nielekeze moja kwa moja katika mchango wangu katika suala zima la ajira.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishuhudia nchi zinazoendelea na zisizoendelea kukitokea machafuko kwa sababu ya ukosefiu wa ajira. Tulishuhudia Ufaransa miaka miwili iliyopita tulishuhudia Tunisia yule kijana ambaye alikuwa amehitimu chuo Kikuu akawa anauza mboga lakini kwa ajili ya unyanyasaji aliamua kujilipua.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wa Kitanzania wana tatizo kubwa la ajira tumekuwa kila siku tukiongelea tatizo hili la ajira hapa Bungeni wanasiasa mbalimbali wamekuwa wakiliongelea lakini hatuoni mafanikio yoyote. Ninapoongelea suala la ajira naongelea vijana wenye taaluma na vijana mbalimbali kama wamachinga.

Inasikitisha sana kuona kijana wa Kitanzania anakosa mlo mmoja kwa siku kwa ajili ya ukosefu wa ajira huku wageni wakiwa wanafanya biashara ambazo wanaweza kuzifanya kijana wa Kitanzania. Tumeshuhudia wamachinga mpaka Kariakoo wamachinga wa kigeni, vijana wetu hawana ajira lakini itapatikana wapi, usalama wa raia utapatikana wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, vijana wakikosa ajira wanajiingiza katika masuala ya uhalifu. Tunaomba sana Serikali itilie mkazo suala hili la ajira vijana wa Kitanzania wapate ajira na wawe na amani na furaha katika nchi yao. Tumekuwa tunaona watu wanafikia kipindi cha kustaafu wanastaafu lakini wanaongezea miaka ya kufanya kazi na huku vijana wetu wapo, vijana wazuri wenye taaluma nzuri tu wakikosa nafasi za kazi. Tunaomba Serikali iangalie upya suala zima la vijana ili waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, nielekee katika afya ya uzazi, mama na mtoto. Tumekuwa tunaona kila siku viongozi mbalimbali wanasema tupunguze vifo vya kina mama wajawazito, lakini tunaona sehemu nyingi sana tatizo hili bado linaendelea.

Naomba nitolee mfano katika mkoa wangu wa Arusha tarehe 13 Lilian Frank alikuwa anaumwa uchungu wa kuzaa mtoto wake wa nne akapelekwa katika Hospitali ya Daktari Wanjara, alipofika pale wakamlaza tarehe 14 akawa anafanyiwa *operation* umeme ukakatika *generator* likawa halina mafuta mama yule alipoteza maisha na mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, hii inasikitisha sana na ni jambo la aibu sana katika Serikali yetu ya Tanzania na Wizara ya Afya. Ina maana hawafanyi ukaguzi katika vituo vya Afya na Hospitali hii ipo dakika 10 tu kufikia Hospitali ya Mkoa. Siyo Arusha tu, juzi nimeona katika gazeti la nipashe wanaeleza Hospitali ya Sinza Palestina wamekimbiza wajawazito Mwananyamala kwa ajili umeme ulikatika *generator* likawa bovu.

Mheshimiwa Spika, hali kama hii inasikitisha sana katika nchi yetu na inahuzunisha sana, akina mama hawatendewi haki. Akina mama wajawazito wanakufa kila siku. Tunasema tunapunguza tatizo la watoto yatima, tatizo la watoto wa mitaani, lakini kwa hali hii mimi nadhani tunaongeza tu tatizo la watoto wa mitaani.

Vile vile hii Hospitali ambayo ipo Mkoani kwangu Arusha ina kashfa nyingi nyingi sana naomba Serikali ijitahidi sana kufuatilia vituo hivi vya Afya, maana kila siku tumekuwa tunashuhudia wanafunzi wasichana wadogo wadogo wakipanga mstari kwenye ile Hospitali hatujui kitu gani kinachoendelea huko tunaomba Serikali izingatie sana haya katika ile Hospitali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa kila siku tukizungumza kuwa watoto wa mwaka mmoja, mpaka miaka mitano wana hatari kubwa sana ya kufa na Malaria. Tumekuwa tukipata misaada mbalimbali kutoka kwa wahisani tunaambiwa tutumie vyandarua kwa ajili ya Malaria. Lakini cha kusikitisha Dar es Salaam kwenye foleni tunauziwa vyandarua kwa bei ya 6,500/= ambazo tumepewa na wahisani kabisa vyandarua kimeandikwa hakiuzwi lakini imekatwa na tunauziwa.

Je wahusika ni kina nani? Wizara ya Afya inafanya nini au wenyewe ndiyo wanahusika tunaomba sana Serikali iangalie kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu suala hili watoto wanakufa kwa malaria wahisani wanatusaidia vyandarua vinauzwa vimeandikwa kabisa *UK AID.* Kwa hiyo ina maana vyandarua vile tumepewa na Serikali ya Uingereza lakini vinauzwa mitaani, naomba sana Serikali iangalie, Wizara ya Afya iangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze moja kwa moja katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha inakabiliwa na changamoto ya miundombinu ambayo ni barabara na maji. Kina mama wamekuwa wakitembea umbali mrefu wanaamka alfajiri kwa ajili ya kutafuta maji. Naomba sana Serikali iangalie suala hili ili wakina mama waepukane na kero hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, naomba niingie moja kwa moja katika suala zima la udini. Kumekuwa kukiendelea kila siku

machafuko ambayo yanatokea katika nchi yetu yameanza kutokea kwa ajili ya haya mambo ya udini. Tangu enzi za Mwalimu Nyerere tumezoea kukaa kwa amani. Tanzania ni ya Waislamu, Tanzania ni ya Wakristo Tanzania ni ya Wapagani, Tanzania ni ya kila Kabila.

Lakini mimi naona kama Serikali inakuwa inaviachia sana mpaka pale linapotokea tatizo ndiyo tunashtuka. Tumeona Masheikh wanatoa *DVD* mbalimbali, tumeona Maaskofu wanatoa dini zote zinaleta machafuko, tunapokea *message* kwenye simu *TCRA* wanafanya nini. *Message* za udini machafuko katika nchi yetu watu wamekuwa wanatumiana *message.* Lakini *TCRA* inatakiwa iwe makini sana kwa *message* kama hizi kwa sababu *message* moja ninapoipata mimi nikimtumia mwenzangu ni kosa. Kwa hiyo, iwe *strict* kwa suala kama hili ama sivyo tutakuja kushtuka machafuko yameshatokea ndiyo tunaangalia tatizo liko wapi. Naomba Serikali iwe inaangalia kabla hatujapata madhara makubwa ndiyo iwe inaangalia vitu kama hivi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Nakushukuru sana kwa kuniachia dakika nitangaze hawa wanaoleta matangazo yao walichelewa. Kwanza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba na robo kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Namba 231 na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya kilimo, mifugo na maji.

Mheshimiwa Profesa Peter Msolla anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba saa saba na robo watakuwa na kikao chumba Namba 219 na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo wenyewe watakutana saa tano kutakuwa na kikao kwenye ukumbi wa Msekwa B.

Halafu tunaambiwa kwamba mamlaka ya vitambulisho vya Taifa *NIDA* inawatangazia Wabunge wote ambao hawajachukua vitambulisho vyao wafike katika jengo la ukumbi wa Msekwa. Aidha, Wabunge wanaotaka kuthibitisha taarifa zao zilizomo ndani ya *chip* kwenye kitambulisho, kufanya hivyo kwenye ukumbi huo huo kwa sababu juzi kuna mtu ..... ana *gender* basi mkaangalia kweli kama cha kwako kimebakia jina na *gender* lakini tunadhani kuna habari nyingi zaidi.

Halafu kuna hizi Kanuni mpya tulizozipitisha vitabu viko kule kwenye *pigeon holes* Wabunge mkachukue kwa ajili ya matumizi ya humu ndani. Halafu moja Waheshimiwa Wabunge wajibu wa Ofisi yangu ni kusimamia ujenzi na kukamilisha Ofisi za Wabunge huko mnakotokea. Sasa kuna Ofisi 75 ambazo zilishakuwa zimejengwa na zaidi ya 45 ndiyo angalau ziko katika hali nzuri ya kuweza kukaliwa. Kwa hiyo, sisi tulifikiria kwamba *furniture* tunazotakiwa kuweka kule tusinunue kwenye maduka. Kwa hiyo, tumeomba wenzetu wa Magereza watutengenezee *sample* ya *furniture* hizo ambazo zitakuwa za Wabunge katika Ofisi zao na tulichoangalia ni ule uimara, *durability* kwa sababu haiwezekani tuwe tunanunua *furniture* baada ya mwaka mmoja yanakuwa matakataka tunatupa huko.

Kwa hiyo, hizo *sample* ziko hapa chini *basement* ukipata muda pale Mheshimiwa Mbunge nenda ukaangalie kule *basement* mtakuta hizo *sample* liko *desk* la *secretary,* kwa wewe Mheshimiwa, Viti vya Ukumbi na meza utavikuta. Kwa hiyo, mnaalikwa kwenda kuangalia kule chini kwa wakati wenu ni leo na kesho. Wote mnaenda kuangalia huko *basement* zimekuwa *displayed* na magereza halafu na *comment* zetu mtapeleka kwa Katibu wa Bunge. Tunaendelea na michango mingine Mheshimiwa Suleiman M. N. Suleiman, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose K. Sukum na atafuatiwa na Mheshimiwa Rachel M. Robert.

**MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa ulliyonipatia . Kwanza nianze kwa kutoa pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kishapu

kwa mafuriko makubwa waliyoyapata, yaliyoleta athari kubwa kwa kaya 232 mbuzi, ng'ombe, kuku wakachukuliwa na maji Kata ya Bulambiyu na baadhi yao Kata ya Gubiki, Kitilima na kule Mamwalasa nawapa pole sana wananchi wangu na nataka niwahakikishie uwakilishi wangu kwao upo makini na watapata msaada kama ambavyo Mheshimiwa wangu DC Ng'ondiape ambavyo alikimbia haraka sana na kuunda Kamati ya dharura na tayari misaada imeanza kumiminika kwa ajili ya kuwasaidia wanachi walio katika makambi kutokana na mafuriko hayo.

Nianze kuongelea suala la njaa jimbo la kishapu kila mwaka limekuwa na utaratibu ama mazoea ya kutopata mvua nyingi. Tunalo tatizo kubwa sana la njaa. Nilipeleka maombi yangu ya dharura, nimekwenda na Mkuu wa Mkoa kumwona Mkurugenzi wa maafa, Mkurugenzi wa *NFRA* kwa ajili ya kupata chakula cha msaada kwa wananchi wetu. Sasa mimi nilitaka niseme na niwaambie viongozi hawa Mheshimiwa Waziri Mkuu nilimwona alinisaidia sana na akanitambulisha kwa hawa watu nikaenda nikawaona na walipata taarifa kwamba tuna njaa ya dharura vikongwe wanapata tabu, lakini tangu nimekwenda leo takribani siku 45 dharura ile haijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka nitoe angalizo kwamba kuna masuala ambayo ni ya msingi. Inapotokea dharura Mheshimiwa Spika hapa kikilia kengele sisi wote tutatoka nje bila kujali umri, bila kujali itifaki lakini wananchi wangu wanamatatizo ya njaa mpaka leo hii, atu wanasuasua. Naomba sana wananchi wa Kishapu hawakupata mvua za kutosha, mvua zimekuja zimeleta mafuriko na athari kubwa naomba chakula cha njaa kiende kwa mtindo wa dharura.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la maji ya ziwa Victoria. Suala hili nimelipigia kelele sana Serikali inahitaji kutenga bilioni 13 peke yake kukamilisha mradi wa maji wa Ziwa Victoria yatakayopita Kata ya Songwa, Mwadui Luhumbo, Kata ya Kishapu yatakapoishia wananchi hawa watanufaika na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii inasomwa sasa takribani mara ya tatu. Suala hili halijapewa kipaumbele cha kuridhisha. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo kwamba maji yaende Kishapu.

Lakini sijui tumekuwa na utaratibu wa kuishi kama Kambale, maana kambale akizaliwa leo, ana ndevu hampi shikamoo mkubwa. Kama maelekezo yametoka kwa viongozi naomba tutekeleze Ilani ya Chama chetu na ahadi za viongozi.

Naomba sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe achukulie suala hili la maji. Bunge lililoisha aliniahidi, atakuja Kishapu na atashughulikia masuala ya Mabwawa, Visima na Maji ya Ziwa Victoria, na atatoa majibu kwa wananchi. Haikufanyika hivyo, najua ni kutokana na majukumu mengi, nina imani baada ya Bunge hili atafika mara moja na kutoa majibu kwa wananchi wangu.

Mheshimiwa Spika, suala la maji lipo pia katika Mji wa Shinyanga. Tuliomba hizi Taasisi mbili za Kashiwasa na Shiwasa ziangaliwe namna ambavyo zitaboreshwa na Taasisi moja, ivunjwe ili wananchi wanufaike na maji kwa bei rahisi. Ninaomba sana Waziri mwenye dhamana, ashughulikie Maji ya Mji wa Shinyanga. Sisi hatutakubali wananchi wapate huduma ya maji kama biashara. Maji ni huduma na ni wajibu wa Serikali kutoa huduma kwa wananchi wake.

Mwaka jana tulipata ahadi angekuja akashughulikia, lakini kama alikuja hakushughulikia suala hilo na bado tatizo hilo ni kubwa. Naomba sana Bunge hili na Waheshimiwa Wambunge. Maji ni muhimu kwa wananchi wetu, kila mmoja atakaye inuka hapa aunge mkono suala la maji. Ili hata wale wa Tabora, Igunga na maeneo mengine waletewe maji ambayo yatakuwa ni ya gharama nafuu. Mkilichukulia suala hili mzaha na ninyi mnaoletewa maji yatakuwa ya bei ya juu na yatakuwa biashara na siyo huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo kubwa la hosipitali ya Wilaya ya Kishapu. Vigezo moja wapo vya kuwa Wilaya, ni lazima ukidhi mahitaji mbalimbali ikiwemo Hospitali ya Wilaya. Wilaya ya Kishapu tangu 2003, haijakamilisha hospitali yake ya Wilaya kutokana na Historia ya Wilaya ya Kishapu. Tumeleta maombi maalum zaidi ya mara tatu na safari hii tumeleta, ninaomba sana Serikali izingatie, ifikirie na kuthamini Afya za wananchi wangu wa jimbo la Kishapu. Tupate fedha zile, kwa sababu hata kama tungelikuwa tunatenga kidogo kidogo, Bajeti hii mpaka sasa tunavyoongea, pesa tuliyoipata haizidi 25%. Sasa tutajenga vipi miradi ya maendeleo?

Naomba sana Waziri mwenye dhamana, Hospitali yetu ya Wilaya, nakuomba sana sana! hatuna hospitali ya Wilaya, hatuna Dawa za kutosha, hatuna hata *Mortuary* ambako tutatunza maiti zetu. Pale kutunza maiti ni kama stoo na mwaka jana niliongea, ninaomba sana sana!

Tunalo tatizo kubwa sana kwenye Migodi ya Almasi Kata ya Songwe. Wananchi wangu wamekuwa wakipigwa risasi, wamekuwa wakiuwawa, wamekuwa wakitendewa dhuluma, wamekuwa wakiona migodi ikifanya kazi lakini hakuna chochote katika huduma tano ambazo mwananchi wangu anatakiwa apate za haraka. Maji, Afya, Elimu, Barabara na masuala mengine. Ninaomba sana Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na timu yake, wafike Kishapu, Mgodi ule umeanza kuchimbwa Almasi toka mwaka 1963.

Bado tunayo matatizo makubwa na hata mahusiano siyo mazuri. Wananchi wamekuwa wakipigwa risasi, wanavunjwa miguu, wanakatwa miguu, wanakuwa vilema, matatizo ni makubwa nimepiga kelele sana. Nawaomba ndugu zangu, najua Wizara imetuahidi kufika na kushughulikia suala hili, lakini lipewe kipaumbele na wananchi waweze kunufaika na rasilimali ambazo walizitunza tangu enzi na enzi.

Ninalo tatizo jingine ambalo ni kubwa sana, tatizo la ubadhirifu wa fedha. Sisi tumepotezewa fedha zetu zaidi ya bilioni 6.7, ambazo zingekwenda kwenye miradi ya maendeleo. Aliyepoteza kwa kiasi kikubwa fedha zile ni Benki

ya *NMB,* awamu iliyoisha Bunge la mwaka jana nilisema, *NMB* ndiye aliyetunza fedha zile. *NMB* ndiye aliyeshiriki kwa kiasi kikubwa na watendaji wa Halmashauri kufanya ubadhirifu kwenye fedha zile. Tumekusudia kuishitaki *NMB,* na naomba serikali isimamie iishitaki *NMB* kwa sababu ndiyo iliyotunza fedha zetu na ndiyo iliyopoteza fedha zetu. Sisi tulipwe fedha zetu ili tukamilishe miradi ya maendeleo, iliyokusudiwa kwa wananchi wa Jimbo la Kishapu.

Suala la kilimo, tunalo tatizo kubwa Kishapu. Nilimwomba Baba Mkwe wangu atume watendaji, kwa ajili kuifanya Kishapu iwe ni miongoni mwa Wilaya ambazo zitapata kilimo cha umwagiliaji kutokana na historia ya kutokuwa na Mvua nyingi.

Kwa kweli, ninaweza nikaongea kwa masikitiko kidogo. Tulikubaliana wafanye tathimini, watutengenezee michoro kwa sababu leo Mungu anafungua Koki zake, Maji yanamwagika, kesho Mungu akisema *stock* imeisha tutakimbilia wapi?

Mungu anatupa maji, yanamwagika, yanatiririka, yanapotea hatujali, kesho akitujaribu kwa kusema kwamba, niliwapa *stock* ya miaka mitano mbele, tutakimbilia wapi? Naomba sana, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, moja ya mikakati mikubwa itakayo mkomboa Mtanzania, ni kumsaidia kwa suala la kilimo. Asilimia themanini na nane *point* mbili (88.2%) ya wananchi wa Jimbo la Kishapu, wanategemea Kilimo na ufugaji. Kilimo na ufugaji vinategemea sana Maji. Mito ni Mingi, ardhi yetu ni kavu sana, kwa sababu ndivyo Mungu alivyotujalia, lakini tukihifadhi mabwawa, tungeyatumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA**: Ahsante sana, Mheshimiwa Rose Kamili Sakum, baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, halafu Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu ajiandaye.

**MHE. ROSE KAMILI SAKUM**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, lakini pia nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

**SPIKA**: Una dakika tano tu!

**MHE. ROSE KAMILI SAKUM**: Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la pato la taifa kukuwa kwa asilimia sita *point* tisa, (6.9%). Sekta zilizochangia ni Mawasiliano, Fedha, Viwanda, Ujenzi, Madini, Biashara na Utalii. Nasikitika sana kwa serikali hii kutokutambua Mifugo kwamba inachangia pia, asilimia kubwa kwa sababu hawaagizi minofu nje ya nchi. Hawaagizi samaki wala hawaagizi nyama ya Ng'ombe, wala hawaagizi nyama ya Nguruwe kwa wale wanaokula Nguruwe.

Mheshimiwa Spika, naomba serikali itambue hilo na ituambie kwamba kwa kutokuagiza nyama nje ya nchi. Je, hawa mifugo au hiyo minofu imechangia kiasi gani cha asilimia kwa kutumia fedha kutoka nje?

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia suala la kupanda kwa mbegu mbaya ambayo ni ya ubaguzi wa kikabila. Utakuta wafugaji au wakulima sasa hivi kwa maeneo mengine hufukuzwa. Mfano, Kiteto, Kilosa, Lindi, Kisarawe, Mbeya, Kilombero pamoja na Chunya. Hawa wananchi wanaohamia kule ni kama Watanzania wengine wanao hamia.

Kwa nini sasa ifikie mahali wanaanza kufukuzwa? Hasa wafugaji kulipishwa faini kubwa kama Chunya, Mfugaji mmoja analipa faini ya milioni 19, hivi kweli ni halali au ni matumizi mabovu ya madaraka ya watumishi wetu kule?

Mheshimiwa Spika, nakuomba Waziri Mkuu, angalia suala hilo kama linaanzia kwako kwamba, wafukuzwe! Kwa sababu utakuta Wakuu wa Mikoa ndiyo wanao waagiza kwamba waondoeni hawa wafugaji, sasa waende wapi wakati katika Hotuba yako hapa, hujaweka sehemu ya kuwetengea wafungaji, bali umeagiza Halmashauri watenge maeneo.

Sasa Halmashauri watatenga wapi na wakati hawana haya maeneo? Mimi niliuliza wakati uliopita, Bajeti iliyopita kwamba, hebu tusaidieni, kuna hekta zaidi ya milioni 60, hebu tuambieni Wafugaji watapewa eneo lipi ili wakakae kwa usalama na utulivu? Hapa umeweka kwenye Bajeti kwamba, watatengewa eneo la malisho. Watatengewa sehemu ipi wakati wanafukuzwa kila mahali. Sasa hivi Kilindi wameanza kuwafukuza, Kiteto wamewafukuza wakulima na wafugaji, wanabaki Makabila ya huko. Sasa tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, hili naomba liangaliwe sana na serikali kwa sababu tunasema migogoro ya Dini, tunasema migogoro sijui ya Kisiasa, lakini pia suala la ukabila limekwisha ingia hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la TAMISEMI. TAMISEMI ni Wizara ambayo, Wizara nyingine zote zimepitishwa TAMISEMI. Sasa kunatokea matatizo, kwa watendaji wetu kule Halmashauri, kutokusimamia vizuri mapato na matumizi, ambayo fedha zinatolewa na serikali kwa ajili ya miradi. Lakini hakuna wa kufuatilia kule chini masuala ya *value for money*. Sasa inabidi mfanye vizuri kwa mfano, Wizara ya Kilimo isimamie Kilimo, isimamie miradi yake yenyewe kutoka Wizarani, siyo kwamba inapitia tena kwenye TAMISEMI, Wabunge tukubaliane na hilo kwa sababu sasa limekuwa janga la Taifa.

Fedha zinapelekwa kwa mfano, bilioni 75 za *Voucher*, zinatumika vibaya. Mwenyekiti ni *DC* anayesimamia ni Mkurugenzi. Sasa nani anayewajibika kwenye hizo fedha? Mimi nashauri serikali, hakuna sababu ya kupeleka zile bilioni 75 kwa ajili ya pembejeo. Mimi naomba ziende kwenye umwagiliaji ili kila mtu aweze kumwagilia, kwa sababu suala la pembejeo, mwananchi mwenyewe au mkulima mwenyewe anaweza kununua hiyo Mbegu yake,wala hakuna sababu ya kuwapa burebure, kwa sababu matumizi yamekuwa mabaya sana.

Mheshimiwa Spika, suala la Utawala Bora, inaonekana kwamba sasa hivi wananchi wakitaka kufanya jambo lao katika vijiji, Mtendaji amekula hela na mwenyekiti au serikali yake. Wananchi wakitaka kumwondoa madarakani, Mwenyekiti au Mtendaji, serikali inaingilia kati kuwakamata wale ambao wanataka kumwondoa madarakani na wale wanaokula fedha za umma. Kwa kweli, suala la watumishi pia liangaliwe.

**SPIKA**: Dakika tano zimekwisha! Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert,

**MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nijikite kabisa kwenye suala la ajira. Pamoja na serikali kuwa inakamilisha *program* ya kitaifa ya kukuza ajira kwa vijana na vijana laki tatu na elfu moja, wataweza kuajiriwa na kujiajiri.

Pia ongezeko la asilimia sita nukta saba(6.7%) kwa mwaka 2011. Nilikuwa nataka kuomba kwa Waziri Mkuu, mwaka huu ambao unaisha 2012/2013 ajira zikoje? Nikifuatilia hotuba ya Rais ya mwaka 2006 alipokuwa anahitimisha kilele cha Mwenge Ruvuma. Alizungumza kwamba ni Vijana laki saba wanamaliza vyuo pamoja na Taasisi tofauti na vijana elfu thelathini mpaka elfu arobaini wanakuwa wananajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nauliza, hiyo ni mwaka 2006. Lakini sasa hivi idadi itakuwa imeongezeka. Sasa tunawafanya nini hawa vijana? Kwa sababu wamekuwa mitaani, wanamaliza Chuo, lakini kazi hawapati. Hawa vijana wanatia huruma sana, kwa sababu wengine wanaishi kwenye mageto, unaweza ukawakuta ukawauliza utaoa lini? Anajibu kwamba bado yupo yupo! Kwa sababu atamwoa mwanamke atampeleka wapi? Wanakaa kwenye Mageto. Hili suala kwa kweli ni la kuangalia, kwa sababu tunatengeneza vijana ambao, mwisho wa siku hatuwezi kujua athari na madhara ambayo yatakuja kwenye serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la upatikanaji wa maji Vijijini. Nashukuru Manispaa pale tunapata maji kutoka Ziwa Victoria, lakini kuna maeneo mengi sana ambayo ni makame. Visima vinachimbwa virefu lakini havitoi maji. Sasa mimi najiuliza hawa Wahandisi walioko kwenye Halmashauri wanafanya Kazi gani? Kwa sababu huwezi ukachimba sehemu, unahisi kuna maji? Au serikali haina ving'amuzi vya kugundua hapa kuna maji. Mimi kuna haja sasa, serikali ione kuwa, kuna umuhimu wa kuweka ving'amuzi vya kujua, ukienda kuchimba hapa unapata maji. Unatumia pesa nyingi sana kuchimba visima virefu lakini havitoi maji, hii inakuwa haitusaidii.

Mheshimiwa Spika, Suala la vyandarua. Nilikuwa naomba nilizungumzie kwa sababu ninaona katika maeneo ninayotoka. Hotuba ya mwaka jana ya Waziri Mkuu, alisisitiza sana wananchi kutumia vyandarua vinavyotolewa na serikali. Lakini hivi viyandarua havifai! Havifai kabisa, mimi ninahisi labda vinawafaa watani zangu watu wa Morogoro! Kwa sababu mtu kama mimi nikiiingia kwenye kile chandarua sifai! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuchukua labda vipimo kutoka kanda ya Ziwa mtakuwa mmetusaidia. Lakini hivi vyandarua havifai na wala havifai kwa matumizi. Ndiyo, maana watu wengi siku hizi wanatumia vyandarua hivi kufugia kuku. Hata wenye minara ya simu wanatumia kuzuia nyuki wasiingie, kwenye mitambo yao waliyo iweka juu.

Kwa kweli hili jambo ni la kusikitisha, kwani ni vyandarua ambavyo havina viwango.

Mheshimiwa Spika, pamoja na serikali kutoa madawa kwenye vituo vya Afya pamoja na serikali. Juzi nilikuwa katika hospitali ya Mkoa, nimeona Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga pamoja na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Shinyanga. Nashangaa Hospitali ya Kolandoto imeteuliwa kuwa Hospitali Teule, lakini sikuona kama imepata mgao, wala kupata ruzuku! Mimi nashindwa kuelewa, hivi hospitali mnapoziteuwa kuwa Hospitali Teule, halafu mnazitelekeza, sielewi maana yake nini! Kwa kweli zinatakiwa, kama ni ruzuku zipate na madawa zipate, kwa sababu mmeshaziteuwa kuwa hospitali Teule.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hili deni la *MSD* nilikuwa naomba lilipwe, kwa sababu linachochea dawa kutopatikana katika hospitali zetu za Manispaa.

**SPIKA**: Mheshimiwa Mbunge, naona umemaliza vizuri, ahsante sana, sasa nimwite Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, atafuatia na Mheshimiwa Deogratious Ntukumazina.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nimwombe kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye suala la madeni ya walimu. Ni busara kuangalia sasa madeni yote ya wafanyakazi wa nchi hii. Ni vyema wakati tukiwa tunazungumzia madeni ya walimu, tuangalie pia umuhimu madeni ya waaguzi, madaktari, wanajeshi, polisi na wafanyakazi wote wa nchi hii, tulipe mara moja tuondokane na matatizo ya madeni.

Mheshimiwa Spika, Sensa, inaonyesha Dar es salaam sasa tuko milioni nne. Mimi niwaombe Wabunge kwa heshima zote, hebu tuitazame Dar es salaam kwa jicho la huruma. Maana yake leo, Dar es salaam tunaongezeka tu. Kila mwananchi wa Wilaya tofauti anapenda kuja Dar es salam, na akija hataki kuondoka. Ni muhimu tukaangalia umuhimu wa kuiona Dar es salaam, suala la msongamano linatisha.

Mimi nitoe mfano tu, njia ambayo unapita wewe Mheshimiwa Spika na Mawaziri na Viongozi wengi. Ukitokea nyumbani kwako na Nyumbani kwa Mawaziri, ukifika *Osterbay Police*, kuvuka mjini ni masaa mawili na nusu. Kwa hiyo, tuone umuhimu wa kuiongezea uwezo Dar es salaam ili kuondoa msongamano.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuondoa msongamano Dar es salaam, kama reli ya kati hujaiimalisha, hujaipa pesa za kutosha. Itasaidia mizingo mingi mikubwa kusafiri kwa njia ya reli. Pia kuna geti namba 13 na 14 bila kuhakikisha mageti yale pale Bandarini yanajengwa vizuri ili mizigo iweze kuchukuliwa, bado msongamano utakuwa haujaondoka Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii, huwezi ukaacha ziendelee Wilaya tatu. Mimi niwaombe kabisa, aidha mwongeze Wilaya na Majimbo, si mbaya pia mkifanya Dar es salaam ikawa na mikoa mitatu, siyo mbaya. Dar es salaam, tunazo hospitali ya Temeke, zenye hadhi ya Mikoa na Rufaa, lakini cha kusikitisha hakuna dawa yoyote wanayopewa, hakuna vifaa vyovyote wanavyopata kutokana na heshima hiyo ya kupandishwa Daraja. Wanaambiwa bado watumie Bajeti za Manispaa.

Cha kusikitisha leo, kwangu Temeke, pesa za maendeleo, tulitarajia kupata kutoka Hazina bilioni sita *point* moja (6.1 bilioni) lakini hadi kufikia leo, tumepata bilioni moja *point* moja, sawaswa na asilimia kumi na nane. Tutaendesha kweli nchi namna hii!

Mheshimiwa Spika, suala la msongamano Gereza la Keko na naamini Magereza yote. Keko ilijengwa mwaka 1957, ilitakiwa iwe inachukua Mahabusu 350, lakini hivi leo ninavyoongea kuna Mahabusu karibu 950 mpaka 1000. Gereza toka lijengwe halijafanyiwa ukarabati sasa linavuja na lina nyufa. Lakini cha kusikitisha kuna Mahabusu mle ndani wana miaka saba, nitolee mfano mahabusu mmoja ana miaka mitatu, alishikwa na madawa ya kulevya Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, wakayatoa tumboni madawa hayo, lakini hadi leo tunaambiwa ushahidi haujakamilika.

Sasa akaniuliza Mheshimiwa Mbunge, wanachotaka ushahidi ni kuhakikisha hili tumbo ni la kwangu au siyo la kwangu. Mahabusu mwenyewe anaongea, dawa wametoa kwenye tumbo langu leo wanasema ushahidi haujakamilika, lakini yameuzwa, na ushahidi hakuna. Kwa hiyo, hebu tuangalie hawa wapelelezi wetu wanapeleleza nini? Mbona kesi zao wanazozitaka upelelezi unakwenda kwa haraka haraka? Mbona hizo ushahidi unapatikana?

Mheshimiwa Spika, liko suala la kusikitisha pale Dar es Salaam, linalohusu *UDA.* Linasikitisha sana kwa sababu sasa linahusisha Ofisi ya Waziri Mkuu na linahusisha Ofisi ya Wizara ya Fedha, kwamba zinahusika katika upendeleo huo. Yule mtu wa *UDA*, Mwekezaji, amewekeza kwa milioni 300, tena milioni 300 zimeingia kwa mtu, lakini leo hata sisi wenye mali pale *UDA* tunafukuzwa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba ile ripoti ya *CAG* isomwe hapa Bungeni, ripoti zote zinasomwa, ripoti ile ni kwa nini?

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuomba sana, Wabunge wa Dar es Salaam na Wananchi wa Dar es Salaam siyo vyema kusema lakini wako chini ya miguu yako, walikuwa wanapenda ile ripoti isomwe na suala la *UDA* lizungumzwe.

Tumekuwa na vikao vitatu, lakini kila kikao tukifikia suala la *UDA*, Kikao kinaahirishwa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba kabla ya Bunge halijaisha, tupate taarifa ya *UDA* tujue kulikoni! Wapo wanaohusika, wengine ni viongozi wa kisiasa nao tunataka wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa suala la *China, Tanzania Logistics* pale Shimo la Udongo, wananchi wamepokea vizuri, wanatarajia kulipwa kwa haraka ili mradi ule uanze. Lakini na wananchi wa Kurasini wanauliza, wao watalipwa lini na watu wa Dar es Salaam, watu wa Temeke ni wastaarabu, hawapendi fujo. Kwa hiyo, na wale tuwalipe ili waweze kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, sasa ni suala la wananchi kujiajiri pamoja na shughuli za Vikoba. Wananchi wengi sana wamepokea, lakini tatizo ni uwezo. Kwa hiyo, mimi niiombe Serikali, nimwombe Waziri Mkuu, nimwombe Mama Yangu Mheshimiwa Mary Nagu, vile vikundi ambavyo viko tayari, pale Temeke. Nina vikundi viko tayari na tumewachangishia karibu Shilingi milioni sabini (70,000,000/=) tutakwenda kuwakabidhi wakati wowote tukiwa na Kiongozi wa Serikali, tukiangalia havikopesheki, kikundi kina milioni karibu sabini benki, lakini kukopesheka mara mbili ni ngumu. Ndani ya Bunge tunaongea hivyo, viongozi wanasema hivyo, lakini utekelezaji ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la umeme. Dar es Salaam leo umeme umekuwa siyo wa uhakika kama ipasavyo. Leo pale Kata 14 wamekaa, wamekaa siku tano jana ndiyo wamepata umeme na hali hiyo iko Tambuka Reli, iko Chang'ombe, hali hiyo iko mpaka kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, sasa sijui kuna tatizo gani kwa Ndugu zetu wa *TANESCO.* Nakushukuru sana, narejea kwa Mzee Pinda na naunga mkono hoja hii, lakini naomba yote haya, hasa la *UDA* ulifanyie kazi. *(Makofi)*

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, mimi nianze kusema bayana kabisa suingi mkono hoja kwa asilimia 100 kwa sababu zifuatazo:-

Siungi mkono hoja kwa sababu kila anayeona atakuwa shahidi kwamba Serikali siyo sikivu kwa vitendo na Serikali yetu imekuwa na tabia ya kufunika kombe ili mwanaharamu apite. Siungi mkono hoja, kwa sababu Serikali yetu imevaa miwani ya mbao na imeziba masikio. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani hebu ondoeni maneno hayo ya miwani ya mbao. Nani anavaa miwani ya mbao? Hebu ondoa maneno hayo tafadhali.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, mimi miwani yangu niliyovaa ni miwani ya *tinted.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naomba uondoe maneno tusibishane, uondoe maneno ya miwani ya mbao, wewe sema unachotaka kusema, haya endelea.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imekuwa siyo serikali sikivu. Naondoa maneno ya miwani ya mbao. Inasikitisha sana kuona kwamba viongozi wetu wa Serikali yetu wamekuwa wakifanya mambo wanayotaka wao, wao viongozi, na hawafanyi mambo wanayotaka wananchi na mifano tunayo.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwepo humu ndani, siku ile wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anaapa, hapa ndani, aliapa siku ile kuilinda Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini badala yake kinachotokea sasa wamekuwa wakilindana wao Mawaziri na Katiba wameiweka pembeni. Tuna Mawaziri 60 hapa, ukitazama kwa harakaharaka, Mawaziri wanofanya kazi ipasavyo, inavyotakikana hawazidi kumi (10), na nina weza kuwataja kwa majina.

Mheshimiwa Spika, liko jambo kwamba Elimu yetu ni mbovu, elimu yetu imeshuka, ni kweli takwimu zinaonyesha kwamba shule za sekondari zimeongezeka toka 1700 mpaka 4000, ni kweli kwamba wanaofaulu wameongezeka toka laki nne mpaka milioni moja na nusu. Lakini mimi niseme ni afadhali ukawa na wanafunzi laki nne tu, ni afadhali ukawa na shule 1700 tu peke yake kuliko kufaulisha wanafunzi milioni moja na nusu ambao hawajui kusoma na kuandika. Tunawafaulisha, tunapeleka wanafunzi wanaokwenda kusoma kidato cha kwanza ambao hawajafaulu.

Ni afadhali kuwa na wanafunzi wachache wenye ubora kuliko kuwa na uwingi usiokuwa na ubora. Mimi nimewashangaa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakipiga kelele kwa nini matokeo mwaka huu yamekuwa mabovu kidato cha nne. Tulipaswa kupiga kelele mwaka jana na mwaka juzi, wakati wanafunzi wamefaulu 11,000, hawajui kusoma na kuhesabu, hawajui K3, yaani kuandika, kusoma na kuhesabu, tulipaswa kushangaa wakati ule. *(Makofi)*

Kama walioingia *Form One* wako vile watakaotoka *form four* watakuwaje? Takwimu zinaonyesha kwamba elimu inashuka, ni takwimu za Serikali, tunacho kitabu hapa na Tume zilikwishaundwa, Tume ya Mzee Francis Liboi, imetumia mamilioni ya fedha, 2010/2011. Badala ya watu kuwajibika, tunaunda Tume nyingine kufunika kombe ili mwanaharamu apite. (*Makofi*)

Sasa tunaweza tukasema huu ni upepo utapita, lakini Watanzania wanajua. Watanzania wanaona elimu ya msingi ni bure lakini siyo bure. Mara ya mwisho tumefuta ada ilikuwa shilingi 3000/= kwa mwaka, leo hii michango wanayochanga wazazi baada ya kufuta ada kima cha chini Wilayani kwangu Ludewa ni shilingi 6,000/= inakwenda mpaka shilingi 12,000/= . *(Makofi)*

Ni vyema basi tukarudisha ada ijulikane moja kwa moja kwamba sasa elimu ya Msingi siyo bure tena na wazazi watajiandaa. Huku tunawaambia wazazi kwamba elimu itakuwa ni bure, lakini huku tunatoza michango mingi kuliko ada. Elimu yetu siyo nzuri, nadhani na uwajibikaji haupo, tunaishia kuunda Tume, ukiona imeundwa Tume ujue mambo yameshakwisha, kwa sababu Tume nyingi zinaundwa na matokeo yake hatuayaoni.

Tume nyingi zinaundwa, zinawekwa kwenye Makabrasha. Tume nyingi ziundwa zikisema huu ni upepo na itapita. Mimi niseme bayana, tufike mahala, Waheshimiwa Wabunge wenzangu sisi viongozi, hasa sisi wa Chama Tawala tubadilike, tuache kubeza kila hoja ya Upinzani! (*Makofi*)

Tusiwabeze, badala yake tuchukue hoja zao tuzipime na tuzifanyie kazi. Kuna msemo unaosema kwamba ukiona Kobe yuko juu ya mti ujue amebebwa na kuwekwa pale. Sisi tumepewa dhamana na Watanzania, Watanzania wametupa heshima ya kuwaongoza na kuwatumikia, dhamana hiyo waliyotupa wenzetu tusii-*abuse*. Tumepewa dhamana ya ku-*deliver*, badala ya ku-*deliver* tunatumia muda mwingi kufanya kazi za kuwabeza wenzetu ambao ni wachache. ( *Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi ambao ni wazazi kimsingi, tukitimiza wajibu, hawa watakuwa siyo wapinzani, watarudi, kipimo chetu kiwe ni utendaji kazi na siyo kulumbana bila hoja za msingi. Tunakuja humu Bungeni tunafanya kazi za Nape Nauye, Nape Nauye atafanya kazi gani sisi tukifanya kazi zake? (*Makofi*)

Ndiyo maana ninasema kuna matusi, watu wameacha kufanya kazi zao wanafanya kazi za watu wengine! Tuna mifano ya wazi kabisa, kwamba tuki-*deliver* wapinzani wanaelewa na tuna Mawaziri hapa walikuwa upinzani, wameelewa kwamba tunafanya vizuri, wamerudi CCM, wameacha kuwa wapinzani.

Kwa hiyo, hoja yangu mimi ni kwamba sisi tusiwabeze wapinzani, tubadilike, sisi tukiwapenda na kuwaheshimu wao, wataacha kutudharau, wataacha kututukana kila siku. Nchi hii ni nchi yetu sote, wananchi watatupima kwa utendaji wetu na kwa ku-*deliver*.

Mimi jimboni kwangu Ludewa, wananchi wangu wanataka vitu vichache tu, wanataka vitu vidogo tu. Meli ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila mwaka inasomwa, kinachofanyika hakieleweki. *MV. Songea, MV Iringa* mbovu hazifanyi kazi, Meli mpya, hakuna kinachoendelea kule chini na niseme bayana kama hatupati Meli kwa ajili ya wananchi wa Ziwa Nyasa kule, na sisi, tutakwenda kuandamana. Tutakusanya Sare zetu za Chama cha Mapinduzi (CCM), tutavaa *shirts* zetu za kijani na suruali zetu nyeusi, tutakwenda kuandamana barabarani, bila kujali ni Juma tatu, ni Ijumaa au ni Jumapili, ni lazima tuwe na barabara ya lami kutoka Njombe mpaka Ludewa.

Mkoa mzima, Iringa na Njombe, Wilaya zote zina barabara za lami kasoro Wilaya ya Ludewa tu, wananchi wamefanya nini hawa? Wananchi kule Ziwa Nyasa wanafika mahali wanauliza Joyce Banda atatuchukua lini tuwe sehemu yake, maana yake tunaona ninyi wenzetu mmetutelekeza! Tumewaacha.

Wananchi wa Ludewa, wanataka Chuo cha *VETA*, hawataki vitu vingi wanataka vitu vichachetu. Badala ya kuwapa tunawapiga blaablaa, tunawapa maneno ya bure, ukimwuliza swali Waziri hapa atakujibu natoa wito, mchakato, tumejipanga vizuri, atasema wadau, upembuzi yakinifu na kadhalika.

Mimi niseme tumechoshwa na hii staili ya uongozi, tunataka utendaji, tunataka uwajibikaji na nia yetu ni njema. Nchi hii ni lazima wananchi wa Tanzania na wananchi wa Ludewa wajisikie pia kuwa wao ni sehemu ya Watanzania, ni lazima wananchi wa Ludewa wajisikie pia wao wananufaika pia na matunda ya Uhuru kama wanavyofaidika maeneo mengine ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba suingi mkono hoja, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa mpaka hayo niliyoyasema yatakapotekelezwa na nafuta kauli yangu ya miwani ya mbao kama ulivyonitaka, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kabla ya kuchangia ningeomba kusema maneno kidogo.

Mheshimiwa Spika, siku zote Serikali ilikuwa inatafuta, inahangaika sana inapata taabu kutafuta ni nani wanaochochea udini katika nchi hii. Lakini jana kwa sababu Mwenyezi Mungu hafichi wale walio na maovu, ilidhilirika na akatuonyesha ni nani wanaochochea udini katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishuhudia na Watanzania wote waliona ni nani wanaoleta udini na kutaka kuitafutia maangamizi nchi hii. *Quran* na Biblia inaingia katika jengo hili Takatifu siku ya kuwaapisha Wabunge tu, badala ya hapo inakuwa hakuna tena anayeingia nayo. Kwa sababu Rais wetu katika hotuba yake ya mwisho wa mwezi alitutahadharisha sana na jambo hili la udini na Mtanzania yeyote ambaye alikuwa na akili yake timamu aliyesikiliza hotuba ile, basi alikuwa na tahadhari kubwa na alijua kuwa tukiifanyia kazi, tutaepukana na matatizo haya ya kuingiza udini Bungeni, sisi mambo ambayo yatatufikisha pabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini leo Mbunge anathubutu kuingia na Biblia humu, kwa kuja kuikashifu Serikali pamoja na kutukashifu sisi wanawake. Nawaomba Waheshimiwa wanawake wenzangu ambao ni Wabunge, jambo hili tulikemee.

Mheshimiwa Spika, nadhani wewe upo karibu miaka 30 inakaribia katika Bunge hili, ulishawahi kuona Mbunge akiingia humu na Biblia au hii ndiyo mara ya mwanzo kwa ajili ya kutukashifu tu na kuikashifu dini?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nataka niende kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi, nichangie hoja. Tume ya Taifa ya Uchaguzi jengo lake liko katika yaani ofisi ya Tume ya Uchaguzi iko katika jengo ambalo limepangishwa. Tume hii inaigharimu Serikali kutumia karibu milioni 234,387,648/= kwa mwaka, ambapo kwa miaka 10 Tume inatumia shilingi za Kitanzania bilioni 2,343,876,680/=.

Mheshimiwa Spika, tunaifanya Serikali iingie katika hasara kubwa. Mimi naishauri Serikali iachane na tabia hii ya kupangisha majengo kwa ajili ya ofisi za Serikali. (*Makofi*)

Serikali yetu bado inakubalika, inaaminika na inakopesheka, naishauri Serikali ijenge ofisi zake yenyewe, kwa sababu tatizo hili haliko katika ofisi ya Tume ya Uchaguzi tu. Ofisi nyingi za Serikali ziko katika majengo ya kupanga ambayo Serikali inaingia hasara kubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iachane na mambo haya ya kupangisha katika majengo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka sasa niende kwenye hii hii Tume ya Uchaguzi. Tume ya Taifa iwe na daftari lake Zanzibar! Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kutumia *ZEC* kuwa Wakala wake kule, basi inakuwa Watanzania wengine wanakosa haki yao!

Daftari la *ZEC* lina mapungufu mengi, kwa mfano mimi hapa ni Mbunge, ni Mzanzibari, ni Mtanzania, lakini Mama yangu au Baba yangu hayumo katika Daftari la *ZEC*, kwa sababu tu hana Kitabulisho cha Uzanzibari, na Kitabulisho cha Uzanzibari huwezi kukipata mpaka uwe na Cheti cha kuzaliwa, wazee wengi waliozaliwa kwenye miaka ya 70, hawana vyeti vya kuzaliwa!

Kwa sasa naomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi isitumie *ZEC* kuwa ni Wakala wake, kwa sababu sisi Wabunge tuliomo humu Tumechaguliwa na Sheria mbili tofauti, kuna Wabunge wa Zanzibar ambao walitumia Daftari la *ZEC* wamechaguliwa na Sheria nyingine na hao ambao wako Bara walichaguliwa na Tume ya *NEC*, wao wamechaguliwa pia kwa sheria nyingine.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali kutumike daftari la *NEC* kule Zanzibar kwa sababu tuko katika mchakato wa Katiba, ili Watanzania wote waweze kupata haki yao katika kutoa maoni yao kwenye Katiba hii mpya.

Baada ya kusema hayo, nataka sasa niende kwenye kero ambayo ni sugu kwa Wazanzibari. Kero ya Wafanya biashara ya Zanzibar kulipishwa kodi mara mbili hili ni kero sugu na tusitafute nani huyu?

Kero hii tunaizungumza siku zote, katika mwaka ulipita tuliizungumza na tukasema kuwa imepatiwa ufumbuzi, kuwa bidhaa yeyote inayoingizwa nchini kupitia kituo chochote cha Forodha kilichomo ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Basi haitalipishwa tena kodi mara mbili! Lakini namwomba Waziri Mkuu atupe ufafanuzi ni adhabu gani za kisheria na kinidhamu zilizochuliwa kwa Maafisa na Watendaji wa Serikali, wote walioshindwa kutekeleza agizo hili la kisheria, haiwezekani kuwa Serikali iko *serious* katika hili na watendaji wa Serikali na Maafisa wa Forodha wakalipisha kodi mara mbili, lakini hii yote ni ya kuwa ni maneno yanayofanywa lakini utekelezaji ni kuwa labda wanaambiwa wasitekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna anayekataa Muungano, hakuna anayekataa umoja, lakini kero hii imekuwa sugu na inaudhi na inaumiza pia. Naomba Serikali itupe ufafanuzi dhidi ya hili.

Baada ya kusema hayo, mimi sasa nataka nijielekeze kwenye hili tatizo au kadhia iliyolikumba nchi yetu katika wiki mbili zilizopita.

Mheshimiwa Spika, sitaki nizungumze jambo ambalo lipo Mahakamani, lakini nataka niulize; kuna jengo lilianguka Chang'ombe kama miaka kumi, wahusika waliosababisha jambo lile nataka nijue wamehukumiwa vipi ili tujue ile hukumu waliyopewa ni ipi? Kuna jengo lilianguka Kisutu likaua Watanzania, tunataka tujue wenye jengo lililosababisha mauaji ya Watanzania wale hukumu yao ni ipi? *(Makofi)*

Hukumu hizi kama zingekuwa wazi ingekuwa pengine ni funzo kwa hili lililotokea juzi. Nataka pia niiambie Serikali kuwa, *NHC* hata wakiruka Kimasai ni wahusika wa hili. Haiwezekani hata siku moja kuwa wao wana ubia na wao ndiyo waliotoa kiwanja cha kujengwa jengo lile. Jengo lijengwe mpaka lifikie ghorofa 16 wakati makubaliano ni ghorofa kumi wao wasijue; haiwezekani! Haiwezekani hata siku moja, wala wasitudanganye, ni wahusika wakuu na wawajibike wote waliosababisha maafa yale. Naomba Serikali aliyehusika hata kwa *fullstop* kwenye matatizo yale basi tuhakikishe naye anawajibishwa. Iweje Waswahili wanasema mjenzi na mjengewa iwe wao hawakuweka *Engineer* wao wa kukagua jengo lile ambalo na wao pia kuna *share* yao pale; haiwezekani hata siku moja! Nasema wale wote waliohusika na wao wawajibishwe na waingie kwenye mkumbo huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nigusie kidogo tu kuhusu TAKUKURU. Ikiwa kweli Serikali iko *serious* kupambana na rushwa katika nchi hii, basi TAKUKURU wapewe meno, haiwezekani mtu asiye na meno akaambiwa atafune andazi hata siku moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Idd Azzan.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa. Nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kabla ya yote, napenda kuunga mkono kwa asilimia mia moja Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu amegusa maeneo yote ambayo ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, huwa nasema nchi yoyote Duniani ili ipate maendeleo, lazima ijikite kwenye elimu. Sasa tuna tatizo kubwa kuona kwamba kiwango cha elimu cha nchi yetu ya Tanzania kinashuka chini na hii itasababisha nchi yetu ianze kurudi nyuma. Matokeo ya mwaka jana wanafunzi asilimia 60 kufeli mtihani kweli hii ni hatari. Sasa nasikitika kidogo kuona kwenye masuala ya elimu wanaonekana wanasiasa ndiyo wataalamu, ndiyo wanaochanganua mambo kumbe elimu ina mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kwa Serikali kwamba, Maprofesa ambao tunao kwenye Vyuo Vikuu na wasomi ambao tunao kwenye nchi yetu, tuwape nafasi ili waweze kujadili vizuri masuala ya elimu. Utakuta hata kwenye Vyuo Vikuu watu wanapenda kujadili siasa, sasa hivi hata Maprofesa wote wanataka kukimbilia kwenye siasa, Madaktari wote wanataka kukimbilia kwenye siasa. Sasa mimi najiuliza; hii nchi yetu inakwenda wapi na elimu inashuka chini?

Natoa wito kwamba, hawa wasomi tuwape nafasi waweze kujadili vizuri na kuunda *structure* nzuri ya elimu yetu tuweze kupanda *chart*. Sasa hivi tunakoelekea siyo kuzuri sana na baadaye tutakuja kupata wanasiasa ambao hawajasoma, matokeo yake tutaanza kugongana sisi wenyewe. Kwa sababu kama mtu hujapata elimu vizuri huwezi kuongoza vizuri hata masuala ya utawala, ni lazima

upate elimu nzuri. Sasa, naiomba sana Serikali kwamba, wasomi wetu tuwaheshimu, tuwape nafasi ili waweze kujadili vizuri masuala ya elimu nchi yetu iweze kusonga mbele.

Suala la pili ni kwamba, Wabunge wengi sana wanachangia kuhusu suala la maji. Tatizo la maji ni kubwa sana na ukiangalia kila Jimbo na kila Wilaya kuna tatizo kubwa la maji. Naiomba Serikali kwamba, kipaumbele tutenge fedha nyingi sana kwenye Wizara ya Maji. Wizara ya Maji kama haitapewa fedha nyingi, hili tatizo la maji tutakuwa tunaongea kila mwaka. Mbunge yeyote akienda kwenye Jimbo lake, Wananchi swali la kwanza la kuuliza ni maji. Hata kwenye Jimbo langu, Serikali kwa kushirikiana na Wananchi iliweza kujenga matanki ya maji karibu 12, lakini mpaka leo hayatoi maji. Ukienda Sawara kuna tanki la maji, ukienda Kibao kuna tenki la maji, ukienda Nyororo pia kuna tanki la maji, ukienda Igowole kuna tanki la maji, ukienda Maduma kuna tanki la maji na pia ukienda Nyigo kuna tanki la maji na yote hayatoi maji. Ukiangalia katika Wilaya ya Mufindi kuna mito mingi sana na Serikali ilijitahidi kwa kushirikiana na Wananchi, ikaweza kupeleka maji kwenye matanki hayo, lakini ni ya miaka ya 1970, mpaka hivi sasa hakuna wataalamu ambao wanaweza wakatengeneza miundombinu ikafanya kazi Wananchi wakapata maji. Sasa nataka niiombe Serikali kwamba, Wizara ya Maji lazima itengewe bajeti ya kutosha ili waweze kufufua miundombinu iliyoharibika. *(Makofi)*

Suala lingine ambalo naliona kwenye Wizara ya Maji ni kwamba, bado kuna tatizo kubwa, naomba Wizara ya Maji iiangalie Wizara ya Ujenzi inavyofanya kazi vizuri. Kwa mfano, unaweza ukaona katika Mikoa sasa hakuna Bodi ya Maji. Utakuta katika Mikoa yote hakuna Bodi ya Maji. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwe na Bodi ya Maji kila Mkoa ili matatizo ya maji yatatuliwe katika Mikoa. Sasa hivi unaweza ukaona una mlolongo mrefu sana, suala dogo tu la kununua *spare* wanasema u-*apply* Wizarani, kumbe ungekwenda kuomba tu Wilayani au katika Mkoa ukapewa vifaa vya maji, hivi sasa miundombinu ya maji imeharibika kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitizie masuala ya maji; ni aibu sana kwa kila Mbunge kila siku tunaongelea masuala ya maji. Sisi Wabunge tunajitahidi sana kuomba hata wafadhili watuchimbie visima kule kwenye Majimbo yetu, lakini Serikali bado haijapeleka fedha za kutosha kwenye Majimbo yetu. Unaweza ukaona mwaka mzima unapita lakini Serikali haijaleta fedha ambayo itaweza kusaidia maji. Sisi Wabunge tumeomba mpaka tumechanganyikiwa kwa sababu kila nchi tunapeleka *proposal* tunaomba maji; tunaiomba Serikali itusaidie.

Nimetoa mfano mdogo sana, nimesema maji yapo, hatuwezi kusema hayapo, Mungu ameshatupatia maji na hakuna nchi yoyote yenye maji mengi kama nchi yetu ya Tanzania. Sasa ni aibu kubwa kuona Wananchi wanakosa maji. Naomba Serikali iweke kipaumbele kwenye suala la maji.

Suala la pili ambalo napenda niliongelee na wenzangu wameliongelea ni la barabara. Barabara ni muhimu. Kwanza, naipongeza Serikali kuna barabara imejengwa kwa kiwango kizuri cha lami kutoka Iringa mpaka Mafinga, ni kizuri! Mkandarasi naomba ajenge hata sehemu nyingine kwani ni mzuri, hata ukienda kukagua ile barabara imekaa vizuri. Sasa naomba kwa Serikali, kuna mpango ambao nilileta swali hapa bahati nzuri Wizara ya Ujenzi ilishakubali kujenga barabara ya kutoka Nyororo - Igowole mpaka Mgololo kwa kiwango cha lami. Sasa naomba Serikali hebu imwangalie yule Mkandarasi ajenge ile barabara ikae vizuri ili Wananchi wangu waweze kusherehekea na ile barabara. Yule Mkandarasi ni mzuri sana, bahati nzuri Serikali ilishakubali na ninategemea kwenye bajeti inayokuja, Barabara ya Nyororo mpaka Mgololo kwa kiwango cha lami itakuwa imeshakuwa *budgeted*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu barabara inayotoka Mafinga mpaka Mgololo, ile barabara mpaka hivi sasa haipitiki. Yule Mkandarasi anayeweka vifusi kila mwaka na hata mwaka jana nilizungumza, nikasema barabara za kwetu sisi kuna mvua nyingi sana kule huwezi kuweka udongo

wa tope weka kokoto. Sasa nawaomba watu wa *TANROADS,* masuala ya kuweka udongo wa mfinyanzi ambao unasababisha magari kukwama yaishie leo. Serikali inatenga fedha kwa ajili ya barabara, sasa baada ya kwenda kuchukua kokoto ambazo zinafaa kwenye barabara unakwenda kuchukua kifusi. Haya ni matumizi mabaya ya fedha, tunaanza kuilamu Serikali wakati ukiangalia kwenye bajeti tayari imeshatenga fedha lakini watendaji wanatuangusha. Naomba watu wa *TANROADS*, mwaka huu tukiona mnaendelea kuweka ule udongo ambao unasababisha matatizo na ninyi mnajua kabisa kule kuna mvua mvua tutawazuia. Afadhali fedha ibaki isitumike kuliko kutumia vibaya wakati Serikali inajitahidi kila siku inatafuta fedha halafu mnakwamisha mnaweka udongo ambao haufai. Hii itakuwa ni aibu, Watendaji wanatuaibisha sana na baadaye tutaanza kuilamu Serikali hapa, kumbe Serikali tumeshatenga bajeti, Wabunge tunatenga bajeti, lakini watendaji wanatuletea kitu ambacho sicho. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu umeme na bahati nzuri Waziri wangu alijibu vizuri sana swali nililouliza wiki iliyopita kwamba, Malangali watapewa umeme. Sipendi niongelee sana, lakini naomba utekelezaji kwa sababu sisi kule kwetu hata nguzo zipo halafu umeme kutoka Makambako mpaka Malangali nadhani ni kilomita 20 tu. Ninaomba hilo ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Iddi Azzan, atafuatiwa na Mheshimiwa Salvatory na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie. Nianze tu kwa kuungana na Wabunge wenzangu wa Dar es Salaam, ambao walikuwa wanaomba tuangaliwe jinsi ya kuongeza Wilaya nyingine ama kuanzisha Mkoa mwingine pale Dar es Salaam kwa sababu tumeelemewa, idadi ya watu ni kubwa, lakini na maeneo yamezidi kupanuka. Ukimwangalia Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Mecky Sadick, hivi sasa amezeeka siku si zake ni kwa sababu ya mzigo mkubwa alioubeba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nizungumzie suala la mapato ya Halmashauri. Tulikubaliana na Serikali ilikubali na ikaruhusu kwamba, Halmashauri sasa ziwe zinakusanya kodi ya leseni ama ada ya leseni na zilijipanga vizuri kwa ajili ya kukusanya ada hiyo, ikaweka mipango mizuri pamoja na Miradi mingi ya maendeleo iliyowekwa kwa ajili ya makusanyo ya ada ya leseni. Cha kushangaza, mpaka leo hii Halmashauri zimeshindwa kukusanya ada ya leseni, kwa sababu ya taratibu ambazo Serikali haijazikamilisha ili Halmashauri ziweze kukusanya ada hiyo. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iweze kukamilisha taratibu hizo ili Halmashauri zote nchini ziweze kukusanya ada ya leseni kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi wetu. *(Makofi)*

Jambo lingine ni kodi ya majengo kwa Mkoa wa Dar es Salaam, ilitolewa miaka mitano ya majaribio na nafikiri inaisha mwezi Julai, 2013. Ni kweli kazi nzuri imefanywa na *TRA,* lakini bado tunashauri na tunaitaka sasa Serikali irudishe utaratibu uliokuwepo zamani wa Halmashauri kuweza kukusanya zenyewe kodi ya majengo, kwa sababu tumeona faida tuliyokuwa tunaipata na hasara ambayo tumeipata baada ya *TRA* kuanza kukusanya kodi hii. Naomba *TRA* waendelee na kazi zao nyingine za kukusanya mapato mengine, lakini hili la kodi ya majengo ni vyema sasa Serikali ikaanza utaratibu kabla ya mwezi wa saba ili Halmashauri zetu ziweze kuruhusiwa kukusanya kodi ya majengo ili tuweze kupata mapato ya kutosha kwa ajili ya Miradi yetu ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wenzangu waliotangulia walizungumzia suala la hospitali zetu ambazo zilipandishwa hadhi na mimi nasisitiza kwamba, hospitali zimepandishwa hadhi kuwa za rufaa na za mikoa lakini hadi leo hazijapata ikama, Madaktari na Madaktari Bingwa hakuna, madawa hakuna ni yaleyale ya enzi ya Wilaya, kwa hiyo, Wananchi wanapata tabu sana. Kwa mfano, Hospitali ya Mwananyamala ukiangalia kwa siku watoto wanaozaliwa ni kati ya 65 - 80 lakini vitanda vilivyopo ni 18 tu. Kwa hiyo, bado tuna matatizo makubwa. Tunaomba tupate bajeti hiyo ili tuweze kufanya hospitali zetu hizi zitoe huduma zinazotakiwa kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lilizungumziwa suala la usalama na ikatolewa na idadi ya ujambazi ambao umetokea au uhalifu ambao umejitokeza. Niseme kwamba, uhalifu ambao tumeuona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sawa ndiyo huo, lakini tufahamu kwamba, huo ni uhalifu ambao umeripotiwa Polisi, lakini yapo matukio mengi sana ya uhalifu yanayofanyika na Wananchi wanashindwa hata kwenda kuripoti Polisi kwa sababu hata ukiripoti ni kazi bure tu.

Ujambazi umekuwa wa kutisha sana katika Jiji la Dar es Salaam na bahati mbaya sana wapo vijana ambao wamejiajiri kwa kutumia bodaboda na wanafanya vizuri kwa maana ya kupata kipato, lakini wapo ambao wanazitumia bodaboda hizo vibaya. Upo ujambazi ambao unaendelea kwa kutumia pikipiki za bodaboda, wanapora, wanaua na wanakimbia, hakuna hatua zozote ambazo zinachukuliwa. Baya zaidi, tunazo silaha nyingi sana mtaani pamoja na kwamba kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba, tumedhibiti uingiaji wa silaha holela kwenye mipaka yetu lakini zipo silaha ambazo ziliingia tangu ya miaka 1993 - 1994 wakati wa vita au wakati wa machafuko ya Rwanda na Burundi, silaha zile zipo nyingi sana mtaani. Siyo ajabu mtu akakutolea bastola ukiwa baa au barabarani anakupora simu. Kwa hiyo, tunazo silaha nyingi ambazo zinafanya ujambazi mitaani na kwa kweli kwa hali ambayo ipo hivi sasa na wingi wa watu wa Dar es Salaam, Jeshi la

Polisi limeshindwa kudhibiti hali hiyo kwa sababu limezidiwa, Askari ni wachache, Wananchi tumekuwa wengi na uhalifu umezidi kupita kiasi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 niliwahi kuomba kwamba, tuangalie sasa uwezekano kama nilivyoomba wakati ule nikichangia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani mwaka 2006 kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kuwatumia Askari wetu ama wa Jeshi la Wananchi au Jeshi la Kujenga Taifa washirikiane na Polisi, kufanywe operesheni maalum ya kuwasaka majambazi na kusaka silaha ambazo zipo mitaani.

Mheshimiwa Spika, hatutakuwa tumefanya dhambi na hiyo itatufanya tumuenzi vizuri aliyekuwa Waziri Mkuu wetu, Marehemu Edward Moringe Sokoine. Kama tunakumbuka, miaka ya 1980 wakati anapambana na wahujumu uchumi, ilifikia wakati mtu anachukua hela zake ndani anakwenda kuzitupa kwa sababu hakuzipata kihalali anaogopa kukamatwa, ilifika wakati watu walitoa vitu vyao kama *TV* ambazo wakati huo zilikuwa haziruhusiwi wanakwenda kuzitupa na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Polisi walifanya kazi nzuri sana kudhibiti hali hiyo. Kwa hiyo, haitakuwa ajabu hivi sasa tukatumia Jeshi la Kujenga Taifa kupambana na uhalifu ambao umekithiri katika nchi yetu hivi sasa na hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Naomba Serikali iliangalie sana jambo hili na ikiwezekana tuone tunasaidia vipi ili kupambana na uhalifu. Hali ni mbaya sana katika Jiji la Dar es Salaam kwani uhalifu unatisha sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kulipongeza Bunge pamoja na Serikali kwa kurudisha sheria ambayo inawataka wanafunzi wanapomaliza au wanapohitimu Kidato cha Sita waende kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Ni jambo zuri na hilo limefanyika na kuanza kutekelezwa mwaka huu na katika kuliunga mkono jambo hilo nami pia nilijiunga na JKT na nimepata mafunzo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachoomba sasa ni kuhakikisha kwamba, Polisi ambao wanaajiriwa ama Askari Magereza,

badala ya kuwatoa mitaani ni vyema waangaliwe wale ambao wamepitia Mafunzo ya JKT ili waweze kupata ajira hiyo, kwa sababu wapo vijana wengi JKT ambao wanapata mafunzo lakini mwisho wa siku wanashindwa kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu jambo ambalo limejitokeza humu Bungeni na umelikemea leo; nashawishika sasa kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuitengeneza tena vizuri sheria hii, badala ya kuwataka wanafunzi waende JKT, sasa tuwatake hata wale wanaotaka Ubunge, kabla ya kupata Ubunge nao waende JKT. Wawe wamepitia JKT ndiyo waje wagombee Ubunge ili wapate uzalendo, nidhamu, tusije tukapata Wabunge ambao wanakuja kusema ama kuropoka maneno ambayo hayastahili kuropokwa humu Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu sasa kwa kuiomba Serikali, hii ni *quarter* ama ni robo ya nne ya mwaka wa fedha wa 2012/2013, lakini mpaka hivi sasa Halmashauri yangu ya Kinondoni fedha ambayo tumepokea haizidi 60%, kwa hiyo, tunaomba pesa hizi ambazo hazijaletwa ziletwe tuweze kukamilisha Miradi yetu ya Maendeleo.

Tunaomba kuondoa msongamano Dar es Salaam, fedha za Mfuko wa Barabara ziandaliwe ili Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam hususan Halmashauri ya Kinondoni, iweze kupata fedha za kutosha kutoka Mfuko wa Barabara tuweze kukabiliana na hali ya msongamano ambao umekithiri na unatisha sana.

Naomba pia barabara ambayo iliahidiwa, yaani Barabara ya Kigogo Dampo kwenda Mandela Road nayo kwenye mwaka huu wa fedha iangaliwe ijengwe ili tuweze kuondoa msongamano.

Lakini pia tuangalie barabara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Azzan.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante na sasa nitamwita Mheshimiwa Salvatory Machemli, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, kwa dakika tano.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii.

Muda mfupi sana tangu matokeo ya Kidato cha Nne yatoke na nchi yetu bado inaomboleza msiba mkubwa wa kufeli kwa wanafunzi hao. Tumepiga kelele sana hasa Kambi ya Upinzani, tukimtaka Waziri wa Elimu pamoja na Wasaidizi wake wote wawajibike; tulichokiambulia ni kubezwa. Dawa halisi iliyopo ni kukaa chini tuangalie upya ni wapi tumejikwaa na tusiangalie tulipoangukia.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mitaala inayotumika kufundisha katika shule zetu imepitwa na wakati haipo kabisa. Mheshimiwa James Mbatia, alikuja hapa na hoja kwamba, Serikali haina mitaala tukaibeza, tukamwona hafai.

Mheshimiwa Spika, leo mtoto wa darasa la kwanza anasoma masomo manane mpaka tisa. Kwa kichwa kidogo alichonacho ni kum-*overwork*. Sisi wakati tunaanza shule wote ni mashahidi, tulikuwa tunasoma masomo matatu; maarufu kama KKK, Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Hakuna mtoto au kijana anayezaliwa halafu akatembea muda huo huo, tulitakiwa tuwaweke katika mazingira ya kuwaandaa kubeba mzigo wa elimu wanaokuja kuubeba juu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni vitabu vinavyotumika kufundishia mashuleni; sasa hivi ukienda kwenye shule zetu kuanzia shule za msingi mpaka za sekondari, kila shule ina kitabu chake. Ukienda Shule ya Msingi Nansio utakuta wanasoma Kitabu cha Nyangwine, ukienda Shule ya Msingi ya Nyarwengo ambayo ipo kwenye Wilaya

ile ile wanasoma Kitabu cha Mutamwega darasa lile lile. Halafu wanaotunga mtihani hawajali kwamba hawa wamesoma Kitabu cha Nyangwine na hawa wamesoma Kitabu cha Mutamwega. Ndiyo maana wanafunzi wanapigwa chenga na tunaanza kuwatupia lawama, tunawaingiza kwenye matatizo na kuwaleta uraiani wanakaa bila kazi. Hili ni janga.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi; nimemsikia rafiki yangu Mheshimiwa Idd Azzan pale anakisema kwamba, tuandae Wabunge kabla hawajaenda kugombea, waende kwanza JKT wakanolewe. Hii siyo dawa, kuna wengine wamekwenda JKT, mwenzangu Mheshimiwa Livingstone Lusinde, ameenda lakini alipotoka hakujifunza uzalendo amekuja kutapika matusi humu ndani. Kwa hiyo, kwenda Jeshini siyo kujifunza uzalendo. (*Kicheko/Makofi*)

Bado nipo na Jeshi la Polisi; Jeshi la Polisi linacheza siasa. Naomba kupitia ngoma hii sisi tucheze na wanasiasa wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kumekuwa na kesi nyingi za kubambikizwa, nimemsikia Mbunge mmoja akilalamika hapa ndani kwamba kesi inayowahusu upelelezi unafanyika haraka, kesi isiyowahusu upelelezi bado haujakamilika. Tuwaombe Jeshi la Polisi waachane na siasa, wanalipa kodi kwa fedha zetu sisi za walipa kodi wanazolipwa mishahara wasiwe na upendeleo. Kesho sisi tutakuwa watawala watafuata matakwa ya nani?

Mheshimiwa Spika, jiografia ya Kisiwa changu cha Ukerewe kimezungukwa na maji. Jeshi la Polisi linashindwa kudhibiti majambazi, matokeo yake linawatetea majambazi. Kuna tukio juzi limetokea, watu wawili wafanyabiashara wa samaki wameuawa katika Kisiwa cha Kyara. Wananchi kwa uzalendo wakapeleka majina Polisi, wale watu wakafikishwa kituoni, baada ya siku nane wakaondoka wapo uraiani wanatishia kwamba wao wapo juu ya sheria. Wauza madawa na wengine wanakamatwa siku mbili wanaachiwa

kwa sababu wana maslahi ya Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, Jeshi litende haki, kimsingi, lisiwe na upendeleo.

Mheshimiwa Spika, usafiri katika Ziwa Victoria ...

*(Hapa Kengele ililia kuashiri kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante nashukuru. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niende moja kwa moja ukurasa wa 31 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, ambapo anaongelea kuhusu kuimarisha mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Sasa hivi Serikali inafanya maongezi na Benki ya Rasilimali ya *TIB* ili Halmashauri ziweze kukopa waweze kufanya shughuli zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba TAMISEMI waweke mwongozo mzuri ili hizi Halmashauri zitakapokopa zihusishe Madiwani wote, zifuate taratibu zinazohusika ili mikopo hiyo isiwe ya siri hatimaye kuleta malalamiko.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna mgogoro mkubwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, ambao umesababishwa na mambo kama hayo. Mahali ambapo Kamati ya Fedha kwa kushirikiana na Meya inakopa fedha ambazo Madiwani wengine hawajui kinachoendelea na hatimaye kuiweka Halmashauri kuwa katika madeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaishauri TAMISEMI isaidie; kukopa ni vizuri , Halmashauri ziweze kujiendesha lakini uwepo utaratibu ambao utakuwa wazi, utakaowashirikisha Madiwani katika hatua zote, yaani kuanzia maandiko na mambo mengine ili kusiwepo na mizozo kama inayotokea katika Halmashauri yetu ya Manispaa ya Bukoba.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niongelee gharama ya makisio ya uendeshaji wa Miradi katika nchi yetu, yaani *quotations*.

Mheshimiwa Spika, nimeshangaa sana kuona *quotations* za Serikali ni kubwa mno kuliko hali halisi ya gharama zilivyo katika maduka. Kwa mfano, unaweza kukuta mfuko wa sementi, niongelee Bukoba ambako gharama ya ujenzi ni kubwa, ni shilingi 20,000, lakini unaweza kukuta Halmashauri au *quotations* zake za ujenzi au kununua vifaa vingine mtu anaandika mfuko wa sementi ni 50,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kuiuliza Serikali ni jinsi gani imeandaa gharama hizi, makisio, yaani *quotations* zinakuwaje? Mimi ninafikiri hizi *quotations* ni kigezo kimojawapo ambacho kinafanya Miradi mingine ikwame kwa sababu gharama zinakuwa kubwa. Naomba jambo hili liangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haraka haraka naomba niongelee viporo vya Miradi ambayo ipo katika Halmashauri. Ni jambo ambalo limekuwa la kawaida kuona hii Miradi, nasema inaanzishwa kisiasa kwa sababu huwezi kuanza Miradi mipya wakati Miradi mingine haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, mimi nipo katika Kamati ya TAMISEMI, Kamati hii imetembelea Hospitali ya Singida, tulikuta Hospitali hii ili ikamilike inahitaji bilioni 150, lakini Serikali imekuwa ikitoa bilioni mbili tu kila mwaka. Sisi tumefanya makisio tukaona kwamba, kama Serikali itaendelea kutoa bilioni mbili kila mwaka, ina maana inahitaji miaka 75 kuikamilisha Hospitali hiyo. Cha kushangaza ni kwamba, unakuta majengo mengine yamekamilika baadaye yanaanza kuwa na nyufa, yanakuwa na popo na mambo mengine. Kwa hiyo, Serikali inaingia gharama, lakini pia kuwasimamisha wakandarasi mtapaswa kuwalipa kwa sababu mnakuwa mmesitisha mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliangalie jambo hili, ihakikishe kwamba, Miradi inapoanzishwa basi ipewe muda

maalum. Tunaweza tukasema tujenge hospitali moja ya rufaa katika miaka minne ikamilike halafu tunajenga hospitali nyingine. Kwa hiyo, hii Miradi itakuwa na uwezo wa kukamilika.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu usafiri wa ndege. Kuna swali liliuzwa hapa, tulitaka kujua nauli zinapangwaje, Waziri wa Uchukuzi akasema, kuna Mashirika ambayo yamepunguza nauli na akalitaja Shirika la *Fastjet.*

Mheshimiwa Spika, ni kweli Shirika la *Fastjet* limepunguza nauli, lakini unalipia mizigo, unapolipa mizigo kifurushi chochote kile hata kama kina kilo kumi unakilipia shilingi 15,000. Cha kushangaza, hizo fedha hazitolewi stakabadhi wanaweka tu ndani ya droo. Sasa mimi nataka Serikali itueleze kama mizigo inalipiwa labda ndiyo utaratibu; hizi fedha zinaunganishwa katika mapato ya Serikali wakati hazitolewi risiti.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri hata haya mashirika ya ndege, Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Wizara zake aangalie namna gani yana-*operate* katika nchi zetu. Yanaweka utaratibu kama huo watu wanalipia mizigo, wanadhulumiwa, wanakuwa na usumbufu mkubwa, yaani hayatoi hata ile *guarantee* ya kilogramu 20. Sawa unalipia lakini hizo fedha zinahesabiwa vipi? Shirika lile la *Fastjet* linabeba watu 150; kwa mfano, katika ndege wote wanalipia mizigo, fedha hizo huwa Serikali inafuatiliaje na zinaunganishwa wapi kama haziko katika tiketi ya ndege na kama hazikatiwi stakabidhi?

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi naomba nianze kwa kuipongeza Tume ya Mabadiliko ya Katiba, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwenda na wakati kama ilivyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Spika, nitoe tahadhari moja tu, hatuna sababu ya watu kulumbana kusema kwamba sijui Mabaraza huko ya kwenye Kata, CCM wamechakachua, hapana, tusifukuze vivuli vyetu, tuangalie uhalisia. Uhalisia unatokana na kwamba, katika matokeo ya chaguzi tulizokuwa tumezifanya za Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, Chama cha Mapinduzi kilishinda kwa asilimia zaidi ya 90. Halikadhalika, kwenye Udiwani zaidi ya asilimia 70, kwenye Ubunge sina sababu ya kusema picha halisi tunayo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hoja. Mkoa wa Pwani na Mikoa mingine yote inajikita zaidi kwenye kilimo. Moja ya zao ambalo tunalima sisi Mkoa wa Pwani ni Korosho. Cha kusikitisha zaidi, wakulima wengi na ni Wananchi wengi, asilimia kubwa ya Wakazi wa Mkoa wa Pwani ni Wakulima wa Zao la Korosho. Wanayumba na korosho zao, kila msimu zinakutana mle ndani, wauzaji wanataka kuuza, wanunuzi wanakuja na bei ambayo haijapangwa na Serikali. Sasa ni lini Serikali itaweka mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba, fedha zinazotolewa kwa ajili ya watu kununulia korosho zinafanya kazi hiyo na bei inayowekwa inafuata bei ile ambayo Wananchi wanaweza wakauza.

Mheshimiwa Spika, watu wengi hawakupeleka watoto wao mashuleni, wanashindwa kununua chakula, wanashindwa kujihudumia huduma za kwenda hospitali kisa hawana fedha, mali ipo ndani pesa hazipatikani. Hilo ni tatizo kubwa sana. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yake, ahakikishe kwamba, tunapata viwanda katika Mkoa wa Pwani. Viwanda vya korosho vitasaidia kwa sababu kukiwa na viwanda mtu atakwenda moja kwa moja kiwandani atauza korosho zake kwa bei atakayokubaliana na wenye kiwanda, lakini kama bei haiko hadharani na viwanda hakuna, hilo nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui jukumu la kiwanda cha korosho liwe kwa nani, ukiwauliza Wizara ya Viwanda na Biashara wanakwambia hili ni suala la Wizara ya Kilimo, Kilimo wanakwambia hapana sisi tunashughulikia kilimo, viwanda

ni huko huko kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara. Basi kama ni hivyo ni ombi tu, hata pamba, viwanda vya pamba visiwe chini ya Wizara ya Viwanda ya Biashara iende huko huko kwenye Kilimo ili tujue wanaosimamia kilimo wasimamie na viwanda vinavyohusika. Kama alizeti iende Kilimo isiende kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, lingine, mwanzo nimesema asilimia kubwa tuliyoipata Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji, lakini watu hawa Serikali inawatazama namna gani? Tunatumia mamilioni ya shilingi katika uchaguzi kuhakikisha tunapata viongozi wa kutusaidia kazi za usimamizi kwenye ngazi ya vijiji, mitaa na vitongoji. Wao ndiyo walinzi wa usalama na amani, wao ndiyo wawakilishi wa jamii katika mikutano ya ngazi za juu yao, wao ndiyo wanaotoa na kuthibitisha kwamba Mwananchi huyu ni mkazi halali wa kijiji au mtaa unaohusika, iwe Polisi, iwe Benki na kadhalika, lakini mtu huyu anafanya kazi kwa kutumia pesa zake mwenyewe. Hivi tunamsaidiaje, tunampa nguvu za aina gani ili aweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie kama ilivyoangalia maeneo mengine ya kuhakikisha wanawatengea posho watu hawa, basi isiwe kila mwezi hata kwa mwezi mara tatu au mara nne. Naomba hilo pia lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, maendeleo yoyote hayaji bila ya kuwa na barabara nzuri. Mkoa wa Pwani hatuna barabara za kutosha na barabara zetu ni mbaya; nyingine zimetolewa ahadi ya Rais toka mwaka 2005, leo tupo mwaka 2013 barabara hazijaisha, iwe Wilaya ya Bagamoyo, iwe Wilaya ya Kisarawe, iwe Wilaya ya Mafia, barabara hizo zote hazijakamilika. Naomba Serikali itenge fungu, iwe na uhakika wa kusema angalau kila mwaka wa fedha ijenge basi hata kilomita moja ili itupe imani na sisi. Kama hazijengwi hizo barabara tunategemea maendeleo yatapatikana na huo Mkoa utatokana na umaskini? Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara zinazohusika basi zinipatie majibu katika hoja hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la umeme, umeme ni adha, umeme ni tatizo, kwa bahati nzuri sitaki kusema bahati mbaya, nguzo kubwa zote za umeme lazima zipite Mkoa wa Pwani. Siyo mara yangu ya kwanza kulisema hili, toka nimeingia ndani ya Ukumbi huu nalizungumza, naomba Serikali iangalie Wilaya zetu zipate umeme, Kisarawe nguzo zimeanza kuwekwa lakini uendelezaji wa Mradi ule unasuasua. Sasa sijui tatizo lipo Wizarani au *TANESCO*; tunaomba tupatiwe majibu.

Mheshimiwa Spika, hatuna sababu ya Watanzania kulia njaa kuagiza mchele kutoka nje. Tunawakaribisha katika Mkoa wa Pwani, tuna mabonde mpaka ukipita wewe mwenyewe unasikia raha. Tunaiomba Wizara ya Kilimo, kwa kuwa ndiyo Wizara hiyo hiyo inayoshughulika na umwagiliaji, tuna wasomi wengi, tuna Wananchi wengi wanalima kwenye mabonde hayo; kwa nini Serikali isihakikishe inachangia kuwawezesha wakulima wa kwenye mabonde hayo iweke skimu za kutosha?

Mheshimiwa Spika, Rufiji kuna mabonde ya kutosha, Bagamoyo kuna mabonde ya kutosha, Wilaya zote za Mkoa wa Pwani zina mabonde ya kutosha, Mungu ametupa neema na utajiri tunashindwa kuutumia. Wananchi wanahangaika kwa kipato chao kidogo, lakini Serikali ikiwawezesha iingie ubia tu na wakulima, iwachukue wanafunzi wanaomaliza *UDOM,* wamalize kusoma masomo ya kilimo wawachukue wawaweke katika kila Wilaya wawasaidie Wananchi kuhakikisha wanalima kilimo cha kisasa, tuone kama tunaweza tukaenda kuchukua mchele kutoka Thailand, mchele sijui kutoka wapi huko, hatuna sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kuna haja ya kufanya hivyo. Niombe tu Serikali, siyo mara ya kwanza kulisema hili na nitaendelea kulisema mpaka nitakapoona mabadiliko ya kilimo yanaingia katika Mkoa wa Pwani. Nawaomba sana tuwaondolee umaskini Wananchi wa Mkoa wa Pwani. Tuhakikishe nchi yetu inapata zao la mpunga,

inapata zao la mchele, zao la mahindi na matunda halikadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba sana haya niliyoyasema tuhakikishe yanafanikiwa. Yakifanikiwa haya sidhani kama kutakuwa na sababu kila mwaka Mkoa wa Pwani uwe unahesabiwa kutoka chini kwa umaskini na sisi tunataka tuwe hapo juu kidogo.

Mheshimiwa Spika, suala la maji; maji ni tatizo. Mkoa wa Pwani kama ulivyokuwa na mabonde, una mito mingi sana. Ni vyema tukahakikisha kwamba, Miradi ya Maji inayotengenezwa basi kwanza Waswahili wanasema faida ya mti ni kile kivuli. Sasa sisi tuliokuwa kwenye hiyo mito ndiyo tufaidi kivuli cha huo mti, lakini maji yale mabomba yanapita yanakwenda katika maeneo mengine. Sisi pia tunahitaji kuwa na maji ya bomba na tunataka maji yanatoka kwa utaratibu unaoeleweka, badala ya kupata maji ya shida. Tunapata maji ya visima, tunaishukuru Serikali, lakini maji ya visima mengi yana chumvi. Fanyeni utaratibu wa kutafuta dawa ya kutoa chumvi ili na sisi tuone yale maji yawe mazuri, yawe safi na salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nipatiwe majibu ya mambo ya korosho na viwanda. Vilevile naomba nipatiwe majibu ya masuala ya mabonde ya mpunga. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Desderius Mipata, atafuatiwa na Mheshimiwa Salvatory Machemli na Mheshimiwa Martha Mlata ajiandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naanza na suala moja la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 63, unazungumzia juu ya kuimarisha huduma za afya. Mimi nijielekeze kwenye Hospitali yetu ya Taifa ya Muhimbili.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naanza na suala moja la kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 63 unazungumzia juu ya kuimarisha huduma za afya. Mimi nijielekeze kwenye hospitali yetu ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili Kitengo cha Mazoezi, kuna changamoto nyingi, na kwa kujua kwamba ni hospitali ambayo tunaitegemea nchi nzima, na ni-*declare interest* kwamba nina mtoto wangu anatibiwa kwa sasa. Nimeziona changamoto ambazo kwa kweli zinatakiwa zishughulikiwe kama Taifa. Kitengo kile kimesahauliwa sana.

Moja ya changamoto zilizopo ni kwamba hawana majengo ya kutosha. Mazoezi wanafanya, hamna *privacy,* lakini kwa vile hakuna majengo, kiutaratibu yale maeneo ambayo Idara zote zinatakiwa zikae pamoja, ikiwa ni pamoja na Idara ya Masikio na Kusema, Idara ya Mazoezi ya Miguu na Mgongo, Mazoezi ya Ufahamu na Mikono inatakiwa yote iwe pamoja kwa mujibu wa wataalamu wale. Lakini sasa unakuta wako mbali kiasi kwamba hawaendi kwa pamoja, wanatakiwa waende kwa pamoja na majengo yawe pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile utakuta hakuna hata choo, mambo madogo kabisa! Choo kiko kimoja, haki-*flash,* hakina jinsia kwamba kuna mtu wa kike na wa kiume. Ni vitu vidogo vidogo ambavyo kwa kweli unaweza ukakuta vinaleta maambukizi bila ya sababu ya msingi.

Vile vile vifaa vya mazoezi hakuna. Unakuta umeme ukikatika hakuna jenereta ambayo inaweza ikasaidia. Kwa hiyo, umeme ukikatika, na kwa joto la Dar es Salaam, maana yake huduma haziendi. Watumishi wako wachache hasa kwa upande wa *Occupational Therapy* wako wachache wako wanne tu na tunawapelekea Watanzania wote hapa kwa hospitali yote ya Muhimbili. Kwa hiyo, naomba wahusika walione hili. Hatuna sababu ya kuacha changamoto hizi na kuwepo mahali ambapo tunakusanya Watanzania wapate huduma.

Mheshimiwa Spika, vilevile Watumishi hawaendelezwi, hawasomeshwi. Wakitoka KCMC ili waweze kuendelea, lazima waende nje. Wakitaka kwenda, wanatakiwa wajilipie zaidi ya Shilingi milioni 30. Utapata wapi? Serikali lazima iangalie uwezekano wa kuendeleza Kitengo hiki, ni muhimu sana. Nimeona jinsi kinavyobadilisha watu akiwepo mtoto wangu.

Mheshimiwa Spika, niende Jimboni. Katika hospitali yetu ya Mkoa zipo changamoto kubwa sana. Nakumbuka hivi karibuni Mheshimiwa Mama Kikwete alitutembelea akatuletea zawadi kubwa kupitia Shirika lake la WAMA. Aliweza kutupatia msaada zaidi wenye thamani ya vifaa zaidi ya Shilingi milioni 700. Sasa tuna changamoto ya wataalamu. Hamna wataalamu wa kutumia vile vifaa.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaomba ikiwezekana tukubaliwe katika maeneo mbalimbali tuwasomeshe wataalamu ambao wanaweza warudi. Tuwa-*recruit* pale pale na warudi kufanya kazi kwa sababu sisi kwetu hatupati watumishi na hii lazima iende pamoja katika Halmashauri zetu na maeneo ambayo yapo mbali na *centre*.

Mheshimiwa Spika, kwenye hospitali yetu ya Wilaya ya Nkansi vilevile ina changamoto hizo hizo. Hakuna Madaktari, hakuna Wauguzi, hakuna Watumishi wa Maabara na ukizingatia hospitali ile ndiyo inategemewa Wilaya nzima. Lakini pia kuna Chuo ambacho kina-*train* Watumishi wa Maabara na Wauguzi. Sasa tutawapa mafunzo watu katika hospitali ambao ni *sub-standard* kama ile!

Naiomba Wizara ihakikishe kwamba inatuletea Waganga wazuri, wataalamu wa Maabara na madawa yanapatikana ili hata wale ambao wanapata ujuzi katika Chuo cha Saint Bakita waweze kupata ujuzi unaotosheleza na kukidhi haja kuliko ilivyo sasa. Tumeshamwandikia Katibu Mkuu kumwomba gari. Hatuna gari la wagonjwa kuwafuata kule vijijini. Vifo vya akina mama na watoto vimeongezeka kwa sababu hatuna gari. Tunaomba majibu katika hili, ukizingatia tuko mbali, tuna haki ya kupata.

Jambo lingine ambalo nililotaka kuzungumzia ni suala la barabara. Tunashukuru Serikali barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, inakwenda vizuri, lakini kuna changamoto kubwa kwa barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Kibaoni, haiendi kabisa. Wananchi wanahoji, kuna nini? Mbona imesimama? Kama imesimama namna hii, maana yake nini? Basi Wizara ituambie, kuna shida gani hapa? Hawamlipi Mkandarasi? Au hana hela? Taratibu zinasemaje? Maana yake wananchi wanaitegemea barabara kwa haraka, hawaioni.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni barabara za vijijini. Nina barabara moja ambayo nilikuwa nikiisema sana hapa ya Kitosua, Mpembe, Kanakala pamoja na Ninde Namanyere. Barabara hizi bado ni changamoto. Naishukuru TAMISEMI kwa kusikia

na kunipatia fedha kwa barabara ya Kanakala zaidi ya Shilingi milioni 400. Nawaomba wasimamizi wa pesa hii wawe makini sana. Hizi hela zitaondoka na mtu. Nitazisimamia kwa karibu shilingi kwa shilingi, nataka kuona inafanya kazi gani. Atakayeichezea ataondoka nayo. Nasema wazi hadharani. Tumezitafuta kwa jasho kubwa sana.

Namshukuru sana Waziri Mkuu, Katibu Mkuu wa TAMISEMI na dada pale *Engineer* Kayanda, amenisaidia sana katika kumpigia kelele za mara kwa mara. Naomba asiishie hapa, angalia na barabara nyingine ambazo zinatusumbua. Kwa mfano barabara ya Katani kwenda Chonga mpaka Miula, barabara ya kutoka Milundiko kwenda Kisura, barabara ya kutoka Katongolo, Namansi mpaka Linde, barabara zote ni changamoto kubwa. Naomba sana hizo barabara watusaidie.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni mawasiliano ya simu. Natambua vizuri sana jitihada ambazo zinafanywa na wenzetu wa Wizara hii, lakini naamini kwamba watakuwa wanakwamishwa na utaratibu fulani. Kwa sababu nimewapelekea mara nyingi na wanatambua na kwa kweli wanaonyesha nia ya kutusaidia.

Wizara hii nadhani wanakwama jambo fulani. Serikali kama Serikali tuangalie, kule Wampembe, Kala na Ninde ni Watanzania ambao wamekosa kupata mawasiliano. Ukisimama Bungeni hujalisema hili, hawaoni kama unawasemea. Bora niseme wasikie kama tunasema, lakini hayatekelezwi.

Naomba Wizara au Serikali iangalie utaratibu mzuri zaidi. Huu utaratibu tulioufanya wa *UCAF* nadhani utakuwa umefeli mahali. Maana tunapata ahadi ahadi

na ukienda kwa Waziri unakuta kweli ameweka, wakati mwingine Makampuni yenyewe yanayowekeza hayataki kuwekeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Wampembe ni mahali ambapo kuna watu wengi kabisa na Kampuni itakayowekeza pale itaweza kufanya biashara sana hata Kala. Kwa hiyo, ningetoa wito kwa Makampuni yanayotaka kuwekeza waje wawekeze kwetu.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme. Umeme tumeupata lakini changamoto tunayoipata ni kwamba pale pale Namanyere wanatakiwa kutawanyika. Hivi ninavyosimama hapa nyumbani kwangu hakuna umeme. Kama nusu kilomita kutoka eneo umeme unapopita. Sasa ni changamoto hiyo.

Kwa hiyo, utawanyike sasa pale na vijiji vya njiani vya Nkundi, Chala, Kipande, Kasu utawanyike ndiyo utatuletea tija tunayoitarajia. Lakini pale Kilangala kuna Kituo cha Afya cha Kulelea Watoto pale, hakuna umeme. Naomba tusogezewe umeme.

Kadhalika, Kalundi, Miula, Chonga, Katani, Miula Chalatila mpaka Kate, tungeweza kupata hapo ingetusaida sana. Lakini vilevile Kata ya Isale yote na vijiji vyake, kutokea Namanyila ni jirani mno. Nitoe wito vile vile kwa wafanyabiashara, tuna umeme sasa Namanyere. Njooni mwekeze kwenye mazao ya kilimo ili kilimo chetu kiwe na thamani ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika kilimo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kuruthum atafuatiwa na Mheshimiwa Mshama.

**MHE KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikiwa salama kabisa.

Mheshimiwa Spika, nataka nijielekeze kwanza katika nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tuliwaweka Wakaguzi katika Halmashauri zetu, tumeweka Wakaguzi Kitaifa kwa ajili ya kukagua nidhamu ya matumizi ya fedha katika Serikali yetu hata katika Halmashauri. Lakini mimi napata kigugumizi na nashangaa sana kuona kwamba Wakaguzi wanapokwenda katika Halmashauri zetu, watumishi wa Halmashauri hususan Wakurugenzi, Wahasibu ambao ni Ma-*DT*, wanakataa kuwapa Wakaguzi taarifa muhimu za fedha, zile risiti, zile *imprest.* Hivi hawa watumishi wa Halmashauri wanapata wapi jeuri ya kuwanyima Wakaguzi risiti za malipo?

Mheshimiwa Spika, nasema kwa uzoefu kutoka Kamati ya *LAAC.* Kwa mfano, mwaka 2010/2011 takribani Halmashauri 22 zilikataa kuwapa hati za malipo Wakaguzi zaidi ya Shilingi bilioni 1.5. Tunafanya nini sasa? Wakaguzi wanafanya kazi gani kama watumishi wa Halmashauri wanakuwa na jeuri ya kukataa kutoa vipatanishi kwa Wakaguzi wetu?

Mheshimiwa Spika, pia kama haitoshi, vitabu vya malipo zaidi ya 2,990 za stakabadhi ya malipo katika Halmashauri zetu Wakaguzi wameshindwa kuzipata

kutoka kwa watumishi wa Halmashauri. Sasa tunaweka hizi Mamlaka za Ukaguzi kwa kuangalia nidhamu ya matumizi ya fedha kwa faida gani ikiwa watumishi wa Halmashauri wanakuwa na jeuri ya kuwanyima Wakaguzi taarifa muhimu ambazo zinasaidia kujua ubovu wao? Hapo ndio wizi unapofanyika.

Mheshimiwa Spika, hivi kama mtumishi hujaiba, kwa nini ukatae kutoa *imprest,* vocha? Una tatizo gani kutoa vocha kwa Wakaguzi kama hujaiba? Lakini haitoshi, utashangaa baada ya miezi mitano, baada ya mwaka *imprest voucher* zimepatikana. Zinapatikana wapi na mara ya kwanza wanapopata wanazificha wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atueleze, wanazificha wapi na wanazipata wapi? Tusiruhusu wizi. Huu ni wizi wa waziwazi.

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee kidogo katika suala la uwekezaji hasa katika ardhi. Kumekuwa na mkanganyiko mkubwa ambao unaleta ugomvi mkubwa sana katika Halmashauri zetu katika suala la ardhi. Watu wanapewa ardhi, wawekezaji wanapewa ardhi ambazo hawaziendelezi, lakini pia hata takwimu zetu zinakanganya.

Mheshimiwa Spika, mimi nina kitabu cha Mpango cha Mheshimiwa Wassira mwaka 2013/2014 ametueleza hapa katika kitabu kabisa kwamba Rufiji wawekezaji, anasema kuna *Agro Forest.* Naomba ninukuu tafadhali.

"*Agro Forest* wamepewa ekari 20 Muhoro Rufiji; anasema Tawi Utunge kuna watu wa *Frontline* wamepewa ekari 20, lakini hapo wapo anasema kwamba kuna watu wa *Eco Energy* Ruvu wamepewa ekari laki mbili na thelathini na saba sijui ngapi elfu. Lakini pale Rufiji kuna Taasisi ya RUBADA ambayo inaendeleza bonde la Mto Rufiji, wanakuja na takwimu katika

Halmashauri yetu, anasema *Frontline* amepewa ekari 5,000, anasema *Agro Forest* wamepewa ekari 6,000 hizi takwimu za mezani zinatoka wapi? Hii ni Serikali gani ambayo inakuja na takwimu hizo? Serikali ni moja, RUBADA ni taasisi ya Serikali, Mipango inatoka Serikalini, ardhi nao wanakuja na takwimu zao. Ardhi wana takwimu zao, RUBADA wana takwimu zao. Mheshimiwa Wassira mpango wa nchi nzima, takwimu zinatoka wapi za mezani.

Mheshimiwa Spika, hizi takwimu za mezani ndizo zinaleta mkanganyiko kwa wananchi wetu. Hapa anakuja mwekezaji anasema amepewa ekari 20,000, mwingine anasema nimepewa ekari 5,000 wakati takwimu ziko tofauti. Tunatoa wapi hizi takwimu? Naomba Ardhi, RUBADA, Mipango waje na takwimu za uhakika kwa watu wa Rufiji. Wanaleta mkanganyiko na ugomvi. Huu ndiyo usugu mkubwa katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini nashukuru umetupeleka *UDOM* katika lile kongamano la *Gender Coalition.* Tatizo la ardhi linawaathiri sana akinamama. Tumeona watu wa Kanda ya Mashariki, watu wa Mvomero, kuna Waheshimiwa viongozi kule wana maekari, mtu ana ekari 10,000, ekari hizo haziendelezwi hata kidogo. Sasa hivi wanakodisha kwa wananchi wale wale. He! Tunarudi katika Nyarubanja *System!* Tumetoka katika ukoloni na tunarudi tena katika *system* ya zamani ya ukoloni! Tumetoka katika ukoloni, tatizo liko wapi? Kwa nini watu wachukue ardhi, wapewe ardhi ambayo hawaiendelezi, tena wanakuja kukodisha wananchi wetu wale wale wenye ardhi yao?

Hii inasikitisha sana! Viongozi waliochukua ardhi Mvomero, Morogoro na sehemu nyingine. Warudishie kwa wananchi! Wananchi wanakosa ardhi ya kulima wao, sasa wanatukodisha. Tunakuwa watumwa,

tunakuwa wakimbizi ndani ya nchi yetu. Akina mama wanalalamika wanahamahama ovyo, ardhi wanayo watu, ni misitu hawaiendelezi. Hao ni wawekezaji au wababaishaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sana wawekezaji kwa sababu wawekezaji wanaleta ajira, wanaboresha kilimo, lakini kwa nini Serikali inaendelea kuwakumbatia wawekezaji wababaishaji, hawaendelezi chochote? Naomba Serikali iangalie hii ardhi ichukuliwe kwa watu ambao hawawezi kuiendeleza warudishe kwa wananchi wapate fursa ya kutumia ardhi yao na siyo kwamba wafanye ubabaishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenzangu kidogo amegusia TAKUKURU hapa. TAKUKURU wanafanya kazi nzuri sana, lakini TAKUKURU sasa wamekuwa kama hawana meno, wanaishia kuchunguza chunguza wanapeleka taarifa kwa *DPP* kesi haziendi. Wenzetu India na nchi nyingine TAKUKURU wana fursa ya kuchunguza na kushitaki. TAKUKURU wana ushahidi wote wa kutosha. Kabisa umethibitishwa! Lakini tunaambiwa kwamba ooh, kesi ipo kwa *DPP,* miaka sita watu wanaendelea kupeta, watu wanaendelea kutunyonya wanyonge, watu wanaendelea kututambia wanyonge.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU wapewe fursa waweze kuchunguza na kushitaki. Tuache mambo ya ubabaishaji kwa kesi ambazo haziishi kwa miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia Shule za Kata. Tumejenga shule nyingi sana za Kata, tunaishukuru Serikali, zimejengwa Shule za Kata nyingi sana kwa minajili ya kwamba watu wasome karibu na maeneo yao. Nataka nitoe mfano kwangu kule Rufiji, watoto wanatolewa Kibiti, Ikwiriri wanapelekwa kusoma kilomita

80 Mwaseni kwenye Kata ambayo ipo kwenye mbuga, hakuna umeme, hakuna maji wala hosteli, halafu mnasema Shule za Kata hoyee! Watu wanafaulu. Watu watafaulu wapi?

Mheshimiwa Spika, tunatarajia watapata watu ambao wanafaulu kutoka katika shule ile ambayo haina umeme, haina maji, mwalimu mmoja; unamtoa mtoto Ikwiriri ambapo ni mjini kuna umeme, kuna maji unampeleka kusoma Mwaseni ambapo hakuna mwalimu, wala hakuna maji.

Shule za Kata tunazipenda lakini pale kuna shule Ikwiriri Kata ya Umwe pale, sasa hivi ina takribani miaka sita haiishi, watu wamejenga mpaka madarasa yanabomoka.

Kwa hiyo, ni urasimu wa watu wachache tu, kwa sababu ya mambo ya kisiasa kwamba Kata inaongozwa na watu wa *CUF.* Tunafika wapi? Tutawapeleka wapi watoto wetu? Tunachukua watoto wa wanyonge tunawapeleka porini ili wakapate *zero* halafu watoto wetu sisi viongozi tunawapeleka shule nzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana, tuangalie hili tunadidimiza wanyonge, wenzetu sisi tuna pesa tunapeta, hii siyo haki.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru tuna umeme wa gesi kutoka Somanga Fungu. Lakini sasa tushakuwa wababaishaji. Sasa hivi tunakaa pale Rufiji kila siku umeme unakatika zaidi ya masaa kumi. Umeme ukiwaka saa tatu, saa nne haupo. Ukiwaka saa nne saa sita haupo. Kuna matatizo gani? Ukiwaambia *TANESCO* wanakwambia ooh, sijui nini.

Tunaomba zile mashine pale wamepeleka mashine ambazo zimechakachuliwa, mashine hazifanyi kazi, mashine mbili zimekufa. Watupelekee mashine nzuri wakatengeneze watu wapate umeme. Naomba sana msichakachue watu wa Kusini jamani, tumechoka kuchakachuliwa. Tunaomba umeme pale mzuri ili watu wapate wafanye kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kidogo niende kwenye Maliasili. Nimelalamika kweli humu ndani, Kamati ya Ulinzi imekuja kufanya uchunguzi kule Mloka, lakini mpaka leo hakuna majibu ya msingi. Wamekuja wakasema watachimba mabwawa, mabwawa hayo yaliahidiwa na Mheshimiwa Maige.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza natoa shukrani mbele ya Mungu na mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na naomba tu kwa ruhusa yako niseme na-*declare interest* kwamba mimi ni Mchungaji. Kidogo tu niombe sana kwamba siyo vibaya kusema maneno ya Mungu, lakini ni vizuri kuyasema yanayopaswa kusemwa.

Kwa mfano, ukisoma Thimotheo ya kwanza mstari wa kwanza sura ya pili, mstari wa kwanza hadi wa pili unasema: “Basi kabla ya mambo yote nataka dua na sala na maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu

wote kwa ajili ya Wafalme na wote wenye mamlaka. Tuishi maisha ya utulivu na amani katika utawa wote na ustahimilivu."

Mimi nadhani ndiyo maneno mazuri ya kuwaambia Watanzania ya kwamba mamlaka yoyote iliyopo imewekwa na Mwenyezi Mungu na inastahili kuheshimiwa. Hivyo siyo kuwararua. Kazi kubwa tuliyopewa ni kuwaombea na ukiona yanakwenda vibaya ni kwamba watu hawajaomba. Nasema na hapo na hapo ndipo ninapokwenda kuungana na Mama Spika alivyosema kwamba tuwe na heshima, tuheshimu nchi yetu na Watanzania ndipo wataona kweli tumewawakilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niongelee suala la uchumi. Katika hotuba ya Waziri Mkuu alitueleza kwamba uchumi wa Tanzania umekua na akataja vigezo vya kukua kwa uchumi, lakini naomba tu niongee kuhusu pato la Mtanzania. Amesema pato la Mtanzania limetoka Sh. 869,436/= mpaka Sh. 965,298/=.

Mheshimiwa Spika, ukimwambia mtu kitu kukua huwa kinaonekana kwa macho. Unaposema mti unakua unauona unaongezeka kimo, unapoona mtu amekua unamwona ameongezeka kimo, lakini unaposema uchumi wa Tanzania umekua wakati Mtanzania wa leo hana uwezo wa kula milo mitatu, nahisi uchumi wa Tanzania haujakua kama inavyosemekana. Uchumi kukua inatakiwa uonekane kwa macho, watu waone kweli uchumi umekua, wapate chakula chao, wale, wanywe, waseme kweli uchumi umekua. Nashindwa kuelewa! Nilikuwa naomba kusema, tunaweza kutumia maneno mengine badala ya kusema uchumi umekua ili kusudi iweze kueleweka.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kiwango kinachopatikana kwa Mtanzania ni kwamba anaishi kwa Sh. 80,000/= tu ambazo sijui walipokuwa wanatafuta hivyo vigezo walichukua Mikoa mingapi. Kwa Mkoa wa Kagera inaonekana kabisa uchumi wetu ni Sh. 430,000/=, lakini kwenye maandishi hapa inaonyesha kwamba Sh. 900,000/= na kitu. Mimi ninaona kwamba Mikoa mingine inabaguliwa kwa kupima uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali itusaidie iweze kuwa na takwimu za kutosha za mikoa yote na hapo ndipo tulete takwimu za kusema kipato cha Mtanzania ni kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kwamba unaposema Sh. 85,000/= kwa Mtanzania ni kwamba kila Mtanzania kwa siku ana uwezo wa kupata Sh. 2,766/=. Hivi ni kweli?

Nikirudi kwenye Jimbo langu kule Nkenge Mtanzania hana uwezo wa kupata hata Sh. 500/= kwa siku, hana uwezo wa kupata hata Sh. 300/= kwa siku. Lakini unaleta jumla kwamba Watanzania tunapata Sh. 85,000/= au Sh. 2,766/=. Naona inabidi turudie kufanya utafiti.

Nimeuliza kwa mtaalamu wangu wa Wilaya kwamba wewe katika Wilaya yetu kila Mwana-Misenyi ana pato la namna gani? Hana takwimu. Anasema sisi hatujapata fedha za kuweza kujua kila Wilaya ina uwezo wa pato la namna gani, kwa sababu tumeomba hatujapewa.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu niombe tu kwamba itakapokuja wakati mwingine, hebu tupewe

taarifa za Watanzania wote, hata kwa Mikoa na Wilaya tujue kipato cha kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala *inflation.* Kama kweli tunataka kuondoa mfumko wa bei, naomba nishauri ifuatavyo:-

Unaposema mfumko wa bei kwa sasa hivi ni asilimia ilikuwa 19, sasa ni 10.4 mimi naona kwamba siyo kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotuletea hizi takwimu, alikuwa anasema mfumko umepungua, lakini nikiangalia kiukweli mfumko haujapungua. Ukisoma katika ukurasa wake wa namba 18 utaona hapo vigezo, lakini hivyo vigezo nikiviangalia viko tofauti na mfumko wa bei.

Kwa mfano, unaposema kwamba mfumko umepungua lakini ukakuta mtu Mtanzania huyo hana uwezo wa kununua kilo ya mchele, hana uwezo wa kununua kilo ya unga, utakuwa mfumko umepungua vipi?

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri, kama tunataka kupunguza mfumko wa bei, ni lazima kuwepo chakula cha kutosha kwa wananchi, ni lazima tuangalie kilimo kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tatizo kubwa la mfumko wa bei ni kutokana na Watanzania kukosa chakula cha kutosha. Kama hakuna chakula hamna namna yoyote, unaweza ukasaidia mfumko wa bei.

Naomba tu Serikali ya Tanzania, tumekuwa na misemo mingi, tulikuwa na mambo mengi yakitokea, tukaita hata katika wakati huu tukasema Kilimo Kwanza. Kilimo Kwanza hakijatendewa haki. Kilimo Kwanza

hakijafanyiwa yale yaliyotakiwa kufanyika kwenye Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hii, watu wengi wameajiriwa na kilimo zaidi ya asilimia 70. Lakini ukiangalia Watanzania hao hao, leo wengine wanashidwa, wamekaa kwa sababu hawana nyenzo za kilimo, hawana vifaa vya kulimia na kama tukisema tupeleke pembejeo zinapelekwa wakati watu wameshakaribia kuvuna. Tukisema tupeleke madawa ya kukuzia, tunapeleka wakati wa mavuno. Sasa mimi sijaelewa hiki Kilimo Kwanza kinawezaje kuondoa *inflation*, kinawezaje kutufanya Watanzania tuweze kupata chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, hapo zamani *inflation* ilikuwa asilimia tano, lakini leo *inflation* ni 10.4 yaani ilikuwa asilimia tano, leo ni asilimia kumi. Naomba kuuliza ni kitu gani kilifanyika wakati ule hata tukawa na *inflation* ya asilimia tano na ambacho hakiwezi kufanyika leo tukarudi kwenye *digital* moja ya *inflation*. Naomba kuuliza, nini kilitokea ambacho leo hakiwezi kufanyika na tukarudi kwenye asilimia tano? Nauliza, ni mkakati gani mahsusi ambao Serikali inao kuhakikisha kwamba tunarudi katika *single digit* ya *inflation*.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunaamaanisha, naomba tu nitoe ushauri ni vyema tukarudi kwenye kilimo kweli kweli. Vijana wetu kama sisi watu wa Misenyi tuna mabonde ya kutosha, tuna maeneo mazuri, mvua Januari mpaka Desemba, tuna uwezo wa kulisha ukanda wa Ziwa wote. Lakini leo hawapewi trekta, na ukiangalia tulikuwa tume-*book* hata trekta tumekwenda trekta hamna. Sasa tunawezaje kuondoa *inflation* wakati *inflation* inaleta kigezo kikubwa kuliko vyote ambacho ni ukosefu wa chakula. Ni aibu Tanzania kukosa chakula tukaenda kuhemea kwa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye elimu. Naomba niipongeze Serikali ya Tanzania ya Chama cha Mapinduzi na wananchi kwa ujumla kwa namna ya pekee ambavyo wamejitoa kuhakikisha kwamba tunapandisha elimu, lakini liko tatizo.

Ningependa kuwajulisha Watanzania kuwa hapo nyuma tulikuwa watu wachache, tulikuwa watu milioni 34, leo tuko milioni 44. Siyo hilo tu, leo hii mtoto wa miaka tisa anapata mtoto mwenzake na akishapata huyo mtoto anataka Serikali imsomeshe.

Kuna mtu mwingine ana watoto 14, nilikuwa namwuliza mama mmoja katika Jimbo langu akaniambia anao watoto 14 na yeye akishawazaa anataka Serikali iwasomeshe. Siyo tu kuna wenzetu ambao katika mambo yao na maadili yao wanaruhusiwa kuwa na wanawake zaidi ya wawili, watatu, na akawa na watoto 40 na akishakuwa nao anataka Serikali iwasomeshe. Lakini nilichokuwa naomba Watanzania hebu tusomeshe watoto wetu tukishirikiana na Serikali yetu ambayo ina mikakati mizuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Haya. Ahsante. Ahsante sana.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Ahemed Ali Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa, naomba nianze kuangalia suala zima la maji katika Jimbo la Solwa na hasa huu mradi wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya, mradi huu umekwenda vizuri sana Kahama na Shinyanga kupitia vijiji katika Jimbo la Solwa. Lakini ni pamoja na ahadi ya Rais, ametembelea katika Wilaya yangu mara mbili na kusema kwamba atahakikisha kwamba katika awamu ya pili ya vijiji ndani ya kilomita 12 na vyenyewe vinapata maji. Hivi leo nimeongea na Wakurugenzi wa KASHUWASA ameniambia hakuna fedha ya aina yoyote iliyokuja hata ya upembuzi yakinifu. Sasa huku ni kumdhalilisha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Solwa na maeneo mengine yote katika mradi huu wa Ziwa Victoria wamekuwa na matumaini makubwa sana kwamba katika bajeti ya mwaka huu angalau vijiji nusu na mwaka unaokuja vijiji vinavyofuatia viweze kupata maji ya Ziwa Victoria. Kuna Kata nyingi, kuna vijiji vingi na kuna maeneo mengi ambayo yanahitaji maji ya Ziwa Victoria. Kata ya Salawe, Isamagazi na nyingine hata Kata ya Samuye nayo imo katika mpango huu wa Ziwa Victoria.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atizame hili tupate fedha hata Shilingi bilioni tatu za kuanzia ili angalau vijiji hivi ambavyo vina matatizo makubwa sana ya maji kwa sababu siyo suala la kutafuta maji ni suala la kuunganisha *pipe* na kuwapelekea wananchi maji. Maji tayari yapo kwenye bomba kuu.

Mheshimiwa Spika, visima vya *World Bank*, awamu hii kwa sasa hivi, mimi nashukuru sana tumepata

karibu miradi 10 na sasa hivi mradi huu wa *World Bank* upo katika Kata ya Didia na ya Mishepo. Lakini mpaka hivi ninavyokwambia, *documents* zote ambazo ziko kwenye *final stage* kwa ajili ya kuwapa Wakandarasi zipo Wizara ya Maji. Wizara ya Maji wamezikalia tu zile *documents* sijui hata wameziweka wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri Mkuu alitafutie ufumbuzi hili. Tunaomba m-*release documents* hizi, zije Halmashauri wapewe Wakandarasi kazi ifanyike kwenye Kata ya Didia.

Kata ya Didia ni Kata kubwa sasa hivi, ina watu wengi, ina umeme, ina miradi na ina vitu vingi sana. Sasa ikiwa *World Bank* wametoa fedha, *documents* zinakaliwa na Wizara, nikienda kwenye Kata ya Didia maswali ni mengi, nashindwa kujibu.

Kwa hiyo, naomba wananchi wa Kata ya Didia, Mishepo wavute subira na hata Kata ya Ilola na Vidati kwa maana ya kwamba baada ya zamu hii na wao wanafuata. Ilola nao wanakuwa na maswali mengi naomba wananchi wale wasubiri sasa hivi tunakwenda awamu ya kwao.

Mheshimiwa Spika, tatizo la njaa. Naishukuru sana Serikali na hasa shukrani za pekee zimwendee Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Nakushukuru sana mtoto wa mkulima, umeweza sana kunisaidia tukapata chakula, lakini mpaka sasa hivi hatujapata ila Waziri Mkuu najua kabisa anashughulikia suala hili. Naomba sana niweze kupata. Mvua zilizonyesha wiki iliyopita, zimeharibu mazao vibaya karibu Wilaya zote kwa maana ya kwamba tathmini iliyofanywa mtakuja kufanya tena tathmini ya pili mtupe mgao mwingine.

Mheshimiwa Spika, suala la njaa, nashauri, jamani tuleteeni mtama ule mweupe tuwatembezee, tuwaeleze wananchi wetu namna ya kulima mtama huu. Nimeongea na Mkurugenzi amefurahia, amesema wako tayari hata kununua. Kwa hiyo, suala sio tu suala la kuokoa tatizo la njaa ni suala hata la zao la biashara kwa wananchi wa maeneo hayo ambayo yanapata matatizo ya njaa.

Ushauri wa pili tuzingatie maeneo haya. Hatupendi kuomba chakula kila mwaka. Tunaomba Serikali hebu i-*focus* kwenye suala zima, tunapoleta miradi kupitia Halmashauri kwa ajili ya umwagiliaji au maeneo mengine kwa ajili ya kulima tuondokane na tatizo la njaa hili mtuone. Mnatoa fedha mnapeleka kwenye maeneo ambayo yana mvua, hawana matatizo ya njaa. Hebu tuoneni sisi katika Mkoa wa Shinyanga, Simiyu na Mikoa mingine inayokumbwa na tatizo hili la njaa. Hatupendi!

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya sina tatizo nalo naomba nimkumbushie Mheshimiwa Waziri Waziri analifahamu, najua kabisa atanisaidia. Kazi anayofanya ni nzuri sana Mungu akuweke akupe afya njema. Kwa niaba ya wananchi wa Solwa, kweli nakushukuru kwa kipekee kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha za mwaka 2012/2013 mpaka sasa hivi tumepata labda asilimia 30 tu na tunaingia kwenye *quarter* hii ya nne tunakwenda bajeti inayokuja. Wasiwasi wangu ni kwamba tunaingia bajeti ya mwaka 2013/2014 hii ya mwaka 2012 hatujaipata. Mtindo huu unaendelea kila mwaka tunakosa asilimia 20, 25, 30. Sasa kama tuko Bungeni tunapitisha halafu fedha haziji, hivi mantiki yake inakuwaje? Ni bora twende na ile *actual budget* kabisa moja kwa moja tujue kwamba hapa tunafanya na hapa hatufanyi.

Naomba sana fedha zile ambazo tunazipitisha tuzipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga tangu tupate Uhuru tumechangia sana kwenye pato la Taifa. Almasi na dhahabu tumeuza sana, Kahama ni nyingi, kwangu Solwa dhahabu kibao kwa kweli tumechangia kweli kweli katika Mkoa wa Shinyanga. Naomba na nawaambiea Serikali kwamba wala hatutaweza kuwa na mtindo wa kufanya maandamano na vurugu kama walivyofanya maeneo mengine. Ni watu wa heshima, lakini sasa mtuone, siyo kama tunashindwa, hapana, mtuone! Mkoa wa Shinyanga sasa hivi hata *Airport* tunakwenda kupandia Mwanza. Hivi kweli *Airport* hatuna Mkoa wa Shinyanga na tunachangia kwenye pato la Taifa! Ukisema pato la Taifa la dhahabu ni *billions of billions of money.* Tunakosa *Airport*, tunakosa miundombinu mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu tuoneni kwa hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu lichukue hili tunahitaji *Airport* sasa kwa Mkoa wa Shinyanga na miundombinu itakayoweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliomba kupandishwa hadhi kwa barabara ya Solwa - Didia na tumepitisha kwenye vikao vyote husika pamoja na *RCC*. Naomba sana Wizara ya Ujenzi itusaidie ili kuondokana tatizo hili. Unajua Jimbo la Solwa ni *East.* Jiografia yake asilimia karibu 50 ni mbuga tu.

Kwa hiyo utakuta fedha tunazopata kwa ajili ya barabara zetu hazitutoshi. Mnapochukua hizi barabara na siyo tu kuchukua kwa maana kwamba vinakidhi vigezo, mnakuwa mnatusaidia ili sisi twende kujenga barabara kwenye maeneo ya Kata zote ili wakulima

waweze kunufaika na mazao yao kuuza vizuri na kupanda kwa bei ya mazao.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la magari ya NOAH. Tinde, Kahama daladala NOAH zinafanya kazi sana. Tumeambiwa zimepigwa marufuku kwamba zinaua watu. Hivi zinaua watu vipi? Juzi tu kutoka huko Kusini kuja huku Mjini, mabasi makubwa yale yamepinduka karibu sita. Ukitazama pikipiki zinaua watu ovyo. Hivi zinazoua watu ovyo ni pikipiki, mabasi makubwa au malori au hizi NOAH? Hebu fanyeni utafiti kwa sababu zinaajiri watu wengi sana hasa Tinde, Kahama na Shinyanga, zinaajiri watu wengi, vijana wanasafiri haraka.

Naomba hili mlishughulikie vizuri. SUMATRA wamezuia, kulipia *TRA* wanalipa lakini ikifika barabarani Matrafiki wanazikamata eti kwamba zimezuiliwa. Mimi sioni kabisa mantiki hii. Waziri Mkuu hebu lichukue hili. SUMATRA wanasema wanasubiria maamuzi ya Waziri Mkuu na ndivyo wanavyosema. Sasa Waziri Mkuu nimelileta, lifanyieni kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni suala la Walimu. Walimu vijijini wapeni *incentive* kubwa tu, watakaa vizuri tu. Huu mtindo wa kuhamahama umeanza kupungua. Lakini waongezeeni *incentive* na matatizo yao yaondolewe, mishahara kidogo iongozewe, wanaokaa vijijini watakaa tu. Bahati nzuri sana sisi huku tumeshaanza kujenga nyumba zao za Walimu, tumeshaanza ku-*focus* sana kwenye maeneo kama haya ili wasiweze kupata matatizo ya kuishi vizuri na kufundisha watoto wetu.

Namshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Paul Lufunga anafanya kazi nzuri kwenye Mkoa wangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifahamu hili.

Namshukuru sana Mkuu wa Wilaya anafanya kazi nzuri, namshukuru sana Mkurugenzi, anafanya kazi vizuri, Madiwani wote na hasa hasa Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Ngasa anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema ahsanteni sana nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Sara Msafiri, atamalizia na Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, napenda niende moja kwa moja kwenye uchangiaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuamua kutumia teknolojia ya kisasa ambayo inarahisisha upimaji wa ardhi ambao ni wa gharama nafuu na unaochukua muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda mrefu sana kwenye nchi yetu tulikuwa na migogoro ya ardhi. Kuna migogoro kati ya wakulima na wafugaji, kwa mfano ukiangalia kwenye Wilaya za Morogoro hasa Kilombero, Kilosa na Mvomero; kuna migogoro kati ya wawekezaji na wananchi. Hii migogoro imepelekea wananchi kupoteza imani na Serikali yao waliyoichagua ya Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwa sababu Serikali yetu imeamua kupima ardhi ya nchi ili wananchi watambue maeneo gani ni ya ufugaji, maeneo gani ni ya kilimo na maeneo gani ya uwekezaji. Ninaamini sasa tatizo la migogoro litakuwa limekwisha na wale wachache wetu ambao wanaichonganisha Serikali ya CCM na wananchi wake sasa watapatwa na

kigugumizi watashindwa kuwachonganisha tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mkuu wangu wa Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Joel Bendera na timu yake ya Wakuu wa Wilaya. Tumekuwa na kama miezi minane, viongozi hao wanashinda na kulala porini.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wamevamia Kilombero, wafugaji hawataki kufuatilia sera za nchi maeneo ya uwekezaji, wakulima wamebaki yatima, hawana hela, hawana uwezo, chakula cha mifugo ni mahindi na mazao yao. Niwapongeze sana zoezi hilo limekwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme tu kwamba kumekuwa na maneno mengi sana ndani ya Bunge hili kwamba kuna maeneo ambayo viongozi wakubwa wamekuja wamechukua maeneo kule Kilombero na Mvomero. Mimi nataka niwaambie tu Watanzania wote kupitia Bunge lako.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na timu yake ameshaanza kutambua yale mapori ambayo tunaita mashamba pori na mapori haya yatakuja kugaiwa upya. Sisi viongozi wa Morogoro hatuangalii pori ni la nani. Mradi pori limekaa kwa muda mrefu, halijaendelezwa, sisi tutaligawa tu.

Kwa hiyo, niseme tu wote Watanzania mnajua Mkoa wa Morogoro ni ghala la chakula, wale wote ambao wanataka kulima na kufanya uwekezaji wa kulima, nawakaribisha Morogoro. Tuache kutumia majungu kusema kuna watu wana maeneo makubwa, sasa muda umefika mashamba pori yatatambuliwa, mje muwekeze mfuate sera za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na nitaongelea Mfuko wa Vijana na Mfuko wa Wanawake. Mfuko huu wa Vijana tangu mwaka 1993 mpaka mwaka 2003 ni miaka 20 imepita. Mfuko huu wa Vijana umetengewa Shilingi bilioni moja tu na vijana wa nchi hii asilimia 68 ya Watanzania wote na vijana hawa ndio nguvukazi ya nchi. Tunataka vijana hawa walime, wafanye biashara, wafanye uwekezaji wa aina mbalimbali, vijana hawa walee watoto na wazee. Lakini Mfuko huu hakuna fedha, tutafanyaje sisi vijana? Tutakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge, Madiwani na viongozi wote tumezunguka, tumewahamasisha wananchi na vijana wajiunge na vikundi vya ujasiriamali, vijana wameitikia wito wamejiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali. Lakini fedha hakuna! Tukienda huko kwenye Majimbo na kwenye Mikoa yetu vijana wanatuuliza, tumeshajiunga; sasa mtatusaidiaje? Vijana wametoka kwenye familia za kimaskini, wanamiliki elimu yao waliyopewa ya ujasiriamali au vyeti vyao vya Vyuo Vikuu tu.

Mheshimiwa Spika, tunaona kwamba kila mwaka kuna vijana zaidi ya laki tano wanamaliza elimu ya Vyuo Vikuu, wameanzisha Makampuni yao, lakini wanashindwa kushindana na soko la sasa. Mitaji inayotakiwa ni mikubwa, lakini tumeiona Serikali yetu inatenga mabilioni ya fedha, kwa mfano kuna Shilingi bilioni 440 zimetengwa kwenda kuwanunulia watu wenye kaya maskini chakula na kuwapa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umaskini hautakwisha tukiwapa watu hela mkononi. Tuchukue hizi pesa tukawape vijana, tuwafanye vijana waweke dhamana

vyeti vyao hivyo walivyomalizia Vyuo Vikuu. Wakopesheke! Tunapata kigugumizi cha nini? Vijana wamekopa hela zetu, kila siku Waziri wa Elimu analalamika hapa vijana hawarejeshi mikopo yao. Watarudisha na nini? Hela hakuna, wametoka kwenye familia duni? Serikali inapeleka pesa kwenye nyumba za watu maskini huko. Hebu tuangalie jinsi ya kuwasaidia hawa vijana na hawa ndiyo asilimia 68 ya *population* ya Watanzania. Mimi naomba tuangalie upya sera zetu za uchumi.

Mheshimiwa Spika, tumeona sensa kwa sasa Watanzania ni milioni 45 na hawa wote wanategemea uzalishaji kupitia vijana. Lakini angalia ripoti ya maambukizi ya UKIMWI aliyozindua Mheshimiwa Rais. Vijana kuanzia umri wa miaka 15 mpaka miaka 45 ndiyo waathirika wakubwa wa maambukizi ya UKIMWI.

Ukiangalia ripoti ya mwaka 2012, vijana 20,449 wameathirika na madawa ya kulevya. Hawa vijana ni wengi na tena ni wale walioripoti kwenye vituo vya madawa ya kulevya. Vijana hawa wamepoteza matumaini. Tutakuwaje na Taifa lenye vijana wenye maradhi, vijana wako kwenye umaskini na tunasema kwamba uchumi wetu tuna u-*transform* kutoka kwenye uchumi wa sasa na kwenda kwenye uchumi ulioendelea. Mimi nadhani kuna haja ya kuangalia upya hili kundi la vijana tuweze kulisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TACAIDS* ndiyo waratibu wakubwa wa masuala ya UKIMWI, lakini utashangaa Shilingi bilioni 17 za mapambano dhidi ya UKIMWI ni pesa za nje. Tujiulize, vita gani unapigana silaha unaomba kwa jirani jamani? Mimi naomba tuwatendee haki *TACAIDS*, tuanzishe ule Mfuko wa maambukizi ya UKIMWI, kuwe na pesa za kuwasaidia vijana ambao ndiyo waathirika wakubwa. Taifa linateketea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mfuko unaitwa Mfuko wa Wanawake. Huu Mfuko ulianzishwa mwaka 1993 na wewe ndio ulikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Naomba unisaidie, Mfuko umekwenda wapi? Sisi Wabunge hatuna sehemu ya kusemea huu Mfuko. Sisi Wabunge wa Viti Maalum mmetunyima hela za Majimbo, basi leteni pesa kwenye Mfuko huu wa Wanawake ili sisi Wabunge wa Viti Maalum tupite kule tukasimamie huo Mfuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ukiangalia kwenye *Vote* ya bajeti kwenye Benki ya Wanawake ile *Vote* ambayo ilikuwa ndiyo ya kupitisha pesa ya Mfuko wa Wanawake imekwenda kwenye Benki ya Wanawake. Imekuaje? Nani ameleta Azimio la kutengua Azimio la Bunge la Kuanzisha Mfuko wa Wanawake na wewe ulikuwa ni Waziri?

Tunaomba Wabunge wa Viti Maalum tuambiwe Mfuko huu nani ameufifisha na kwa lengo gani mpaka pesa zinapelekwa kwenye nyumba za watu, sasa tunashindwa kuziratibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mawaziri liliridhia kwenye Baraza Na. 30 la mwaka 1993 kwamba Mfuko huu uendelee, lakini haupo. Maafisa Maendeleo ya Jamii wanawakimbia wanawake. Watakwenda kuwaambia nini?

Mheshimiwa Spika, tumeelimisha na kuhamasisha wanawake kujiunga na *SACCOS*. Wanatuambia hela ziko wapi? Nani anapeleka hizo hela? Benki ya Wanawake iko Dar es Salaam. Wanawake wa Ulanga, Kilombero, Malinyi, Mvomero, Tandahimba watafikiwa lini na ile Benki? Bora hiyo Benki

ife. Benki imekuwa ya wanawake wa Dar es Salaam tu, wanawake wengine wote Tanzania wamesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Anastazia Wambura. *(Kicheko)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia siku ya leo. Kwanza kabisa, kama walivyotangulia wenzangu na mimi naomba nitamke kabisa mapema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Malengo ya Milenia, lengo namba 1, 4, 5 na muda ukiruhusu naweza nikagusia lengo Na. 6.

Mheshimiwa Spika, lengo namba moja, sehemu ya umaskini uliokithiri, ambalo linatutaka kupunguza kwa asilimia 50 umaskini ulikithiri kufikia mwaka 2015. Hii ni changamoto kubwa sana na hasa ukizingatia kwamba hadi mwaka 2007 takwimu zinatuonyesha wazi kwamba Watanzania ambao wanapata kipato cha chini ya dola moja ilikuwa ni asilimia 33.6 na wengi wao wakiwa vijijini ambao ni asilimia 74.

Mheshimiwa Spika, napata shida sana na hili suala. Najiuliza, hivi huko vijijini kuna tatazo gani hadi wananchi wengi kiasi hiki wapate shida? Kwa sababu kilimo kiko vijijini, mifugo iko vijijini, huduma za chakula zote tunapata vijijini. Lakini ukija kuangalia barabara mijini, maji mijini, afya mijini, umeme mijini mpaka Ofisi za Halmashauri za Wilaya za Vijijini ziko mijini. Hivi MKUKUTA unawasaidiaje wanachi wa vijijini? Naiomba

Serikali sasa ielekeze nguvu zake za MKUKUTA katika maeneo ya vijijini ili tuweze kupunguza umaskini huu wa kipato Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo Na. 4 na Na. 5 ambayo nayo yanatutaka tupunguze vifo vya watoto wa chini ya miaka mitano kwa theluthi mbili itakapofika mwaka 2015 na vifo vya uzazi kwa robo tatu itakapofikia mwaka 2015. Kwa mujibu wa takwimu, ukiangalia utaona kwamba vifo vya watoto vinapungua na tunaambiwa kwamba vinapungua kwa kasi inayoridhisha. Lakini vifo vya akina mama vinapungua na watafiti wetu wanatuambia kasi ya kupungua kwa vifo hivi hairidhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini zipo tafiti pia zinazoonyesha kwamba hii hali ya kupungua kwa vifo vya watoto pamoja na akina mama siyo hali halisi ambayo inajionyesha katika maeneo mengi ya nchi yetu. Naomba nitaje mfano mmojawapo na huu unatoka katika kitabu cha Tanzania *Human Rights Reports 2010,* ukurasa wa 16.

Katika maelezo ya hawa watafiti tunaambiwa kwamba inaonekana katika Hospitali ya Mkoa wa ya Ligula kulikuwa na ongezeko la vifo vya uzazi kutoka 189 kati ya vizazi 100,000 mwaka 2004 hadi 258 kwa vizazi 100,000 mwaka 2008. Kwa hiyo, utaona kwamba hii hali halisi inapingana kabisa na takwimu ambazo tunaambiwa kwamba vifo vya uzazi vinapungua. Kwa mujibu wa utafiti tunaambiwa kwamba sababu kubwa za vifo hivi ni ukosefu au uhaba wa wataalam lakini pia ni ukosefu wa tiba za dharura au *emergence treatment. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kitabu cha *Poverty and Human Development Report 2007* ukurasa

wa 33, tunaambiwa kwamba vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara viko juu mara tatu hadi nne ikilinganishwa na Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Watafiti hawa wanashauri kwamba huduma nyingi au nguvu nyingi za Serikali zielekezwe katika maeneo haya yenye matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuiomba sana Serikali izingatie ushauri huu wa wataalam kwa sababu wametumia fedha za wananchi kufanya utafiti. Kwa hiyo, tunapopuuza ushauri wao ina maana kwamba pia tumeharibu fedha za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kujiuliza zaidi, kila mwaka tunapanga bajeti kwa ajili ya kusaidia matatizo ya afya. Lakini: Je, ni kiasi gani kinakwenda kusaidia akina mama na watoto? Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuhakikishe kwamba hili tatizo linafika mwisho wake na litakapofika 2015, basi kweli tuwe tumepunguza vifo hivi vya akina mama na watoto kwa kiwango ambacho kinatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze sasa kwenye maeneo ya Mkoa wa Mtwara, maeneo machache ambayo nilipata taarifa zake kwa kufika mwenyewe mwezi Januari mwaka huu, 2013. Mahuta Tandahimba, ni Kata ambayo ina Kituo cha Afya, tunaishukuru sana Serikali na wananchi wanaishukuru sana Serikali. Kituo cha Afya kimejengwa vizuri sana, kina nyumba ya Daktari na kina-*theater*. Lakini tatizo ni kwamba wanaishi popo. Hakuna wataalam! Naomba wataalam wapelekwe katika Kituo cha Afya cha Mahuta Tandahimba, Mahuta.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna Kata moja ya Kwanyama huko huko Tandahimba, huduma za afya

wanazipata katika Kata ya Namikupa. Ni mlima mrefu sana, kilomita 27 akina mama wajawazito hawawezi kupanda ule mlima. Kwa hiyo, wanalazimika wengi kujifungulia nyumbani na wengi wanapoteza maisha. Naomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliangalie kwa karibu sana hili suala la kupeleka Kituo cha Afya katika Kata ya Kwanyama.

Mheshimiwa Spika, mwezi huo huo Januari kulikuwa na taarifa kwamba katika Hospitali ya Tandahimba hakukuwa na fungu la vifaa tiba mpaka kufikia mwezi Desemba kwa miaka mitano, na akina mama wanalazimika kununua vifaa tiba katika maduka ya madawa. Naiomba Serikali izingatie kupeleka vifaa tiba kwa wakati.

Vilevile Hospitali ya Ligula. *Ultra Sound machine* ambayo iko kwenye *labour ward* Ligula pale inatumika na wagonjwa wote kiasi kwamba akina mama wajawazito wanachelewa kupimwa na inapelekea kupoteza maisha au watoto wachanga kufariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa lengo la Milenia Na. 7 ambalo linahitaji tuhifadhi mazingira na kipimo kimojawapo ni kupunguza matumizi ya mkaa na kuni. Mkoa wa Mtwara sasa hivi umeamka. Kuna maendeleo makubwa ya utafiti wa gesi na mafuta na viwanda, kwa mfano kiwanda cha Dangote, na akina mama wengi wanajitokeza kufanya shughuli za lishe. Hii inaonyesha kwamba mahitaji ya mkaa yataongezeka sana. Akina mama wale wamenituma, Serikali iwakopeshe majiko ya gesi na mitungi ya gesi ili kupunguza matatizo ya uharibifu wa mazingira katokana na matumizi ya mkaa na kuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali sasa iandae *mechanism* ambayo itawezesha kupima

vizuri utekelezaji wa malengo ya milenia ili kusudi itakapofika 2015 tuweze kujua ni kiasi gani tumeweza kuyatekeleza. Lakini baadaye tena nitachangia kwa maandishi mambo mengi ambayo tumeyapata kutoka katika kongamano ambalo limefanyika mwisho wa wiki hii. Akina mama wana kilio kikubwa sana kwenye maeneo ya maji. Kuna mambo yanayotisha sana, sehemu za afya, elimu, kilimo; wananyanyasika na nitachangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mawaziri na Watendaji wanaomsaidia katika ofisi yake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka tatizo kubwa linalowakabili wananchi wa Simanjiro la ukosefu wa maji kwa ajili ya watu na mifugo yao.

Naomba Serikali sasa itueleze ufumbuzi wa mabishano ya nani atatekeleza mradi wa maji kutoka Mto Pangani na Ruvu kwenda Orkesument (Makao Makuu ya Wilaya ya Semanjiro). Haiingii akilini kuacha kuchukua fedha kwa mtu mwenye fedha mkononi badala yake tunaambiwa tusubiri *BADEA* ilhali inaeleweka kuwa kwa wakati huu hawana fedha.

Naomba Waziri Mkuu atukutanishe na Wizara ya Maji na Hazina ili tujue tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, naomba Serikali imalize mchakato wa kugawa eneo la Kitalu C kwenye machimbo ya madini ya Vito *(Tanzanite)* Mererani. Aidha, nashauri ubia uwe kati ya mwekezaji na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kupitia kampuni yake. Nampongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa uwelewa na dhamira yake njema katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Simanjiro katika msimu huu wa mvua tumepata mvua kubwa iliyopelekea kubomoka kwa mabwawa yanayotegemewa na wananchi kiasi kwamba nawasilisha maombi ya fedha za dharura za kukarabati mabwawa haya. Mabwawa yaliyoathiriwa na mvua ni pamoja na Bwawa la Laangai, Bwawa la Irperera la Kijiji cha Lerumo, Bwawa la Lengumuma la Kijiji cha Lerumo, Bwawa la Narakano kijiji cha Narakamo na kukarabati Bwawa la Leramo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa kwa miaka miwili mfululizo Wilaya ilitengewa sh. 1,800,000,000/= kwenye bajeti bila kupelekewa hata shilingi moja. Naomba niikumbushe Serikali wakati wa ziara ya Rais 2010, aliahidi kuwa mwezi unaofuata fedha hizo zitakuwa zimefika Simanjiro ili kupunguza makali ya ukosefu wa maji Wilayani Simanjiro. Swali langu Serikali itatuondolea lini kero hii?

Mheshimiwa Spika, barabara ya *KIA*-Mererani ni ahadi ya muda mrefu ya Serikali ya awamu ya tatu na awamu hii pia. Madhali zabuni ya barabara hii imekwishatangazwa na kufunguliwa, nashauri sasa Mkandarasi apewe fedha ili kazi ianze haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Waziri Mkuu kuwa, wananchi wa Simanjiro wanasubiri kifuta machozi na fidia ya mifugo yao iliyokufa wakati

wa ukame kama ilivyofanywa Wilaya ya Monduli, Longido na Ngorongoro. Naomba mtukumbuke.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, natambua kazi kubwa zinazofanywa na ofisi ya Waziri Mkuu, lakini ningependa nipate ufafanuzi wa masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya watu takribani 4.3 milioni, lakini Mkoa huu una Wilaya tatu tu na Mikoa mingine ina idadi ndogo ya watu, lakini Wilaya zake ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, iwapo Wizara ya Mambo ya Ndani wameweka Dar es Salaam kuwa kanda maalum na Wilaya zote kutambua kama Mikoa. Wizara ya Nishati na Madini *(TANESCO)* nao wamefuata mfumo wa kutambua Wilaya kama Mikoa, Wizara ya Fedha *(TRA)* pia wamefuata mfumo huo huo. Je, iweje leo Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa zisikate shauri Wilaya tatu kuwa Mikoa na kuongeza Wilaya nyingine kupata ufanisi na utendaji wa kazi ulio bora. Lakini iwapo Mikoa itashindikana basi Mkoa wa Dar es Salaam uongezwe Wilaya na Majimbo yote yawe ni Wilaya.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watu imeongezeka lakini bajeti za fedha za Mkoa kasma ni ile ile. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambao ni Kanda Maalum na Wakuu wake wa Wilaya, je, wanapewa posho au mshahara maalum unaoendana na kazi kubwa waliyonayo na idadi kubwa ya watu walionao na wingi wa matukio ya mlipuko yanayojitokeza waliyonayo?

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii tena kuomba kupata maelezo jinsi gani Serikali

itausaidia Mkoa wa Dar es Salaam katika mpango mzima wa uboreshaji wa barabara miundombinu ya maji taka na maji safi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hali ni mbaya sana maji machafu yamezagaa mitaani.

Mheshimiwa Spika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, iwaangalie wananchi wa Kata ya Kwembe, eneo la Mloganzila bado kuna mgogoro wa wananchi na Serikali, utatuliwe tupate maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi waliobomolewa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara. Wataalam wanakwenda kuhakiki na kufanya utafiti ikiwemo na Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi, taarifa imeonesha wazi wananchi wale walistahili fidia kwa mujibu wa sheria kwani barabara imewafuata na walifanyiwa tathimini badala yake walilipwa wachache na wengine walilipwa matapeli si wenye nyumba husika na wengine waligundulika na hata fedha hawakuwahi kuzichukua kabisa majina yao hayajasainiwa. Je, fedha hizo zimekwenda wapi na zimewekwa akaunti gani? Je Serikali inafikiria nini kuhusu wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe maelezo ya kina kwani Vyama vya Siasa ndio agenda yao kuu Mbagala, Mtoni na Kongowe kwamba, Serikali imewadhulumu, hali ambayo inaweza kuleta machafuko na ukosefu wa amani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia na kuitakia mafanikio mema Ofisi ya Waziri Mkuu na bajeti njema 2013/2014.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naanza na barabara za vijijini na vituo vya afya. Kwa namna ya pekee, naipongeza sana Serikali kwa kuendelea kujenga barabara na kufanya ukarabati pia

ujenzi wa zahanati. Ujenzi huu utachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kasi ya huduma muhimu za wananchi hasa wale walio vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala hili mara nyingi Serikali imekuwa ikiwashirikisha wananchi kuchangia ujenzi au kuwataka wananchi kuchangia ujenzi kupita nguvu zao wenyewe kwanza, baadaye ndiyo Serikali inatoa fedha kwa ajili ya uendelezaji.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha ni kwamba kuna baadhi ya vijiji wameamua kujitolea nguvu zao kwa kuanzisha majengo kama hayo kutokana na wanavyopata tabu ya kufuata vituo vya afya masafa marefu sana. Serikali huchukua karibuni miaka mitatu kwa kufanya uchelewashaji wa kuvifungua na kuweka wahudumu wa afya kwa mantiki ya kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini Serikali imeweka utaratibu wa namna hiyo wakati katika kuendeleza ujenzi wa vituo hivyo, Serikali inatoa michango yake ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya elimu nchini, Watanzania walio wengi tumeguswa sana na kitendo cha wanafunzi wa kidato cha nne kufeli kwa kiwango kikubwa.

Suala hili ingawa Serikali imeshaunda Tume ili kuchunguza suala hili, lakini pamoja na kuunda Tume hiyo, naomba nieleze kwamba, ingawa kuna baadhi ya wanafunzi wanafanya vibaya mitihani yao lakini tusibweteke na hilo pia wapo Walimu wanaochangia kwa kiasi kikubwa kutofaulu wanafunzi kwa madai kwamba kiasi cha fedha wanacholipwa na Serikali yaani mishahara ni midogo mno haifanani na ngazi zao, au kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, pili Walimu hao hujifanya kutokuwa na muda mzuri wa kufundisha darasani kama inavyostahili na badala yake Mwalimu anapoingia darasani hachukui muda hutoka na kwenda kwenye mazungumzo au haingii darasani na kusema wanafunzi wanasumbua au ni wengi darasani.

Mheshimiwa Spika, Walimu kutumia muda wa makusanyo ya fedha za maboresho kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, michango isiyofahamika kisheria shuleni kwa kuwachangisha wanafunzi darasani kila mwezi kwa kisingizio cha kulipa mshahara wa walinzi wa shule.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize shuleni kuna wanafunzi 300 kila darasani michango inayotozwa ni kiwango cha shilingi 1,200/= kila mwanafunzi kwa mwezi, mbali ya fedha hizo, sh. 500 kila mwanafunzi za maboresho, hivi kwa shule yenye vyumba 15. Walimu hao wanakusanya hela kiasi gani na wanafunzi na mlinzi wanamlipa kiasi gani? Huu si utaratibu mzuri ni vyema wakaainisha fedha hiyo inakwenda wapi? Hata tungeambiwa kama inajengwa au inafanyiwa ukarabati basi tungeridhika lakini mlinzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu UKIMWI, niungane na maoni ya Kamati kwa kuitaka Serikali kuanzisha Mfuko wa UKIMWI nchini, utasaidia kwa kiwango kikubwa na hata wale wafadhili waliojitoa wanaweza kuona kwamba sasa ipo haja ya kuendelea kuchangia kama ilivyokuwa hapo zamani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzishwa Mfuko huo, Serikali nayo iweke usimamizi ulio bora wa matumizi ya fedha za Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madawa ya kulevya, Serikali inafahamu kwamba, kuna changamoto kubwa kwa watumishi wa Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya kwamba baadhi ya wakati pale wanapokamata madawa, mpaka kufikia katika vyombo vya sheria, madawa yale hubadilika na kuwa kitu kingine. Hivyo, hupelekea watumishi hao kuwa wanyonge na kuona kwamba kazi wanayoifanya haina tija mara nyingine kutokuwa na imani na kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, basi naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuleta sheria Bungeni itakavyowapa Tume mamlaka ya kukamata wenyewe na kuwapeleka Mahakamani watuhumiwa yaani wapewe mamlaka kama waliyopewa TAKUKURU. Hili litasaidia kwa kiwango kikubwa kuonekana matunda kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, katika mchango huu nitajielekeza kwenye matatizo mbalimbali yanayolikabili Jimbo la Bukombe.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu bado inakabiliwa na matatizo lukuki, kuna upungufu wa Walimu katika shule za msingi na sekondari, kuna upungufu wa vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu (shule nyingine hazina nyumba hata moja), shule nyingi za msingi hazina matundu ya vyoo ya kutosha, tatizo la madawati ni kubwa, kuna upungufu wa takriban madawati 9,000. Ari ya Walimu imeshuka sana kutokana na Serikali kutosikiliza madai yao mbalimbali ambayo ni pamoja na kuboreshwa mazingira ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika shule zote tatizo la vifaa (vitabu na kadhalika) ni kubwa, katika shule za sekondari kuna tatizo la maabara. Zipo zile ambazo hazina vyumba vya maabara na zile zenye vyumba hivyo, hazina vifaa.

Mheshimiwa Spika, swali, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kutatua matatizo hayo yahusuyo:-

Vyumba vya maabara, vifaa vya maabara katika shule za sekondari, vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu. Inafaa Serikali ijitahidi ichangie katika maeneo hayo, wananchi wakiachiwa hawataweza kwa sababu uwezo wao kifedha ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, hali ya hospitali ya Wilaya ni mbaya, malalamiko ya wananchi kuhusu hali hiyo ni mengi. Tatizo ni la siku nyingi na hata mwaka jana nililisemea.

Matatizo makubwa ni kwamba, hakuna dawa, huduma ni mbovu, wagonjwa wanalalamika kuwa huchelewa kuhudumiwa, kuna rushwa, uongozi ni mbovu, Mganga Mkuu na wasaidizi wake wanalalamikiwa kwa muda mrefu, lakini hatua zimechelewa kuchukuliwa na watumishi wana kauli mbaya.

Mheshimiwa Spika, swali, Serikali lini inachukua hatua za kubadilisha uongozi wa hospitali ili hali ya hospitali iwe na mabadiliko chanya?

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji; maeneo mengi ya Wilaya ya Bukombe hayana maji safi na salama. Matatizo yaliyopo ni hakuna Bodi ya Maji; fedha inapotengwa (ya wafadhili au ya ndani) inadaiwa

mchakato wa wazabuni huingiliwa na ufisadi wa asilimia kumi kutoka kwa Mkuu wa Idara hivyo, miradi haikamiliki.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kwamba, fedha zinapotengwa kwa mradi mfano mradi wa kilimahewa mradi hautekelezwi kwa taarifa kwamba uko nje ya wakati na fedha inarudishwa Hazina.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana fedha ya mradi wa maji Kilimahewa ilibadilishwa matumizi na kuhamishiwa kwenye mradi wa umwagiliaji wa Bugelenga bila kibali cha Waziri mwenye dhamana. Je, huu si ukiukaji wa taratibu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ardhi; idara ya ardhi ni kichocheo kikubwa cha migogoro baina ya wananchi na Serikali. Afisa Mipango Miji na maafisa wengine ni tatizo kubwa kwani wanapima maeneo na kuyauza bila kufuata taratibu. Serikali iitupie jicho idara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makusanyo ya maduhuli; watendaji wahusika hawana mpango madhubuti wa ukusanyaji kodi. Hadi sasa ni 20% ya makusanyo yaliyotarajiwa kukusanywa ndiyo yaliyokusanywa. Kwa kasi hii mipango karibu yote itategemea fedha ya Serikali Kuu. Halmashauri isaidiwe wataalam wenye weledi wa ukusanyaji wa maduhuli ili mapato ya Halmashauri yaongezeke.

Mheshimiwa Spika, barabara kwa ujumla; barabara za vijijini haziridhishi, nyingine ni mbovu sana, ila matatizo makubwa yako katika maeneo yafuatayo:-

Barabara kutoka Namonge hadi Iyamchele, kunahitajika daraja la uhakika kwenye Mto Mlele.

Daraja kati ya Busonzo na Nakayenze, Daraja kati ya Msonga na Ludeba.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, naishukuru na kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jitihada za kutekeleza ahadi za CCM zilizoko katika Ilani yake. Serikali Kuu na watendaji wake wakuu yaani *DC* na *RC* inafanya kazi nzuri.

Wilayani Tanga barabara ya Tanga – Horohoro imekamilika na kuzinduliwa tarehe 13/4/2013, hospitali ya Wilaya inajengwa na kadhalika. Naomba mkazo uwekwe katika kuimalizia ujenzi hospitali hii na pia ujenzi wa barabara ya Tanga- Pangani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, utendaji wa Halmashauri ya Jiji hauridhishi. Matatizo ni mengi kuyataja yote hapa, lakini yapo.

Ushauri wangu, Wizara iunde Kamati ya kuchunguza na kutafutia utatuzi wa matatizo ya Halmashauri hii kama uthibitisho kwa Halmashauri nyingine Madiwani wote wa CCM wako tayari kushirikiana na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mfuko wa Uwekezaji wa *PPP* uharakishwe. Ukurasa wa 22 wa hotuba ya Waziri Mkuu bado inaongelea matayarisho ya uwekezaji chini ya *PPP*. Miaka mitatu sasa tangu Sheria ya *PPP* ipitishwe na Bunge lako.

Kwa mwenendo huu hatutafaidika kikamilifu kwa mfumo huu wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, amani ya nchi yetu inavurugwa na mambo mengi ya kijamii, ya kikabila na ya kidini. Serikali sio tu ikemee bali ishughulikie kukomesha kabisa na kwa nguvu zote:-

(a) Uuaji wa wenye ugonjwa wa ngozi;

(b) Uuaji wa wezi wadogowadogo kwa wananchi kujichukulia sheria mikononi mwao; na

(c) Chokochoko za kidini ambapo zinaibuka dini mpya ambazo zinaingilia taratibu za ibada za dini nyingine, kwa mfano muadhini wa kiislamu kwa swala ya alfajiri anaingiliwa na hotuba ya *cassette* ya dini isiyojulikana ambayo inahakikisha kukashifu waitwao misikitini na kujitahidi adhana isiwafikie waumini wa dini ya kiislamu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, rushwa imeongelewa kwenye ukurasa wa 70 wa hotuba ya Waziri Mkuu kwa *paragraph* moja tu. Rushwa ni janga la Taifa, rushwa ni adui pekee wa Taifa letu, kuichukia rushwa haitoshi na kupiga kelele kuhusu rushwa haivitoshi. Serikali katika ngazi ya juu sana itabidi ionyshe kwa vitendo vya dhati kulishughulikia tatizo hili kama kipaumbele cha kwanza na kama adui wa pekee kwa sasa kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba uthibitisho kamili kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa Serikali inaichukulia rushwa kuwa ndiyo adui wetu wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze bajeti ya uendeshaji wa hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala kwani hospitali zimepandishwa hadhi lakini bajeti ni ile ile tu. Tunaomba Serikali iangalie bajeti hiyo na umuhimu wa huduma inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watoto wanaozaliwa katika hospitali hizi ni 13,000 kwa kila miezi mitatu, idadi

hiyo ni kubwa na huduma inayotakiwa kutolewa ni kubwa, vifaa vinavyotakiwa ni vingi, hivyo tuongezewe fedha za uendeshaji wa hospitali na hasa Kitengo cha Afya ya Mama na Mtoto.

Mheshimiwa Spika, madeni ya Walimu na watendaji wa Serikali yafanyiwe kazi ya kulipwa, lakini pia Serikali isimamie madeni mengine yasiongezeke kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, Walimu walipwe fedha za likizo kwa wakati na *promotion* zao kwa wakati, Wakurugenzi wasirundike madeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za uhamisho kwa wafanyakazi, kama Serikali haina fedha isitoe uhamisho, wanaongeza madeni kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Serikali katika Wizara; Mawaziri na Manaibu wasaidiwe kazi kwani mambo mengine ni madogo madogo, lakini unakwenda Wizarani mpaka ukutane na Waziri au Naibu, idara za Serikali ziwajibike na ziwe na majibu kwani idara hizi zingefanya vizuri kwa kuwa Wizara nyingi zingepungua, lakini mara nyingi majibu hakuna au ya usumbufu mkubwa (mabadiliko ni muhimu).

Mheshimiwa Spika, mbona bajeti hazitekelezeki, barabara zilizopitishwa bajeti ya mwaka jana bado hazijajengwa kabisa na hatujui nini kimetokea mfano barabara ya Kawawa ilipitisha na fidia zake mpaka sasa fidia imetolewa kwa wachache tu na sioni mwendelezo. Barabara ya Nzasa- Kilungule- Buza, kipande kimewekwa kifusi cha mawe hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara Jijini Dar es Slaam umezusha changamoto nyingi kwa wananchi.

Tunaomba Wakandarasi wawe makini, mafuriko yamekuwa makubwa na tunahatarisha maisha ya wakazi katika maeneo ya Magomeni, Manzese mpaka Kimara.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuishauri Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi. Suala zima la ujenzi wa barabara. Serikali inajitahidi sana kutoa fedha kwa ujenzi wa barabara, fedha ni nyingi zinatumika lakini barabara zinazojengwa sio imara. Kwa kweli tunachakachukuliwa na wakandarasi mbona barabara za China na Japan ni nzuri sana na wakandarasi wa nje wanatoka huko?

Mheshimiwa Spika, tunahitaji *operation* kabambe na utafiti kuona fedha zinazotolewa na barabara zinazojengwa ni sahihi? Ikiwezekana Waziri Mkuu aunde Tume ya Kuchunguza Barabara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO**: Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 14 katika hotuba ya Waziri Mkuu kumezungumziwa suala la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hivyo baada ya viongozi kukaa na kujadili ni namna gani na njia zipi ambazo zitaweza kuuboresha Muungano, wako wale ambao wameanza kuupiga mateke bila ya kuzingatia kasoro ambazo zimo kwenye Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Muungano wetu ni muundo wenyewe wa Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar juu ya kutozingatia maamuzi ya wananchi wa pande mbili za Muungano. Hata hivyo, ni matumaini yangu kwamba, kwa kuwa tunaelekea kwenye Bunge

la Katiba mwezi Novemba mwaka huu na baadaye kuelekea kwenye kura ya maoni maamuzi ya wananchi juu ya mfumo gani wa Muungano wanaoutaka utapatikana. Huo utakuwa ni Muungano wa nchi na nchi, Muungano wa watu na watu na wala sio Muungano wa nchi moja wala mtu na mtu.

Mheshimiwa Spika, licha ya kwamba waasisi wa Muungano huu wa Tanganyika na Zanzibar hawakuwa wapumbavu wala wenye akili taahira hawakujua wanalolifanya, waasisi wa Muungano huu walielewa ukubwa wa Tanganyika na pia udogo wa Zanzibar. Waasisi wa Muungano huu walijua pia uwepo wa idadi kubwa ya watu walioko Tanganyika na idadi ndogo ya watu walioko Zanzibar, lakini leo anapotokea mtu au watu wakatumia vyombo vya habari au hata Bunge lako Tukufu kuwakejeli, kuwafedhuli, kuwakebehi na kuwadharau Wazanzibari na Zanzibar kwa sababu ya idadi yao ndogo au kwa sababu ya udogo wa eneo, huo ni umamluki ambao unatumiwa kuvuruga Muungano na pia ni upungufu wa akili wa kutofahamu kwamba Muungano huu ni wa nchi mbili huru. Ni budi watu wa aina hii wakemewe kwani wanatengeneza mgogoro mwingine wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, suala zima la kero za Muungano halijatolewa ufafanuzi ni kwa kiasi gani kero hizo zimepatiwa ufumbuzi unaofaa. Tunaomba tupatiwe maelezo ni kwa kiasi gani SMT imekubali kuiachia Zanzibar masuala yake ya Mafuta na Gesi kama ambavyo tumelidai ili kukuza uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, suala la mazungumzo ya utatuzi wa kero za Muungano yamekuwa ya muda mrefu kwa nini mazungumzo hayo hayatoi suluhisho na mara nyingi majibu yake yanafunikwa funikwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ugaidi; kumetokea hujuma nyingi na hata mauaji upande wa Tanzania Bara na upande wa Tanzania Visiwani. Mfano hujuma aliyofanyiwa Dokta Ulimboka, Mwandishi wa Habari Kibanda, hujuma aliyofanyiwa Sheikh Shazil Soraga, mauaji yaliyofanyika ya *RPC* yaliyotokea Mwanza, yote haya hayajawahi kutolewa kauli hata siku moja na Waziri yeyote kwa Tanzania Bara au Tanzania ina mtandao wa ugaidi, lakini tukio la kifo cha Padri kule Zanzibar, Waziri alithubutu kutoa kauli kwamba Zanzibar ina ugaidi, kuna tofauti gani kati ya aliyofanyiwa *RPC* Mwanza na yale aliyofanyiwa Padri Zanzibar.

Hivyo kweli ndugu zetu washirika wa Muungano wetu mnapotoa kauli kama hizo kutaka kuiangamiza Zanzibar kiuchumi na kimaendeleo na kutafuta namna ya kuikosesha misaada kwa jumuiya za Kimataifa mnakuwa na malengo gani? Hivyo, Wazanzibari tutaamini kiasi gani kama ndugu zetu mnajenga amani na imani dhidi ya Zanzibar na Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo kwanza, sera hii imefeli kwa asilimia mia moja, hivyo ili kufikia malengo ya angalau asilimia hamsini, basi kwanza tuimarishe vyanzo vya maji, tuweke tamko la sera ya maji kwanza.

Mheshimiwa Spika, asilimia 70% ya wakulima wetu wanalima kwa kutumia vijembe vya mkono, kilimo ambacho hakina tija. Walioasisi sera ya kilimo kwanza hawakufanya utafiti wa kina kwani hawakuangalia zana zinazotumika katika kukuza kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, endapo Tanzania itaanzisha sera ya maji kwanza, ikubali kujenga mabwawa ya kina kirefu yatakayoweza kuhifadhi maji kwa wingi jambo ambalo litaleta maendeleo ya uhakika. Sera hii italeta maji ya uhakika mijini na vijijini. Itasaidia kupatikana

umeme wa uhakika, tutakuwa na utunzaji bora wa miji, tutakuwa na utunzaji bora wa mazingira mijini na vijijini, tutaweza kusimamia kilimo bora na cha kisasa lakini katika hili ni lazima na zana za kilimo ziwe za kisasa. Tutakuza na kuboresha uoto wa kijani uliopo nchini mwetu ambao utaboresha misitu na kuweza kuvutia watalii na kuliongezea mapato Taifa la Tanzania.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Ofisi ya Waziri Mkuu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, umeme Wilayani kibondo, napenda kuiomba Serikali ipeleke umeme katika Tarafa ya Mabamba yenye wananchi zaidi ya 150,000 wenye uwezo wa kutumia umeme. Pia eneo hili ni muhimu kwa uchumi wa Taifa kwani biashara za Kimataifa hufanyika hapo kati ya Tanzania na Burundi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna sababu zote za kupeleka umeme huko kwani Wizara ya Ujenzi imetega pia fedha za usanifu wa barabara ya kwenda huko. Naomba sana sana kwa umuhimu wa eneo hilo kiuchumi, kihuduma na kibiashara tupeleke umeme.

Mheshimiwa Spika, barabara Wilayani Kibondo; Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara za lami Kibondo Mjini na ahadi hii iko kwenye kitabu cha orodha ya ahadi za Mheshimiwa Rais. Pili, ni barabara ya Nyakanazi, Kibondo hadi Kidahwe yenye urefu wa kilomita 310. Hizi barabara ndio msingi wa uchumi wa Mkoa wa Kigoma kwani inaunganisha Wilaya na Majimbo yote Mkoani Kigoma na kadhalika.

Pia kiungo cha nchi za Burundi, Rwanda, Kongo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, elimu Wilayani Kibondo inashuka na ni ndio Wilaya ya mwisho Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari Kibondo, shule hii ni miongoni mwa shule maalum za wasichana zilizokuwa zinachukua watoto kidato cha kwanza hadi cha sita lakini baada ya sekondari kutangaza shule hizi kubaki na kidato cha tano na sita, shule zimebaki bila watoto wakati zina madarasa ya kutosha, nyumba za Walimu, maabara na kadhalika.

Hivyo, naomba Serikali itumie majengo haya na mabweni yanayotumiwa na popo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, naiomba Serikali inipatie majibu ni lini vijiji ambavyo havina zahanati katika Wilaya ya Kibondo vitapatiwa huduma hii ya afya. Mfano, Kijiji cha Kigina, Magarama, Nyarulanga, Nyakabosi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, huduma ya simu na mitandao Kibondo, napenda kuiomba Serikali kupeleka huduma ya simu kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote katika Wilaya ya Kibondo ambayo zaidi ya wananchi laki mbili hawapati huduma ya simu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya Serikali kwa nini imehamasisha wakulima walime na wamepata mpunga (mazao ya kutosha). Kwa makusudi Serikali imeleta mchele kutoka nje ya nchi na kuujaza sokoni na matokeo yake mkulima amekosa soko la mchele. Mfano halisi ni wakulima wa mpunga wa Kilombero wameshindwa kuuza mpunga (mchele) hivyo

kushindwa kabisa kujikimu kimaisha. Hivyo napenda Serikali ilete majibu ya kuwakwamua wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali itoe majibu kwa waathirika wa mafuriko ya Kilosa zaidi ya kaya 8000 na ahadi ya Serikali, lakini hadi leo hawajasaidiwa ingawa hotuba ya Waziri Mkuu amewazungumzia waathirika wa Mabwepande na Gongo la Mboto.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu wizi wa madini ya shaba tani 200 kwa mujibu wa gazeti la Mtanzania, wizi uliofanywa na Wachina baadhi ambao sasa wamekwenda Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata maelezo ya kina kuhusu uchimbaji wa urani huko Namtumbo, lakini kwenye hotuba ya Waziri Mkuu haikuzungumzia chochote. Uchimbaji wa urani ni hatari kwa nchi yetu ambapo hakuna sera wala tathimini ya kina iliyofanyika na kutolewa kwa Watanzania kwa faida na madhara yatakayopatikana. Napendekeza uchimbaji wa urani usitishwe hadi tukubaliane kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo sugu pamoja na kuzungumzia maji kwa Jiji la Dar es Salaam, lakini Serikali haijaeleza kuhusu Bwawa la Kidunda Morogoro na malipo ya wananchi wa eneo la kijiji ambapo wamezuiwa kufanya maendeleo yoyote kwa kuwa watahamishwa. Je, nini hatima ya wananchi hao na lini watalipwa na kupatiwa maeneo mengine ya kuendeleza maisha yao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji wa *TAZARA*, je nini hatma ya wastaafu wa Shirika la *TAZARA,* lini watalipwa?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya Mikumi Ifakara yenye urefu wa kilomita 103, kwa uelewa wangu barabara yenye tatizo kubwa katika Wilaya ya Kilombero ni barabara ya Kidatu hadi Mlimba ya kilomita 225. Sasa napenda kujua hizo kilomita 103 ni barabara kutoka wapi mpaka wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji Mji wa Ifakara ambao unaongezeka kukua, Halmashauri ilishatuma maombi ya fedha kwa mradi wa kiburubuta yakihusu kuendeleza upembuzi ambao ulishatumia pesa nyingi pia mchanganuo wa mradi huo, lakini mpaka leo hakuna fedha iliyopelekwa. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ina Kata 23 na Vijiji 97, lakini ina matatizo makubwa ya miundombinu, barabara hazipitiki na kusababisha gharama kubwa za usafiri na usafirishaji mazao.

Mheshimiwa Spika, ukosekanaji wa umeme katika Tarafa nzima ya Mngeta ambapo ndiko kunakozalishwa mpunga, kokoa, mahindi na ndizi kwa wingi. Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya umeme ili wananchi wapate maendeleo?

Mheshimiwa Spika, elimu ya sekondari na msingi, huwezi kuamini katika shule ya msingi Mtyangimbole na shule ya msingi Kidete katika Kata ya Mngeta wapo wanafunzi wa darasa la tano, tatu na la pili, wanaosoma chini ya miti kutokana na Serikali kushindwa kupeleka pesa za kumalizia madarasa na hata madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yamebomoka. Matundu ya vyoo mawili, nyumba za Walimu hakuna, watoto takribani 40 hadi darasa la nne hawajui kusoma na kuandika. Nataka majibu ya Serikali kwa nini hampeleki fedha kama mlivyoahidi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu pembejeo; pembejeo bado ni tatizo kubwa kwa wakulima wa Wilaya ya Kilombero kwani hazikufika kwa wakati, hivyo mpango wa ugawaji urekebishwe mapema.

Mheshimiwa Spika, suala la mfumko wa bei, Serikali imetoa majibu mepesi kwa maswali magumu. Kitendo cha Serikali kuagiza mchele nje ya nchi na kuujaza sokoni, kweli wananchi wa Kilombero wameona hilo ni tendo la kuwahujumu.

Taarifa halisi ni kwamba, hata Benki zinazokopesha wakulima wameshangaa kwani wateja wao wengi ambao ni wakulima waliowakopesha kwa matumaini wakivuna watauza na kurejesha mikopo, wamekwama kutokana na kuporomoka kwa bei ya mpunga. Hivyo Serikali iokoe wananchi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo, Kiwanda cha Sukari Kilombero na Kiwanda kipya cha Konyagi Kilombero. Wakulima wanapunjwa wanapouza miwa kwa mwekezaji kwa kisingizio kuwa sukari imejaa kutokana na kuingizwa sukari toka nje ya nchi na mwekezaji kukosa soko. Hivyo ameamua kuwapunja bei ya kuuzia miwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiwanda cha Konyagi mwekezaji ameajiri wageni wengi kutoka Bara la Asia kwa kazi ambazo Watanzania wanaziweza, hivyo Serikali iingilie kati suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi; migogoro ya ardhi nchini ni kama wimbo wa Taifa, nachukua mfano Mkoa wa Morogoro, Serikali ni vema ikatekeleza kwa haraka suala la utambuzi wa mashamba na mapori na uwazi uwepo katika umiliki na ugawaji upya wa mapori na mashamba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekaji mipaka ya Ramsa, Wilaya ya Kilombero na Ulanga; pamoja na jitihada za uwekaji mipaka ya Ramsa, lakini kumekuwa na matatizo kwani katika uwekaji wa mkuruzo watendaji waliotoka Makao Makuu hawakuwashirikisha hata watendaji wa ardhi katika Wilaya, pia wananchi na viongozi katika vijiji na ushahidi upo.

Mheshimiwa Spika, kingine, pamoja na Serikali kusema wameondoa mifugo hadi sasa bado lipo tatizo kubwa la mifugo ambao ni kero na linasababishwa na rushwa kwa baadhi ya viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, zoezi zima la uondoaji mifugo wasio na maeneo ya malisho Bonde la Kilombero na Ulanga lishirikishe wenyeji na sio nguvu kubwa ya Serikali kwa kutumia gharama kubwa.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote katika ofisi yake, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, napenda kuchangia hotuba hii kwa nia ya kuboresha kama ifuatavyo:-

Kilimo Kwanza, hii dhana ya kilimo kwanza ni nzuri na kama itafanikiwa wakulima watapiga hatua kubwa ya maendeleo. Napenda kushauri Serikali ifanye maamuzi magumu ya kuwapatia wananchi matrekta makubwa katika ngazi ya kijiji hasa katika mikoa ile ambayo inaonesha uwezo wa kuzalisha, lakini tatizo ni ukosefu wa matrekta.

Mheshimiwa Spika, Morogoro imepewa jukumu la kuwa ghala la chakula. Lakini uwezo huo

utawezekana kama Morogoro watapata matrekta ya kukopa kwa masharti nafuu, jembe la mkono linatuchosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi; imeelekea kwamba, Serikali imeweka nguvu nyingi kwenye *Trunk roads* na madaraja yake na siyo kuzisaidia Halmashauri katika ujenzi wa madaraja makubwa ambayo Halmashauri hazina uwezo nayo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isaidie ujenzi wa madaraja katika mito mikubwa inayopita katika maeneo ya barabara za Halmashauri, kwa mfano, daraja la Gizgiz katika Mto Mbezi na daraja la Kisanga Stendi katika Mto Ruvu.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo haya wananchi wengi wamepoteza maisha yao. Hata maendeleo ya wananchi wanaoishi ng'ambo ya mito hii wanashindwa hata kwenda hospitali hasa nyakati za mvua. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kurudisha ujenzi wa madaraja makubwa, Serikali Kuu yaani chini ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu na ufundi; naomba Serikali ione umuhimu wa kujenga Vyuo vya Ufundi *(VETA)* kwenye Wilaya ambazo hazina vyuo hivyo ili vijana wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne waweze kupata stadi ambazo zitawasaidia kujiajiri wenyewe. Pamoja na uwezo wa mafunzo ya ufundi, Serikali iwe na mipango ya kuwapatia mitaji endelevu. Ili hili liweze kufanikiwa ingekuwa jambo la busara kama Serikali itaanzisha kitengo cha kuwasaidia vijana wanaomaliza mafunzo ya *VETA* na Vyuo Vikuu waweze kubuni miradi ambayo itawaajiri wao na vijana wengine. Kitengo hiki kijihusishe pia na miradi ya kilimo, ufugaji pamoja na ufugaji wa samaki na nyuki.

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana, naomba Serikali iangalie na utekelezaji wake uanze ndani ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ndani ya Halmashauri, napenda kushauri kwamba Halmashauri zipewe mamlaka ya kuajiri watendaji hususan wa kada ya chini kama vile Watendaji wa Vijiji, Kata, Wahudumu wa Afya, Kilimo na Madereva.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kushauri kwamba Walimu, Maafisa Mifugo na Maafisa Maendeleo wasipewe ajira kama Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata. Kama inavyofanyika sasa hivi. Walimu hawatoshelezi, hivyo wasipewe wajibu mwingine.

Mheshimiwa spika, kuhusu maslahi ya watendaji; naomba Serikali ilipe marupurupu na maslahi ya Walimu kwani wamekata tamaa. Aidha, matatizo ya kimaslahi yanawaumiza watoto hasa wazazi kutokana na utitiri wa michango inayobuniwa na Walimu kama njia ya kujipatia kipato cha zaidi. Hali hii kwa kiwango kikubwa imechangia sana kufeli kwa wanafunzi wa kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, kuwaachia wananchi jukumu la kujenga nyumba za Walimu, shule za msingi na sekondari ni mzigo mkubwa, hivyo kasi yake itakuwa ni ndogo na matokeo yake shule za vijijini haziwezi ku-*retain* Walimu. Naomba Serikali yetu iangalie uwezekano wa kujenga nyumba za Walimu kwa asilimia mia moja katika shule za sekondari za Kata ili wananchi wabebe jukumu la ujenzi katika shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ambazo bado hazipo kwenye maeneo yao. Napenda kuiomba Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie

Halmashauri ambazo kwa sasa zimeshindwa kupata fursa za kujenga Makao Makuu ya Halmashauri zao kama Halmashauri ya Morogoro haina uwezo wa kujenga Makao Makuu kwa vyanzo vyao vya mapato kwani hayapo. Hivyo, naomba Halmashauri hii isaidiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nikiamini kwamba, Serikali itaona umuhimu wa kuwapatia wananchi fursa ya kupata matrekta makubwa ili tuboreshe kilimo. Nawatakia utekelezaji wenye mafaniko.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge na Waziri Mkuu katika majumuisho, naomba kupatiwa majibu yahusuyo masuala yafuatayo juu ya Sera ya Uratibu na Bunge niliyoyahoji kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2011 na 2012.

Mosi, ujenzi wa ofisi ya Mbunge wa Ubungo au upatikanaji wa ofisi mbadala ya muda. Kwa sasa ofisi ya Mbunge, Ubungo ni ya chumba kimoja ndani ya jengo la Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni ambayo iko nje ya Jimbo la Ubungo. Katika ofisi hiyo ya chumba kimoja, Mbunge anakaa pamoja na msaidizi na maafisa wengine. Hali hii imekuwa ikilamamikiwa na wananchi pale wanapohitaji kuzungumza na Mbunge kwa faragha.

Aidha, ofisi hiyo kuwa katika hali ya mtu kuweza kuingia moja kwa moja na kukutana na Mbunge bila kupitia kwa msaidizi inaweza kutumiwa vibaya au kuhatarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya sasa ambayo Katibu Msaidizi wa Mbunge ameshatoa taarifa polisi juu ya *sms* anazopokea za kutaka ashiriki mipango ya kumdhuru Mbunge, lakini hakuna hatua

zilizochukuliwa. Masuala haya na matatizo mengine juu ya Mbunge ninayaandikia barua kwa Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, Mkuu wa Mkoa na kuhoji katika vikao mbalimbali bila hatua kuchukuliwa. Hata kupatiwa tu vifaa vya kiofisi kama kompyuta, *printer* na kadhalika toka mwaka 2011; pamoja na kukumbusha kwa nyakati mbalimbali.

Pili, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Waziri Mkuu, kwa pamoja ni muhimu kusimamia marekebisho ya mfumo wa utolewaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDCF)* na kuongozwa na mfumo ulio sawa na fedha nyingine za ruzuku zingine za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa fedha hizo kunafanya Mifuko ya Maendeleo ya Jimbo kusababisha hoja toka kwa Wakaguzi *(Audit Query)*. Hivyo, ama fedha zitolewe kwa wakati kama ruzuku zingine zinazokuja kwenye Halmashauri au kuwe na mfumo tofauti wa fedha kuepusha hoja za ukaguzi wa kuwezesha miradi ya maendeleo kufanyika kwa wakati.

Tatu, ni kuhusu sera na uratibu:-

(1) Matokeo ya sensa yaliyotangazwa na Rais 2012 na ripoti iliyozinduliwa na Waziri Mkuu 2013, ni muhimu Wabunge tupewe nakala katika Mkutano huu wa Bunge.

Aidha, Serikali itoe maelezo kuhusu sababu ya takwimu ya idadi ya watu katika Manispaa ya Kinondoni kuwa chini ya takwimu zilizotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho *(NIDA)* 2012 na takwimu za Tume ya Taifa ya Uchaguzi *(NEC)*.

(2) Maelezo yaliyotolewa kwenye aya ya 76 na 77 kuhusu barabara katika Jiji la Dar es Salaam yanaonesha uchelewaji wa utekelezaji kwa kuwa miradi tajwa ilipaswa kukamilika 2011 na sasa ulikuwa wakati wa kutoa taarifa ya utekelezaji wa barabara zilizoahidiwa wakati wa bajeti 2012/2013. Mathalani, barabara za Kimara – Bonyokwa – Mavurunza, Maramba mawili – Kinyerezi, Goba – Mbezi na kadhalika.

(3) Aya ya 104 na 105; kaya zilizohudumiwa mpaka sasa kutokana na maafa ya mafuriko huko Mabwepande ni 1007, ambayo ni 10% ya wanaoishi maeneo hatarishi. Lini wahanga wa Mbezi, Mabibo na kadhalika watapewa viwanja?

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimia Waziri Mkuu yenye ufanisi na matumaini mazuri kwa mwelekeo wa Serikali yetu chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nielekeze kwenye masuala ya uchumi. Hotuba ya Waziri Mkuu imesema kuwa pato la Taifa limeongezeka kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na mwaka 2011 la asilimia 6.4. Katika kuchangia kuongezeka kwa pato hilo sekta ya Kilimo, hakuna.

Mheshimiwa Spika**,** kwa kweli nasikitika sana kwa sekta ya kilimo kutochangia katika kukuza pato la Mtanzania kiuchumi. Sekta ya kilimo bado ina nafasi kubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Katika mkutano wa nchi za *SADC* uliofanyika Maputo, Msumbiji ulilenga kuhakikisha kuwa kila nchi wanachama watenge asilimia kumi ya bajeti ambayo ielekezwe katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ardhi na maji ni neema tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, lakini tunakufuru. Leo kila mwaka bajeti ya Wizara ya Kilimo uwapunguzie na pamoja na bajeti kupungua lakini pesa hawapati kwa wakati ili kufanikisha malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji katika Sekta ya Kilimo naona bado linasuasua, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu liliwakilishe suala hili ili wawekezaji waje kwa wingi kuwekeza katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Uwekezaji, suala la kuwashirikisha wananchi au wakulima wanaozunguka mashamba ya wawekezaji lipewe kipaumbele katika kulima kwa kuhamasishwa na mwekezaji. Kila shamba litakalopewa mwekezaji wawe kama *outgrowers*.

Kama mwekezaji anataka kulima zao fulani na anataka kuzalishia tani kadhaa, naomba apewe ardhi itakayozalisha asilimia sabini na tano (75%) na asilimia ishirini na tano (25%) wawezeshwe wananchi au wakulima wadogo wanaozunguka au jirani na shamba la mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Serikali katika kuwakaribisha wawekezaji katika Sekta ya Kilimo wapewe maeneo ambayo ni pori kabisa ili isilete mgongano au mzozo kati ya wawekezaji na wananchi. Nchi yetu ina maeneo makubwa na mazuri kwa kilimo. Pia wapewe masharti ya kuwapa huduma muhimu wananchi walio jirani hasa maji na masuala ya afya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliona Bunge hili likichukua nafasi yake kikatiba kikamili, kwa maana ya kuwa upande wa umma (wananchi) kuliko kwa upande wa Serikali. Huu ni wakati wa sisi (Wabunge) kutoa dira ya maisha kwa watu wetu kupitia Bunge hili la bajeti.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, kama mtendaji mkuu wa Serikali inayo wajibu wa kuyatekeleza haya bila upendeleo wowote, wala kutanguliza wengine na kuwaacha wengine nyuma.

Mheshimiwa Spika, ughali wa maisha siyo tu unaongeza umasikini kwa Watanzania walio wengi bali unaleta hofu kwa raia.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali kubinafsisha baadhi ya shughuli zake lakini siyo vizuri kuacha shughuli hizo kuachiwa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni Bandari, kwa hali halisi ni vizuri kupanua wigo wa shughuli hizo kwa watu binafsi wenye uwezo huo, ila tatizo wale waliopewa dhamana ya kuanzisha *ICD (Inland Container Depot)*. Kweli hali iliyopo kwenye hili ni mbaya ambayo inaongeza gharama kwa wanaoagiza bidhaa nje na ijulikane kila kinachoongezeka kwenye gharama za uagizaji zitaongezwa kwa mtu wa mwisho (mlaji).

Mheshimiwa Spika, waliopewa dhamana ya kuisaidia bandari na kuweka *ICD* wamekuwa na *hidden charges* nyingi ambazo zimekuwa kero na gharama hizi zimekuwa za kushurutisha.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwepo na maridhiano ya mwagizaji mzigo, ni *ICD* gani anayoiona nafuu kwake ili aweze kuchagua huku wenye *ICD* wawe na ushindni wa huduma na upunguzaji wa gharama. Kuwepo utaratibu wa kujaza fomu maalum kabla ya mzigo kufika na mwagizaji ataona ni wapi pa kuamua mzigo wake uende kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimwa Spika kwa utaratibu huu upo nafuu utakaoonekana kwani wengi watachagua na hii itawashawishi wenye *ICD* kushindana kutoa huduma bora na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kama mapendekezo yangu haya yatafanyiwa kazi basi kwa kiasi kikubwa gharama za maisha zitapungua kwa kuwa asilimia kubwa tunatumia bidhaa za kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la *Regulatory Authority*, zimekuwa mbali na bandari na hivyo mizunguko ya utoaji wa shehena bandarini pia umekuwa na usumbufu mkubwa wenye gharama, tungependekeza *Regulatory Authorities* zote ziwe *under one roof* pale bandarini ili kupunguza usumbufu wenye gharama.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima nategemea kuona matokeo katika hili, kwa kuwa sihitaji majibu ila matokeo.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuangalia upya maamuzi ya Serikali ya kutenga bilioni 440 kwa ajili ya kaya masikini kwa kuwapa fedha za chakula, matibabu na elimu, hili ni vizuri likaangaliwa tena.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha tayari tathmini ya kina iliwahi kufanywa na kuorodhesha watu

(Wilaya zipi ni masikini na watu gani wanaishi kwenye mazingira magumu) ikaonekana Bunda inashika nafasi ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu imefanyika tathmini nyingine na imeanza na utekelezaji wa kero hii kwa Wilaya ya Bagamoyo, hii inaonesha dhahiri kuwa kuna tatizo na hili litapelekea kabisa kuleta sintofahamu kwa wananchi wa Tanzania ambazo zitapelekea mitafaruku isiyo ya lazima katika nchi yetu. Nadhani mliona matokeo ya propaganda ya kuwa gesi inakwenda Bagamoyo na nini kilitokea.

Mheshimiwa Spika, pengine nia ni nzuri kabisa, lakini utaratibu ni mbaya kabisa. Napendekeza tathmini ifanyike haraka kwa nchi nzima na mgawanyo wa fedha hizi ufanyike kwa pamoja bila watu wa Wilaya fulani kutangulia. Tafsiri yake ni kuwa Rais anatoka Wilaya ya Bagamoyo na mwishowe ikanekana ni chanzo na mbegu za Ukabila ambao madonda yake ni vigumu sana kuyatibu.

Mheshimiwa Spika, nategemea mchango wangu huo utachukuliwa na kufanyiwa kazi.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa utaratibu wa kupeleka madaraka kwa umma ili kuwawezesha wananchi kutambua kuwa miradi inayotekelezwa katika Kata zao, Vijiji vyao na hata Halmashauri zao ni kwao na wanatakiwa kushiriki moja kwa moja, lakini kuna changamoto zifuatazo ambazo zinatukabili, zinatakiwa zipatiwe ufumbuzi ili tuweze kupata mafanikio katika miradi inayotekelezwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Halmashauri hususani wahandisi na wasaidizi wao kutoa ushauri kwa

Kamati za Kata za ujenzi pindi wanapotaka kujenga majengo; mfano, soko, zahanati, madarasa katika shule za msingi na sekondari ili kupunguza uwepo wa majengo yaliyo chini ya kiwango ambayo hayafanani na thamani ya fedha iliyotumika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuendelea kuwakumbusha watumishi juu ya dhana ya uwajibikaji na kuwachukulia hatua wote wanaokwenda kinyume na taratibu za kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa makusudi iliamua kuanzisha ujenzi wa shule za sekondari za Kata ili kuhakikisha watoto wanapata elimu ya sekondari katika Kata zao ama maeneo yaliyokaribu na vijiji vyao.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto kubwa katika shule za Kata, kuna baadhi ya vijiji wanafunzi wanapelekwa kusoma katika shule za Kata umbali kati ya kilomita 80; mfano, katika Tarafa ya Ikwiriri, Kibiti wanafunzi wanapangwa kusoma katika Kata ya Mwaseni ni zaidi ya kilomita 80 na hakuna hosteli, umeme, wala maji, wanafunzi wanapanga vyumba na vyakula wananunua wenyewe, je, tunategemea watoto hawa watafaulu mitihani yao?

Mheshimiwa Spika, kuna shule inajengwa katika Kata ya Umwe – Tarafa ya Ikwiriri, sasa ni takribani miaka sita haijakwisha kwa sababu ya urasimu wa watu wachache, wananchi wamechangia nguvu zao, lakini hadi leo watoto wanapelekwa kusoma umbali wa kilometa 80, 60 au 40 katika vijiji ambavyo havina huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inawasaidiaje wananchi hawa ambao wananyanyasika kutokana na urasimu wa watumishi na viongozi wengine?

**MHE. NEEMA MGAYA HAMID:** Mheshimiwa Spika, kuhusu maji; natambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Mijini kutoka 84% mwaka 2010/2011 hadi kufikia 86% 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nipongeze utekelezaji unaofanyika hivi sasa katika kuboresha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na kupanua mitambo ya Ruvu Chini na Ruvu Juu ili kufikia Februari, 2014; tatizo la maji Dar es Salaam limekwisha. Pamoja na yote haya naishauri Serikali isimamie kwa makini zoezi hili ili tuweze kufikia malengo tuliyojipangia ya kuhakikisha tatizo la maji Dar es Salaam linakwisha Februari, 2014.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie maji vijijini, ndio Serikali imefanya juhudi kubwa kuongeza idadi ya watu vijiji wanaopata maji safi na salama kutoka milioni 16.3 mwaka 2006 mpaka kufikia watu 20.6 mwaka 2012. Lakini bado Serikali inahitaji kuweka mkazo mkubwa katika suala la maji vijijini, sababu bado maeneo mengi vijijini hayana maji. Mfano, Wilaya mpya ya Wanging'ombe, kuna Kata ya Saja na Kijombe, Vijiji vyote havina maji, vijiji hivi ni pamoja na Igenge, Isimike, Uhenga, Kijombe, Ukomola, Iyadebwe Iyamluku, Mayala na Iyayi, hali ni mbaya pia katika Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati; naipongeza Serikali kupunguza gharama za kuunganisha umeme kutoka sh. 385,682 mpaka sh. 150,000 kwa vijijini na Mjini sh. 385,682 mpaka sh. 272,000, naipongeza sana Serikali. Lakini umeme vijijini ni tatizo kubwa mfano, Wilaya ya Wanging'ombe kuna Vijiji 102; kati ya Vijiji hivi Vijiji kumi tu ndio vina umeme, 90% ya Vijiji vya Wilaya ya Wanging'ombe havina umeme, tunataka umeme

Wanging'ombe, baadhi ya Vijiji ambavyo havina umeme ni Dulamu, Igagala, Wangama, Kinenulo, Uhekule, Mambegu, Iyayi, Ulembwe, Kingele na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, naipongeza Serikali kwa kuboresha elimu ya msingi na kuongeza idadi ya vijana wanaofaulu kwenda sekondari, niipongeze pia kwa kujenga shule nyingi sana za Kata na kuongeza Walimu. Lakini bado hali mbaya katika elimu ya sekondari, mfano, tumeuona hapo juzi tu katika matokeo ya wanafunzi wa kidato cha nne, takribani 60% ya wahitimu wamefeli.

Mheshimiwa Spika, nakubali hili ni janga la Watanzania wote na hivyo basi Watanzania wote tuna wajibu wa kutatua tatizo hili, kwa maana ya Serikali, wazazi na wanafunzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali iboreshe hizi shule za Kata kwa kujenga maabara, vitabu vya kutosha na Walimu pia waongezwe. Wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao, wanafunzi pia kuwa tayari kusoma na kuachana na mambo ya *facebook* na *twitter*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI; kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2011/2012 wa viashiria vya malaria na UKIMWI, imeonesha kwamba, maambukizi ya UKIMWI yamepungua kutoka 5.7% mwaka 2007/2008 mpaka 5.1% mwaka 2011/2012. Pamoja na kupungua kwa tatizo hili, lakini bado Serikali kwa kupitia taasisi husika wajipange katika kundi la vijana wenye miaka 23-24, wasichana ambao grafu ya maambukizi imekua kubwa 6.6% ukilinganisha na wavulana wenye umri huo wa miaka 23-24 ni 2.8%.

Mheshimiwa Spika, naona kundi hili ni la wale vijana waliomaliza Vyuo Vikuu ambao wako majumbani. Nina wasiwasi sana na nguvu kazi ya Tanzania ambayo itapotea miaka 10 – 20 ijayo. Je, Serikali ina mkakati gani katika kulisaidia kundi hili? Je, hatuna mipango sahihi ya kuwafikia kundi hili? *TACAIDS* kama *TACAIDS* wana mkakati gani katika kulifikia kundi hili la vijana wenye umri wa miaka 23-24? Naomba majibu katika majumuisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya ya mama na mtoto, naipongeza Serikali kwa jitihada zilizofanywa kwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, tuongeze nguvu kazi katika rasimali watu na rasilimali fedha, ndio Serikali inajenga vituo vya afya, imeongeza wafanyakazi katika sekta ya afya na hakika kama tutaendelea hivi tutafikia lengo la milenia. Lakini katika kupunguza tatizo la vifo vya mama wajawazito pamoja na jitihada zote, bado tatizo hili limekuwa changamoto kubwa na sidhani kama tutafikia lengo la milenia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kuhusu wanafunzi wengi kufeli kwenye mtihani wa *form four*, mtihani wa form four wanafunzi wengi wamefeli huu ni mshituko mkubwa kwa Taifa. Mshituko huu ni kwa wazazi, kwa wanafunzi na kwa Walimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mtihani wa mwaka juzi tulitegemea suala la kufeli kwa wanafunzi wengi, Serikali litalipatia ufumbuzi tatizo hili halitorejea tena, lakini badala yake mwaka jana wamefeli wengi kuliko mwaka juzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali yangu ni sikivu, naiomba wanafunzi wote waliofeli warudishwe kusoma tena na baadaye wafanye japo kuwa Jumamosi na Jumapili na Walimu wapatiwe posho kwa hizi siku mbili, bajeti ijayo kipaumbele nambari moja iwe elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madawa ya kulevya; idadi ya watumiaji madawa ya kulevya inaongezeka kila siku na kwa maana hiyo idadi ya uingizaji madawa ya kulevya nchini umezidi, watoto wetu wengi wameathirika kwa madawa ya kulevya na wengi wamekufa.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Zanzibar kwa kila nyumba tano, nyumba moja ina mtoto anayetumia madawa ya kulevya, Serikali imesema inahakikisha milango yote ya kupitisha madawa ya kulevya imefungwa na kusimamia ipasavyo. Sasa naiuliza Serikali, ongezeko hili la madawa ya kulevya nchini kuna mtambo ambao unatengeneza madawa ya kulevya humu nchini?

Mheshimiwa Spika, imefika wakati hawa wanaoingiza madawa ya kulevya wapewe adhabu kali, nayo ni kifo, hawa ni wauaji kwa nini na wao wasiuliwe, hiki kifungo cha miaka 10 au 20 kibadilike, lakini hawa watu wakinyongwa, basi naamini tatizo hili litapungua au litamalizika kabisa.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, naanza na suala la madawa ya kulevya. Serikali yetu haijalichukulia suala hili la madawa ya kulevya kwa nguvu zote na kulifanya lionekane la kawaida tu. Madawa ya kulevya yanaathiri nguvu kazi ya Taifa ambao hasa ni vijana wetu, yanasababisha kuvunjika kwa ndoa nyingi na kusababisha ongezeko la watoto

wa mitaani, pia ubakaji mwingi na kusababisha ongezeko la maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kusema tuna ulinzi wa kutosha katika mipaka yetu huku madawa ya kulevya yanapitishwa katika mipaka hiyo hiyo na kuingia nchini, hata wale wanaokamatwa na madawa hayo hatuoni wanapewa adhabu gani pamoja na Serikali kusema watuhumiwa 45 walikamatwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Waziri Mkuu wakati wa kuhitimisha ijibu watuhumiwa hawa wa madawa ya kulevya 45 waliokamatwa wapo wapi na wamechukuliwa hatua gani? Maana kesi nyingi zimekuwa zikizimwa kimyakimya.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri Serikali kuwa, Tume hii ya Kikosi Kazi Maalum cha Kitaifa cha Kudhibiti Dawa za Kulevya, kipewe kipaumbele sana kwa kupewa meno ili kifanye kazi ya kudhibiti bila kuogopa kutishwa na wala kuingiwa na tamaa ya kupokea rushwa, kwani kazi hii ni hatari, sababu inabeba mabilioni na mamilioni ya fedha na wanaohusika ni watu wetu wa karibu zaidi, wengine ambao huwezi kumdhania kama anaweza kufanya biashara haramu kama hii.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa; suala la rushwa ni suala mtambuka, Serikali isimamie sana suala la rushwa na kuipiga vita ili kujenga imani na amani katika nchi yetu kwa Watanzania wote, rushwa ni adui wa haki, rushwa hupindisha haki, tena ni chukizo kwa Mwenyezi Mungu. Ili kuwafanya Watanzania warudishe imani katika nchi yetu, ni kuhakikisha kila Wizara inachukia rushwa na kupambana nayo.

Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaonesha vema kupambana na adui rushwa, lakini wapo baadhi ya viongozi watendaji wanaoendekeza rushwa kwa ubinafsi wao na tamaa zao na hivyo kuifanya Serikali kwa ujumla ionekane haitilii mkazo suala zima la rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wakilaumu baadhi ya Wizara zinazoendekeza rushwa kwa kuwanyima wananchi haki na huduma muhimu za kimsingi, mfano, Afya. Wagonjwa wamekuwa wakidaiwa rushwa ili wahudumiwe vizuri katika matibabu na hasa wanawake wajawazito. Serikali ilitangaza kuwa, mjamzito hawezi kutoa gharama yoyote anapokwenda kujifungua.

Mheshimiwa Spika, leo hii akinamama wanatozwa fedha ili wahudumiwe vizuri katika kuzalishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara nyingine ni Mambo ya Ndani, upande wa Polisi, unapopeleka kesi lazima utoe chochote kwa askari ndipo mashtaka yako yatekelezwe, usalama barabarani hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara nyingine ni Ardhi. Wizara hii pia inanyanyasa wananchi na kuwafanya wapoteze dira ya maisha yao yote kwa kunyang'anywa mashamba yao na kupewa haki watu wengine wenye pesa zao. Hivyo, viongozi au watendaji Serikalini na katika Halmashauri zote ziwachukulie hatua kali wale wote watakaobainika kutesa wananchi kwa kuwatoza rushwa na kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, uchukuzi Serikali iimarishe magati yote ya Bandari za hapa nchini likiwemo gati la

Bandari ya Karema iliyopo katika Ziwa Tanganyika ambayo kwa muda mrefu ujenzi wake umesimama na kuonekana imeanza kuchakaa huku ujenzi haujakamilika. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akihitimisha, atueleze sababu za kusimama ujenzi wa gati la Bandari ya Karema na hatima ya usafiri wetu itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu korosho; Lindi na Mtwara sasa hivi kuna ugomvi wa malipo ya pili ya wakulima baada ya kulipwa 600/=. Kwa hiyo, malipo ya pili, wanalipwa nusu yake, wananchi wamekataa kupokea pesa hizo na sasa wananchi wanaandaa fujo kama zile za gesi za kutuchomea moto nyumba, tafadhali tusaidieni walipwe, tunaishi kwa hofu Lindi na Mtwara, tutauhama mji bila kupenda na chaguzi za mitaa zinakaribia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii; vipi Mheshimiwa Mjusi wetu *Dainasoo*, mbona hakuna maelezo yoyote, atarudi au harudi?

Mheshimiwa Spika, barabara Kibiti – Lindi itakwisha? Tunaomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chumvi/afya; madini joto tunayoweka katika chumvi ni agizo la Wizara ya Afya ili kuzuia ugonjwa wa *goiter,* je, Serikali haiwezi kusaidia kutoa madini joto bure kwa wakulima wa chumvi? Ni ya ghali sana, kuna hatari ya wakulima hao kutotia madini joto kabisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. REV. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia migogoro ya dini; wajibu wa Serikali ni kulinda nchi na watu wake (raia wake) Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeweka wazi uhuru wa kuabudu kwa raia wake.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za karibuni kumetokea mitafaruku/migogoro kati ya waumini wa madhehebu ya Kikristo na Kiislam, vurugu ambazo zilipelekea uharibifu wa mali/na hata mauaji ya viongozi wa dini, matukio kama kuchomwa kwa Makanisa Zanzibar na Dar es Salaam inatia mashaka kwa vitendo hivi kutokea hali Serikali imekaa kimya. Ni hatari kwa Serikali kukosa kutoa Kauli katika matukio haya yote.

Mheshimiwa Spika, si dhambi kusema kwamba, Serikali kwa namna moja au nyingine ina maslahi nyuma yake ndio maana imekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, suala la Udini, Serikali ya CCM ndio waasisi. Rejea mwaka 2005 kwamba *CUF* – Chama cha Udini (Uislam) na matokeo yake yaliyokuwa mabovu. Mwaka 2010 CHADEMA, Chama cha Udini (Ukristo) hizi propoganda mbovu za kisiasa ziachwe mara moja kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ya CCM haihusiki kwa nini haichukui hatua?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugatuaji wa madaraka; Serikali ifanye haraka kurudisha suala la ajira ya watumishi wa ngazi za chini (katika Halmashauri) ifanywe kule kwenye Halmshauri zetu kuliko Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Serikali za Vijiji kwa maeneo ambayo wananchi walijiondoa kwa tuhuma mbalimbali, kwa mfano, Kijiji cha Chemchem,

katika Halmashauri ya Karatu kwa takribani miaka miwili sasa hakina viongozi, hakina Serikali ya Kijiji na wananchi hawakupewa haki ya kuchagua viongozi wao. Hili tunahitaji majibu ya haraka ili wananchi hao wapewe haki yao kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa kiwango cha ufaulu kidato cha nne 2012. Naiomba Serikali iwe na utamaduni wa kuzifanyia kazi tafiti mbalimbali ili kuboresha elimu kinyume na ilivyofanya sasa, kuunda Tume ili hali kuna Tume iliyokwishafanya kazi ile ile 2010 na ripoti yake kutolewa Juni, 2011. Ripoti hiyo iliainisha mambo yote yanayopaswa kuangaliwa. Hii ni kuiongezea gharama kubwa nchi na ni matumizi mabaya ya fedha za umma yasiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, suala la pembejeo liangaliwe upya, *package* iendane na hali ya eneo husika na pembejeo itolewe kwa muda muafaka, kuwe na uwazi na haki itendeke kwa wanufaika wote.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue fursa hii muhimu kwangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa miongoni mwa Wabunge watakaochangia hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie msongamano wa mahabusu na wafungwa katika Magereza yetu. Magereza yetu yana msongamano mkubwa sana ambao unahatarisha afya na uhai wao.

Mheshimiwa Spika, wafungwa na mahabusu wamekuwa wakipoteza maisha kunakosababishwa na msongamano. Magonjwa yafuatayo ni hatari na usumbufu kwao; Malaria, UKIMWI, Kipindupindu, Kuharisha, Anemia, Homa ya Uti wa mgongo na *TB*.

Mheshimiwa Spika, Magereza yetu takwimu zinaonesha uwezo wake ni watu 21,552 kwa wakati mmoja. Hata hiyo, kwa sasa inaonekana wapo wafungwa na mahabusu takribani 35,126.

Mheshimiwa Spika, tofauti iliyopo kati ya uwezo wa Magereza na watu waliopo sasa ni 4464. Hii ni idadi kubwa sana kwa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 – 2013 kwa maelezo ya Kamishna Jenerali wa Magereza John Minja, wafungwa na mahabusu 463 wamefariki kutokana na magonjwa mbalimbali niliyoyataja nyuma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mtu ukimweka mahabusu ama ukimfunga umemkosesha uhuru wa shughuli zake zote ikiwemo udhibiti nafsi yake kimaradhi. Je, Serikali itakuwa na mikakati gani kuondoa msongamano katika Magereza yetu? Je, Serikali inawaambiaje Watanzania kuhusu magonjwa mbalimbali yanayoangamiza wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Magereza yetu wanawake wana sehemu zao maalum na akinababa vile vile na sehemu zote hizo zinalindwa sababu zipi za msingi za ongezeko la UKIMWI magerezani?

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutoa hoja kuwa, naunga mkono hoja hii ya Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hapa naorodhesha matatizo mbalimbali yanayohusu hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, maji bado ni tatizo kubwa Wilayani Nanyumbu. Katika Wilaya nzima ya Nanyumbu, kero kubwa kwa wananchi ni suala la maji.

Akinamama wanatembea mwendo mrefu kutafuta maji tena ndoo moja tu ya maji. Tarehe 7 Juni, 2010 mama mmoja aliuawa na ndovu Kijiji cha Mafuguru katika harakati za kutafuta maji. Tunaomba Serikali ichimbe mabwawa makubwa Wilayani Nanyumbu kupunguza tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Nanyumbu, lakini nachelea kusema kwamba, dhana ya kilimo kwanza Wilayani Nanyumbu haipo kabisa, bado wananchi wa Nanyumbu wanatumia zana duni za kilimo, hivyo kuwafanya wananchi wazidi kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, matrekta Wilayani Nanyumbu yanayoweza kuongeza uzalishaji wa tija hakuna. Wilayani Nanyumbu kuna skimu za umwagiliaji. Tuna maji mengi tu ya Mto Ruvuma ambayo yanatiririka kwenda baharini bila faida yoyote. Sambamba na hilo bei duni ya mazao ya biashara nalo ni tatizo, wakulima wa zao la korosho wanadhulumiwa sana, wakulima wa mazao mchanganyiko nao wanauza kwa bei ya chini ambayo hailingani na gharama ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wananchi wa Nanyumbu watabakia kuwa masikini kutokana na zana duni za kilimo na bei ndogo ya mazao yao. Nanyumbu tunaomba matrekta, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapojumuisha naomba aniambie Nanyumbu tutapatiwa matreketa mangapi?

Mheshimiwa Spika, huduma za afya Wilayani Nanyumbu ni duni, Wilaya ya Nanyumbu ina vituo vya afya vitatu na zahanati 15, wananchi walio wengi hawapati huduma za afya hasa akinamama wajawazito, watoto na pia wazee hawapati huduma hizi licha ya kuwa na umri wa zaidi ya miaka 65.

Mheshimiwa Spika, kuna uhaba mkubwa wa watumishi katika sekta hii ya afya, naomba Wizara husika ituletee wahudumu wa afya Wilayani Nanyumbu. Naomba pia tupatiwe gari ya wagonjwa (*Ambulance*) kwenye kituo cha afya cha Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu kama zilivyo Wilaya nyingine imejitahidi kujenga shule nyingi za Kata, hata hivyo bado tatizo kubwa ni uhaba mkubwa wa Walimu wa shule za msingi na za sekondari, hatuna hosteli za wanafunzi na hasa za wasichana, maabara na kuna uhaba mkubwa wa nyumba za Walimu. Tatizo la uhaba wa hosteli linasababisha wasichana kupata mimba. Pia kuna uhaba mkubwa wa vitendea kazi na vitabu vya kiada na ziada.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Nanyumbu kuna tatizo kubwa la mawasiliano ya simu za kiganjani. Minara ya simu ni haba, hivyo kupelekea tatizo kubwa la mawasiliano. Naomba Wizara husika kwa kushirikiana na Makampuni ya Simu tuwekewe minara ya simu Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunaomba kujua mchakato wa kuundwa kwa Mkoa mpya utakaozijumuisha Wilaya za Masasi, Nanyumbu, Tunduru na Nachingwea umefikia wapi? Nakuomba utakapofanya majumuisho uwafahamishe wananchi wa Wilaya hizo Mkoa huo utaanzishwa lini.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wa majumuisho anipatie maelezo ya mambo yafuatayo:-

Kwanza, ukaguzi wa *KNCU;* yako malalamiko mengi kuhusu Chama Kikuu cha Ushirika cha *KNCU,* Serikali ilituma wakaguzi kuona kufuatilia tuhuma hizo. Nitafurahi kusikia taarifa hiyo itatolewa lini?

Pili, masoko ya Kimataifa; Serikali imeahidi kujenga masoko mawili ya Kimataifa, soko la Ndizi na mboga mboga njia panda Himo, soko la Nafaka la Lokolova. Naomba kujua masoko hayo yataanza kujengwa lini?

Tatu, ujenzi wa Mji Mdogo wa Himo; ingawa Serikali imetangaza Himo kuwa Mji Mdogo lakini hakuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika. Bado kuna Serikali za Vijiji na vitongoji katika Mji Mdogo wa Himo. Naomba kujua ni lini Serikali itafanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Mji Mdogo wa Himo?

Nne, utekelezaji wa ahadi ya Rais ya barabara; ahadi ya kutengeneza barabara za lami Marangu Mtoni – Kilema Sokoni, Kawawa - Nduoni ilitakiwa iwe imetekelezwa mwishoni mwa mwaka jana, nitashukuru kujua ujenzi huo utakamilika lini?

Tano, usambazaji wa maji katika Kata za Mwika Kaskazini na Mwika Kusini; Mashirika ya Kilutheri ya Ujerumani yamechanga shilingi milioni 151 kwa ajili ya kusambaza maji katika Kata za Mwika Kaskazini na Mwika Kusini, Rais alipopita Mwika alitoa ahadi kwamba angeona mipango yetu ya usambazaji maji Mwika angetusaidia.

Mheshimiwa Spika, nilimpatia Programu ya maji ambayo ilionesha kama Serikali itatoa shilingi bilioni 230 zingeweza kutatua tatizo la maji Mwika Kaskazini na Kusini.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu anisaidie kumkumbusha Rais juu ya jambo hili.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wizara zote anazoziongoza kwa kazi nzuri zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa jengo la Bunge, ni vema jambo hilo likapewa uzito stahiki. Binafsi nimeshiriki ukaguzi wa jengo hili na kubaini baadhi ya upungufu ambao ni vema ukapatiwa ufumbuzi wa haraka, lakini jengo hili limejengwa kwa mkopo na halina muda mrefu na matatizo mengine ni ya kiufundi/ utekelezaji na naamini mkopo bado haujalipwa. Je, gharama hizo zitagharamiwa na Bunge na Mifuko haitahusika?

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni vema jibu litolewe kufuatia michango ya Wabunge waliosema (Upinzani) kuwa bilioni sita zitatumika kwa ajili ya kuziba tundu dogo tu, ni maneno ya kilofa, lakini yana *impact* kwa wananchi kuiona Serikali yao haina *feeling* ya matatizo ya wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, naungana na michango ya Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Komba na Filikunjombe juu ya umuhimu wa Serikali kuangalia kwa jicho la pekee juu ya matatizo ya wananchi wa maeneo hayo ya Nyasa na wapewe kipaumbele. Lakini nikiwa kama mwananchi wa maeneo hayo Kata ya Kihagara.

Mheshimiwa Spika, sikubaliani kabisa kuwa, sisi wananchi wa Nyasa tunamwomba Rais Banda kuhamia Malawi, kama matatizo yapo maeneo mengi ikiwemo Dodoma, nao hao watahamia wapi? Hiyo si sahihi na ni jambo la uchochezi tena kwa nchi ambayo tayari

tuna mtafaruku na mpaka. Ni vema pia suala hili litolewe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya 2011/2012, niliomba juu ya hospitali ya Kata ya Kihagara, 2012/2013 nashukuru ujenzi umeanza angalau jengo moja linaonekana, lakini fedha ni kidogo za kuendeleza ujenzi huo. Naomba jicho la ziada liongezeke.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai, lakini maji bado ni tatizo kubwa hasa maeneo ya vijijini, iko haja ya kuharakisha Mfuko wa Maji vijijini kama ilivyo kwa *TANROADS.* Naamini itasaidia kwa kiwango kikubwa kwani itaongeza *attention,* maji yasiyo salama yanachangia magonjwa mengi kupelekea kuwa na jamii hafifu na kupanda kwa gharama za hospitali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo; suala la wafugaji/wakulima lipewe uzito wa Kitaifa kama ilivyo kwa Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhufu ufugaji wa nyuki; faida ni kubwa, lakini bado elimu inahitajika, watu wamewekeza mawazo yao kwa shughuli nyingine za mazoea, ndio maana hata baadhi ya Wabunge wanahoji. Hivi Wabunge walishapata semina ya eneo hili?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. RAMADHAN HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika sekta ya elimu, elimu ndio mkombozi wa mwanadamu katika nchi yetu, suala la elimu bado limekuwa changamoto hali ambayo inaweza kupelekea vijana wengi kutokuwa na kazi za kufanya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Serikali ichukue hatua za makusudi ili kuweza kulikabili tatizo hili. Kwa upande wa shule za msingi kumekuwa na matatizo makubwa hali inayopelekea, hata mazingira ya shule bado hayaruhusu, shule nyingi ambazo ziko katika Kata zimekosa huduma za kijamii kama maji, vyoo, Walimu na vitendea kazi hali ambayo hata Walimu hawawezi kufundisha vizuri.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai wa kila kiumbe, lakini katika nchi yetu maji yamekuwa tatizo kubwa kwa baadhi ya vijiji vingi hapa nchini, maendeleo hayawezi kupatikana kama miundombinu ya maji haijarekebishwa, watu watatumia muda mwingi katika kutafuta maji badala ya kufanya kazi za kutafuta maendeleo. Nashauri Serikali itenge fedha ambazo zinaweza kutosha kujenga miundombinu ya maji na kama bajeti ya Wizara hiyo haitoshi, basi zikopwe katika sehemu yoyote ambayo haitaathiri kazi nyingine kuendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, kupanda kwa gharama za usafiri *SUMATRA* imetangaza rasmi kupanda kwa gharama za usafiri kuanzia mwezi Aprili, suala ambalo hatimaye limepata baraka za mhusika kwa maana ya Waziri wa Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, sina hakika kama Waziri Mwakyembe ametoa baraka kwa jambo kubwa ambalo athari zake si kidogo kwa maana ya shilingi 100 kama ambavyo wengi wanataka kuwaaminisha wananchi na kwamba ni kitu kidogo ambacho hakina athari kubwa kwenye uchumi wa Mtanzania wa kawaida kwa maisha ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, ninachomaanisha hapa ni kwamba, ongezeko hilo la nauli litakuwa na athari kubwa mno kwa wananchi wetu. Ni wazi kwamba, bei ya nauli haiwezi kupanda kama bei ya mafuta haijapanda, bei ya mafuta ikipanda huwa inasababisha pia bei za vitu vingine kupanda. Kwa hiyo, tusichukulie kuwa kupanda kwa nauli kama jambo la kawaida. Matokeo yake ni mfumko wa bei ambao kila wakati tunaupigia kelele. Tunaitaka Serikali itafakari upya bei za usafiri ili kunusuru kupanda kwa bei za bidhaa nyingine na kumgandamiza mwananchi mwenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maafa; hivi majuzi Taifa limepata msiba mkubwa kutokana na kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16 ambapo watu 36 walikufa na wengine 17 kujeruhiwa. Serikali kupitia Waziri Mkuu imeunda Tume ya kuchunguza chanzo cha kuporomoka kwa jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Mheshimiwa Lowasa alipokuwa Waziri Mkuu aliunda Tume ya uchunguzi baada ya kuporomoka kwa jengo la *Chang'ombe Village* lilokuwepo Temeke. Taarifa ya uchunguzi huo ilibaini kuwa zaidi ya maghorofa 100 katika Jiji la Dar es Salaam yamejengwa chini ya kiwango.

Kinachonishangaza ni kwamba, ni kwa nini Serikali ilitumia fedha nyingi za walipa kodi wa Tanzania kuunda Tume ya uchunguzi juu ya kuporomoka kwa ghorofa hilo wakati kuna taarifa na mapendekezo ya Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Lowasa alipokuwa Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Lowasa mwenyewe amenukuliwa na vyombo vya

habari akiishauri Serikali kuifanyia kazi ripoti ya Tume iliyoundwa wakati akiwa Waziri Mkuu ili kunusuru vifo vya Watanzania wasio na hati vinavyotokana na majanga yanayotokana na uzembe wa watendaji wa Serikali katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, hivi kama Serikali hii ya CCM inayojiita sikivu, haisikilizi wala haizingatii ushauri inaopewa na aliyekuwa Mkuu wa shughuli za Serikali, itamsikiliza nani? Kama Waziri Mkuu anapuuza kazi alizozikuta mezani za mtangulizi wake wa ofisi atamsikiliza nani? Naomba Serikali isitapanye fedha za umma kwa kuunda Tume ambazo hazina tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu tumechoka na Tume zinazoundwa kuhusu kuporomoka kwa elimu ya Tanzania. Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naitaka Serikali iweke hadharani ripoti zote kuhusu elimu ili zijadiliwe Bungeni. Mitaala yote ya elimu iletwe Bungeni ili Bunge kama chombo cha uwakilishi, lijadili na kuamua aina ya elimu tunayotaka Watanzania wapate.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuajiri Walimu sasa uangaliwe upya, Walimu wafanyiwe usaili kama kwenye ajira nyingine ili tuwe na Walimu wenye sifa. Kusomea ualimu peke yake kisiwe kigezo pekee cha sifa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, Itilima ni mojawapo ya Wilaya mpya na kama ilivyo kawaida yafuatayo tunaomba yashughulikiwe:-

Kwanza, Halmashauri mpya ianzishwe mara moja na bajeti ya Halmashauri itengwe kutoka

Halmashauri ya Bariadi *DC*. Vitabu vyetu tulivyopewa havionyeshwi bajeti ya Itilima.

Pili, maji ya Lagungabili Makao ya Wilaya hayapo, tunaomba kisima kirefu na Mto Simiyu utumike ili kupata maji ya uhakika kwa mji mpya.

Tatu, hospitali ya Wilaya ya muda iliyoko Nkoma ipewe watumishi na vifaa tiba ili hospitali hii iliyofunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu itusaidie. Kwa muda mrefu hospitali ya Wilaya ianze kujengwa Lagangabili. Aidha, wananchi wamejenga Dispensari ya Nanga na Nangali lakini ni Dispensari ya Nanga tu itapewa dawa, watumishi na vifaa tiba, lakini Nangali haimo. Naomba Nangale pia iongezwe mwaka huu 2013/2014.

Nne, umeme tumeahidiwa kwa Vijiji vya Budalabujiba mpaka Lagangabili na vijiji vyote vilivyofanyiwa ukaguzi na *REA*. Aidha, kwa bwawa la Nkoma nimeomba umeme ili tupate umeme wa hospitali na wa *pump* ya maji kutoka bwawa la Nkoma.

Tano, kuhusu maji kutoka bwawa la Nkoma, dhana ya kukusanya maji bila kujenga miundombinu ya kusambaza, kusafisha maji haitawezekana. Bwawa la Nkoma lilikamilika mwaka 2000, leo ni miaka kumi na tatu maji hayajaja, bado kuwekewa miundombinu ya kuhudumia maji haya kwa matumizi ya binadamu na kumwagilia mazao zaidi kwa mbuga ya Ng'wambagwa.

Sita, daraja la Ng'waswale ni kiungo kizuri sana kwa Kata hiyo ya Ng'waswale na kwa misingi hiyo madaraja mawili ya Madilima na Bukingwaminzi yaliyojengwa kwa fedha ya Mfuko wa Barabara, naomba daraja hili lifikiriwe kwa bajeti ya mwaka huu.

Saba, kusambaza maji ya Nkoma tulizungumza na Waziri Mkuu alipokuja Jimboni. Aidha, nimezungumza na Wizara ya Maji na Katibu Mkuu wa TAMISEMI, nimeangalia katika mipango ya maendeleo hakuna fedha za mradi huu. Kutoweka miundombinu ya kutumia maji haya ni matumizi mabaya ya fedha za umma, nami sitaunga mkono bajeti ya TAMISEMI mpaka nipate jibu la kuridhisha.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, masuala ya sera nchini yanahitajika kufafanuliwa vema kwani masuala mengi yakiulizwa majibu huwa hakuna sera

Mheshimiwa Spika, swali, sera ni nini/scope ya sera na naomba Wabunge wapewe semina. Masuala mengi huenda kienyeji *adhoc* mfano, masuala ya maafa, sera ya maafa inasemaje? Idara ya sera ina mpango gani wa kuwa *Accessible* ili Wizara, Idara zingine za Serikali waweze kuonana nao na kujadili masuala ya sera. *Example* utoaji haki kwa mujibu wa Ibara ya 107 ya Katiba ni suala la mhimili wa Mahakama lakini sera gani inayoruhusu Wizara ya ardhi kusimamia Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera; aidha, Sera lazima zitekelezwe, inakuwaje pale ambapo sera hazitekelezwi na Wizara na Idara, *what is the sanction?*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge, tumekuwa na utamaduni wa kumtumia *AG* (Mwanasheria wa Serikali) je, Bunge lina Wanasheria na Mkuu wa Kitengo ni nani ambaye anapaswa kujulikana, kuwashauri Wabunge *Accessible office of the Lawyer of Parliament*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala itaongezewa lini *Expert* wa *Reseach attached to Committee* ili aweze kufanya utafiti wa masuala ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuteua safari za Wabunge kwenda nje ukoje na vigezo gani hutumika? Kwenye *file* langu miaka (3) sasa sijawahi kuombwa na Bunge kuwakilisha mkutano wowote, angalia *file* langu tangu niapishwe? Malalamiko hayo yapo kwa Wabunge wengi, tunaomba safari za nje mtupe vigezo/ uwazi kama tunavyochangia Bungeni *Equality* iwepo, Bunge ni mhimili muhimu.

Mheshimiwa Spika, je Makatibu wa Kamati huwa wanapewa *Training?* Namna ya kufanya kazi na kuwa-*treat* Wabunge? Je, *Institution* ipo *happy* na *treatment* na *behavior* za Makatibu Kamati wote?

Je, Wabunge wanapewa semina namna ya kuwa-*treat* Makatibu? Lini itakuwepo semina ya Wabunge na Makatibu Kamati wao? Je, Bunge lina kitengo cha *Reseach?* Ni *research* zipi zinafanyika na Wabunge wanaruhusiwaje kushiriki hizo r*esearch* za Bunge na *study* mbalimbali. Lini pia jengo la Bunge litakarabatiwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Government Printers,* Serikali itanunua lini mitambo mipya ya mpiga chapa wa Serikali hususani tunavyoelekea chaguzi za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inachapisha wapi *ballot papers* na nyaraka za chaguzi za Serikali za Mitaa na rasimu ya Katiba mpya. *Retention* ya 26% ina lengo gani? Madhumuni yake ni nini? Lini Serikali itaboresha mazingira ya ofisi ya *GP* na maslahi ya wafanyakazi

Mheshimiwa Spika, kuhusu *CDA*; eneo la Chinyoya, Kata ya Mlimani lina malalamiko makubwa ya wakazi.

Mheshimiwa Spika, ombi, *CDA* wakakae na wananchi wa Kata ya Mlimani, Chinyoya kusikiliza kero zao mapema, Serikali iwe na utaratibu wa kuwasikiliza wananchi, *Dialogue*, *Opinion box* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini *CDA* watakwenda kusikiliza hoja za wananchi wa Mlimani Chinyoya kwani kuna kero kubwa Kata ya Mlimani

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu kuongeza Mapato ya Halmashauri; kuna malalamiko kuwa Serikali Kuu imechukua sehemu ya kubwa ya vyanzo vya mapato vya Halmashauri nchini. Nashauri hili liangaliwe kuongeza uwezo wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ipate kampuni za wataalam, wapewe kazi ya kutathmini vyanzo vya mapato kwa Sheria zilizopo. Tuteue mtaalam mmoja kila mkoa afanye tathmini ya Halmashauri katika mkoa husika, hii itasaidia sana Serikali kutambua *potentials* zilizopo badala ya Halmashauri kulalamika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itoe waraka kwa kila Halmashauri, iwe na Wakala mmoja tu katika ukusanyaji wa ushuru wa masoko ndani ya Halmashauri. Hii itasaidia uwajibikaji na zaidi itaongeza mapato badala ya utaratibu wa sasa ambapo Halmashauri yenye masoko 60 inakuwa na Mawakala 60, hali inayopelekea rushwa, uzembe na udhaifu wa makusanyo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuboresha ubora wa ujenzi wa Halmashauri; sehemu kubwa ya mapato ya Halmashauri inatumika katika ujenzi wa barabara, visima, majengo. Ubora wa ujenzi wa namna zote bado ni duni sana. Nashauri Serikali ianzishe mamlaka ya ujenzi kwa Serikali za Mitaa *(Roads and Building Agency for Local Government).* Hii itasaidia sana kusimamia ubora. Mfano mzuri, ni *TANROAD* ilivyo mfano. Tukiwa na *Agent* kama hiyo itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, tatu, mpango wa kuondoa *VEO* na *WEO* wasio na viwango. Mipango ya sasa ya Serikali hairuhusu mtu mwenye kiwango chini ya elimu ya Sekondari kusimamia maendeleo ya Vijiji au Kata.

Natambua umekuwepo mpango wa muda mrefu kutatua tatizo hili, lakini hakuna utekelezaji kwa miaka mingi. Serikali itambue kuwa *WEO* na *VEO* ndio watendaji wa Serikali walio karibu kabisa na wananchi, udhaifu wao una madhara makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nne, Wakurugenzi wa Mashirika na Halmashauri wapewe ajira za Mikataba. Nashauri hili kama njia ya kuongeza ufanisi wa Halmashauri na mashirika nchini. Bado Wakurugenzi wa Halmashauri na Mashirika hawafanyi kazi kwa viwango kwa kuwa hawawekewi vigezo vya kimikataba. Bado Halmashauri zinaweza kuzalisha na kuchangia Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, tano, ushirika na China uwe kimkakati; China imeahidi kujenga Kituo cha Viwanda Afrika hapa Tanzania. Eneo lilipangwa la *Industrial Base* pale Kurasini ilitakiwa Serikali ilipe fidia kiasi cha bilioni 60 ili China ianze kazi. Nchi nyingine za Afrika zinapigania fursa hiyo. Ni aibu kutenga bilioni tano kati ya bilioni 60.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia japo ni kwa njia ya maandishi. Tumeona kwa kweli Serikali yetu imejitahidi kupeleka huduma za maji, afya na nishati ya umeme kwa wingi sana. Ni wakati sasa wa kusaidia Watanzania wanaoishi vijijini nao wana haki ya kupata huduma hizo muhimu sana kwa Watanzania. Masikitiko yangu ni kuona bado vipaumbele vinawekwa kwenye Majiji na Mijini tena kwa kiwango cha juu sana na kusahau kabisa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aifumue bajeti yake na kuongeza pesa kwa huduma za maji, afya na umeme vijijini. Ni aibu kubwa kwa Tanzania, nchi yenye maji mengi duniani watu wake wanakufa kwa kiu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yetu kuendelea kuleta matrekta mengi zaidi na kuondoa kabisa jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, nashauri Serikali yetu kuweka kipaumbele kwa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Dodoma kwenda Mvumi Mission ambako kuna hospitali teule ya Wilaya ya Chamwino ambako kuna kitengo kikubwa cha kutibu macho. Vile vile ni muhimu sana Serikali ikajenga barabara ya lami kuunganisha lami inayotoka Dodoma kwenda Iringa katika Kijiji cha Mlowa barabara ya kwenda Mvumi Hospitali. Kwa kuwa kujengwa kwa barabara hiyo mpya kutaleta ajali nyingi, pia katika eneo hilo hakuna Hospitali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ili kupunguza gharama na matumizi yasiyo ya lazima ya

Serikali, nashauri tuwe tunatazama vifaa vyenye thamani kubwa sana vinavyotaka kununuliwa katika utekelezaji wa majukumu yaliyo mbele yake. Kama kazi ya vifaa/mitambo hiyo/hivyo vinafanana na katika mazingira ambayo Wizara au Taasisi kazi zake zinafanana siyo lazima kununuliwa kwa kila Taasisi peke yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tuna kazi ya vitambulisho vya Taifa, lakini pia kuna uboreshaji wa daftari la wapiga kura, kazi ambazo zitahitaji wananchi kupata vitambulisho vya uraia na cha mpiga kura, hivyo kazi hizi mbili zitahitaji *camera* na mashine za kuchukulia alama za vidole na kazi hizi pia zinatakiwa ziwe zimekamilishwa kabla ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, sioni ulazima wa kila taasisi hizi mbili kununua peke yake vifaa hivyo kwa kuwa vinahitaji fedha nyingi, mabilioni kwa vifaa vyake, kwa nini visinunuliwe na vitumike kwa pamoja (*as a joint mission*). Naamini kwa teknolojia iliyopo sasa ya hali ya juu haitashindikana kuzitawanya taarifa zake picha, alama za vidole kwenda katika kila taasisi hizi mbili kufanya kazi zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hii itapunguza *Dublication of Disbursement of Public Fund for the similar mission.* Nyingine unakuta, uhamiaji wanataka Boti, Police Boti, mafuta, matokeo yake zinanunuliwa kwa gharama kubwa, halafu zinakosa bajeti za kuzi-*run* halafu zinaoza majini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa chini ya Wizara ya Kilimo na Bodi ya Tumbaku kusaidia kukua kwa zao la tumbaku na kufanya zao hili kufanya marekebisho mbalimbali ya mfumo wa uzalishaji na soko ambao ulisaidia kuongezeka kwa zao toka tani (40,000)

mwaka 2005/2006 na kufikia tani (129,000) mwaka 2010/ 2011, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa toka tumbaku kuanza kuzalishwa nchini na kutoa pato kubwa na kuwa la kwanza linaliuza nje na kuingiza fedha za kigeni mfululizo. Lakini kumejitokeza jambo kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika ambalo likiachiwa litawakatisha tama wakulima wa tumbaku kulima zao hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lenyewe ni baadhi ya viongozi wa Vyama Vikuu wanagushi mikopo ya wakulima na wanayopitisha katika makisio yao ya kukopa katika mikutano mikuu ya Vyama vya Msingi na kuiongeza na kwenda kusimamia hadi kupatikana, lakini mgawanyo wa makisio ya Vyama vya Msingi unakwenda kama kawaida, lakini ile ziada waliyoiongeza bila ridhaa ya wakulima wanaitumia wao wanavyojua, lakini deni lote analipa mkulima.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iingilie kati Wilaya yetu na sehemu zote zinazolima tumbaku wakague na wachukuliwe hatua wahalifu hao kwani kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha.

Mheshimiwa Spika, jambo hili si la kuchelewesha kwani limewapa mzigo mkubwa wa deni wakulima na kwa kuwa ushirika wana sheria yake ambayo iko *gorvern* kwa mujibu wa taratibu za ushirika, lakini Serikali kuu inayo uwezo wa kuingilia kati na kuisimamia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye kujaa mikakati ya miradi mbalimbali itakayotekelezwa kupitia bajeti ya mwaka wa fedha

2013/2014 ikiwemo miradi ya maendeleo kadhaa ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa William Lukuvi; Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Agrey Mwanri na Mheshimiwa Kassim Majaliwa; Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba nzuri ya Waziri Mkuu na kwa utendaji wao uliotukuka kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali ya rufaa, Mkoa wa Singida; pamoja na ukweli kuwa Serikali imekuwa mstari wa mbele kutenga fedha za kuchangia ujenzi wa Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Singida, ujenzi huu uliibuliwa chini ya uongozi wa Mkoa wa Mheshimiwa Dkt. Parseko Kone, *RAS* na watendaji wote wa Mkoa bila kuwasahau Wabunge wote wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum, kwa kuwa bajeti ya 2012/2013, Serikali ilitenga shilingi milioni 1.8, lakini fedha ambazo zimekwishapelekwa ni shilingi bilioni moja tu. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa naomba sasa salio la shilingi milioni mia nane ili Mkoa uweze kununua samani kuweka kwenye majengo ambayo tayari yameshakamilika ili majengo hayo yaweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwa kukubali kutenga shilingi bilioni 3.5 ili ujenzi wa jengo kubwa la uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza, mfano, kansa, kisukari na kadhalika jengo ambalo litagharimu Sh. bilioni nane. Ili jengo hili ujenzi wake ufike nusu tunatakiwa tuwe na sh. bilioni nne. Naiomba

Serikali ikubali kutuongezea shilingi milioni mia tano ili ujenzi huu ufike nusu na bajeti ijayo itenge shilingi zingine bilioni nne kumalizia jengo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa hospitali hii ikikamilika na kufunguliwa itasaidia wananchi wa Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Manyara, Dodoma na Mkoa husika wa Singida. Nina mategemeo makubwa Serikali yetu yenye kuwajali watu wake itakuwa tayari kuleta sasa shilingi milioni mia nane na kutuongezea shilingi milioni mia tano.

Mheshimiwa Spika, riba kubwa kwenye benki zetu; natambua wazi kuwa ajira bado hazitoshelezi kwa wahitimu wote nchini, nawapongeza Watanzania wote walioamua kujiajiri kwa kuainisha miradi mbalimbali ya kujitegemea wakiwemo wanawake na vijana. Tatizo linalowasumbua ni riba kubwa wanayodaiwa kupitia mikopo wanayokopa kwenye mabenki.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kukaa na mabenki haya yanayokopesha kupunguza riba ili wanawake na vijana wanaokopa waweze kupata faida. Sasa hivi faida kubwa yananufaika mabenki mfano *CRDB* riba ni asilimia 22, ipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, harakati za kupambana na UKIMWI bado zinakwamishwa na mambo mbalimbali; hivyo, napenda kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha za UKIMWI hazina matumizi mazuri, hii ni kwa sababu Kamati za UKIMWI wajumbe wake hawana dhamira thabiti ya kulinda fedha hizi. Ushauri, naomba muundo wa Kamati hizi zitazamwe upya wateuliwe wale wenye *NGO* walioko kwenye Halmashauri husika bila kuwasahau Wabunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, waratibu wa UKIMWI Mikoani wapatiwe magari ili waweze kufutilia vizuri masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sera ya kuanzisha Mfuko wa UKIMWI Tanzania, tayari Baraza la Mawaziri lilikwisharidhia, naomba Muswada uletwe Mkutano wa Bunge la Kumi na Mbili ili Bunge liweze kupitisha Mfuko wa UKIMWI uanzishwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali iajiri waratibu wa UKIMWI wa Wilaya ili waweze kusimamia vema fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu kwani sasa hivi wanaosimamia ni watendaji wenye idara zao, hivyo wanakaimu.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti Mtendaji wa *TACAIDS* aungwe mkono na timu yake kwa juhudi zao nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madawa ya kulevya; ni ukweli usiopingika kuwa UKIMWI na madawa ya kulevya, matatizo haya yana uhusiano wa karibu. Ili mapambano haya ya madawa ya kulevya yafanikiwe, ni lazima vita vyake viunganishwe na waratibu wa UKIMWI washughulikie pia madawa ya kulevya ili mapambano haya yaende Mikoani hadi Wilayani kuliko ilivyo sasa mapambano yako Dar es Salaam wakati madawa yako nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, vile vile Tume hii iongezewe fedha ili iweze kukabiliana na wafanyabiashara haramu wa madawa ya kulevya ambao wanayo nguvu ya fedha na watendaji wetu maskini vile vile wapewe madaraka ya kujitegemea, hatua zote za ukamataji hadi kuwapeleka Mahakamani kama TAKUKURU inavyofanya. Hii itapunguza tatizo la kupotea kwa

ushahidi mfano, madawa yalikamatwa na Polisi mwisho yakawa sukari.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja, nikitegemea mchango wangu utafanyiwa kazi na Serikali.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake yenye hoja za msingi za maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo umma wa Watanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutenga maeneo mapya ya utawala ya Mikoa na Wilaya. Katika hili, naishauri Serikali itoe kipaumbele cha kuyapatia maeneo haya mapya fedha za kutosha kwa ajili ya kuyaendeleza, ikiwemo upimaji wa mipango miji.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme ni mhimili wa maendeleo na uwekezaji, katika sekta hii ya madini, ni la kufa na kupona hasa ikizingatiwa kwamba nchi yetu inaendelea kwa kasi katika masuala ya kiuchumi na nyanja zinginezo.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme kwa njia ya maji kwa sasa hautabiriki kutokana na kutokuwa na mvua za uhakika, hivyo ni vema tukaanza kuwekeza kwa nguvu zaidi katika gesi asilia, makaa ya mawe, nguvu za upepo na nguvu za jua.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa umeme wa uhakika kutasaidia kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuharakisha katika uanzishaji wa viwanda ambavyo vitaajiri Watanzania wengi na hivyo kupunguza kasi ya ongezeko la upungufu wa ajira kwa

vijana wetu wanaohitimu katika vyuo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la ongezeko la watu nchini linatisha hivyo ni rai yangu kwa Serikali kwamba, idhibiti ongezeko la watu na ongezeko la mifugo. Matokeo yake ni uhaba wa ardhi na matokeo yake ni kukosa chakula na magomvi baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA bado haujaeleweka vizuri baina ya wananchi na vyombo vya fedha nchini. Wapo wananchi wamemilikishwa ardhi zao kwa sheria za kimila lakini hati za Kimila zitumike kuwawezesha kutumia kama dhamana katika vyombo vya fedha ili zisaidie wakulima kuboresha maisha yao na pato la Taifa.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la Makao Makuu ya Serikali kuhamia Dodoma ni la miaka mingi, ningeomba sasa Serikali itoe tamko ama iachane na wazo la kuhamia Dodoma au iamue sasa kuhamia Dodoma mapema iwezekanavyo.

Kwa kushindwa kutekeleza suala hili, Serikali imejikuta ikiingia gharama kubwa za uendeshaji kwa kuhudumia Ofisi mbalimbali, yaani Dar es Salaam na Dodoma. Mfano mzuri ni huduma inayotolewa kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara. Waziri au Katibu Mkuu anapewa nyumba Dodoma na Dar es Salaam, zinazohudumiwa na Serikali kwa asilimia mia moja kuanzia samani mpaka *house keeper* na *house girl* na gharama hizi zinajumuisha makazi yote ya Dar es salaam na Dodoma. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Serikali ingeamua moja, kusingekuwa na matumizi haya ya fujo na badala yake fedha hizi zingetumika kununua madawa, vifaa tiba, vifaa vya hospitali na zingeweza kuboresha maisha ya walimu, shule na kuinua maisha ya Watanzania kwa ujumla. Naomba kutoa ushauri kwamba, kama Serikali imeona sababu za kuhamishia Makao Makao ya Serikali zimepitwa na wakati na nisisitize ni kweli zimepitwa na wakati, basi siyo dhambi kusema kwamba Makao Makuu yawe Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba, Serikali imekamilisha taratibu za kuanzisha Halmashauri mpya 31 ili kusogeza huduma karibu na Wananchi na moja ya Halmashauri hizo ni ya Wilaya ya Ikungi (Singida); ningeomba Halmashauri hii ipewe kipaumbele ili ianze kufanya kazi kwa sababu Halmashauri ya sasa ya Wilaya ya Singida inajumuisha majimbo matatu; Singida Magharibi, Singida Mashariki na Singida Kaskazini. Mkurugenzi anaelemewa na uzito mkubwa wa kuendesha Halmashauri hii kutokana na ukubwa wa eneo na hivyo shughuli za utawala kutokuwa na ufanisi.

Nahitaji majibu ni lini Halmashauri hii itaanzishwa ili kuwahusisha watendaji katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba nzuri, lakini pia ninapongeza uendeshaji mzuri wa shughuli.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kupewa Wilaya mpya. Huku ni kulifanya Jimbo la Kyerwa kuwa Wilaya mpya ya Kyerwa pamoja na Halmashauri ya Kyerwa.

Tunashukuru mpango wa kuanza shughuli za ujenzi. Tunaomba utaratibu huu wa ujenzi uende haraka.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pesa zinazotolewa kwa kila Wilaya kwa ajili ya ujenzi zisilingane. Kyerwa toko pembezoni na mfuko wa *cement* ni shilingi 24,000, Morogoro ni shilingi 14,000, tofauti shilingi 10,000.

Vilevile mafuta ya Diesel Kyerwa ni shilingi 2,600, Morogoro shilingi 2000. Ninapendekeza tupewe haki sawa lakini wa pembezoni tuongezewe *hardship factor* ya kufidia bei ya vifaa.

Mheshimiwa Spika, dawa ya upotevu wa pesa dawa kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (*Internal Audit Unit*). Mkaguzi wa Nje anafaa lakini husubiri mambo yaishe ndiyo atuletee kilio wakati pesa imekwishaliwa. Yeye hutuletea yaliyoisha. Anayezuia ni *Internal Audit.* Yupo kwenye shirika. Tuwape nguvu, tuajiri wasomi. Utaratibu wa kuwa na *Supreme Internal Auditor* ufanye kazi vizuri. Wawe huru.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, ninachukua fursa hii kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu katika mambo ya msingi kama nitakavyoandika na kueleza kwa ufupi na umakini.

Mheshimiwa Spika, Dunia inapitia kwenye wakati mgumu sana wa changamoto ya mazingira na Taifa letu kama sehemu ya Dunia, tunaishi katika changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, kama hatua muhimu na za hakika zisipochukuliwa kuhusu suala la mazingira, hakika ni kwamba, Taifa letu na Dunia kwa ujumla, litaingia kwenye wakati mgumu na mbaya siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, ningependa niishauri Serikali itilie mkazo wa makusudi katika suala la mazingira na Serikali kupitia Halmashauri zake itengeneze mikakati ya upandaji miti na itungwe sheria ambayo italazimisha kila kaya zenye nafasi katika makazi yao kupanda miti kwa lazima, kwani hakuna sababu tena ya kuangalia Taifa linakuwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile Halmashauri zetu kote nchini, zitengeneze *plan* za upandaji miti katika Halmashauri zao bila kujali aina na *location* ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kila kinachofanyika leo katika Taifa letu, kitaendelea sana kutegemea hali bora ya nchi yetu hasa katika Sekta hii muhimu ya Mazingira.

Hivyo basi, ni bora Serikali ikaona umuhimu mkubwa wa ustawi wa Taifa letu utathibitika kwa kujenga na kuimarisha mazingira katika nchi yetu katika mikakati mbalimbali na suala la mazingira lipewe kipaumble muhimu sana. Kwani tofauti na hivi, Taifa letu litapotea na kuwa sehemu mbaya ya kuishi kwa vizazi vinavyokuja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuongelea ni uwajibikaji; kuna tatizo kubwa sana katika Idara mbalimbali za Serikali na hata Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa umakini sana, ukifanya utafiti utagundua kuwa Ofisi mbalimbali za Serikali zinaendeshwa bila kuzingatia sheria, maadili na haki za kazi. Hii inasababishwa na kutokuwepo na dhana ya kujitoa na kuwajibika, ambayo pia imesababishwa na uzembe wa matumizi ya akili ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kuiomba Serikali itafute njia maalum na muhimu kusaidia kujenga uwezo kwa watu wake hasa wafanyakazi kutambua umuhimu wa kufikiri chanya, kwani mambo mengi yanakwama kwa sababu ya uwezo duni wa kufikiri ambao unasababishwa na kutokuwepo na uwajibikaji kwanza katika fikra ambako ndiko kunakoanzia nguvu ya fikra na uwezo wa kufanya na kushinda.

heshimiwa Spika, maji ni uhai, katika Jimbo langu la Uchaguzi la Arusha Mjini, Wananchi wengi takriban asilimia 70 hawana maji safi au hawapati maji bora na salama.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali itambue kuwa, suala la maji haliwezi kujadiliwa muda mrefu bila ufumbuzi, kwani hakuna mbadala wa maji katika maisha ya binadamu; hivyo basi, Watanzania wa Arusha wamechoka kuvumilia kuishi bila maji. Wanaitaka Serikali iwajibike mara moja siyo kutafuta sababu na changamoto kwa nini watu hawana maji bali kutafuta *solution* ya kuleta maji haraka iwezekanavyo kwani familia na watoto wanateseka sana na mimi kama Mbunge wao nimechoka kuvumilia kuona mateso yao.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwa vile maji ni uhai, basi Serikali itaangalia kwa makini suala hili ambalo ni tatizo nchi nzima na hasa Arusha.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala la kero za Muungano, kwani limeundiwa kamati ambayo ni ya muda mrefu na mpaka sasa si chini ya miaka 40. Cha ajabu, kila kikao hiki kikikaa, hatuambiwi lolote kuhusiana na ufumbuzi wa kero hizo. Mfano, katika Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 14 na 15 ameelezea kuwa,

Tume hiyo imekutana, yaani kutoka SMT na SMZ, lakini hatujui nini kinaendelea mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tuambiwe kinachoendelea katika Tume hiyo ili kujua nini kinaendelea katika Tume hiyo kuhusiana na masuala yote ya kero za Muungano ambayo bado ni kero kubwa. Toka Tume iundwe mpaka sasa ni muda mrefu, lakini hakuna hata kero moja iliyopatiwa ufumbuzi, ni vyema kujua kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU imekuwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wake kama ambavyo inaelezwa katika kifungu cha 57 cha Sheria ya TAKUKURU. Kinainyima Taasisi hii mamlaka ya kushtaki katika kesi kubwa kubwa (Nyangumi) na kupewa tu mamlaka ya kushitaki vidagaa (kesi ndogo ndogo). Hii ni hatari na pia Taasisi hii inahujumiwa haki ama nafasi ya kufanya kazi zake kwa kina na upana zaidi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 27 cha Sheria ya Takukuru kinahusu wanaojilimbikizia mali na katika suala hili kuna kesi zisizopungua 100 Mahakamani. Hivyo ni vyema kesi za Taasisi hii ziwekewe mfumo maalum wa kumalizwa haraka bila ya kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya TAKUKURU inayoeleza adhabu dhidi ya mhalifu ina upungufu kwani adhabu kubwa au faini kubwa mwisho wake ni shilingi milioni 10 tu, wakati wahalifu wanaona pesa hizo ama adhabu hiyo kwao si kitu. Napendekeza sheria hii ya adhabu na faini iangaliwe vizuri na pia adhabu ama faini ithaminishwe na uzito wa kosa au thamani ya kiasi ambacho mhalifu amekutwa nacho.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushahidi (*Evidence Act),* ambayo tunaitumia Tanzania imepitwa na wakati

kwani ni ile ya mwaka 1872 ya India. Hivyo, ni vigumu kwa Sheria hii iliyopitwa na wakati kuleta haki na ushahidi wake pia upo ki-*technically* zaidi. Ni vyema pia *Evidence Laws* tunazotumia ziwe zinalingana na wakati ndiyo itatenda haki zaidi.

Hivyo basi, maoni yangu ni kuongeza Wafanyakazi wa TAKUKURU kwani ni wachache. Pia sheria zote zenye upungufu na hasa nilizozitaja hapo juu, zifanyiwe marekebisho ili kuondoa kero katika Taasisi hii na kuongeza ufanisi. Vilevile ipewe mamlaka ya kushtaki kesi za aina zote (Nyangumi na Vidagaa) ili kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Bila kuisahau Bajeti yake kwani yote hayo bila ya ongezeko la bajeti hayawezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, tumeona baadhi ya Kambi za Jeshi zinazalisha chakula lakini bado wanalipa mzabuni kwa kuwauzia chakula na kununua toka kwake hali ya kuwa hanunui nafaka ama vyakula vinavyolimwa katika Kambi hizo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwe na sheria inayomlazimu mzabuni kununua vyakula kutoka katika Kambi husika; mfano, mahindi, mchele, mayai ya kuku, matunda na kadhalika. Kufanya hivyo, kutapelekea kupungua gharama za kulipia chakula.

Mheshimiwa Spika, katika Kambi za Jeshi ni vizuri kuwe na mafunzo ya kiufundi ya *VETA* ili kuwasaidia vijana waliopo kambini kuwa na ujuzi na endapo anatoka Kambini au kuhitimu mafunzo, aondoke na ujuzi wake ambao utamsaidia anapokwenda kuweza kujiajiri na siyo kusubiri kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, namna ya kuajiri vijana wanaomaliza mafunzo yao, kuwe na utaratibu maalum

unaotumika kwani utaratibu uliopo sasa unaonekana kuwa na sura ya upendeleo na kuwakatisha tamaa vijana ambao hawana ajira, hali ya kuwa wanafahamu vizuri namna ya kutumia silaha na kubaki mtaani bila ajira yoyote. Hivyo, ni rahisi kwao kuingia katika magenge yasiyofaa. Kuwajengea *VETA* wataondoka na ujuzi na kuutumia uraiani endapo watakosa kuajiriwa na kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na maafa mbalimbali yaliyopoteza watu wengi kwa muda mfupi bila ya kupatiwa ufumbuzi; mfano, kuzama kwa Meli ya Mv Bukoba, watu wengi walipoteza maisha bila kuokolewa. Vivyo hivyo katika Mv Spice na Mv Skaget. Isitoshe pia kumekuwa na tatizo la vifaa vya uokoaji hata kwa upande wa nchi kavu.

Mfano mzuri, juzi tu kama siku mbili kabla ya Bunge hili, watu wawili wamepoteza maisha kwa kukosa msaada wa uokozi. Hivyo basi, mapendekezo yangu kwa eneo hili ni suala la kuwa na vyombo vya uokozi.

Katika bajeti hii ya ni vizuri Serikali kutenga kiasi maalum kwa ajili ya maafa, siyo tu kwa kutoa pole au fidia kwa waliopatwa na maafa, bali ni vyombo vya kuokolea watu ambavyo vitatumika kuokolea maisha ya watu endapo patatokea suala lolote.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, reli ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. Reli ya Kati haifanyi kazi ipasavyo na kusababisha magari makubwa ya mizigo kuharibu barabara zilizojengwa kwa gharama kubwa.

Serikali itoe kipaumbele katika kutengeneza Reli ya Kati ili pia iongeze mapato kwa kubeba mizigo ya nchi jirani za DRC, Rwanda na Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Spika, Serikali isaidie wakulima kupata soko la mazao yao, wanahangaika sana kuuza Tumbaku, Pamba, Korosho, Pareto hata mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, pembejeo haziwafikii wakulima kwa wakati na kuathiri mazao na kukatisha tamaa wakulima.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji ni kubwa sana Mkoani Tabora na hasa Wilayani Urambo. Serikali ina mpango gani wakuwapatia maji?

Mheshimiwa Spika, Wafanyakazi hawatoshi katika Hospitali na Zahanati. Utaratibu uliopo wa kuwapata wafanyakazi uangaliwe upya ili wapatikane katika zahanati hasa vijijini. Urambo kuna zahanati tatu hazina wafanyakazi na zimekamilika zikiwa na nyumba za wafanyakazi.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri zishirikiane na Baraza la Madiwani ili ziruhusiwe kuwaajiri watumishi, badala kutegemea TAMISEMI kuajiri watumishi wa ngazi zote wakati wanaokuwa karibu na watumishi hao ni Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi kuna watumishi wengi wanakaimu nafasi za Ukuu wa Idara na wanakaimu kwa muda mrefu. Naomba Serikali iliangalie hili ili walio na sifa waweze kuthibitishwa kwenye nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, *Tender Board* iunganishe Madiwani wote na watoe maamuzi ya pamoja, isiwe Wakuu wachache wanatoa mapendekezo na kufanya kazi hiyo kuwa ngumu. Wapo baadhi ya watu hutoa tender kwa marafiki au ndugu zao na kushindwa

kufanya kazi kama inavyotakiwa na hivyo kuleta usumbufu.

Mheshimiwa Spika, naomba vijiji ambavyo vina matatizo ya umeme ambavyo viliahidiwa kuupata tangu bajeti ya mwaka 2011 vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, maji ni kero kubwa; Jimbo la Korogwe Vijijini maji ni kero kubwa sana, naomba Serikali iangalie suala hili.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA**: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi (TAMISEMI) na Manaibu wake, pamoja na Watendaji wa Wizara kwa kuanza kuifufua Misungwi kutoka katika wizi uliokithiri hadi kufikia hati yenye mashaka, kwa sababu ya *Audit Queries* zaidi ya 100. Vikao vya Halmashauri ya Wilaya sasa vinafanyika kwa utulivu na kwa muda mfupi na kwa kujadili *issues* badala ya mrundikano; tunaomba hali hii ilindwe na kudumishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya matatizo ambayo yamekuwepo kwa zaidi ya miaka 15, naomba Wilaya hii iangaliwe kwa jicho la huruma ili Wananchi waweze kupata huduma ambazo kwa muda mrefu hawakuzipata. Naomba tupewe Wakuu wa Idara katika eneo la Ujenzi, Afya, Maji na Afisa Elimu Sekondari.

Mheshimiwa Spika, vilevile nashukuru kwa kupata *DED, DT* na Afisa Mipango, ambao wameonesha ushupavu na mabadiliko yameonekana.

Mheshimiwa Spika, Binadamu hatuishi kuomba, lakini hii inasababishwa na hali halisi; mwaka jana tulikuwa na ukame tukawa na njaa, mwaka huu tumepata mafuriko na Wananchi wengi hawana

makazi, tunaomba msaada wa haraka. Kuzisaidia familia ambazo hazina mahala pa kukaa (zaidi ya familia 100) vilevile miundombinu ya barabara imeharibika sana na vijiji vingi havifikiki kabisa. Tunaomba msaada wa haraka kurudisha mawasiliano katika maeneo haya. Vilevile msaada wa haraka wa chakula katika maeneo yaliyoathirika utolewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na yenye kuleta matumaini makubwa kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iiangalie upya Sheria ya Manunuzi *(PPRA)* ili kuondoa urasimu, gharama kubwa na kusababisha baadhi ya Miradi kutotekelezwa; kwa mfano, uchimbaji wa kisima cha maji chenye gharama halisi kuwa shilingi milioni 40, lakini kwa kupitia Sheria ya Manunuzi *(PPRA),* gharama hizo hufikia shilingi milioni 400! Huu ni upotevu mkubwa wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa mbolea ya ruzuku kwa vikundi kupitia Benki uangaliwe vizuri na usianzishwe mwaka wa fedha wa 2013/2014 ili Serikali iweze kufanya matayarisho ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naipongeza hotuba yake kwa maelezo mapana na ya kina.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa dhati jitihada za Serikali za kuwaletea maendeleo Watanzania. Hata hivyo, napenda kutoa ushauri kuhusu matumizi ya Serikali ambayo yanakua kwa kasi mwaka hadi mwaka ikilinganishwa na mapato ya ndani (mapato yatokanayo na kodi, mapato yasiyotokana na kodi na mapato ya Halmashauri).

Kulingana na sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/2014, Bajeti itakuwa na nakisi ya shilingi takriban trilioni mbili. Hii inamaanisha kuwa, makusanyo yetu ya ndani hayakidhi hata matumizi ya kawaida na hivyo kutegemea misaada na mikopo ya kibajeti kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo. Kwa kipindi kirefu, Serikali imekuwa ikiahidi kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, lakini kwa kiwango kikubwa ahadi hizo haziendani na hali halisi, kwani matumizi ya maendeleo hadi sasa hayajafikia asilimia 35 ya matumizi yote kama Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unavyotaka.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iangalie upya matumizi yake, kama ununuzi wa magari ya kifahari, gharama za kuendesha na kutunza magari hayo, semina, kongamano na warsha, posho na kadhalika. Serikali ije na mkakati unaoonesha itakavyopunguza matumizi mengi yasiyo ya lazima ili *savings* zielekezwe kwenye matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye Mradi wa Kuimarisha Miundombinu na uwezo Katika Miji (*Urban Local Government Strengthening Project – ULGSP)*, ambao ulianza kutekelezwa na Serikali katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013. Mradi huo katika awamu ya kwanza ya miaka mitano, unahusisha Halmashauri za Manispaa kumi na moja na Halmashauri za miji saba ikijumuisha Mji wa Bariadi ambao pia ni

Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa makubaliano kati ya Serikali yetu na Benki ya Dunia, kigezo cha msingi cha kugawa rasilimali fedha chini ya Mradi huo ni idadi ya watu wanaoishi katika mipaka ya Halmashauri husika. Wakati Mradi huu unaasisiwa, Mji wa Bariadi ulikuwa na wakazi wasiopungua sitini elfu. Jambo la kushangaza na kusikitisha, takwimu zinaonesha kwamba, Mji wa Bariadi ulikuwa na wakazi 15,000 tu.

Mheshimiwa Spika, napenda wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha hoja yake, awaeleze Wakazi wa Mji wa Bariadi nini hasa kilichojiri na hivyo kupelekea kupindisha kwa makusudi idadi ya wakazi wa Mji wa Bariadi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uamuzi huu wa udanganyifu ni kuunyima Mji wa Bariadi na Wakazi wake (watu 154,500 kwa Sensa ya Watu na Makazi 2012), mgao stahiki wa rasilimali fedha. Ukweli huu unadhihirishwa na mgao wa fedha unaopendekezwa kwa Halmashauri za Miji saba kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kama inavyooneshwa katika *Vol. IV Part A* kama ifuatavyo:-

| **Mji** | **2013/2014** |
|---|---|
| Kibaha | Sh. 276,864,000/= |
| Geita | Sh. 259,560,000/= |
| Babati | Sh. 229,896,000/= |
| Mpanda | Sh. 168,096,000/= |
| Korogwe | Sh.192,816,000/= |

| | |
|---|---|
| Njombe | Sh.121,128,000/= |
| Bariadi | Sh. 54,384,000/= |

Mheshimiwa Spika, nashauri Wakazi wa Mji wa Bariadi watendewe haki kwa kupewa mgao stahiki wa rasilimali fedha kwa kuzingatia idadi halisi ya Wakazi wa Mji huo na siyo idadi ya kufikirika ambayo imetumika.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha maeneo mapya ya kiutawala, yenye tafsiri ya kusogeza huduma karibu na Wananchi. Utaratibu huu umeanzisha Wilaya mpya ya Kalambo na Halmashauri ya Kalambo, yenye Makao Makuu yake Mji Mdogo wa Matoi.

Kwa kuzingatia umuhimu wa ujenzi unaozingatia makazi bora, Uongozi wa Wilaya ya Kalambo ulisitisha ujenzi na kutopimwa viwanja mpaka mpango kabambe *(Master Plan)* iwe tayari ili kujenga mji wa kisasa, wenye kuainisha vizuri maeneo na matumizi yaliyowekwa bayana.

MheshimiwaSpika, pamoja na jitihada nzuri za Wilaya na Halmashauri kuhakikisha ujenzi unaofanyika baada ya *Master Plan* kuwa tayari, ni jambo lisiloingia akilini kwamba, Serikali haijatenga pesa kwa ajili ya kutayarisha *Master Plan.* Cha kushangaza zaidi, pesa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi na nyumba za watumishi. Tafsiri yake ni kuomba ofisi

na hizi nyumba zijengwe bila kuzingatia utengaji na matumizi bora ya ardhi na kupanga miji yetu.

Naiomba Serikali ihakikishe kwamba, pesa inatengwa ili *Master Plan* iweze kuandaliwa kwa kutumia Chuo Kikuu cha Mbeya *(MUST),* kwani tumeshafanya nao maongezi ya awali, lakini pia kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili kufanikisha suala hili.

Mheshimiwa Spika, kupatiwa kinyemela mali ya Watanzania Shirika la Usagishaji la Taifa Arusha; juzi niliuliza swali nikitaka Serikali ifanye utafiti juu ya bei halisi ya zao la mahindi na bei ya unga wa sembe.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuongeza thamani kwa kusaga mahindi na kuwafikishia Wananchi kwa bei nafuu, hauwezi kufikiwa kwa kuiachia sekta binafsi kwani nguvu ya soko kwa mazingira yetu haiwezi kuwa ufumbuzi wa kumhakikishia mlaji bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, ni suala lisiloingia akilini, kuchukuwa Shirika la Usagishaji lililokusudiwa kusaga mahindi ili kusambaza sembe kwa mlaji kwa bei nafuu, itakayomfikia mlaji wa kipato cha chini na kumkabidhi mtu binafsi, ambaye *motive* kwake yeye ni *profit maximization* bila kujali *purchasing power* ya mlaji. Naiomba Serikali iingilie kati mkataba tata huu kati ya huyo anayejiita mwekezaji asiyekuwa na mtaji wowote na kuchukua *miling machine* kwa manufaa yake.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Pili, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uongozi wake mzuri wa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015. Hata hivyo, nina hoja mbili ninazopenda kuchangia.

Kwanza, je, kuna mikakati gani mahususi ya kupunguza maambukizi ya UKIMWI/VVU kwa wasichana wa umri wa miaka 23 -24?

Hakika nimeshtuka sana na takwimu ya viashiria vya Malaria na UKIMWI 2011/2012 iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Machi, 2013, ambapo pamoja na mengineyo, inaonesha kuwa, maambukizi ya UKIMWI/ VVU kwa wasichana wa umri wa miaka 23 - 24 ni asilimia 6.6, ukilinganisha na wavulana wa umri huo asilimia 2.8.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni hatari sana ya kufikia maambukizi ‘o’ na ni changamoto kubwa sana katika mapambano dhidi ya UKIMWI Tanzania. Wanawake na wasichana hawa ndiyo hasa wapo katika kipindi cha uwezo wa uzazi.

Je, ni vipi tutaweza kufikia maambukizi sifuri? Je, ni kwa nini vijana wa kiume wa umri huu maambukizi ni madogo kuliko kwa wasichana?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu - *TACAIDS* itueleze ina mikakati gani mahususi na ya haraka ya kupambana na maambukizi ya Ukimwi/ VVU kwa wasichana wa umri huu wa miaka 23 - 24? Naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika Halmashauri ulianzishwa kutokana na Azimio la Bunge Mwaka 1993 na kupitishwa rasmi na Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mwezi Agosti, 1993.

Kwa mujibu wa Waraka wa Serikali, Halmashauri za Wilaya na Mji zina wajibu wa kuchangia asilimia tano ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya kuchangia Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona Halmashauri nyingi zinachangia kidogo au hazichangii kabisa Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, sihitaji kueleza umuhimu wa Mfuko huu kwa maendeleo ya wanawake na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Mfuko huu ndiyo mkombozi wa kweli wa wanawake hasa walio vijijini katika kupata mikopo yenye masharti na riba nafuu kwa ajili ya kupata mitaji ya kuendesha shughuli mbalimbali za kujipatia kipato.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nipatiwe maelezo Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ina mikakati gani ya kuhakikisha Halmashauri za Wilaya na Miji zinachangia asilimia tano ya mapato ya ndani kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NAMELOK E. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi nyingi duniani bado haujaimarika na huenda itachukua miaka mingine miwili ama zaidi hali ya kiuchumi iimarike. Pamoja na misukosuko hiyo ya kiuchumi, nchi yetu imeweza kuendelea kufanya vizuri, uchumi wetu umekua kwa asilimia 6.9. Hakika tunastahili kujivunia mafanikio hayo. Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto zinazotukabili, kwani ukuaji huo wa uchumi haujawafikia Wananchi wote, si wa mijini wala vijijini. Kwa wastani pato la Mtanzania kwa mwaka sasa limekua na kufikia Sh. 995,298.00, yaani Sh. 82,941.50 kwa mwezi. Kiasi hiki kikilinganishwa na gharama halisi za maisha ni dhahiri hakitoshi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dkt. Mohamed Bilal, Waziri Mkuu

- Mheshimiwa Mizengo Pinda, Katibu Mkuu Kiongozi - Mheshimiwa Balozi Sefue na Viongozi wote wa Serikali, kwa uamuzi wa kuanzisha utaratibu mpya wa mfumo wa kusimamia utekelezaji, ufuatialiaji na tathmini ya Miradi ya Maendeleo *(PEMADU).*

Tumeelezwa kuwa chini ya Mpango huo nchi itaweza kupata maendeleo ya haraka. Maeneo yaliyojadiliwa na kupewa kipaumbele ni sita. Kilimo ni moja ya maeneo hayo ya kipaumbele. Mpango huu ukifanikiwa, pamoja na mikakati mingine inayotekelezwa ya kuinua kilimo, tutaweza kufikia Usalama wa Chakula *(Food Security*) na kuwa na ziada ya kuuza nje. Pato la Taifa na la mkulima litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kuwa, tusipobadili mikakati yetu, bado tunaendelea kuwa wauzaji wa bidhaa ambazo hazijaongezwa thamani. Ni vizuri Serikali ikaangalia umuhimu wa kuongeza Sekta ya Viwanda katika Sekta zilizopewa umuhimu wa kwanza chini ya utaratibu wa *PEMADU.*

Sekta ya Kilimo inavyoendelea kukua, Sekta ya Viwanda nayo inatakiwa ikue, tuzalishe bidhaa zilizoongezwa thamani kwa ajili ya soko la ndani na la nje. Hii itatusaidia kupunguza uagizaji wa bidhaa ambazo tunaweza tukazalisha wenyewe na tukaokoa fedha zetu za kigeni. Tukabaki kuagiza bidhaa ambazo uzalishaji wake nchini ni ghali na ambazo hatuna uwezo wa kutengeneza.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu imepewa kipaumbele chini ya utaratibu wa *PEMADU.* Pamoja na mikakati mbalimbali iliyopo na itakayobuniwa ya kuendeleza Sekta nzima ya Elimu, ningeshauri umuhimu wa pekee uwekwe kwenye mafunzo ya ufundi (*Technical Course*), kwa kiwango cha *Certificate* na

*Diploma*. Nchi kama Ujerumani, Japani na zingine nyingi, hazikuendelea kwa vile zina ma-*engineer* wengi. Naomba nieleweke kuwa, sina maana ya kuwa tusiwe na ma-*engineer,* la hasha, maana yangu ni kuwa kazi kubwa zinafanywa na wenzetu wenye *Certificate* na *Diploma* kwani wao wanakuwa wameandaliwa kwa ajili ya *hands on the job* kwa kufuata maelekezo ya ma-*engineer*.

Mheshimiwa Spika, tukiweza kuwa na wataalam wengi wenye *certificate* na *diploma,* tutaweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo, kwani uzalishaji viwandani na hata katika Sekta ya Kilimo utaongezeka. Ili kupata wataalam hao, lazima tuwe na utaratibu utakaowavutia vijana wetu wengi kuchukua kozi za *certificate* na *diploma*. Tunatakiwa tuwathamini na mishahara yao iboreshwe iweze kuwavutia.

Aidha, tuendeleze mpango uliopo sasa wa kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe na kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo ambavyo vitatengeneza bidhaa bora za viwango vya kimataifa. Hatua hiyo itasaidia kupunguza umaskini na tutakuwa tumefanikiwa kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilipochangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nilielezea matatizo ya ardhi tunayokumbana nayo wenyeji wa Mkoa wa Arusha. Lipo tatizo la ardhi kati ya Wilaya ya Monduli na Wilaya ya Longido, lipo tatizo la ardhi kati ya Wilaya ya Arumeru na Longido, halikadhalika Wilaya ya Ngorongoro.

Tunaomba matatizo haya yatafutiwe ufumbuzi kwani yanagharimu maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W.),* kwa neema na rehema zake kwangu na nchi yetu kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni tatizo kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa rushwa kubwa za mikataba na uwekezaji. *PCCB* pamoja na juhudi zake za kupambana na rushwa, lakini bado haina nguvu za kisheria za kupambana na rushwa kubwa. Utashi wa kisiasa unahitajika sana ili Taasisi hii ipewe nguvu za kisheria kupambana na rushwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, udini, yaani ubaguzi katika kutoa haki za raia kwa kuangalia dini zao au watu kunyimwa fursa au kutokuwa na uwazi ni tatizo. Kuondoa tatizo hili ni kuweka uwazi katika kila hali kwa maendeleo ya watu wetu na nchi. Haki sawa kwa wote ndiyo dawa pekee ya kuimarisha amani na utulivu wa nchi yetu hii nzuri ambayo wengi hawaipendelei mema.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi na umaskini wa Wananchi wetu; katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo 2012/2013, ukurasa wa pili; mwaka 2012 uchumi ulikua kwa asilimia 6.8 na mwaka huu 2013 kwa asilimia 7.0. Vigezo hivi ni kwa mujibu wa *IMF*. Suala hapa ni kwa namna gani uchumi unakua lakini hali ya maisha ya Wananchi inazidi kuwa mbaya au ni kulingana na maslahi wanayoyapata *IMF* kutoka kwetu? Maslahi yao yakiongezeka uchumi umekua na yakipungua uchumi umeshuka?

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam na ubovu wa miundombinu. Dar es Salaam ndiyo sura ya nchi yetu, uchafu uliokithiri na mifereji ya maji machafu iliyoziba na isiyokidhi, inatia aibu haiba ya uzuri wa jina

la Jiji letu (Dar es Salaam). Barabara zote zina mashimo yasiyozibwa daima.

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeshindwa kazi na badala yake inaongeza tatizo la uchafu Jijini kwa kupandisha zaidi ya asilimia 100 ada ya kuzoa taka ngumu. Kila kaya sasa (nyumba) ni Sh. 5,000/= kwa mwezi badala ya Sh. 200/=; maduka ya rejareja Sh. 30,000/= badala ya Sh. 10,000/=; *restaurants* Sh. 150,000/= badala ya Sh. 30,000/= na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni Sh. 150,000/= badala ya Sh. 30,000/=.

Pamoja na ada hizo kupanda kwa kiwango kikubwa sana, huduma zinazotolewa haziridhishi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo la kutowajibika ipasavyo kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam, kuna tatizo la mwingiliano wa kimaslahi kwa Taasisi za Serikali zinazosimamia Jiji la Dar es Salaam. Hii inasababisha kazi zisifanyike.

Mheshimiwa Spika, nashauri Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ivunjwe na iundwe Taasisi moja tu itakayosimamia shughuli zote za Jiji la Dar es Salaam ikiwemo Barabara za Jiji, majengo yote na hata viwanja vilivyoko katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Katiba, Sheria na Utawala Bora; Katiba ni nguzo kuu na dira ya kuongoza nchi.

Mchakato unaoendelea wa kutafuta Katiba Mpya, naiomba na kuisihi Serikali iiwekee mfumo usiohongeka na Tume isipotoshe wala isijipotoshe yenyewe ili jambo hili kubwa, zuri na muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu hii nzuri, liende vizuri na liishie

vizuri ili tupate Katiba mpya nzuri itayotuelekeza kubadilisha utawala na uongozi vizuri bila ya chuki, fitna, bugudha na bila kupigana wala kubaguana kwa misingi ya dini, kabila, jinsia na hata eneo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mwenyezi Mungu, atuongoze katika njia nzuri na atuepushe na shetani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kimsingi, sababu zinazotolewa kuhusu kutokuanza rasmi Halmashauri ya Mji wa Kasulu ni za kisiasa zaidi. Sababu kubwa inayotupiwa kapuni eti idadi ya Madiwani ni ndogo kutokana na kile wanachodai TAMISEMI kwamba, kuna Kata tano ambazo hazijafanyiwa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, hizo Kata tano ni Kata hewa, ambazo zilikuwa zianzishwe mwaka 2010 kabla ya uchaguzi, lakini hazikuanzishwa hadi leo hii. Hivyo, madai yataanzishwa rasmi Halmashauri ya Mji wa Kasulu ni kutowatendea haki Wananchi wa Kasulu hasa ikizingatiwa kwamba, tayari Serikali ilishatangaza kuwepo kwa Halmashauri hiyo. Tatizo limebaki kwa TAMISEMI kuipatia Mkurugenzi, Wakuu wa Idara na *full mandate* ya kuanza kuisimamia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya uchache wa Madiwani siyo sahihi na sababu ya kuzuiwa kuanza kwa Halmashauri hiyo hasa kwa sababu Halmashauri ya Mji wa Kasulu ina Kata nane za uchaguzi wa Madiwani na Viti Maalumu, ambao kwa ujumla wao wanaweza kufikia 15 au zaidi kwa sasa. Hiyo ni idadi inayowezesha Halmashauri kuanza na hivyo kuwawezesha Wananchi kupata huduma karibu kwa urahisi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taarifa zisizo rasmi zinazodai kwamba, lengo la kuzuia kwa Halmashauri hiyo ni za kisiasa pamoja na CCM kuhofia kupoteza nafasi za Uwenyekiti za Halmashauri za Wilaya za Kasulu na hii mpya ya Mji wa Kasulu.

Nimeona inawezekana ikawa na ukweli hasa ikizingatiwa kwamba, hata ilipokuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kasulu, bado kulikuwa na mizengwe mingi kwa Wenyeviti wa Vitongoji kukosa fursa za kukaa katika Baraza. Hakuna Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kasulu lililowahi kukaa tangu uchaguzi wa Serikali za Mtaa wa 2009 hadi Mamlaka ya Mji wa Kasulu ilipotangazwa kwa mara nyingine 2011 kuwa ni Halmashauri ya Mji wa Kasulu.

Wenyeviti wa Vitongoji wamehoji sana juu ya hali hiyo, ilhali Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kasulu imekuwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka isiyokuwa na Baraza. Kwa maoni na uwelewa wangu, hali hiyo ni kinyume cha Sheria, ni kama njama za ubadhirifu wa fedha na Mali za Umma. Tujiulize huyo Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo na sasa ni Halmashauri ya Mji wa Kasulu anasimamiwa na nani kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iachane kabisa na mfumo wa kufanya mambo yake kisiasa, kwa kuwa kufanya hivyo ni kukwamisha maendeleo ya nchi yetu. Vyama vya Siasa vitufanye sisi Wanasiasa na Wananchi kuwa maadui.

Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, apime sababu hizi yeye mwenyewe na kisha ajaribu kuwa *objective* sana katika kufanya maamuzi juu ya hilo na ninaamini atakuwa pamoja nami Mbunge wa Kasulu Mjini, kwa kuwa nimeelewa kinachoendelea kufanyika dhidi ya kutoanzishwa kwa Halmashauri hiyo ya Kasulu.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nianze na uchumi. Tukiangalia takwimu kama zilivyoainishwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kueleza kuwa mfumko wa bei umepungua kutoka asilimia 19.4 mwezi Februari, 2012-2013.

Sambamba na jitihada za Serikali, lakini bado maisha ya Watanzania ni magumu na gharama za vyakula na bidhaa zinazidi kupanda. Hivyo, ni vyema Mheshimiwa Waziri Mkuu anapofanya majumuisho, alieleze Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, ni hatua gani ya dharura zitachukuliwa na Serikali ili kupunguza makali ya maisha kwa Watanzania ili angalau kila Mtanzania apate milo miwili kwa siku.

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunaendela kujadili mafanikio ya Serikali kupunguza mfumko wa bei na kuona gharama za maisha zinapanda, nauli za usafiri zinapandishwa kiasi kwamba hata usafirishwaji wa bidha utakuwa wa shida na gharama za bidhaa zitapanda bei mara mbili. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ajaribu kuangalia hali halisi ya Watanzania na suala hili la kupanda kwa nauli liangaliwe upya kwa faida ya Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, Elimu ni sekta nyeti lakini lenye matatizo makubwa na ambayo yanahitaji utatuzi wa dhati na wa haraka ili kukuza Elimu.

Elimu ya msingi, ndiyo elimu mama lakini imetupwa na haipewi kipaumbele. Kwa manufaa ya Taifa, kama Serikali ingeweza kutatua matatizo na upungufu unaoikabili Sekta hii, nina imani elimu ingepanda.

Mheshimiwa Spika**,** katika Hotuba ya Waziri Mkuu, ameongelea maendeleo ya miundombinu ya elimu

ikiwa ni mafanikio ya MMEM I na MMEM II. Matatizo ya elimu ni mengi na yanaonekana na hatuwezi kusubiri Mpango wa MMEM kuboresha na kutatua matatizo hayo, kwani hali ni mbaya hasa vijijini. Wanafunzi wanasoma katika mazingira magumu sana, walimu wanafundishwa katika mazingira hatarishi; hawana vitendea kazi, hawana nyumba za kuishi, wana madai mengi ambayo hayana ufumbuzi wa kulipwa. Hali hii ndiyo huchochea migomo baridi ambayo husababisha watoto kufeli, kwani muda mwingi walimu wanakuwa kwenye shughuli binafsi za kutafuta kipato ili waendeshe maisha yao badala ya kuwa darasani kufundisha watoto.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwa Shule za Sekondari, wakiwa na misingi mibovu, wanaendelea kuwa wabovu, hivyo kufanya elimu kushuka kwa kiwango kikubwa. Naomba Serikali iangalie upya suala la elimu kwa manufaa ya Taifa, huku ikiboresha Sekta ya Ukaguzi. Idara ya Ukaguzi au Kitengo kipewe kipaumbele kwa kupewa fungu zuri ifanye kazi ya ukaguzi katika elimu na kubaini upungufu inaoikabili Sekta hii ya Elimu. Tusilie na mchawi; mchawi wa Sekta ya Elimu ni mipango mibovu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ipitie upya Mipango ya MMEM na MMES ili kuboresha utekelezaji wa miundombinu ya elimu kwa faida ya Umma.

Mheshimiwa Spika, tatizo la vituo vya utoaji huduma za afya nchini hasa vijijini bado linahitaji ufumbuzi kwani kule ndiyo kuna wazalishaji wakubwa kiuchumi. Vituo vingi vya afya havina madawa ya kutosha, pia vifaa na vitendea kazi. Hospitali za Mkoa hazina mashine za kupimia magonjwa kama Xray na kadhalika. Zahanati za Vijijini ndiyo kabisa, dawa zinapelekwa chache na ni wiki moja tu zimekwisha,

Wananchi wanaelekezwa kwenda kununua dawa zile zile za *MSD* katika maduka ambayo mengine wamiliki ni madaktari. Je, Serikali inatamka nini kwa madaktari wanaochukua dawa za Serikali na kwenda kuuza katika maduka binafsi?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapojumuisha Hotuba hii, nipewe majibu mazuri. Ahsante.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, TAMISEMI ijikite kukamilisha uhakiki wa mipaka ya kiutawala hasa ile ya Wilaya ya Kiteto na Chemba, Kiteto na Kilindi, Kiteto na Gairo na Chamwino na Kongwa.

Ili kumaliza migongano kati ya Wakulima na Wafugaji, kila Halmashuri nchini ipewe *time frame* ya kuandaa *framework* ya kutenga maeneo ya makazi, huduma, kilimo, ufugaji na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, naiomba TAMISEMI iimarishe Kitengo cha Ukaguzi ili kudhibiti ubora wa ufundishaji na viwango stahiki vya elimu ya sekondari.

Kozi maalumu ianzishwe Hombolo na kila Mtendaji wa Kijiji alazimike kufuata kabla ya kuanza kazi. Kozi hii itumike kujenga weledi kwa Watendaji wa Vijiji. Hii itasaidia kuongeza ufanisi wa utawala na maendeleo vijijini.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Hotuba nzuri. Hata hivyo, napenda kutaka kujua mambo yafuatavyo:-

1. Kanda ya Ziwa imekuwa tegemezi kwa chakula kwa Mikoa ya Kusini licha ya uwingi wa maji

katika Maziwa na Mito; lakini pia kutokana na hatua ya kulisha idadi kubwa ya watu walioko Kanda ya Ziwa. Je, ni lini Serikali itaanzisha mpango maalum wa kilimo cha umwagiliaji katika Kanda ya Ziwa kama ilivyofanya kwa *SAGCOT* Kusini mwa Tanzania?

2. Pensheni ya Wazee iliyoahidiwa na Serikali kwa miaka miwili mfululizo lini itatekelezwa?

3. Tangu mwaka 2011 wahitimu wa vyuo vya kilimo hawaajiriwi na Serikali licha ya uhaba mkubwa wa wagani katika Vijiji na Kata. Pamoja na uhimizaji wa Sera ya KILIMO KWANZA; ni lini Serikali itatoa ajira kwa vijana hawa?

4. Tatizo la mgongano kati ya wakulima na wafugaji sasa limekuwa sugu katika nchi yetu kama vile hakuna Wataalam wa Mifugo, Kilimo, Ardhi, Maji na kadhalka. Serikali imeshindwa kuitambua Sekta hii na jinsi ambavyo ingeweza kulipatia Taifa letu pato kubwa kutokana na mauzo ya wanyama hai, nyama, ngozi, maziwa na mazao mengine na hivyo kuishia kwenye ushabiki tu wa wafugaji na wakulima, badala ya kutafuta suluhu za kitaalam na kufanya Sekta hiyo ilete utajiri kwa wafugaji na Taifa. Masuala yanayohusu mifugo yanagusa Wizara nyingi; ni lini sasa Serikali italiangalia suala hili kwa dhati badala ya ushabiki na uonevu wa *DCs* na *RCs?*

5. Mipango ya kuendeleza Shule za Sekondari za Kata inachukua muda mrefu sana kiasi cha kufanya wanafunzi wengine wasipate elimu bora. Ni lini kwa hakika ujenzi wa shule mbili kwa kila Halmashauri utaanza? Ni lini ujenzi wa nyumba za walimu utaanza? Hivi vyote vimesemwa kwenye mipango ya Serikali tangu mwaka juzi. Tunapenda vitendo.

6. Kamati ya Maafa imeonesha udhaifu mkubwa katika ugawaji wa chakula kwani nimeshuhudia chakula kikigawiwa bila uwiano. Maeneo ya Vyama vya Upinzani ndiyo yanapata chakula; hivi njaa ina ubaguzi? Kuna hujuma katika Kamati hii inabidi imulikwe.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nianze na utulivu na amani katika nchi yetu. Ni wajibu wa Serikali kusimamia na kuhakikisha amani inaendelea kuwepo, bila kuogopa kuchukua hatua pale inapobidi ili kunusuru hali hii. Pia ni wajibu wetu sote kama Viongozi kuhimiza umoja na mshikamano wetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti ambazo tunapitisha katika Bunge lako hazitekelezeki kwa kukosekana kwa fedha. Fedha hazipelekwi kwenye Halmashauri yetu; kwa mfano, Hospitali ya Wilaya ya Mpanda imepokea *Basket Fund* mpaka mwanzo wa *Quarter* ya mwisho, shilingi 243 milioni katika shilingi 972 milioni zilizotengwa. Kwa hali hiyo, hatuwezi kuona matokeo tunayotarajia. Aidha, Hospitali ya Mpanda ipo katika hali mbaya ya uchakavu wa majengo na upungufu wa wodi. Kwa kuwa sasa Mpanda ni Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi, ipo haja na ulazima wa kujenga Hospitali ya Mkoa ili kuinusuru Hospitali ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Elimu; kuna upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa, madawati, vitabu na matundu ya vyoo katika shule nyingi nchini. Kwa mfano Shule ya Msingi Mbuguni iliyopo katika Jimbo langu, watoto 262 tu ndiyo ambao wanakaa katika madawati na watoto 1071 wanakaa chini kwa Shule yenye wanafunzi 1333. Ipo hoja Serekali kuwa na mpango mahususi wa muda mfupi au mrefu wa kukabiliana na hali hii.

Upungufu wa walimu katika Shule zetu za Msingi na Sekondari ni tatizo ambalo halijapata ufumbuzi, lakini pia maslahi na madai ya walimu kutoshughulikiwa, tunavunja ari kwa walimu wetu na matokeo yake yanaonekana katika mitihani ya mwisho kwa wanafunzi kufeli kwa kupitiliza. Bila kuboresha hali na maslahi ya walimu, tutaendelea kuiona hali na matokeo haya ya kufeli kwa watoto wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wa Mpanda kwa mapendekezo yao wanataka eneo la kutoka Milupwa, Mpanda Mjini hadi Mtisi liwe eneo lao. Nashindwa kujua eneo la Mihama kama lilivyopendekezwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu limependekezwa na nani? Wachimbaji wadogo katika maeneo yao wasiondolewe.

Mheshimiwa Spika, barabara za kuunganisha Mkoa wa Katavi na Rukwa – Kigoma – Tabora ni lazima sasa ziwekwe katika mpango wa Serikali kwa umuhimu unaostahili. Kazi ya ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Kibaoni umechukua muda mrefu bila kukamilika na kuongeza gharama; ni lini sasa barabara hii itakamilika? Barabara za Mpanda – Kigoma, Mpanda – Tabora zinahitaji matengenezo makubwa na ya haraka baada ya hizi nvua za masika.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo katika nchi yetu, ningependa kujua mkakati na mpango wa muda mrefu au mfupi wa kukabiliana na tatizo la maji na uvunaji wa maji ya mvua ili kuongeza akiba ya maji.

Mheshimiwa Spika, imefikia wakati sasa wa kuhakikisha Wazee wanapata Bima ya Afya ili wawe na uhakika wa kupata madawa kama ilivyo sasa, kwani wana dirisha la kupata matibabu bure, wakati dawa za matatizo yao hazipo katika Hospital zetu. Uwepo

utaratibu wa kupewa kibali cha kuchukua dawa katika maduka ya dawa maalum na Halmashauri ilipie dawa hizo ili nia ya kuwatibu bure wezee iwe imetekelezwa.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya fedha za Umma na usimamizi wake ni wakati mwafaka sasa wa kuwawajibisha watendaji ambao wameshindwa kujibu hoja za Mkaguzi na pale inapobidi wafikishwe Mahakamani. Tusipofanya hivyo, hali hii itaendelea mwaka hadi mwaka na hoja hazina majibu. Hatua hizo zichukuliwe sasa.

Mheshimiwa Spika, usafiri na usafirishaji unatumia fedha nyingi katika Halmashauri zetu, lakini hazifahamiki kwa kuwa Kitengo cha Usafirishaji kipo chini ya Ofisi ya Utawala, wakati katika kila Halmashauri yupo Afisa Usafirishaji, ambaye anawajibika kwa Mkurugenzi. Kitengo hiki hakina bajeti mahususi ya kukiendesha na wala kushirikishwa katika mipango ya bajeti; hivyo, inapelekea wakati fulani kutoa fedha katika Miradi ya Maendeleo ili magari na vyombo vya moto vipate fedha za kujiendesha, kwa sababu hakuna fedha inayotengwa na kiasi kinachotengwa hakitoshelezi gharama halisi ya Kitengo hiki na wala hakuna taarifa zinazotolewa katika Mabaraza ya kujua hali halisi ya vyombo vya moto katika Halmashauri na gharama za uendeshaji.

Ningependa kujua mkakati wa Serikali kufahamu gharama za Kitengo hiki na maelezo kuhusu matengenezo ya magari ya Serikali na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa misimu ya kilimo inafahamika; kwa nini sasa pembejeo zinachelewa kufika kwa wakati? Vilevile ningependa kujua ni kwa nini msimu uliofuata mgawo wa mbolea katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda ulipungua na kuleta

malalamiko mengi kwa Wananchi na nini mpango bora wa kupata mbolea za vocha na husused kwa wakulima wanaoishi mijini?

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme katika Mji wa Mpanda limekua la kujirudia kwa uchakavu wa mitambo ya kuzalisha umeme na upatikanaji wa vipuri. Ningependa kufahamu ahadi ya Serikali kuleta *engine* mpya mbili inatekelezwa lini ili kuondoa adha iliyopo sasa ya mgao wa umeme?

Kwa kuwa mahitaji ya umeme yanaongezeka kwa kasi na ili kuwa na umeme wa uhakika ni lini sasa Serikali itaunganisha Mji wa Mpanda na Mkoa wa Katavi na Rukwa katika Gridi ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kufahamu ni lini sasa Miradi ya Umwagiliaji katika Jimbo la Mpanda Mjini, Kata ya Kakese na Mwamkulu itakamilika kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mpunga katika eneo letu na kuongeza pato kwa wakulima? Miradi hii imekuwa ya muda mrefu, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu itoe maelezo ya kutosheleza na ahadi ya kukamilishwa kwa Miradi hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Elimu; sheria ibadilishwe au ifanyiwe marekebisho kulingana na mazingira, kwani shule nyingi za Sekondari za Kata hazina Wajumbe wa Bodi. Hii ni kutokana na kutokupatikana kwa Wajumbe hao, kulingana na sifa zilizoainishwa na pia kukosa fedha za kulipa Bodi hizo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa hauna hata Chuo kimoja cha Ufundi cha *VETA,* Serikali ijenge Vyuo hivyo.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali itanzue migogoro ya mipaka kwa kuzingatia *GN* ya 1961. Mgogoro wa Sikonge na Manyoni pale Kijiji cha Makale, Kitongoji cha Matagata na Kijiji cha Kajui, Kitongoji cha Mwamatiga, naiomba Serikali ichukue hatua za haraka kumaliza tatizo hili lililosababishwa na Wilaya ya Sikonge kutwaa maeneo hayo kinyume cha utaratibu. Tatizo pia lipo upande wa Chaya mpakani na Wilaya ya Chaya. Taarifa juu ya matatizo ya maeneo hayo imewasilishwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), muda mrefu sasa. Naomba awaite na kuwaagiza Wakuu wa Mikoa wa Tabora na Singida wamalize tatizo hili mapema.

Mheshimiwa Spika, kusuasua kwa Miradi; mfano, Barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya inayojengwa na Kampuni ya *Sino-hydro-corporation*. Barabara hii yenye urefu wa km 89 inayojengwa kwa kiwango cha lami, inasuasua na iko nyuma ya muda uliopangwa na imepangwa kumalizika Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, iko nyuma kutokana na Mradi huu kucheleweshewa fedha mara kwa mara. Fedha za ndani hazitolewi kwa wakati. Naishauri Serikali itoe fedha kwa wakati au la ikope kwa wafadhali kama ilivyofanya kwa Barabara ya Iringa – Dodoma – Kondoa ambapo Japani imekopesha shilingi 127 bilioni kuijenga Barabara hii. Aidha, fedha za kigeni zinachelewa kutolewa na wafadhili au kutotolewa kutokana na watendaji wetu kutowasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi kwa wakati; inasikitisha. Naishauri Serikali iwachukulie hatua watendaji hawa ili wapate

kuwajibika. Ni kweli kuwa bado tunahitaji msaada wa wafadhili katika kuijenga nchi yetu, fedha zinapokwama kwa sababu ya uzembe ni kuhujumu juhudi nzuri za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Manyoni kuna maelezo au ahadi ya Serikali iliyotolewa kujenga Bandari ya Nchi Kavu Manyoni, eneo la Iwelewele mpakani mwa Wilaya ya Manyoni na Wilaya mpya ya Ikungi. Eneo hilo limepimwa na Wananchi kuarifiwa wajiandae kupisha, lakini inastua kuona Iwelewele au Manyoni haikutajwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itupe majibu ili tuweze kuwaeleza Wananchi ukweli ni upi. Majengo ya kuanza kwa Mradi huu yapo pale mpakani, tuliomba tupatiwe Wilaya ya Manyoni kwa ajili ya Chuo cha Ufundi, lakini taarifa ikatolewa kuwa yametengwa kwa ajili ya Bandari ya Nchi Kavu. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa – Makongolosi – Mbeya, iko kwenye Ilani ya Chama na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nyumba zimepigwa X muda mrefu sasa, lakini bado hatujaona dalili zozote za maandalizi ya ujenzi wa barabara hii muhimu sana. Naomba majibu ya suala hili ambalo limegeuka kuwa kero na kuwatia watu wetu wasiwasi wa kama wafanye ujenzi kupisha barabara au la.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida kuwa maskini zaidi ya Mikoa yote nchini, tunaomba takwimu sahihi juu ya kauli ya Serikali maana takwimu haziendani na hali halisi ya maendeleo ya Mkoa huu. Umeondokana na nyumba nyingi za tembe na nyasi na kilimo cha alizeti na tumbaku kimeinua Wananchi wengi; mfano, karibu nyumba nyingi zina usafiri wa baiskeli na pikipiki.

Mheshimiwa Spika, tunaomba matrekta mengine ya *Farmtrack* na *New Holland* yaletwe kwa wingi Mkoa wa Singida. Wananchi wengi wamejiandaa kununua.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali kutafsiri Sera na Mkakati wa Kukabiliana na Maafa, ambavyo vimetayarishwa kwa Lugha ya Kiingereza. Nyenzo hizo zitafsiriwe kwa Lugha ya Kiswahili, tena chepesi, ambacho Watanzania wataelewa watakapovisoma.

Mheshimiwa Spika, tumeona jinsi gani nchi yetu imefanya vizuri katika mashindano ya kushindanisha vivutio vya kitalii kupitia Taasisi ya *The seven Natural wonders*.

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro, *Ngorongoro Crater* na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, vilitupatia ushindi lakini tujiulize Tanzania tuna vivutio vingapi? Ni imani yangu kwamba, kama tunaweka nguvu katika maeneo yetu ya kitalii, Tanzania itakuwa kiongozi Barani Afrika katika utalii. Ukiangalia maeneo ya kihistoria ya Mikindani, Mtwara, Kilwa, Kaole na Mbuga Kubwa ya *Selous,* tunaweza kufanya vizuri kupindukia. Ni jukumu la Serikali kuwekeza vya kutosha katika kuboresha maeneo haya ili kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia utalii.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa ninaiomba Serikali ianzishe Utalii wa Baharini, tuna Bahari nzuri ya Hindi, ambayo itasaidia kuongeza mapato kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa ilivyo sasa, uanzishaji wa Kijiji, Kata, Tarafa,

Wilaya na Mkoa mpya, kunategemea sana aina ya Uongozi unaokuwepo wakati huo, kupenda au kutopenda kugawika kwa maeneo na hii inasababisha maeneo mengine kubaki makubwa sana kiutawala. Mfano ulio hai ni Wilaya ya Mbiga.

Nashukuru kwamba tumepata Wilaya ya Nyasa; hata hivyo, Mbinga ya sasa bado ni kubwa, ina Tarafa sita, Kata 34 na Vijiji 160. Jimbo la Mbinga Mashariki, mipaka yake ndiyo hiyo. Hivyo, ni Wilaya kubwa na Jimbo pia ni kubwa.

Serikali inaweza kuendelea na utaratibu uliopo, lakini napendekeza kwamba, iunde jopo la wataalam watakaoangalia mipaka ya maeneo ya Wilaya, Mikoa na Majimbo ya Uchaguzi na ipendekeze mipaka mipya kuzingatia idadi ya watu na hali halisi ya maeneo. Maeneo mapya yanaanza, Serikali ijiandae kukusanya vitendea kazi na si kugawana samani chakavu na majengo katika Halmashauri mama.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* linasemekana linatumia karibu shilingi bilioni tano kwa siku; hii inachangiwa na matumizi makubwa ya *diesel*. Sioni kwa nini Serikali kupitia *NDC* au Taasisi nyingine zozote ikiwemo *TANESCO,* isijenge mtambo wa kufua umeme pale Ntunduwaro Mbinga, pamoja na kujenga *transmission lines* ili kusambaza umeme vijiji vyote vya Mbinga na ziada kuingiza Gridi ya Taifa na hivyo kuachana na *Diesel.*

Jambo hili siyo vyema tukawaachia wageni peke yake. Kuhusu wachimbaji wadogo; naomba maeneo ya Kitai, Amani Makoro, Paradiso, Ruanda, Ndongosi na Mkako, yatangazwe kuwa maeneo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wa kampeni 2010, Mheshimiwa Rais, aliwaahidi Wanambinga yafuatayo:-

(i) Ujenzi wa barabara za Mbinga – Litembo (Hospitali); na Nyoni – Maguu – Mkoha, kwa kiwango cha lami;

(ii) Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbinga kupewa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbinga;

(iii) Wakulima wanaodai Chama cha Ushirika – *MBICU* shilingi milioni 400.4 kulipwa; na

(iv) Kilichokuwa Chuo cha Ualimu Mbinga na sasa *Mbinga Day Secondary* kuwa tena Chuo cha Ualimu.

Mheshimiwa Spika, wakati hatua fulani fulani zimechukuliwa kuanzia (i) – (iii), hakuna chochote kuhusu namba (iv). Naomba chuo chetu kirudishwe.

Mheshimiwa Spika, Wafanyabiashara wa Kahawa Mbinga wameiomba Serikali ifikirie kuwapa fidia ya hasara waliyoingia katika msimu wa 2012/13, baada bei za kahawa kushuka kuliko bei elekezi.

Mheshimiwa Spika, tatizo sugu la maji Mbinga Mjini na Vijiji vya Kata ya Litumba Ndyosi; chanzo cha maji Mbinga Mjini kina maji mengi lakini Mji hauna maji. Pia Vijiji vya Luhagara, Mabuki, Litumba Ndyosi na Kingoli vina adha kubwa ya maji. Wilaya haiwezi, naomba msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hali ya Hospitali ya Wilaya ni nzuri hasa *Theatre,* lakini Wilaya haina magari ya wagonjwa *(Ambulances)* hata Hospitali ya Wilaya haina *Ambulance.*

Naomba mgawo ufikirie Mbinga. Mji unakua na una mahitaji makubwa ya gari la kunyonya maji machafu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa maandishi katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kweli hupatikana tu pale ambapo pana amani na utulivu wa kweli. Nchi yetu imejaliwa amani na utulivu, hii ni tunu tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Zaidi, tuwashukuru sana Waasisi wa Taifa letu, Mwalimu Nyerere na Mzee Abeid Aman Karume, kwa kutuachia tunu hiyo ya amani na utulivu.

Hivyo basi, amani na utulivu huo usichezewe hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iwadhibiti wanasiasa wote wanaochochea vurugu nchini. Serikali ionekane inatawala, isiruhusu maandamano yanayoitishwa na baadhi ya wanasiasa ambayo lengo lake ni kujenga au kuleta chuki kati ya Serikali na Wananchi. Amani na utulivu wa nchi yetu ilindwe kwa gharama yoyote ile kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, viwango vya pensheni vinavyolipwa kwa wastaafu wetu ni vya chini sana. Kiwango cha chini kabisa ni shilingi 51,000 kwa mwezi; hebu fikiria mtu ambaye ametumia karibu nusu ya maisha yake katika utumishi wa nchi yake, anastaafu na kuishia kulipwa shilingi 51,000; huyu mtu ataishi maisha gani kama siyo kudhalika?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iliangalie suala hili upya kwa kurekebisha viwango vya pensheni viendane na hali halisi ya maisha ya wakati huu. Sanjari na hilo, naomba Serikali iendelee kuangalia uwezekano wa kulipa pensheni kwa wazee zaidi ya miaka 60, ambao hawana uwezo na ambao hawakuwa Watumishi wa Maofisini au Serikali, ili nao pia waweze kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kabisa, wapo wazee wengi vijijini ambao hupoteza maisha kwa sababu ya kukosa huduma muhimu kama vile matibabu, chakula, malazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu mpya wa mbolea ya ruzuku 2013/2014 utakaohusu utoaji wa mikopo kupitia vikundi vya wakulima, utakuwa na tija tu iwapo wigo wa watakaofaidika utaongezeka. Aidha, utaratibu huo utakuwa na manufaa zaidi iwapo mikopo itakayotolewa itamuwezesha mkulima kulima zaidi ya ekari moja. Nataka pia kujua ni kwa kiwango gani Serikali imejiandaa kuona utaratibu huu mpya hautaleta usumbufu kwa wakulima. Je, riba za mabenki hazitakuwa mzigo kwa wakulima; na je, masharti ya mabenki hayatakuwa kikwazo kwa wakulima? Haya niliyoyasema ni baadhi tu ya mambo ambayo yasipoangaliwa, yanaweza kukwamisha utaratibu mpya wa mbolea ya ruzuku kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kufanya mazungumzo na Chama cha Walimu (CWT) kuhusu maslahi ya walimu na makundi mengine.

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu inayodhaniwa kusababisha matokeo mabaya ya Kidato cha Nne mwaka 2012 ni mgomo baridi wa walimu. Inadhaniwa walimu walitumia njia hiyo kueleza

kutoridhishwa kwao na mishahara yao pamoja na marupurupu mengine.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mahakama iliagiza kwamba, Serikali iendelee kuzungumza na CWT kuhusu mishahara na marupurupu yao; lakini baadhi ya vyombo vya habari vilitoa taarifa kwamba, Serikali haipo tayari kuendelea na mazungumzo na walimu kupitia Chama chao cha CWT.

Kama habari hizo zina ukweli, basi siyo za heri sana, maana njia ambayo walimu wanaweza kuendelea kuitumia ni mgomo baridi. Sote tunajua kwamba, wanapogoma walimu wanaoathirika ni wanafunzi, lawama haziendi kwa walimu bali kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iendelee kuzungumza na CWT na ni imani yangu kwamba, kama Serikali itawasikiliza na wakakubaliana, basi itakuwa heri zaidi kwa wanafunzi. Sanjari na kuangalia mishahara na marupurupu ya walimu, Serikali iendelee kuangalia na kuongeza mishahara na marupurupu kwa Watumishi wote Serikali, kwani ni ukweli mishahara ya Watumishi wengi wa Serikali ipo chini sana, hailingani kabisa na hali halisi ya maisha inayosababishwa na mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. RACHEL R. MASHISHANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mambo kadha wa kadha katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunaposema hali ya uchumi wa nchi na Mtanzania imekua, tunaamanisha kuna

*some indicators* ambazo zinaonesha hali ya uchumi kukua, lakini nachokiona hapa ni uwingi wa magari barabarani pengine ndiyo *indicator* ya uchumi kukua.

Mheshimiwa Spika, tunasema pato la Mtanzania limeongezeka sijui tunalipima vipi wakati asilimia 80 ya Watanzania hali zao ni mbaya, pengine mpaka wameshasahau kunywa chai na pengine hawajui walikunywa mara ya mwisho lini. Sukari imezidi kupanda hadi kufikia shilingi 1950 kwa kilo, ambapo mwaka jana ilikuwa shilingi 1500. Mchele nao yale yale na mikate nayo imepanda bei. Hili suala la kupanda pato la Mtanzania liko wapi wakati Watanzania wanaahirisha kula na kunywa kwa sababu ya mfumko wa bei?

Mheshimiwa Spika, nionavyo mimi, pato hili limeongezeka pengine kwenye mifuko ya matajiri na si kwa Watanzania waishio vijijini na pengine mijini lakini ni hohehahe.

Mheshimiwa Spika, suala la upatikanaji wa maji vijijini na mijini limekuwa ni kitendawili kisichoweza kuteguka. Maeneo mengi ya nchi hasa vijijini, yamekuwa yanaongoza kutokuwa na maji safi na salama. Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana kuchimba visima virefu ambavyo havitoi maji kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu ya Serikali kuhusu kutumia fedha nyingi kuchimba visima visivyotoa maji. Halmashauri zote zina wahandisi na *technicians* ambao wangeweza kusaidia kwa kuyatambua maeneo ambayo yanaweza kuchimbwa visima na maji yakapatikana. Sasa hawa wahandisi wanafanya kazi gani? Fedha zinazopotea ni bora zikaelekezwa kwenye maeneo ambayo yana ukame lakini visima vikichimbwa maji yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie sana suala hili kwani fedha nyingi zinapotea bila kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, suala la madini ni nyeti sana, lakini limejaa migogoro baina ya Wananchi na wachimbaji au watafiti pamoja na wachimbaji wadogo na wakubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la utoaji wa leseni za utafiti na uchimbaji. Kumekuwa na matatizo mengi ambayo yanatokana na utoaji holela wa leseni za utafiti, utaratibu unaotumika sasa siyo mzuri kabisa kwani unaleta mgongano kati ya Wananchi na Watafiti.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa leseni siyo rafiki hata kidogo, suala la kutoa leseni wakati umekaa ofisini na *computer* yako kwa kuangalia kwenye *google* au ramani siyo haki. Ninaomba Serikali ihamishe kitengo hiki kwenye Mikoa husika ili zoezi lifanyiwe *field* kuepuka usumbufu na migogoro itakayojitokeza mara baada ya utafiti kupewa leseni wakati kuna Wananchi wanaishi pale miaka nenda rudi.

Mheshimiwa Spika, vile vile watafiti hawa na wachimbaji hawa wamekuwa wakiripoti kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya tu, huku Wabunge na Madiwani wa maeneo husika hawashirikishwi; na hii inajenga kutoheshimiana kwa wanasiasa hawa na makampuni hayo ya uchimbaji na utafiti.

Kiufupi, wanasiasa wanadhalilika sana mbele ya makampuni haya wakati ndiyo hasa wawakilishi wa Wananchi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, mara makampuni haya yanapokwenda kuripoti kwa Wakuu

wa Mikoa na Wilaya, basi yafanye hivi kwa Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya mwaka wa fedha wa 2011/12, alisisitiza sana Watanzania kutumia vyandarua vinavyotolewa na Serikali (vibajaji), havifai kabisa kwani havina *(TBS)*. Viwango ni vyandarua ambavyo ni vifupi sana, kwa sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa ni mtihani kuvitumia kwani miguu yote inakuwa nje.

Mheshimiwa Spika, nafikiri vyandarua hivi walipimwa watani zangu kutoka Morogoro, maana wao vinaweza kuwatosha hata wasipochomekea.

Naiomba Serikali iviangalie upya kwani asilimia kubwa vinatumika kukuzia mboga, kuku (vifaranga) au kufanyia *fence* kwa ajili ya kuzuia kuku kuharibu mboga katika bustani.

Siyo hilo tu, hata baadhi ya minara ya simu wamekuwa wakivitumia kuziba mitambo yao ili nyuki wasijenge.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na nia njema kabisa kutoa vyandarua, lakini naomba viwe na ubora unaoridhisha ili hata sisi warefu tuweze kuvitumia bila kuvichomeka jamani!

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa. Naomba kuwasilisha.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mipango ya kusaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha mapato yake na sasa inaongea na Benki ya Rasilimali *(TIB),* ambayo imeonesha nia ya kuzikopesha Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naishauri TAMISEMI iweke utaratibu na kuzielekeza Halmashauri kuwa wazi na kufuata taratibu zinazotakiwa, zitakazowezesha Madiwani wote kupata taarifa na kushiriki kupitia Mabaraza ya Madiwani katika hatua zote za ukopaji. Ushiriki wa Madiwani wote utaondoa malalamiko au migogoro kama inavyotokea katika Halmashauri ya Manispaa Bukoba.

Mheshimiwa Spika, vipo viporo vingi vya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri zetu na hata Miradi ya Kimkoa ambayo imeshindwa kumalizika; mfano, madarasa, vituo vya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa ianze kujikita katika kuikamilisha kabla ya kupanga Miradi mipya. Miradi inayohitaji fedha nyingi, ipangiwe muda maalum wa kukamilika; hivyo, Serikali itenge fedha za kutosha katika muda uliopangwa, Mradi ukamilike kabla ya kupanga Miradi mipya; mfano ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, itazame upya makadirio ya gharama za manunuzi ya vifaa vya ujenzi na matumizi (*Quatations*) mengine. Makisio haya yanakuwa juu kulinganisha na bei za kawaida na hivyo Miradi hutumia gharama kubwa kuliko inavyopaswa kuwa na kushindwa kukamilika.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi yapo katika nyumba ya kupanga; hii huisababishia Tume kulipa pango la Sh. 234,387,648/= kwa mwaka.

Kwa miaka kumi wanalipa Sh. 2,340,387,648/=. Pesa ambazo zinatosha kujenga jengo zuri la ghorofa sita hadi saba. Kwa nini Serikali haitoi fedha likajengwa jengo badala ya kupangishwa kwa gharama kubwa kiasi hiki? Tatizo hili lipo katika Ofisi nyingi za Serikali ambazo zimepanga kwa gharama kubwa sana. Serikali ifikirie ni namna gani ya kufanya, iwe ni kwa kukopa katika mashirika makubwa ya kimataifa au kutoa fedha yenyewe, lakini iondokane na kupanga majengo kwa ajili ya Ofisi za Serikali kwa gharama kubwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda niende kwenye kero sugu ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kulipishwa kodi mara mbili.

Mheshimiwa Spika, juu ya kuwa suala hili lilizungumzwa mwaka uliopita na kwa kuwa kero hii ilipatiwa ufumbuzi kuwa bidhaa yoyote itakayoingizwa nchini kupitia kituo chochote cha forodha kilichopo ndani ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, basi hazipaswi tena kulipa ushuru mara mbili.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe ufafanuzi ni hatua gani za kisheria na kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya Maafisa na Watendaji wa Serikali, walioshindwa kutekeleza maagizo haya yaliyotolewa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie kuhusu Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Chombo hiki ni kwa nini hakipewi mamlaka ya kuweza kuchunguza na kupeleka Mahakamani moja kwa moja badala ya kupeleka kwa *DPP*? Chombo hiki kikipewa mamlaka haya, basi kitaweza kupunguza rushwa nchini. Naishauri Serikali iongeze fedha katika Fungu la Taasisi hii ili waweze kufanya kazi katika Mikoa yote nchini.

**MHE. REBECCA MICHAEL MNGODO:** Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu imejulikana kwamba, Makampuni ya Simu au Mawasiliano, hayalipi kodi stahiki. Kodi ndiyo inayosaidia katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Mfumo wa kuratibu huduma za mawasiliano unaojengwa na Serikali *(Traffic Monitoring System),* uharakishwe kwa kutengewa fedha za kutosha ili kuleta ufanisi katika Sekta ya Mawasiliano kwa kudhibiti na kukusanya kodi stahiki kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la ugaidi ambalo limeibuliwa hapa Tanzania, limeichafua Tanzania katika sura ya Dunia. Huenda hata watalii wengi wamepata hofu ya kutembelea Tanzania kwa kuhofia uwepo wa ugaidi, ambao bado hatuna uhakika kama ni kweli upo. Ni vyema Serikali ikawa makini katika kushughulikia masuala yote yanayoweza kutupotezea amani kwa kutumia utaalam iliyo nayo badala ya ku-shout katika vyombo vya habari kuhusu ugaidi ambao haujathibitishwa. Hii itasaidia kulinda sifa ya nchi yetu na hivyo kuendelea kuwa na mawasiliano mazuri na nchi nyingine za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya elimu hapa nchini siyo ya kuridhisha. Asilimia sitini ya wanafunzi waliofeli ni kuwaharibia watoto wetu maisha yao ya baadaye. Kwa kuwa ni jukumu la Serikali kuangalia maisha ya kila Mtanzania yanakuwa bora, Serikali iangalie jinsi ya kuwaokoa wanafunzi hao kutoka shimo walilotumbukia. Ikibidi, wanafunzi hao wapatiwe nafasi ya kurudia mwaka mwingine na Serikali iweke mazingira mazuri ya kufanya hivyo. Pia inawezekana kabisa wanafunzi wakaangaliwa upya maksi zao kwa kulinganisha matokeo hayo na yale ya *Mock* na hivyo kupata ulinganisho wa matokeo hayo ili kuwasaidia watoto hawa kwani ni kweli kabisa maisha yao ya baadaye

yanategemea msingi wao ulivyo. Serikali pia iharakishe katika kuweka maslahi mazuri ya walimu ili kuwapa motisha katika kazi yao ambayo ni ya muhimu sana katika kutujengea wataalamu wa kesho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, hali ya mazingira ya utoaji elimu hapa nchini bado hairidhishi. Shule nyingi za Kata, kwa utafiti uliofanywa na *Tanzania Coalition on Debt and Development (TCDD), January 2013*, zipo katika mazingira ya pori, siyo salama kwa wanafunzi kwa kukosa uzio na pia siyo rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Katika utafiti huo, shule nyingi zilionesha wanafunzi wengi kutembea kuanzia kilometa tano hadi kumi hasa maeneo ya vijijini. Umbali wa kilometa kumi wanaotembea wanafunzi kwa siku ni sawa kilemeta 50 kwa wiki.

Hali hii pia huchangia kuporomoka kwa elimu na ongezeko la mimba kwa wanafunzi wa kike. Kuna umuhimu wa kutengeneza utaratibu utakaoondoa adha hii kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu ikiwemo ujenzi wa mabweni. Maeneo yaliyofanyiwa utafiti ni Masasi, Mbarali, Morogoro, Kibaha, Kiteto na Iramba. Kimsingi, maeneo mengi ya Tanzania, hali ya vijijini hairidhishi; shule nyingi hazina maktaba, maabara, umeme, vyoo vya kutosha, nyumba za walimu, madarasa ya kutosha na majiko ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa elimu ndiyo msingi wa maisha, Serikali iongeze nguvu na kuweka umuhimu mkubwa katika suala la elimu na mazingira bora ya elimu hapa nchini; vinginevyo, tunarudi nyuma badala ya kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha nyingi za Serikali zinazotengwa kwa ajili ya kufanikisha na kutekeleza shughuli za maendeleo, fedha hizo hazitumiki

zote bali asilimia fulani huishia katika mifuko ya maafisa wasio waaminifu. Ni vyema Serikali ikazingatia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* aliyoitoa Juni, 2012 na hivyo kuwachukulia hatua wale wote ambao wamehusika na uzoroteshaji wa maendeleo na ubadhirifu wa fedha za maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya *CAG* iko wazi na itakuwa ni jambo la kushangaza kama haitafanyiwa kazi. Ni muhimu wale wote waliobainika kutotimiza wajibu wao kwa uadilifu, wakachukuliwa hatua za kinidhamu na hata kushitakiwa mahakamani, kwani ushahidi ni Ripoti hii ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ripoti inasema kwamba, bado mishahara hewa inaendelea kulipwa katika baadhi ya Halmashauri zetu. Shilingi 693,132,772 zililipwa katika Halmashauri 24, ikiwa kama mishahara kwa wastaafu, watoro, watumishi waliofariki, watumishi walioacha kazi au walioachishwa kazi kupitia akauti zao za benki.

Mheshimiwa Spika, mapato ya shilingi bilioni 3.9 yalipotea katika Halmashauri ya Arusha kutokana na Halmashauri kutoza bei ya chini ambayo ilikuwa na tofauti kubwa kulinganisha na bei ya soko na vibanda walivyopangisha ambavyo vinamilikiwa na Halmashauri. Ripoti hiyo inaonesha kuwa, hati za malipo ya shilingi 4,996,689 na viambatanisho vyenye jumla ya shilingi 1,075,263,998 havikuwasilishwa wakati wa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua kali haraka kwa wale wote waliohusika kutoza bei ya chini tofauti na bei iliyopangwa katika Halmashauri hii ya

Arusha, kwani ni kuipotezea Serikali mapato ambayo yangeweza kutumika katika kukwamua hali yetu ya elimu, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali ya uwindaji haramu hapa ndani katika Mbuga zetu za Wanyama bado inaongezeka badala ya kupungua. Ripoti ya *CAG* inathibitisha kuongezeka kwa uwindaji haramu; je, wanaohusika na usimamizi wa wanyamapori wamechukuliwa hatua gani za kisheria? Uwindaji haramu haukugundulika leo, hatua za kinidhamu zingekuwa zinachukuliwa dhidi ya wasimamizi wa wanyamapori, wasingelegea katika kutimiza wajibu wao. Tembo 110 katika mbuga saba waliuawa mwaka 2011/12, jambo ambalo linaathiri sana Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wizi wa fedha za Serikali umeendelea kuonekana katika baadhi ya Halmashauri kwa kutozingatia Taratibu na Sheria za Manunuzi. Serikali ichukue hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine na hivyo kutumia kwa usahihi fedha zinazopelekwa katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, zao la chai ni tegemeo la Wananchi wengi Wilayani Rungwe. Chai inalimwa na wakulima wakubwa ambao wana kiwanda chao kimoja kinachofanya kazi na wakulima wadogo ambao pia wana viwanda viwili. Wakulima wadogo wameunda Chama chao cha *RDTGA*, ambacho kinaendesha viwanda vyake kwa ubia na *Wakulima Tea Company (WATCO). WATCO* au *RSTGA* inatoa ruzuku ya mbolea, inasaidia ujenzi wa shule na zahanati na ukarabati wa barabara. Maelewano yametoweka kati ya wakulima wakubwa

na *RSTGA*, kwa sababu wakulima wakubwa wanakwenda vijijini kununua chai (ambayo ni haki ya *RSTGA)*, kwa kisingizio cha soko huria.

Mheshimiwa Spika, mashamba ya wakulima wakubwa yakiangaliwa vizuri, yanaweza kutoa majani ya kutosha kwa kiwanda chao. Matokeo yake ni kwamba, Kiwanda cha *RSTGA/WATCO* kinapata uhaba wa majani ya chai na kina hatari ya kufungwa. Suala limefikishwa Wizara ya Kilimo muda mrefu, napenda kupata taarifa ya hatua iliyofikiwa na Serikali katika mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, changamoto ya udini ni kansa inayoligawa Taifa letu kwa kasi sana. *Sentiments* za udini *is real* huko mitaani. Viongozi wa Dini wanaeneza pia sumu hii. Misikiti na Makanisa vinatumika kugawa sumu hii kwa waumini wao.

Misikiti na Makanisa yametumika kuelekeza Wananchi wao kupiga kura kuchagua Wananchi wenzao kwenye Mabaraza ya Katiba. Mfano, ipo na ni dhahiri maana sisi Viongozi tunasali na kuswali kwenye Makanisa na Misikiti hii.

Hapa Bungeni, Wabunge huchagua wawakilishi mbalimbali kwa misingi ya dini. Suala hili ni dhahiri. Tatizo suala hili tunalishughulikia kwa kuficha takataka chini ya kapeti. Hatutafika hata kidogo. Suluhisho la suala hili ni kuliongelea kwa uwazi ili iundwe Tume ya Uchunguzi ya Kibunge, kuchunguza kuongezeka kwa mifarakano ya kidini na udini nchini. Lazima tupate ukweli wa suala hili na kupata ufumbuzi wa kudumu. Tuunde sasa *Parliamentary Inquiry on Religions Tension.*

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo hapa nchini hivi sasa ni Serikali kukosa mapato kugharamia uendeshaji wa reli. Miradi ya Maendeleo inaathiriwa zaidi. *Tax evasion* hufanywa zaidi na Makampuni makubwa yanayowekeza nchini na hata Wafanyabiashara wa Kitanzania. Uwezo wa *TRA* kudhibiti ukwepaji umekuwa ukiongezeka lakini hautoshi. Kampuni za Simu zinaongoza kukwepa kodi kwa kufanya uwekezaji holela ambao hauangaliwi na Taasisi yoyote ile ya Serikali. *PAC* ilipendekeza kwa Waziri wa Fedha kwamba, katika *Financial Act, 2013,* tufanye mabadiliko ya Sheria ya Mawasiliano kwa kuweka kifungu kinachoipa *TCRA* mamlaka ya kufanya uchaguzi kwenye uwekezaji unaofanywa na Kampuni za Simu**.**

Uzoefu tulioupata kwenye *TMAA* sasa tuhamishie pia kwenye Sekta ya Mawasiliano. *TRA* kwa kutumia takwimu za *TMAA* wameweza kugundua $431 milioni ziliwekwa kimakosa kwenye Kampuni ya *Bulyanhulu Gold Mine* peke yake.

Dunia nzima sasa inakabili *tax evasion,* ni wajibu wa Wananchi wetu kufanya *crackdown* on *international tax avoidance and evasion.* Tukatae kabisa wawekezaji kutoka *tax havens*. Tukatae Watanzania kuweka fedha *off shore.*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu na nitalenga maeneo machache, yaani elimu, mazingira na afya.

Mheshimiwa Spika, elimu yetu hasa ya msingi na sekondari inazidi kudidimia. Watanzania tulishuhudia *performance* mbaya ya wanafunzi wa Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri mambo machache yafuatayo ili tuweze kunusuru elimu yetu. Ushauri wangu wa kwanza ni kuwa Serikali iwaruhusu wanafunzi waliofeli, waliopata sifuri, warudie mwaka, wafanye tena mtihani wa Kidao cha Nne.

Ushauri wa pili ni uandikishwaji Darasa la Kwanza uoanishwe (wanafunzi watakaoingia Darasa la Kwanza wawe na umri inaolingana), wasiwepo wanafunzi wenye umri mkubwa kuliko wengine. Kwa mantiki hii, Wakala wa Vizazi (RITA) hawana budi kuhakikisha kila mtoto anayezaliwa katika karne hii anaandikishwa na hivyo kupata vyeti vya kuzaliwa ambavyo vitasaidia uandikishwaji wa wanafunzi Darasa la Kwanza.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashauri Serikali itathmini upya matumizi ya teknologia kupitia simu za mikononi kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Simu zimekuwa chanzo cha kuwafanya wanafunzi kutokuzingatia masomo yao. Inawezekana kabisa Serikali ikapiga marufuku simu zisifikishwe shule, lakini pia zikafikishwa shule na kuwa *deposited* katika *pigeon holes* (eneo mahsusi) mpaka muda wa mwanafunzi kutoka darasani.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali irekebishe mitaala iliyoko kwa Shule za Msingi, iendane na mfumo ulipo duniani. Kama Elimu anayopata mwanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari impe uwezo wa kufikiri zaidi na kuchambua mambo, kuwa na ubunifu hata kama kwa kiwango kidogo.

Mheshimiwa Spika, elimu ya sekondari ndiyo maandalizi ya maisha ya mwanafunzi yeyote. Mitihani ya *multiple choice* hasa katika Hisabati ipunguzwe hasa kwa elimu ya msingi, mitihani impe mwanafunzi fursa ya kutumia akili na *IQ* yake yote.

Mheshimiwa Spika, mitihani ya Darasa la Nne na Kidato cha Pili iwekewe umuhimu. Huu ndiyo mchujo wa awali. Mitihani hii ionekane vile kuwa pamoja na Darasa la Saba, ndiyo michujo ya mwanzo ya kumwandaa mtaalam katika fani yoyote nchini. Mwanafunzi anayeshindwa mchujo huu, aruhusiwe arudie darasa. Inawezekana kufeli kumetokana na *immaturity* ambapo akirudia darasa inawezekana kwa mwaka mzima akakua zaidi na hivyo kujitambua na kuwa makini katika masomo na katika mitihani.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mkazo katika ukaguzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Idara hii ndiyo jicho la Serikali kujua yanayofanyika mashuleni. Wakaguzi hawaendi kukagua shule kwa sababu hawana usafiri wa uhakika, na wakiwa nao hawana mafuta. Mara nyingi hata pale wanapokagua taarifa zao hazifanyiwi kazi. Wakurugenzi, *REOs* hawazifanyii kazi taarifa za Wakaguzi ipasavyo. Laiti zingefanyiwa kazi, hali ya elimu yetu leo ingekuwa tofauti. Mwaka 2012 nilishauri hili na mwaka huu naendelea kushauri.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko bado kuhusu stahili za wataalamu. Kuna umuhimu Serikali iyafanyie kazi ili lawama ya kufeli kwa wanafunzi isiwe ni kwa sababu wao kutokulipwa stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *PPP* inaruhusu sekta binafsi ishirikiane na Serikali katika kuleta maendeleo katika maeneo mengi nchini. Halmashauri ya Wilaya zigawe maeneo kwa sekta binafsi katika maeneo yanayozunguka Shule za Msingi na Sekondari kwa makubaliano, wajenge nyumba za kukodisha ambazo Walimu watazikodisha. Kwa mpango huu, kutakuwa hakuna uhaba wa nyumba za Walimu za kuishi, tena maeneo mengi Tanzania wananchi wanaweza kutumia tofali za kuchoma ambazo ni za gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie ni kwa namna gani wazazi watashirikishwa zaidi katika elimu ya watoto wao. Sasa hivi kila mzazi anajifanya yuko *too busy* na mambo mengine kiasi cha kukosa muda wa ku-*inspect* daftari la motto. Serikali itafute namna ya kubana wazazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu 2013 nchi yetu imepata vivutio vitatu vilivyoingizwa katika Maajabu Saba ya Dunia. Kivutio kimojawapo ni Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro unakadiriwa kuipatia Serikali ya Tanzania Shilingi bilioni 80 kwa mwaka. Athari za mabadiliko ya tabia nchi yameleta athari kubwa katika hifadhi ya mlima huo. *Deforestation* inafanyika kwa kasi kubwa na barafu katika mlima huo inatishiwa kuyeyuka ifikapo mwaka 2025.

Maeneo ya kaskazini Manyara, Arusha na Kilimanjaro yamekubwa na ukame kwa takriban miaka minne mfululizo. Serikali haijasema ina mkakati gani wa kunusuru mlima huo ili Watanzania waendelee kupata pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ile Mikutano ya Mazingira imefanyika *Cancun* na *Qatar*, 2013 ambayo wafadhili waliahidi kuanzisha Mfuko wa *Green Climate Fund*. Serikali ilifuatilie ili kusaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi. Serikali ifuatilie ufadhili wa *EU* kujenga kituo cha mabadiliko ya tabia nchi Mkoani Kilimanjaro kama ambavyo *EU* iliahidi mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais katika Mkutano uliofanyika London mwaka 2011, ulihusu Azimio la Abuja ambalo nchi zilikubaliana kuweka mkakati wa uzazi wa mpango katika nchi husika na Mheshimiwa Rais alikubaliana na Azimio hilo la Uzazi wa Mpango. Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonyesha idadi

ya Watanzania milioni 44.9 na *rate* ya kuzaa ya 2.7% iko Mikoa ambayo kiwango chao cha kuzaa ni zaidi ya wastani wa kiwango cha Taifa cha 2.7% mfano Mkoa wa Kigoma Wilaya ya Kasulu kiwango chao cha uzazi ni 4.8% (utafiti wa asasi ya *ACQUIRE*, 2010).

Tafiti za mama na mtoto 2010 zinaonyesha uzazi wa watoto sita kwa kila mwanamke mwenye umri wa kuzaa. Kiwango cha kukua kwa pato la Taifa ni 6%. Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ili kujua kama ongezeko la watu linakwenda sambamba na ukuaji wa uchumi wetu? Tafiti hizo pia zinaonyesha 42% ya watoto chini ya umri wa miaka mitano wana utapiamlo *(undernourished)* na 67% wana upungufu wa damu. Je, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012) umeisaidiaje tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi wa maswali mawili niliyouliza, na naunga mkono hoja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mungu kwa kunihudhurisha siku hii ya leo. Napenda kuchangia kwa machache kwanza nikianza na Wizara ya Elimu nikianzia na matokeo mabaya ya mitihani kuanzia na Darasa la Saba na hata wa Kidato cha Nne. Kwa mawazo yangu, naona ile hali ya kutokuwa na vitabu vya kiada sawa kwa nchi nzima, maana vitabu hivi kutofautiana kati ya shule au Wilaya. Matokeo, mitihani ijapo, baadhi ya shule hizo huwa yale wanayoyakuta ni mageni kwao.

Vilevile baadhi ya masomo huwa hawayapati kabisa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji katika maeneo mengi, kilio ni kikubwa sana. Maeneo mengine kama vile Wilaya ya Masasi walipata ule mradi wa visima virefu

kumi. Kwa bahati mbaya visima hivi havitoi maji, hata kama sehemu nyingine vijana kama vile Nanganga wanachimba visima vifupi tu na vinatoa maji ambayo inawapa mradi wa kuendeshea maisha yao. Visima hivyo hutumika kuchotwa kwa makopo tu. Inashangaza kuona visima virefu visitoe maji. Naiomba Serikali ifuatilie vijiji vya aina hii ili itoe na iongezee nguvu ili kutatua tatizo hili. Kwa Wilaya hii ya Masasi, Mto Ruvuma upo karibu kiasi maji yake yanawezakana kusambazwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, linguine ni kuhusu afya. Hospital ya misheni Ndanda Wilayani, Masasi waliahidiwa kuwa itakuwa ni ya rufaa. Niliwahi kuleta madai yao, lakini sijui hadi leo Serikali imechukua hatua au imefikia hatua gani. Pia watumishi ni wachache, wengi wamehamia Serikali kwa kukimbia mishahara midogo. Ile ni hospitali mkombozi kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ione umuhimu wa kutekeleza haya.

Mheshimiwa Spika, utawala bora nijuavyo mimi ni kwamba, isemwapo Vyama vya Siasa ni pamoja na CCM. Ila hiki kimekuwa madarakani, sasa ajabu ni kwamba mara nyingi zitokeapo nafasi za utendaji kama vile zile za utendaji, wakati wa uandaaji wa masuala ya uchaguzi, watapewa nafasi wa Chama Tawala kwa madai kwamba nafasi hizo wasipewe watu wa Vyama vya Siasa. Huu ni uonevu. Isitoshe kwa mfano vijiji vinavyoongozwa na Vyama pinzani baadhi ya viongozi hupuuzia shughuli za ujenzi wa maendeleo na kuziria Chama kilichochukua uongozi pale.

Mheshimiwa Spika, ninao ushahidi wa kutosha kwa kijiji cha Mpulima Lulindi, ni uongozi wa CUF. Shule

iliangushwa na kimbunga viongozi walifika wa Serikali na kushuhudia lakini ikaachwa watoto wanapata shida wakati shule ile hawasomi, *CUF* tupu. Nilichukua hatua kuwakuta Mkurugenzi na Afisa Elimu na kuwasihi waone umuhimu wa kujali. Ofisi ya Kijiji pia walijenga wao. Nami nilichangia bati nane kumalizia. Hali kama hii siyo nzuri, na siyo hayo tu. Hivyo naomba hali isiwepo, Baraza la Katiba Kata ni kinyemela na ni wa CCM tu. Siyo vizuri! Hali irekebishwe, Katiba ni ya wote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu, sina upande, pamoja na kwamba nipo kwenye Chama cha Upinzani, wala sibagui.

Napenda nichukue nafasi hii kwa nia njema kabisa juu ya hali inayokuwepo Bungeni kati ya CCM na CHADEMA. Waswahili wanasema, mtu ukimjua, hakusumbui. Hawa ni watu wa kuwapuuza na kuwaona ni wa kawaida. Wameishiwa na mipango na mawazo pia. Kwani hata wenyewe baadhi yao wanakiri kabisa kuwa tabia yao siyo mzuri. Ugomvi wa mume kwa mke, kama mke hajibu, matokeo yake mume hujifuma ujinga, mwisho hunyamaza. Na hawa wakipuuzwa bila kuwajali, watajifuma ujinga, wataacha tabia hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kilimo, kuhusu suala stakabadhi ghalani. Pamoja na maelezo mazuri ya Naibu Waziri, leo kinachoumiza zaidi ni juu ya makato mengi yanayowanufaisha watu wasio na msaada wowote kwa wakulima.

**MHE.HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kupata ufafanuzi wa sababu za msingi za kutokutengewa *OC* kwa Wilaya ya Ilemela, kwa kuzingatia kuwa Ilemela ni *Municipal* mpya na inahitaji nguvu za kutosha katika kutekeleza majukumu yake.

Hii inatokana na taarifa iliyo katika orodha ya majedwali yanayoambatana na hotuba ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 22 inayohusu ni mgawanyo wa ruzuku ya fedha za matumizi mengineyo(OC) kwa Halmashauri kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa hotuba nzuri yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kuishauri Serikali juu ya mfumo wa manunuzi uangaliwe upya. Kwani mfumo huu unasababisha Serikali kutumia fedha nyingi ambazo haziendi sehemu husika. Ni vizuri Serikali ikarudi kwenye mfumo wa zamani ambao una unafuu katika kuokoa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo, naomba Serikali iongeze bajeti kwenye kilimo, kwani Wizara hii imebeba Watanzania walio wengi ambao wanatakiwa kuwezeshwa na Serikali hasa katika kuweka ruzuku ya Serikali kwenye pembejeo kama mbolea, madawa, pamoja vyombo vya kurahisisha vitendea kazi kama *tractor, power tiller* na *plau*.

Jambo lingine ni kuangalia mfumo wa kuwalinda wakulima wadogo wadogo kwa kutoagiza mchele nje ya nchi. Kufanya hivyo ni kuua kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji ambao watasababisha madhara makubwa sana katika nchi hii. Naomba Serikali itenge maeneo ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, maji suala la matatizo ya maji ni suala ambalo ni kubwa katika nchi. Naishauri Serikali ichukue hatua thabiti katika kuhakikisha tatizo la maji linamalizwa. Ni vyema Serikali ikaelekeza nguvu kubwa katika kutatua tatizo la maji ambalo ni kero kubwa katika nchi hii hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, lingine ni miundombinu Mkoa wa Katavi ni Mkoa Mpya ambao haujaunganishwa na Mikoa jirani. Naiomba Serikali itengeneze barabara ya Mpanda – Kigoma, ijengwe kwa kiwango cha lami, sambamba na barabara ya Mpanda - Tabora ambayo ni muhimu sana katika kuunganisha mtandao wa barabara wa Mikoa ya pembezoni. Ni vyema Serikali ikaongeza kiwango cha fedha ili kufanikisha kumaliza tatizo la usafiri kwa kuimarisha barabara.

Mheshimiwa Spika, suala linguine ni mawasiliano. Tuna tatizo kubwa la maeneo ya Jimbo la Mpanda Vijijini hasa vijiji vya Katuma, Kabungu, Sibwesa, Kasekese, Ifukutwa, Majalila na kadhalika, havina mawasiliano. Naomb Serikali itatue tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo katika eneo la kilimo, Serikali iliamua kutoa ruzuku za pembejeo ikiwemo mbegu na mbolea. Ruzuku hizi zimekuwa kwanza hazifikii maeneo husika kwa wakati, kupotea kwa vocha ama kuharibika. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kubadilisha mtindo huu unaotumika kwa sasa? Kwani haumfaidishi mkulima. Lakini pia ruzuku hii imekuwa ikitolewa kwa ekari moja tu.

Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikaongeza angalau ekari tatu kwa kila mkulima ili kuongeza tija na kuzuia uharibifu wa mazingiara na pia kukifanya kilimo kuwa ajira na chenye tija kwa mkulima? Kwani kwa kufanya hivyo mkulima atazalisha kwa mfano, mahindi mengi na hivyo kuweza kuyaongezea thamani badala ya kuuza mahindi, anaweza akauza unga na kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya JKT, Serikali iangalie namna ya kuwatumia vijana wanaokwenda kwa kujitolea mara wamalizapo mafunzo hayo, kwani kuwaacha wakarudi vijijini bila shughuli yoyote ya kueleweka, ni kupoteza pesa za Taifa.

Mheshimiwa Spika, elimu katika sekta ya elimu ni vyema Serikali ikaangalia upya utaratibu wa ada kwa Shule za Sekondari, kwani uzoefu unaonyesha wazazi wengi wamekuwa wakishindwa kulipa ada hizo na hivyo kuwafanya wanafunzi kuacha ama kukatiza masomo. Ni vyema Serikali ikafuta ada hizo ili kuwezesha wanafunzi wengi kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Spika, pili, asilimia mbili za mshahara anazokatwa Mwalimu bila ridhaa yake mpaka sasa ni kiasi gani, na zinawasaidiaje walimu? Je, wanapostaafu, pesa hiyo wanarudishiwa? Kama sivyo, je, Serikali iko tayari kuleta Muswada wa Sheria ili kujadili kufutwa/kukatwa kwa pesa hiyo?

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuzungumzia kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani. Naomba Serikali iangalie upya likizo za maaskari, yaani waende likizo kila mwaka kama watumishi wengine wa Serikali badala ya kuwaacha kwa miaka mitatu ndipo waende likizo.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, napata taabu sana kuona suala la elimu liko katika mihimili miwili. Ikiwemo Wizara husika na nyingine TAMISEMI. Nilichobaini ni kwamba, hakuna usimamizi thabiti kwani kila upande unamsingizia mwenzie pale suala linapoharibika. Hivyo nashauri suala la elimu liwekwe katika Wizara moja tu, iwe Elimu ya Juu, Sekondari, Msingi (za Kata) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukaguzi imebainika kwamba Serikali haijalitilia mkazo suala la ukaguzi mashuleni, kwani kazi hiyo haipewi nyenzo, hauwezeshwi kifedha, wataalamu wapo kidogo na magari hakuna. Hivyo kukosekana kwa huduma hizo kunadumaza usimamizi wa elimu nchini na ndiyo sababu ya vijana wetu kufeli kwa idadi kubwa. Kutokana na kadhia hiyo, nashauri Serikali kuwekeza kifedha, vifaa na kila kinachohitajika katika suala la ukaguzi ili kazi hiyo isisite kila inapohitajika.

Aidha, nashauri kuwa kazi ya ukaguzi iwe ni Kitengo Maalum kinachojitegemea na kipatiwe fedha ya moja kwa moja. Vinginevyo, ikiwa kukifanya Kitengo kwa kazi hiyo, uangaliwe utaratibu wa kutafuta Wakala wa kufanya kazi ya Ukaguzi kwa niaba.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la Muungano. Kuna suala la malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar ya kutozwa kodi mara mbili na mgawanyo wa mapato. Ninavyojua mimi hadi leo na sasa, kodi inatozwa mara mbili hasa Bandarini, unapoleta gari lazima ulipe tena kodi ya mapato *(TRA),* vile vile na kodi za biashara na kadhalika. Hivyo, kutokana na kadhia, naitaka Serikali kufanya kikao cha mwisho cha kutoa maamuzi sahihi ili tatizo hilo liondoke tena, wananchi wamechoka kusikia suala hilo linazungumzwa tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la madai ya Walimu, nasikitishwa sana na Kitendo cha Serikali kuwa hadi sasa Walimu wanadai maslahi yao na hawajalipwa na Walimu wengine, tayari wameshawasilisha madai yao Wizarani lakini bado wanapigwa *tiktaka* na tukijua suala la madai ni muhimu sana ambapo Walimu wakilipwa wataweza kuingia ari ya kusomesha. Hivyo, naiomba Serikali imalize kulipa madai ya Walimu kabla ya kumaliza mwaka 2012/2013.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba mimi ni Askari mwenye namba *AKC 4317 SG,* Ritta Kabati. Naipongeza Serikali kwa kurudisha tena mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kurudi kwa mafunzo haya ni imani yangu sasa tunarudisha yale maadili yaliyomomonyoka, vijana wetu watalitumikia Taifa lao wakiwa na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kwa Serikali, nimehudhuria mafunzo haya katika Kambi ya JKT Msange, kikosi cha 1823 KJ, Tabora. Ili mafunzo haya yaweze kuwa na tija kwa vijana wetu, Serikali inatakiwa kutenga pesa ya kutosha katika Makambi haya ili vijana wanaopelekwa katika hizo Kambi wasionekane wanapelekwa kwenye mateso na vifo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe changamoto nilizoziona katika Kambi niliyohudhuria mafunzo ya Msange. Kambi haina umeme kabisa toka imeanzishwa, hakuna gari la usafiri la kikosi wala gari la wagonjwa *(Ambulance)*, Kambi ina ukosefu wa madawa na vifaa tiba, Kambi inahitaji marekebisho ya miundombinu ya maji taka na maji safi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama Kambi hii ingekuwa na umeme, pamoja na kusaidia hata kuwa na mitambo ya kukamua mafuta kwa alizeti na karanga zilizolimwa katika kambi hiyo na kusaidia kujiendesha yenyewe bila kutegemea ruzuku ya Serikali kwa kuuza mafuta yao.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili nitachangia kutoka ukurasa wa 30.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji pamoja na mikakati mizuri iliyowekwa na Serikali kwa kupanua eneo la kilimo cha umwagiliaji, ningependa kupata ufafanuzi wa vigezo vinavyotumika katika kugawa pesa hizo katika maeneo yetu na kwa nini Serikali inaanzisha miradi mipya wakati miradi ya zamani, tena mingi haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi miwili katika Manispaa ya Iringa ambayo ni *Kitwiru Irrigation Schem* na Mkoga) Kisaila, Kitwiru unahitaji Sh. 526,480,000/= na Mkogwa Sh. 549,256,000/=.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ni ya muda mrefu sana ambayo tayari kuna nguvu ya wananchi na ya Manispaa imeshaanza kutumika. Ningeomba Serikali kutoa kipaumbele kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie kuhusu Sera ya Taifa ya wazee ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, sera hii pamoja na kuwa na upungufu mwingi lakini bado mpaka leo haijatungiwa sheria. Je, ni lini tutaletewa rasmi?

Mheshimiwa Spika, siyo siri, wazee wengi wa nchi hii wanapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu matamko na maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Siku ya Wazee Duniani, 1St Oktoba, 2009 Dodoma na 2010 huko Morogoro ya kuwa kila hospitali itenge chumba na Daktari wa Wazee, lakini sehemu kubwa hayajatekelezwa hata baadhi ya maeneo yalikotekelezwa, wazee wanaambiwa dawa wakanunue, hivyo hulazimika kurudi nyumbani bila dawa.

Mheshimiwa Spika, nitachangia ukurasa 50 kuhusu ujenzi wa barabara wa madaraja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri na kubwa iliyofanyika katika ujenzi miradi ya barabara na madaraja nchini.

Mheshimiwa Spika, ningependa Serikali itambue kuwa lipo daraja la Tagamenda katika Manispaa ya Iringa, Jimbo la Iringa Mjini ambalo limekuwa ni tatizo kubwa. Wananchi wanaozunguka eneo hilo, daraja hilo ni kiunganishi kati ya Jimbo la Iringa na Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu unaonyesha daraja hilo linahitaji Shilingi bilioni 1.1. Kuna wananchi takriban 4000 wakiwemo wanafunzi wa Shule ya Sekondari Tagamenda, Shule ya Msingi na Chuo cha Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri haina uwezo wa kujenga daraja hilo. Hivyo ningeomba Serikali ichukue tatizo hili ili kunusuru maisha ya wananchi ambayo karibu kila mwaka daraja hili huwa linaleta maafa na kusababisha vifo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mbeya - Chunya - Makongorosi ulianza mwaka 2007. Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi barabara hiyo mwaka 2008.

Kwanza, ujenzi huo ilipewa kampuni ya ujenzi toka Kenya. Kampuni hiyo ilishindwa na *Tanroads* katika utekelezaji. Baadaye zilipewa kampuni mbili toka China. Cha kusikitisha ni kuwa mpaka leo hakuna hata mita moja ya lami. Kuna miradi mingine iliyoanza baada ya mwaka 2007, imekamilika. Kwa nini barabara hii inasuasua namna hii? Hivi wananchi wa maeneo hayo wanajionaje baada ya kuona barabara yao haipewi kipaumbele? Naiomba sana Wizara ya Ujenzi angalau imalizie kipande kimoja tu cha Mbeya hadi Chunya. Itasaidia sana kuwaonesha wananchi wa sehemu hizo kuwa Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili fedha ipatikane ya ujenzi wa barabara hiyo.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja pamoja na changamoto zinazoikabili Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ucheweshwaji mkubwa wa fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri zote nchini, mfano Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mpaka sasa imepokea nusu tu ya fedha zilizopitishwa kwenye bajeti. Suala hili linavunja mioyo wananchi ambao wameanzisha ujenzi wa Zahanati, Vituo vya Afya, madarasa, nyumba za Walimu na kadhalika kwa kujua Serikali itawashika mkono.

Mheshimiwa Spika, suala la kuajiri watumishi katika Halmashauri zetu bado ni tatizo kubwa kutokana na urasimu unaofanywa na Wizara ya Utumishi na Sekretarieti ya Ajira. Ni kwanini suala hili lisirudishwe kwenye Halmashauri husika? Mfano, Halmashauri ya Shinyanga imeomba kuajiri madereva zaidi ya miaka minne sasa na Ikama ya mwaka 2012/2013 inaonyesha Halmashauri itaajiri madereva sita. Taratibu zote zimefuatwa, lakini mpaka sasa kibali hakijatoka. Naishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kurudisha suala hili katika Halmashauri zetu kuliko kuliachia Utumishi na Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchangia kuhusu Kamati za Kudumu za Halmashauri kutokukagua miradi ya maendeleo ilhali Kamati moja tu ya Fedha, Utawala na Mipango ndiyo inayokagua miradi yote ya Halmashauri kwa siku mbili tu. Suala hili ni tatizo kubwa katika Halmashauri zote nchini, kwani linasababisha miradi mingi kuwa chini ya kiwango kwa sababu haikaguliwi kwa wakati. Ni vyema utaratibu wa zamani wa Kamati zote kukagua miradi husika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, namaliza kwa umuhimu mkubwa kuomba Serikali itimize ahadi iliyotolewa na Waziri Mkuu Mstaafu 2007 ya kuchimba bwawa la umwagiliaji katika kijiji cha Masengwa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napongeza utendaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Napenda kutoa maelezo na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, chombo kitakachoanzishwa *(President's Delivery Bureau)*, lengo la Mawaziri wa kisekta na Watendaji kuwajibika kusimamia utekelezaji

wa miradi ya kipaumbele ni muhimu na sehemu ya majukumu yao. Tutamke ongezeko la chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, kuorodhesha na kusimamia utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais, tumekuwa tukisikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge kukumbushia ahadi za Mheshimiwa Rais Bungeni na hata wakati wa ziara za Mheshimiwa Rais Majimboni. Nashauri tupunguze kero hizi.

Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa fedha wa Halmashauri, wamejenga tabia ya kutotoa taarifa halisi za mapokezi ya fedha kutoka Hazina.

Kamati za Fedha na Mabaraza ya Madiwani hawapewi taarifa kwa wakati. Lengo ni kuhodhi fedha hizo na kuzitumia vibaya. Pia hakuna uwazi katika upelekaji wa fedha katika Kamati za Serikali za Vijiji na Shule na hivyo kuwezesha matumizi mabaya ya fedha za miradi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni tatizo la maji Muheza. Maji kutoka Mto Ziggi Tarafa ya Amani Wilayani Muheza ndiyo yanayotumika katika Jiji la Tanga, lakini Muheza haina maji (Mjini). Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2005 na 2010 ni kuiwezesha Muheza Mjini kupata maji kutoka chanzo cha Mto Ziggi. Ahadi hiyo haijatekelezwa hadi leo, sambamba na ahadi ya kutengeneza barabara ya Muheza Amani kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la maji, nimeomba Wizara ya Maji, na imeandaa mpango wa dharura katika miradi mitatu; Kisima cha Polisi Muheza Sh. 100,000,000/=, kisima kirefu cha Kitisa Sh. 806,000,000/= na uboreshaji wa chanzo cha sasa – Magoroto/Mkurumizi Sh. 707,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, tumetekeleza mradi wa kisima cha Polisi. Nimeandika kuomba msaada Ofisi ya Waziri Mkuu na kukabidhi barua kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mwezi Februari, 2013. Mheshimiwa Waziri (TAMISEMI), Februari, 2013 hadi leo 16 Aprili, 2013 sijapata hata jibu! Je, ni lini Muheza itasaidiwa kuondoa kero hii ya maji? Upembuzi yakinifu kwa barabara ya Muheza Amani umeanza, utakamilika lini na ujenzi kuanza lini?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la udini na taarifa za Usalama wa Taifa na upelelezi nchini.

Mheshimiwa Spika, Taarifa za Usalama wa Taifa, Maafisa Upelelezi nchini na vyombo vya usalama vimekuwa vikilihusisha hili suala na Vyama vya Siasa hususan CHADEMA. Lakini ukweli siyo huo, bali tatizo hili limeasisiwa na Usalama wa Taifa na Serikali kwa malengo ya kisiasa. Taarifa za kulihusisha Taifa na Udini lilianza tangu mwaka 2000 wakati Chama cha *CUF* kilipokuwa kinatuhumiwa kuwa ni Chama cha Kiislam na Chama kinachohusishwa na ugaidi, lakini mpaka sasa Serikali haijawahi kukanusha shutuma hizo. Hofu yangu ni kuwa, Taifa linapoelekea siko na matokeo ya kupandikiza hilo yameanza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, suala la imani halina Chama, halina ndoa wala umri. Itakapofika wakati, kila mtu atalinda imani yake. Serikali imekuwa nzito kuchukua maamuzi juu ya jambo hili. Hivi ni nini tunachotarajia? Tunaiomba Serikali itoe tamko juu ya nyaraka za Makanisa (Maaskofu) kama inazitambua ama haizitambui ikiambatana na sababu za kwanini wanatambua ama hawatambui? Na mpaka sasa suala hili limefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, wafugaji wamekuwa wamepata mateso makubwa sana kwenye maeneo wanayofuga mifugo yao, tena hii ni pamoja na viongozi wa Serikali, Polisi na Halmashauri kuwakamata, kuwaua wanapoingia kwenye hifadhi. Kwa bahati mbaya, mara nyingi wakikamatwa, wanachukuliwa mifugo yao na kutozwa fedha nyingi ikiwemo rushwa. Hivyo, wafugaji wanataka kujua haki yao ya kimsingi kuishi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, kwa kuwa wafugaji wengi wanatoka Shinyanga na Mwanza na maeneo mengine Tanzania. Serikali ingejitahidi kutenga maeneo ya kulishia mifugo, kuwachimbia mabwawa kutokana na ukame wa maeneo yao ili kupata maeneo mazuri ya malisho na kuondoa utata huu wa wafugaji na Serikali.

Mheshimiwa Spika, maji ya Ziwa Victoria ni mradi mzuri na uko katika mkakati wa kuyapeleka kwenye vijiji vilivyo ndani ya kilometa 12, lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa mpaka sasa. Naomba Serikali kupanga na kutenga fedha ili mradi huu uweze kwisha. Napenda kujua pia mradi wa kutoka Kahama kwenda Nzega utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliahidi kukamilisha Halmashauri ya Wilaya ya Iselamagazi ambayo sasa iko asilimia 30%, tumebakiza 70%. Tukamilishe kwa kutegemea fedha za Halmashauri, Halmashauri haitakuwa na uwezo wa kuikamilisha haraka. Hivyo, matumaini yangu ni mwaka huu, naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, Shinyanga kwa muda mrefu sana tumekuwa tukichangia pato kubwa sana katika pato la Taifa, lakini tumekuwa tunapata maendeleo

kidogo sana, kwa mfano *Airport* ya Shinyanga mpaka sasa haijajengwa na kukosa huduma ya usafiri kabisa na kufanya kwenda Mwanza.

Naomba tupate majibu ya kuyamaliza matatizo haya yote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, utoroshaji wa fedha nje ya nchi (*Illicit Financial out Flow)* katika Bunge la mwezi Februari, Bunge liliazimia kuwa Serikali ilete taarifa ya jinsi ilivyoshughulikia urejeshwaji wa fedha na raslimali za umma zilizotoroshwa na kufichwa nje ya nchi na kwamba Bunge la mwezi Aprili lilipewa taarifa. Lakini cha kushangaza, kwa mujibu wa ratiba iliyopo, suala hili halimo kwenye orodha ya shughuli zitakazoshughulikiwa na Bunge. Kwanini taarifa ya utoroshaji wa fedha za umma nje ya nchi haimo katika ratiba?

Katika toleo la kwanza *(first draft)* la Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, suala la utoroshwaji wa fedha nje ya nchi lilielezwa kuwa ni kikwazo kikubwa cha kupiga hatua za kiuchumi na maendeleo nchini, lakini toleo la mwisho *(final draft)* kipengele hicho kimeondolewa.

Mheshimiwa Spika, kwanini kipengele hicho kiliondolewa katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano? Kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu kina kurasa 82 na kimegusia mambo mengi muhimu kwa ustawi wa Taifa letu. Lakini licha ya ukubwa wa tatizo la utoroshaji wa fedha nje ya nchi ambalo limelalamikiwa na Watanzania wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Taasisi mbalimbali Waziri Mkuu hajagusia wala kuzungumzia suala hili.

Wakati kuna kiasi cha Shilingi trilioni 13 zinadaiwa kufichwa nje ya nchi, mfano nchini Uswiss pekee zinadaiwa kufichwa kiasi cha Shilingi bilioni 315.

Mheshimiwa Spika, fedha na raslimali za umma ambazo zingetumika kutoa huduma kukuza uchumi na kuleta maendeleo zinatoroshwa na kufichwa nje ya nchi kwa maslahi ya watu wachache na kuwaacha Watanzania wengi katika lindi la umasikini wa kutupwa, lakini Serikali haionyeshi nia ya dhati kuweza kuzirejesha fedha hizo. Kwanini Serikali imegubikwa na kigugumizi kikubwa katika kushughulikia suala hili?

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(FYDP 1)* kwa mujibu wa hotuba ya Waziri Mkuu, ni dhahiri kwamba Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umefeli na hivyo ni muda muafaka sasa Watanzania wakafahamishwa.

Bunge lilipopitisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2011/2012 ilipitisha pamoja na vipaumbele vyake. Hivyo kusema kuwa kuna Serikali imeunda chombo maalum *"President's Delivery Bureau"* kitakachochambua vipaumbele ambavyo vitatoa matokeo ya haraka. Huu ni mpango ndani ya mpango, kwani shughuli zilizoainishwa katika *FYDP 1* ndizo tulizokubaliana kuwa zitatoa matokeo ya haraka ndani ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa mpango, vipaumbele vinafahamika, wala haihitaji wadau kuchambua vipaumbele. Kinachohitajika ni kupeleka fedha za kutosha kutekeleza mpango.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayokwaza utekelezaji wa mpango wetu ni kama ifuatavyo:-

- Serikali kutokutenga fedha za kutosha za ndani kugharamia mpango kama ilivyokubalika. Mfano, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ilitenga Shilingi trilioni 2.2 tu badala ya Shilingi trilioni 2.9 ikiwa ni pungufu ya Shilingi bilioni 700.

- Serikali kuendelea kutegemea misaada na mikopo toka nje kutekeleza mpango fedha, ambayo imekuwa hailetwi kwa wakati na mara nyingi huletwa pungufu ya fedha iliyoahidiwa.

- Ucheleweshaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika kila mwaka wa fedha, Wizara, Taasisi na Halmashauri hulalamikia ucheleweshaji mkubwa wa fedha za miradi ya maendeleo ambazo kwa wastani hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha huwa zimepokea 30% tu ya fedha zinazostahili kupokea.

Mfano, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Shirika la Reli nchini, *(TRL)* lilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 85.27, lakini hadi robo ya pili inamalizika, Serikali imepeleka Shilingi bilioni 12.2 tu sawa na 14.3%.

- Kutokushirikishwa kikamilifu kwa sekta binafsi katika kutekeleza mpango huu kupitia utaratibu wa *PPP.* Aidha, Serikali haijaiandaa sekta binafsi na wala haijaweka wazi miradi ambayo inataka ushiriki wa sekta binafsi, licha ya mpango huu kubakiza miaka miwili ya utekelezaji.

- Serikali kushindwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kwamba kuna udhaifu mkubwa katika ukusanyaji wa mapato.

Mfano, hata vyanzo vya mapato vilivyoainishwa katika mpango ukurasa wa 82 - 96 Serikali haijaanza kukusanya mapato hayo mpaka sasa.

- Serikali imeendekeza matumizi ya anasa huku miradi ya maendeleo ya wananchi ikitengewa fedha kiduchu. Kwa ujumla matumizi ya Serikali yamegubikwa na ufujaji, wizi na rushwa.

Hivyo hata kama tutakuwa na‘*President’s Delivery Bureau’,* lakini Serikali ikashindwa kuzishughulikia na kuziondoa changamoto hizo hapo juu, hakika mpango hautekelezeki.

Mheshimiwa Spika, kwanini Serikali inapoteza muda na pesa nyingi kubuni mikakati na mipango badala ya kujikita katika utekelezaji wa mpango? Kwanini Serikali isilete taarifa ya utekelezaji wa mpango kwa miaka yote mitatu iliyopita ili Watanzania kwa ujumla waweze kujua na kutathmini hatua iliyofikiwa?

Mheshimiwa Spika, fedha za miradi ya barabara katika Serikali za Mitaa (*Road Fund),* fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ni kidogo na hata kiasi hicho kidogo hakipelekwi chote katika Halmashauri husika. Kiasi hicho cha fedha hakiendani na mitandao ya barabara iliyopo katika Serikali za Mitaa.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ilitenga Shilingi bilioni 194, lakini ilipeleka Shilingi bilioni 73.7 tu na mwaka 2012/2013 hadi kufikia robo ya tatu Serikali imetumia Shilingi bilioni 57 tu kati ya Shilingi bilioni 128.9 zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha. Huu ni mzaha kwa Serikali. Barabara nyingi katika Halmashauri hushindwa kufanyiwa matengenezo na hivyo kutopitika katika muda wote.

Mheshimiwa Spika, fedha zinatengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara pekee, lakini siyo kuchonga barabara mpya. Licha ya Watanzania wengi

waishio vijijini kuendelea kukosa miundombinu ya barabara, Serikali haina mkakati madhubuti wa kuwajengea barabara ili kurahisisha utoaji huduma na shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, fedha ni kidogo zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri za Wilaya. Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambako ndipo tunatarajia miradi maendeleo iliyo karibu na wananchi, inatekelezwa kama miundombinu ya elimu, afya, maji, barabara na kilimo, lakini imetengewa fedha kidogo sana, yaani Shilingi bilioni 640.6 tu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu mbaya wa mgawanyo wa rasilimali za Taifa, tutaendelea kushangaa kwanini uchumi unakua wakati wananchi wanaendelea kuwa katika lindi kubwa la umasikini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wataendelea kutushangaa aina ya maendeleo ambayo tunajivunia wakati miradi yao mingi imeshindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya Waziri Mkuu, hususan eneo la UWEZESHAJI.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha vikao vya majadiliano kati ya Baraza la Uwezeshaji, Benki Kuu, Wizara ya Fedha, Ushirika na Maendeleo ya Jamii na Taasisi zinazowezesha.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali vikao hivyo vifanyike kila robo mwaka, kwani kwa sasa tunajenga msingi wa kuwezesha wananchi vizuri na kushauriwa na kushauriwa njia bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuwafanya wananchi wengi washiriki shughuli za uchumi, napenda mafunzo yaliyotolewa kwa *SACCOS,* lakini bado tunahitaji mafunzo zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sekta binafsi bado ni change, Serikali ijitahidi kukuza sekta binafsi, hususan kwa Watanzania wazawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 31 na 44, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza wazi mwenendo wa bei za mazao makuu ya biashara nchini, jinsi ambavyo umekuwa ukibadilika mara kwa mara na hivyo kuwaathiri sana wakulima wetu pale bei zinaposhuka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametaja kabisa mazao hayo ni korosho, pamba, kahawa, chai, tumbaku na pareto.

Mheshimiwa Spika, *"concern"* yangu iko kwenye zao la korosho, maana ndiko ninakofahamu jinsi ambavyo wakulima wa korosho wanavyopata shida; siyo jinsi ya kupata pembejeo za ruzuku tu, hata jinsi ya kuuza korosho za ruzuku imekuwa ni kazi kubwa. Kila mara, kila mwaka tangu niingie ndani ya Bunge hili, tumekuwa tukilalamika jinsi ambavyo wakulima wa zao la korosho wanavyopata mateso makubwa, ama kupata pembejeo za ruzuku, ama kuuza korosho zenyewe.

Mheshimiwa Spika, korosho hazinunuliwi kwa wakati na hata zikinunuliwa hazipati bei nzuri kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia katika *speech* yake ukurasa wa 31.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale tumevuna korosho mwezi wa Tisa, 2012, korosho zimeuzwa mwezi wa Tatu, 2013. Ukihesabu ni miezi saba wakulima wamesubiri korosho zao kununuliwa.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawa wana matatizo yao ya kifamilia, wameshindwa kuyatatua kwa kipindi cha miezi saba wakisubiri korosho zao zilizoko katika magodauni kununuliwa kwa kipindi cha miezi saba. Haya ni mateso makubwa sana wakulima hawa wanapata.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 31 na 32 wa *speech* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametamka wazi kwamba tatizo la kubadilika mara kwa mara kwa bei za mazao ya biashara kunaathiri sana wakulima na kwamba Serikali inaangalia uwezekano wa kuanzisha Mfuko Maalum wa kufidia bei za mazao kwa wakulima pale zinaposhuka *(price stabilization funds).*

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Waziri Mkuu kwamba Serikali isiangalie uwezekano wa kuanzisha Mfuko huu Maalum wa kufidia bei za mazao, bali ni wakati muafaka sasa wa Serikali kuanzisha Mfuko huu Maalum wa kufidia bei za mazao ya biashara mara moja. Ikiwezekana msimu ujao wa korosho, mfuko huu uweze kutumika endapo tatizo la kushuka kwa bei litatokea.

Mheshiwa Waziri Mkuu, sambamba na uanzishwaji wa Mfuko huu Maalum, Serikali iangalie upya Mfuko wa Stakabadhi Ghalani, uboreshwe ili wakulima hawa wa korosho wasiendelee kupata mateso haya ambayo yamekuwa wakiyapata.

Mheshimiwa Spika, boresho mojawapo la Mfumo wa Stakabadhi Ghalani linaloweza kufanyika ndiyo hili

la kuanzisha Mfuko Maalum wa kufidia bei za mazao ya biashara. Itasaidia sana.

Kama marekebisho hayatafanywa, suala la Stakabadhi Ghalani, huko mbele kuna hatari ya wakulima kuukataa mfumo huu, kwa maana kwa sasa unaonekana kushindwa kufanya kazi vizuri, hasa kwa Wilaya ya Liwale, Ruangwa na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kuhusu zao la korosho, ningependa kufahamu, hivi inakuwaje matajiri wanaokuja kununua korosho kila mwaka wanasumbua? Ni kwa nini kama hawahitaji kununua korosho wanapewa lesseni? Ni kwa nini wanunuzi hawa wanabembelezwa kila mwaka kununua korosho? Hatma ya utaratibu huu ni nini?

Mheshimiwa Spika, nitaomba nipate majibu katika majumuisho ya hatuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 59 No. 87, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia Sekta ya Elimu, Idara ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, Serikali imejitahidi kuwekeza na kuboresha Sekta ya Elimu. Pamoja na yote yaliyotajwa ndani ya hotuba hii, hali halisi iliyopo katika Shule za Sekondari bado ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, shule zile kubwa kubwa tunazozifahamu na ambazo viongozi wengi wa Serikali wamesoma katika shule hizo, kama vile Kibaha Sekondari, Mzumbe Sekondari, Kilakala, Ilboru, Msalato, Tosamaganga, Lindi, *Mtwara Technical*, Pugu, Tanguani, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, shule hizi zina hali mbaya kuanzia uchakavu wa majengo, chakula, vifaa vya Maabara, vitabu mpaka Walimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijipange upya kufanya maboresho makubwa. Katika Idara ya Sekondari ningependa kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, ningeishauri Serikali, zile shule kubwa zote kwa maana ya zile Shule zenye *Form I - VI* na zile zenye *Form V-VI* tu zingerudishwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Maana yake ni kwamba, shule hizi ziwe chini ya Wizara ya Elimu kama zilivyokuwa mwanzo na shughuli zote za uendeshaji wa shule hizo utafanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Shule za Kata zilizobakia zenye *Form I - IV* ziendelee kubaki na kuhudumiwa na TAMISEMI. Mgawanyiko huu unaweza kusaidia kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Liwale lina Shule za Sekondari 16 lakini asilimia 90 ya shule hizo zina Walimu wawili wawili tu. Mwalimu wa kwanza – Mwalimu Mkuu Msaidizi. Walimu hawa wawili wanafundisha masomo sita, kutoka Kidato cha I - IV. Hakuna Mwalimu wa *Physics*, wala wa *Chemistry, biology* na *mathematics*.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaona katika hali hii, tutegemee matokeo gani? Bila kujipanga upya, matokeo ya mtihani ama ya Kidato ch IV ama ya Kidato cha VI yataendelea kuleta vilio kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, TAMISEMI na Serikali kwa ujumla, hebu pateni takwimu halisi za hali halisi za shule zetu kwa sasa hali ikoje?

- Je, kuna *facilities* za kutosha za bweni, chakula na kadhalika?

- Vitabu, vifaa vya maabara na kadhalika?

- Vyumba vya Maabara vilivyokamilika vyenye vifaa vya kufanyia *practice* zote?

- Hali ya majengo ikoje?

- Je, Walimu wa kutosha kwa masomo yote wapo katika shule hizo?

Mheshimiwa Spika, hali bado siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nishati, la kwangu ni dogo tu. Wilaya ya Liwale ilikuwa na kilio kikubwa sana cha ukosefu wa umeme wa uhakika. Kwa jitahada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na kwa juhudi za Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda, Liwale sasa ina umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kuletewa *generators* mbili zenye uwezo wa kuzalisha KWs 840 ambazo zinatosha kabisa kwa Mji wa Liwale na kubaki. Japokuwa imekatazwa kushukuru wakati wa kuchangia, mimi naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wana Liwale kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililoko sasa ni nguzo na vifaa vingine kama vile vikombe, nyaya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, umeme ulioko pale ni mwingi sana na wananchi

wanahitaji kuingiza umeme katika nyumba zao na umeme ule ili ulete maana na ulipiwe ni lazima utumike. Naomba Serikali pamoja na ndugu zangu wa *TANESCO,* mefanya vizuri sasa, malizieni zoezi hilo la kupeleka nguzo za kutosha pamoja na vifaa vingine ili wananchi waweze kuingiza umeme huo katika majumba yao.

Mheshimiwa Spika, nguzo pamoja na *meter* za Luku ni mali ya *TANESCO.* Mimi ningeomba nguzo pamoja na *meter* za Luku ziletwe na zifungwe, wananchi watozwe gharama kidogo tu za kulipia *service line,* wananchi watapata umeme, watalipia *bill* zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Napenda nielekeze mchango wangu hasa kwenye migogoro ya ardhi.

Suala la migogoro ya ardhi limekuwa suala au janga ambalo kila kona ya nchi limekuwa gumzo la kawaida. Suala hili la ardhi ni wazi kuwa ni suala mtambuka na kwa vile ni suala mtambuka, linapaswa kughushulikiwa na Wizara zaidi ya moja.

Aidha, pamoja na wataalam hawa kufanya kazi pamoja, lakini pia ushirikishwaji wa wananchi wa sehemu husika ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, leo hii, Serikali kama sehemu ya jukumu lake la msingi ni kuhakikisha wananchi wake wanaishi katika maeneo ambayo hawabughudhiwi, wanazalisha chakula cha kutosha, wanafuga vizuri.

Aidha, pamoja na shughuli zote zinazohusu kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Kwa misingi hiyo, Serikali ndiyo maana imepima maeneo mfano vijiji, maeneo tengefu, hifadhi na maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Miaka zaidi ya hamsini wananchi wanaishi eneo husika, wamezaana na kupata wajukuu na vitukuu, lakini Serikali hii iliyopo madarakani leo wanaambiwa wananchi hawa kuwa wanaishi kwenye eneo la hifadhi. Hakika Serikali inawakosea haki wananchi hawa. Suala hili limewafanya wananchi kutokuwa na uhakika wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kanika, Kijiji cha Kanika na Mpango ni eneo ambalo Serikali zinapaswa kutoa jibu la haraka sana kuhusu wananchi hawa. Hakika wananchi hawa wameishi hata kabla ya uhuru, vijiji vyote vimesajiliwa; kuna miundombinu endelevu, shule, barabara na kadhalika; na shule kila mwaka inasajili watoto na wengine wanachelewa kuhitimu Darasa la Saba. Swali la kujiuliza: Je, wakati Serikali inajenga shule hizo, haikujua kuwa eneo lile ni eneo la hifadhi? Serikali wakati inajenga barabara haikujua kuwa eneo lile ni hifadhi?

Mheshimiwa Spika, suala hili linasumbua sana wananchi hawa, kwani mashamba yao yanaharibiwa na Askari Maliasili, bado wanaambiwa wasilime mazao katika eneo lile. Swali ni kwamba, kama wananchi wanakataliwa kulima: Je, wananchi hawa wataishije? Je, Serikali ipo tayari kuwasaidia chakula cha msaada wakati makosa ni ya Serikali? Kama Serikali iliona na kutambua kuwa eneo lile lilikuwa hifadhi, kwanini wananchi hawa hawakufahamishwa mapema iwezekanavyo kama ilivyokuwa *operation* ya vijiji?

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha hoja yangu kwa kuitaka Serikali kurudia tena maamuzi yake ya kuangalia suala la mipaka.

Aidha, eneo lililotengwa kwa matumizi Fulani, basi matumizi hayo yaheshimiwe. Kabla ya kufanya maamuzi haya, ni vizuri kurejea kwenye nyaraka zake mbalimbali na kurejea kumbukumbu hizo. Hivyo ni vyema Serikali ikatoa tamko la haraka kuhusiana na hoja hii ili wananchi wasibughudhiwe.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 18, imeeleza hali ya uchumi na kwamba pato la Mtanzania kwa mwaka 2012 ni Sh. 995,298/=. Kwa hesabu hii, ni sawa na wastani wa Sh. 2,798/= kwa siku. Hivi matumizi, kilo ya mchele ni Sh. 2,200/= na kwa kuwa lazima ugali upate mboga, tunawezaje kujidai kwamba hali ya uchumi imekua wakati hata mlo mmoja wa Mtanzania hawezi kumudu, na kwamba, fedha hiyo ni ya vocha tu?

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu hali ya kisiasa. Kisheria ni lazima tuwe na Wakuu wa Mikoa na Wilaya, lakini siyo jambo jema watu hawa kuwa wanasiasa, maana katika maeneo hayo ndiyo walipo pia wananchi na wapiga kura wote.

Kama hilo halitoshi, viongozi hawa ndiyo ambao wanawateua Watendaji wa Vijiji kwa Bara na Masheha kwa Zanzibar. Lakini watu hawa katika maeneo ya Vijiji na Shehia, ndio wanaopewa mamlaka ya kusema huyo anafaa au hafai wakati wa kutolewa haki ya kuandikishwa kupiga kura na wanasababisha matatizo makubwa. Lakini huku wakifanya kazi ya kusaidia CCM, hata wakati wa Kamati zao za Ulinzi na Usalama zilizopewa nafasi ya kuwajadili wanaotaka kujiunga na majeshi yetu, JWTZ na Polisi, hapa vijana wengine wenye sifa, lakini ambao sio vijana wa CCM hukosa nafasi. Baya zaidi ni kwamba, viongozi hawa wa Mikoa na Wilaya wanafanya kazi ya Chama lakini wanalipwa

fedha za wananchi toka Serikalini. Haiwezekani na huu siyo utaratibu mzuri na ni unyanyasaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hali ya mipaka ya nchi. Kuna taarifa kwamba Brigedia Ntaganda alitokea Ruanda na akaingia Kongo na Wakongo wakampa nafasi, lakini baadaye aliongoza waasi na alipoona ameshindwa, ndipo aliporudi Rwanda na akajisalimisha katika Ubalozi wa Marekani. Sasa inasadikika kwamba viongozi mbalimbali wa vijiji mbalimbali wamekuwa wakiwapa maeneo (wakiwauzia) kwa visingizio vya kuendesha mifugo yao wakimbizi toka nchi mbalimbali jirani. Je, hatuoni kwamba kwa mpango huu tunaweza kutengeneza akina Ntaganda hapa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, lingine ni ardhi. Siyo utoaji wa hati tu na kupima ardhi pekee kunakoleta matatizo kati ya Serikali na wananchi. Lakini pia hata Halmashauri za Miji na Vijiji nazo zinatumia vibaya mamlaka yao kwa kuuza kwa nguvu ardhi zinazokaliwa na watu bila kuwapa taarifa na baadhi ya wakazi kuleta taabu, wanaacha ugomvi na mzozo mkubwa baina yao na waliowauzia ardhi. Mfano, Halmashauri ya Jiji la Mwanza waliwauzia *NSSF* eneo la ardhi lililopo Bugarika na wakalipwa, lakini wakashindwa kuwalipa wakazi wa eneo hilo na hadi leo hapajawa na muafaka mzuri na walikataa kuondoka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari. Pamoja na makubaliano hayo ya kuanza kwa ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, lakini bado kuna matatizo makubwa katika eneo la Bandari kwa wale wanaoleta au kuingiza mizigo yao humu nchini. Watu wananyanyasika, rushwa zimetawala, lakini pia bado kungali kuna usumbufu kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoingiza mizigo yao katika bandari za huku Bara. Jambo hili ni tatizo la

zamani na hadi leo bado linaendelea. Naishauri Serikali ilitatue jambo hili haraka sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa zinazozikabili Halmashauri zetu ni ukusanyaji wa mapato, hali inayopelekea kushindwa kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo inayojiwekea. Ni kwa asilimia miamoja na mapendekezo ya Kamati ya Bunge, (TAMISEMI) juu ya umuhimu wa Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kukusanya mapato ya majengo. Bado hatua stahiki hazijachukuliwa na Halmashauri zetu licha ya mapendekezo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa ili kuboresha mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu hazina kabisa kumbukumbu *(database)* za majengo yaliyopo ndani ya maeneo yao ya utawala. Maeneo yaliyopo na thamani ya majengo husika katika hali kama hii ni ngumu sana kuweza kufanikisha ukusanyaji wa mapato ya majengo. Halikadhalika, mfumo wa makadirio ya kiasi cha fedha kinachotakiwa kulipwa kama kodi ya majengo imepitwa na wakati na hauzingatii kabisa hali halisi na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kwa Serikali kuliangalia suala hili kwa umakini mkubwa sana hasa katika Miji/Majiji, kwani yakisimamiwa kwa ufanisi, itapunguza mzigo kwa Serikali Kuu kuhudumia Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni makusanyo ya kodi ya ushuru wa huduma *(service levy),* ambayo Halmashauri zinatakiwa kutoza 0.3% ya mapato *(gross turnover)* ya kampuni zinazoendesha

biashara katika eneo la Halmashauri. Katika Halmashauri yetu ya Kinondoni, kumekuwa na malalamiko makubwa sana kutoka kwa watendaji kwamba kodi ya ushuru wa huduma imekuwa ikitolewa pungufu ya inavyostahili kwa sababu makampuni husika yamekuwa yakishirikiana na watu wa *TRA* kutoa taarifa ambazo siyo sahihi za mapato ghafi ya Makapmuni husika. Wakati mwingine Halmashauri zikitaka taarifa toka *TRA*, za mapato ya Makampuni husika ili wafahamu kama kinacholipwa ni kile kinachostahili, wamekuwa hawapati ushirikiano au wanazungushwa sana.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Serikali, ikaandaa utaratibu, utakaoielekeza *TRA* kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zinapata taarifa ya mapato ya Makampuni yaliyopo ndani ya Halmashauri husika. Ili kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa ushuru wa huduma, na ili kile kinachotozwa ndiyo kiwe kinachostahili. Halikadhalika, Serikali inaweza kufanya ukaguzi maalum kwenye Halmashauri chache ili kujiridhisha.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Nchi yetu iko katika mchakato maalum sana wa kutengeneza katiba ya nchi. Moja kati ya Taasisi ambazo zimepewa jukumu la kuendesha kura ya maoni ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kinyume na majukumu yake mazito, bajeti ya mwaka 2013/2014 Fungu la 61 halikidhi uzito wa kazi wa Tume hii.

Daftari la Orodha ya Wapiga Kura, ambalo linatakiwa kufanyiwa maboresho kila baada ya miaka miwili, halijafanyiwa maboresho mpaka sasa (miezi tisa imeshapita). Ni daftari hili hili linatarajiwa kutumika katika

mchakato huu muhimu wa kikatiba na katika Uchaguzi Mkuu 2015.

Mheshimiwa Spika, makabrasha ya Bajeti (Randama) ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Hotuba ya Waziri Mkuu, haionyeshi ni wapi fedha za maboresho ya daftari husika zilipo, zaidi ya kusema tu, kuna malengo ya kuboresha daftari husika. Kwa mujibu wa Taarifa za Tume, kiasi kinachohitajika kuboresha daftari siyo pungufu ya Shilingi bilioni 294.

Mheshimiwa Spika, naomba niambiwe, fedha husika ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la uendeshaji wa Shule za Msingi na Sekondari. Moja ya changamoto ambazo zimeelezwa katika hotuba ya Waziri Mkuu ni tabia ya kuvamia maeneo ya Shule za Sekondari na Msingi kwa kujenga vibanda na kuendeshwa kwa biashara za nyumba za kulala wageni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, kuna changamoto moja muhimu ambayo inazikabili shule zetu za Umma, nayo ni kutokujua mipaka ya maeneo ya shule.

Hali hii inapelekea siyo tu uwepo wa vibanda vya biashara, bali nyumba za watu za kuishi, Makanisa, Misikiti na kadhalika ndani ya viwanja au maeneo ya shule. Na kwa kuwa shule hazina hati, wala hazijui mipaka yake, inakuwa vigumu kwa Walimu Wakuu au Kamati za Shule kuhoji.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kwa Waziri Mkuu kuwaelekeza Wakurugenzi wachukue hatua za kupima maeneo ya shule za Umma haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, vurugu za kidini na chuki za wazi baina ya Wakristo/Waislamu inazidi kushika kasi. Hakuna hatua za dhahiri zinazoonekana kuchukuliwa na Serikali. Sasa hivi imefikia hatua ya mihadhara ya wazi wazi ya dini moja kukashifu na kukejeli dini nyingine. Serikali ilisitisha kuiruhusu iendelee.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Serikali ikafahamu huku uraiani hali ni mbaya sana. Kama hatua za haraka ni dhahiri kuchukuliwa, Taifa letu liko mbioni kuingia kwenye machafuko ya kidini.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu ya mwaka 2013/2014. Naomba kuchukua fursa hii ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ambayo inalenga kubadilisha maisha ya wananchi hasa wa vijijini kwa kuboresha huduma mbalimbali muhimu za kijamii na uchumi kama miundombinu, afya, barabara, elimu, maji safi na salama, utawala bora, usawa katika kutoa huduma, msisitizo katika Sera ya Kilimo Kwanza na mipango mingine mingi ya kuharakisha maendeleo kwa wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya Waziri Mkuu ya mwaka 2013/2014 kama itatekelezwa ilivyokusudiwa, nina imani kabisa itabadili maisha ya walio wengi ambao hali zao kimaisha na kimaendeleo ni duni na pia itapunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali zetu hapa nchini kama tunavyojua zina matatizo mengi sana. Hayo

matatizo ni changamoto kubwa kwa Serikali. Tumekuwa tukiona jinsi wagonjwa wanavyopata shida pale wawapo hospitalini, inawabidi kulala wagonjwa wawili kitanda kimoja na kwa bahati mbaya ikitokea dharula ya wagonjwa kuwa wengi, basi hufikia kiwango cha wagonjwa kulala chini, yaani sakafuni.

Hali hiyo ni hatari sana kwa wagonjwa, kwani inapofikia kulala chini au wagonjwa wawili kitanda kimoja, inawafanya wagonjwa wazidi kutokupata nafuu.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya pia yapo kwenye upande wa upatikanaji wa madawa. Tatizo la uhaba wa madawa ni tatizo kubwa sana katika hospitali zetu nchini na hii inapelekea watu kupoteza maisha kwa kukosa dawa kwa wakati. Kwa ujumla, hali siyo nzuri katika Sekta ya Afya na kwa kutambua hilo, napenda kuiomba Serikali itilie mkazo wa kutatua tatizo hili na kuboresha hospitali zetu. Kuna tatizo pia la upungufu wa Madaktari Bingwa nchini na hasa Mikoani.

Napenda kuiomba Serikali ipeleke Madaktari Bingwa katika hospitali zote ambazo zina upungufu wa wataalam hao. Kufanya hivyo itasaidia kupunguza usumbufu kwa wagonjwa kusafiri kuja Dar es Salaam kuonana na hao Madaktari. Pia kuna baadhi ya vipimo vinapatikana Dar es Salaam, ingawa Serikali ikiweza kusambaza vipimo hivyo kote nchini, itapunguzia wagonjwa hawa kusafiri umbali mrefu na kuja Dar es Salaam kuja kupimwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzungumzia hali ya Jimboni kwangu Kibaha vijijini. Tunatambua kila Kata inastahili kuwa na Kituo cha Afya, lakini kule Jimboni kwangu ni Kata chache tu ambazo zina Vituo vya Afya.

Naomba jambo hili liangaliwe vizuri na kwa mapana. Kata ya Mlandizi tuna Kituo cha Afya ambacho kinapokea wagonjwa wengi wapatao matatizo mbalimbali. Tuliomba kituo hiki kipandishwe hadhi na kuwa hospitali. Kwa kuwa kituo hiki ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupandishwa hadhi kuwa hospitali ya Wilaya, cha kusikitisha, mpaka sasa kituo hiki hakijapandishwa hadhi kuwa hospitali, sababu hakijakamilisha vigezo, tunajiuliza, ni vigezo gani vya msingi ambavyo havijakamilika ili kituo hiki kipandishwe hadhi? Asilimia themanini (80) ya vigezo vyote vimekamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu kwa huruma yake atusaidie Kituo hiki cha Afya kipandishwe hadhi na kuwa hospitali. Napenda kunukuu kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri kuwa hata Roma haijajengwa kwa siku moja. Kwa usemi huo, wakazi wa Kibaha Vijijini wanastahili kubadilishiwa Kituo hicho cha Afya na kuwa hospitali, kutokana na Kituo hiki cha Afya, Mlandizi, kutokupandishwa hadhi na kuwa hospitali. Wananchi wanapata taabu pale inapotakiwa kupata huduma za ziada na kutakiwa kusafiri kwenda hospitali ya Tumbi.

Mheshimiwa Spika, wananchi hao hutakiwa kuchangia ama kutoa fedha ya mafuta ili yatumike kwenye gari la kubebea wagonjwa kwa ajili ya kupelekwa hospitali ya Tumbi. Je, hii ni sheria kuwachangisha wananchi hela ya mafuta? Na kama siyo sheria, naomba jambo hili lisitishwe mara moja. Tunaomba Serikali iliangalie hili kwa ukubwa wake na kutekeleza ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais ya kupandisha hadhi kituo hiki na kuwa hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzungumzia mgogoro wa ardhi uliopo kati ya mwekezaji na wanakijiji wa Kijiji cha Kipangege na

Kitongoji cha Kifuru Kata ya Soga. Mgogoro huu unahusu lililokuwa shamba la mkonge ambalo ameuziwa mwekezaji ambaye ni *Mohamed Enterprises Ltd*. Naomba Serikali iuangalie mgogoro huu na kuutafutia ufumbuzi kwani wanakijiji wanataka kuhamishwa katika maeneo yao na kumpisha mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumekuwa na migogoro ya mipaka nchini kote. Nalo hili pia Jimbo la Kibaha Vijijini limekua ni tatizo kubwa kati ya Kata ya Kwala na Kata ya Ruvu, Kata ya Dutumi na Kitomondo, Kata ya Ruvu na Kikongo, mipaka yake haikuainishwa viizuri wakati wanagawa Kata kwani Ruvu ndiyo kata mama. Kwa hiyo, inaleta matatizo makubwa. Naomba Serikali ichukue hatua madhubuti kutatua matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, pia tuna migogoro ya wafugaji na wakulima Kata ya Gwata, Magindu, Kwala, Dutumi na Kata ya Ruvu, kuna migogoro ya wafugaji na wakulima. Wafugaji wametengewa sehemu maalum ya malisho, lakini wamekuwa wakivamia maeneo ya wakulima na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazao na kusababisha mgogoro kuanza.

Vile vile matatizo haya hufika Mahakamani ili hatua za kisheria ziendelee, lakini wakulima wamekuwa wakizidiwa nguvu katika kupata haki. Tunaomba Serikali iingilie kati matatizo haya ili kuepusha vurugu za wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa katika mfumo wa elimu. Mfano uliopo ni matokeo mabovu ya Kidato cha Nne. Hii ni aibu kwa Taifa, kwani tunatambua kwamba Taifa lolote ili liendelee lazima liwe na wasomi wazuri. Kwa mfumo huu

ambao tunao hivi sasa, hakika tunahitaji kuubadilisha ili tuendane na Mataifa mengine ili na sisi tupate maendeleo.

Vile vile Jimbo la Kibaha Vijijini tuna matatizo mengi sana kwenye Sekta ya Elimu, tuna upungufu wa Walimu, madawati, Maabara kwa ajili ya mazoezi ya vitendo katika shule zetu, pia vitabu vimekuwa haba kwa wanafunzi wetu, vilevile tumekuwa na upungufu wa matundu ya vyoo kwenye shule zetu. Napenda kuiomba Serikali kuliangalia hili na kulitafutia utatuzi wa haraka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali kuangalia upya suala la ajira kwa vijana, kwani mpaka sasa idadi ya vijana wasiokuwa na ajira inazidi kukua siku hadi siku.

Vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu kila mwaka ni wengi na wanaobahatika kupata ajira ni wachache mno. Ukiangalia kwa wastani huo utagundua kuwa tatizo ni kubwa sana. Naiomba Serikali iweke utaratibu wa kuwajengea elimu ya ujasiriamali vijana hawa tokea wakiwa Vyuoni. Hali hiyo itawasaidia pale wamalizapo elimu zao kujiajiri wenyewe na siyo kusubiria Serikali kuwaajiri.

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingi za kuweza kuwawezesha hawa vijana waliomaliza Vyuo na kufaulu vizuri. Nashauri ungewekwa utaratibu mzuri wa kuwapatia mikopo midogo midogo kutoka kwenye mabenki yetu ili waanzishe miradi midogo midogo. Kwa njia nyingine, watakuwa wamejiajiri wenyewe. Tunaweza kuweka utaratibu wa kuchukua vyeti vyao vya Vyuo walivyomaliza, yaani *(Original Certificate)* vikawa kama dhamana kwenye hayo mabenki ambayo watapatiwa hiyo mikopo.

Kufanya hivyo itawasaidia na utaratibu huu utasaidia sana pale tu Serikali itakapokaa na haya mabenki yetu na kuzungumza nayo na kuangalia mahali pa kuboresha utaratibu huu, kwani tatizo hili la kukosa ajira likizidi, litageuka kuwa hatarishi baadaye. Pia tuna mifano mbalimbali toka nchi nyingine kwa matatizo kama haya ya asilimia kubwa ya vijana kukosa ajira. Hii imesababisha kutokea vurugu na uvunjifu wa amani na nchi kuingia katika majanga makubwa.

Mheshimiwa Spika, najua Serikali ina nia nzuri sana na wakulima, kwani inatambua umuhimu wao katika nchi na hata ukizungumzia duniani kiujumla wakulima huthaminiwa sana na wana mchango mkubwa sana katika Taifa.

Kutokana na kuboresha Sekta ya Kilimo, Serikali ilikuja na mkakati wa Kilimo Kwanza, lakini imeonekana mkakati huo wa Kilimo Kwanza kutokufanya vizuri, kwani wakulima hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo.

Mheshimiwa Spika, napendeza Serikali ianzishe mkakati wa elimu kwa kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima kwa kuwa wakulima hawa wanaokusudiwa katika Kilimo Kwanza hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo.

Mheshimiwa Spika, tukija na mkakati wa Elimu Kwanza, itasaidia wakulima kupata elimu, kuelimishwa kuhusu kilimo bora na ndipo kupata tija na kilimo safi. Kufanya hivyo itasaidia pia kuwapeleka wataalam wetu vijijini na kutoa mafunzo kwa wakulima.

Niikumbushe tu Serikali kwamba tuna wataalam wengi wa fani mbalimbali hapa nchini, lakini tuna tatizo moja; hawa wataalam hawatumii fani zao ipasavyo ili kuisaidia nchi katika maendeleo.

Naomba Serikali iwapeleke hawa wataalam sehemu husika za fani zao na siyo kukaa Ofisi za Mijini. Hapa naongelea zaidi wataalam katika fani za mifugo, Mabwana Shamba na kadhalika. Kwani itasaidia sana kuinua wakulima na wafugaji na kuboresha sekta hizo na kuinua uchumi wa nchi na kipato.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ni tatizo pia linalokabili nchi yetu. Napenda pia kuipongeza Serikali kwa kujitahidi kuboresha miundombinu yetu, ila kuna ukiukaji wa sheria ambao hufanywa na madereva wachache ambao hupitisha magari yenye uzito mkubwa katika baadhi ya barabara zilizokataza uzito huo ilhali Serikali imetumia kiasi kikubwa cha fedha kuzitengeneza. Naomba usimamizi wa sheria uzingatiwe na adhabu kali zitolewe kwa wale wote watakaobainika kuvunja sheria hizo.

Katika Bunge lililopita, nilizungumzia Sekta hii ya Barabara, hususan ujenzi wa barabara ya Makofia - Mlandizi hadi Mzenga ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi.

Nilipouliza katika swali langu la msingi katika Bunge lililopita, nilijibiwa kuwa walikuwa wanafanya upembuzi yakinifu, lakini baada ya mimi mwenyewe kufanya uchunguzi wangu wa kina, niligundua kuwa hakukufanyika upembuzi yakinifu na hakuna fedha zozote zilizotengwa. Lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake, amesema ile barabara itajengwa kuanzia Bagamoyo mpaka Mlandizi, ikizingatiwa Bandari ya Bagamoyo inayojengwa itafanya hiyo barabara kutumika kwenda Bandari ya nchi kavu Mzenga ambako kuna kituo cha Reli ya Tazara. Lakini pia hakuna uhakika kama itajengwa kutoka Mlandizi mpaka Mzenga; barabara ya Kongowe

– Soga - Kisarawe pia zingepandishwa hadhi kuwa barabara ya Mkoa.

Vilevile barabara za Vigwaza - Kwala na Dutumi hadi Kisarawe pia zipandishwe hadhi kuwa barabara ya Mkoa.

Hata hivyo, barabara za Chalinze, Gwata, Magindu, Lukenge hadi Morogoro vijijini, barabara hizi zimeunganisha Wilaya tatu zikiwa katika kiwango cha lami. Tutakuwa tumefikia lile lengo la kuunganisha Wilaya hadi Wilaya na kuwafanya wananchi wa Wilaya hizo kufanya shughuli zao za kibiashara kwa urahisi. Naomba bajeti ya mwaka huu itilie mkazo katika hili kwani umuhimu wa barabara hizo ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alituahidi kujenga soko la kisasa Mlandizi na kiwanda cha kusindika nyanya, lakini mpaka leo hakuna utekelezaji wa aina yoyote. Tunaomba maelezo kutoka kwa Waziri wa Viwanda na Biashara atakapoleta bajeti yake hapa Bungeni, atuambie hizi ahadi za Mheshimiwa Rais zitatekelezeka lini? Kwani wananchi wa Kibaha vijijini bado wanaendelea kupata hasara kwa kukosa mahali pa kusindika mazao yao kipindi chote hiki.

Pia kuna mradi wa machinjio ya kisasa. Mradi huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais, lakini cha kushangaza mradi huo haufanyi kazi yoyote ikizingatiwa kodi za wananchi ndizo zilizotumika kufanikisha mradi huo, lakini mpaka hivi sasa umeachwa bila kufanya kazi yoyote ilhali wananchi walihamasishwa na kuhamasika, wakanunua ng'ombe wa kisasa ili waanze ufugaji. Lakini hivi leo wanapata hasara kutokana na mradi huo kutokufanya kazi na pia kupoteza ajira. Mradi huo ungeanza kufanya kazi ungetoa ajira kwa vijana na kusaidia tatizo la ajira kwa kiasi kupungua.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini linakabiliwa na tatizo kubwa la maji kwa wananchi wake, ingawa wananchi hawa ndio walinzi wakuu wa chanzo cha maji kinachotoka Ruvu kuelekea Dar es Salaam. Lakini wananchi hao wana matatizo makubwa ya maji. Naomba Wizara husika iwaangalie wananchi hawa kwa jicho la huruma ili na wao waondokane na adha hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, vilevile miradi mingi inasuasua katika utekelezaji wake, mfano mradi wa Chalinze, Magindu hadi Lukenge hadi sasa utekelezaji wake unasuasua. Pia na mradi wa Ngeta ambao unatakiwa upeleke maji katika vijiji vya Kikongo Mwanabwito na Soga na Kipangege. Pia kuna tatizo la muda mrefu la upatikanaji wa maji Kata ya Boko, Mnemela Vijiji vya Boko Kati, Mpiji na Mkalambati. Tunaomba maelezo ya miradi hii kwa Wizara husika na ikibidi utekelezaji wake uanze ili wananchi hawa waondokane na shida ya kutokupata maji safi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kutatua tatizo na kupeleka umeme Kata ya Ruvu. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa ahadi hii ulishaanza kwa Waziri wa Nishati na Madini kufanya ziara katika Jimbo na akaona ukubwa wa tatizo.

Napenda kujua ni hatua zipi zimefikiwa na nini kinaendelea katika utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme katika Kata ya Ruvu, kwani kupeleka umeme katika Kata ya Ruvu kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia upandaji wa nauli ulioanza hivi karibuni. Tunatambua kabisa upandaji huu wa nauli unawagusa moja kwa moja wananchi wa hali ya chini. Kiwango hiki ni kikubwa mno ukilinganisha

na kipato cha mwananchi wa kawaida. Naiomba Serikali iangalie upya mchakato mzima na kama ikiwezekana nauli za zamani ziendelee kutumika wakati Serikali inaangalia uwezekano wa kutatua tatizo hili, kwani mwananchi huyu anayepata mshahara mdogo na anayeishi mbali, yapata kutumia mabasi mawili mpaka matatu kwa siku, hawezi kumudu nauli hizi zilizopandishwa na tayari kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika sera ya uwekezaji, napendekeza Sheria ya Uwekezaji iwekwe bayana kwa kumnufaisha mwananchi. Sheria hiyo iboreshwe kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na wananchi wake. Mwekezaji yeyote wa nje ni lazima awe mbia na mwananchi na hasa katika masuala ya madini. Hapa kwenye Sekta ya Madini tumekuwa tunapata matatizo mengi kutokana na mikataba tunayoingia kutokusimamiwa vizuri na kutokutunufaisha kabisa.

Nashauri Sheria ya Madini iboreshwe ili tufaidike na Madini yetu na tukue kiuchumi, kwani tuna madini mengi sana na mwingine huwezi kuyapata nchi yoyote isipokuwa hapa kwetu Tanzania. Kwa kuzingatia hilo, kulikuwa hakuna sababu ya umaskini kuendelea kutukandamiza, bali tungekuwa tunafaidika na rasilimali hiyo. Kuna wawekezaji katika Sekta ya Madini, wamekuwa hawatekelezi yale yote waliyoahidi kuyafanya kwa jamii iliyowazunguka na hivyo kuwajengea wananchi imani potofu kuona kuwa Serikali yao haifai kwa kuingia mikataba na wawekezaji kama hao. Naomba wawekezaji wa aina hii wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, suala la foleni jijini Dar es Salaam linazidi kuwa tishio na hivi sasa limeanza kutokea katika Miji mingine pia kama Arusha, Mwanza ingawa katika Miji hiyo hali haijafikia katika kiwango kama cha

Dar es Salaam. Kwa mfano, hivi sasa Dar es Salaam kuna huu mradi wa mabasi yaendayo kasi. Napenda kwanza kuipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia kwa mradi huo, lakini kama tujuavyo, changamoto huwa hazikosekani.

Kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali kupitia Wizara husika kuweka utaratibu wa mkandarasi kufanya kazi usiku ili mchana kupisha magari mengine kupita bila kusuasua, kwani kwa hivi sasa kumekuwa na msongamano mkali pale mkandarasi anapofunga njia moja ama nyingine, foleni huwa kubwa sana na kufanya safari moja kutumia masaa zaidi ya matatu mpaka manne. Tukifanya hivyo, itasaidia, kwani muda wa usiku watumiaji wa barabara wanakuwa ni wachache ukilinganisha na mchana.

Pia napenda kushauri upande wa Mikoani kuchukua tahadhari mapema kwa kuboresha miundombinu ili kuepuka hali ambayo inaikumba Miji mingine kwa matatizo ya foleni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashauri watu wa Mipango Miji kuweka mipangilio mizuri na inayovutia katika Miji inayokua hivi sasa ili kuleta mandhari nzuri. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kwa watoa huduma kupanga kutoa huduma kutokana na Miji hiyo ilivyopangwa vizuri na itarahisisha pia kufikika kwa haraka kwenye matukio kama ya moto, kwani tumejionea wenyewe mara nyingi pindi litokeapo janga la moto, ufikaji wa gari la zima moto unakuwa mgumu na pindi linapofika, hufika kwa kuchelewa na lawama kupelekwa moja kwa moja Jeshi la Zimamoto. Lakini tukiwa na Miji iliyopangika itasaidia sana kupunguza adha hii.

Mheshimiwa Spika, ifahamike kwamba matumizi ya fedha za kigeni yanaathiri sana uchumi wetu na watu

wetu pia. Naomba Serikali itilie mkazo na kusimamia hilo na kukaza biashara ndani ya nchi zisifanyike kwa fedha za kigeni na badala yake Shilingi yetu ndiyo itumike katika matumizi yote. Kufanya hivyo kutaleta heshima ya sarafu yetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha vijijini liko mbali na Ofisi za Halmashauri ambazo zipo Kibaha Mjini. Wananchi huteseka kutembea umbali mrefu wa kilometa 40 kuanzia Kata ya Magindu mpaka Kibaha Mjini kufuata huduma muhimu. Kwa maana nyingine huduma wanainunua kwa gharama kubwa huku kipato chao kikiwa ni cha chini, na huacha shughuli zao mbalimbali za kujitafutia kipato.

Nashauri Ofisi hizi zihamishiwe Mji mdogo wa Mlandizi, kwani kuna maeneo hata ya kukodi ili kuwapunguzia wananchi mzigo mkubwa. Ukizingatia hilo, pia kuna tatizo la ukosefu wa Benki. Tunaishauri Serikali itoe msukumo ili tuweze kupata Benki kuwapunguzia adha wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kugusia lililojitokeza siku za usoni. Nchi yetu tangu hapo awali hatukuwahi kuwa na migogoro ya kidini, lakini siku za karibuni tumejionea wenyewe kuanza vurugu la hiyo migogoro. Kwa hali hiyo, napenda kuishauri Serikali kuchukua hatua za dhati mapema na kukemea ikibainika ama kikundi au watu wanaosababisha hali hiyo, wachukuliwe hatua kali za kisheria mara moja ili kuepusha nchi yetu kuingia katika migogoro hiyo ya kidini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri Mkuu (bajeti ya mwaka 2013/2014).

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika vipengele vikuu vitatu. Mgawanyo wa fedha (vipaumbele), elimu (anguko la elimu ya Tanzania), na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia hotuba ya Waziri Mkuu na randama, nimegundua kuwa fedha za maendeleo ambazo Bunge lako Tukufu likiidhinisha kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kiasi cha Shilingi bilioni 91.7 kwa ajili ya maendeleo ni kiasi cha Shilingi bilioni 10.7 tu ndizo zilikuwa zimetumika hadi robo, yaani asilimia 11.7 tu. Cha kutia mshituko zaidi ni pale fedha za matumizi ya kawaida zilivyopewa kipaumbele. Sasa nchi yetu itaendelea lini? Hii inatokana na Majeti ya Maendelo kutegemea fedha za wahisani na siyo fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa hadi Februari, takriban Shilingi bilioni 81 zilikuwa hazijatumika. Hii ina maana hata kufikia mwisho wa mwaka, sana sana 25% tu ndiyo itakuwa imetumika. Hivyo kuacha baki ya zaidi ya Shilingi bilion 65. Bila hata kutilia hili maana, bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa ajili ya maendeleo ni Shilingi bilioni 43.8 ambazo ni pungufu kwa asilimia zaidi ya 52 tena. Hizi Shilingi bilioni 43.8 hazifiki baki ya mwaka unaomalizikia Juni 31, sasa je, hayo maendeleo mengine yamesitishwa au bei/gharama zimeshuka chini? Ni kwa nini Serikali inaendelea kutegemea fedha za wahisani kwa zaidi ya asilimia 86 ilhali ikijua wahisani hawatoi fedha ndani ya muda?

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuzungumzia kuhusu fedha kiasi cha Shilingi bilioni moja zilizotengwa kwa ajili ya kuendeleza mahali pa kuzikia viongozi wa kitaifa. Hivi ni kweli tuna vipaumbele vya kuwasaidia Watanzania? Tunashindwa adha kubwa ya akina mama kuzalia chini na/au kulala kwenye kitanda kimoja zaidi ya wamama watatu.

Vilevile tumeshindwa Watanzania kujitangaza kwenye vyombo mbalimbali vya habari wakiomba msaada ili kwenda kutibiwa katika hospitali za Serikali kama Muhimbili na/au kwenda nje ya nchi (India) ambapo wengi wao wamekuwa wakikosa msaada na kufa. Tena fedha zenyewe huwa ni Shilingi milioni moja hadi kumi. Leo tunashindia fedha, zikitengwa kwa ajili ya kuja kuzika viongozi walio hai. Huu ni uchuro na matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa waasisi wa nchi yetu wamezikwa kwenye maeneo yao. Nataka kujua: Je, ni utashi wa Serikali kufikiri kuendeleza sehemu za kuzikia au kuna viongozi wa kitaifa wameomba mara watakapokufa wazikwe kwenye makaburi ya Shilingi bilioni moja?

Mheshimiwa Spika, napenda pia kujua ni vigezo vipi vinatumika kujua kaya hii ni masikini na inahitaji kupewa msaada wa chakula, lishe bora, huduma ya afya na elimu? Ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa kila kaya kwa lishe, chakula, afya na elimu? Baada ya kujua vigezo husika, naomba kutoa ushauri wangu ambao utatuomba ili kuondoa mianya ya ubadhirifu au rushwa. Ni bora zitolewe vocha/kadi kwa ajili ya huduma ya afya na elimu kuliko kutoa fedha. Nchi za wenzetu wanatoa vocha kwa ajili ya chakula na lishe bora. Pia, hii itasaidia matumizi lengwa ya hizo Shilingi bilioni 440, na hasa katika kaya 3,056 ambazo ndizo tunaanza nazo katika Halmashauri ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie kuhusu wachimbaji wadogo wadogo, na hasa wa Wilaya ya Tarime. Ni dhahiri kwamba wachimbaji wadogo wadogo ndiyo mojawapo ya kitovu cha uchumi wa nchi yetu, na mbaya zaidi baada ya mauaji ya mwaka 2011 kule *North Mara*, Mawaziri wengi, akiwemo Waziri

wa Sera na Mahusiano -Mheshimiwa Wassira waliahidi kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo na kuwasaidia elimu na miundombinu ya kuchimbia. Kwa masikitiko, hadi leo hamna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo, licha ya mwekezaji kuwa tayari kusaidiwa na uwepo wa maeneo mengi kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Leo katika hotuba, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaonyesha kutengwa kwa eneo la Nyakuru tu, na wakati akijibu swali Mheshimiwa Malima alionyesha kutengwa maeneo mengi ya Nyakunguru, Gamasara, Nyahuguru na kadhalika havikubaliki.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sote tunatambua umuhimu wa kuwa na Serikali za Vijiji na Halmashauri zao zinazowajibika kwa wananchi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa, hata hivyo, Halmashauri hizo za vijiji zimekuwa hazisomi mapato na matumizi kwa wakati kwa mujibu wa sheria, tatizo hili linalopelekea wananchi kutojua fedha wanazochanga au fedha zinazofika kijijini, kwa mujibu wa mgao wanaopata kijiji husika kutojulikana, ni kiasi gani kimetumika na kiasi gani kimepatikana na kwa ujumla tatizo hili limekuwa sugu na Serikali kupitia Ofisi ya TAMISEMI kuwa kimya bila kuangalia njia nyingine mbadala ya (au kurekebisha sheria husika) kufanya Halmashauri za Vijiji ikiwa ni pamoja na Wenyeviti wao kuwajibika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, dhana ya ugatuaji wa madaraka ifanyike kwa matendo, hivyo iwe ni pamoja na kuangalia pia muundo wa Halmashauri zetu nchini ili wananchi wafikiwe na huduma kwa urahisi bila urasimu wowote. Naitaka Serikali kuangalia upya muundo huo na kuongeza Idara na Vitengo mbalimbali kama Idara/Kitengo cha Vijana na Habari. Hata hivyo,

kwa kuwa kuna Kitengo cha Utamaduni, ni vyema ikaongezewa suala la michezo.

Mheshimiwa Spika, matumizi makubwa ya fedha za matumizi ya kawaida, tumeshuhudia fedha nyingi zinakwenda katika matengenezo makubwa ya magari ya Halmashauri. Kimsingi sipingani na suala la magari kufanyiwa matengenezo, lakini napingana na mfumo wa usimamizi wa suala zima la kusimamia na kuandaa malipo ya gharama na ujazaji wa *LPO.*

Suala hili limekuwa likiachwa lifanyike kati ya dereva na mzabuni, ndipo hapa udanganyifu unapofanyika na suala la kutokuwa na *Transport Officer (TO)* anayefahamu (ujuzi) wa masuala ya ufundi wa magari ndipo udanganyifu unapoendelea kutokea. Halmashauri nyingi huwapa nafasi hizi watumishi katika Idara nyingine jambo ambalo hawawajibiki moja kwa moja kwa nafasi hiyo ambayo siyo fani yake.

Ni vyema Serikali iifanye Idara hii ya *TO* iwe na mwajiriwa mwenye fani ya utengenezaji magari na kuangalia mali zote za Halmashauri ambazo zipo kwenye mfumo wa vyuma, kwa kuwa ni kweli kuwa Halmashauri haziwezi kutekeleza majukumu yake bila kuwa na magari.

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie kati masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha Wizara ya Ujenzi ilipanga kutumia Shilingi bilioni 1.7 kuanza ujenzi wa barabara itokayo Nyamswa hadi Nansio. *Tanroads* imetangaza *tender* ya kutengeneza barabara ya kilometa 51 toka Nansio – Bulamba.

Mwaka 2013/2014 hakuna fedha yoyote iliyowekwa katika bajeti. Je, huu ni usanii au nini? Mwaka 2012/2013 Wizara ya Ujenzi ilitenga Shilingi bilioni tatu kuanza ujenzi wa barabara ya Makutano, Natta, Mugumu, Loliondo hadi Mto wa Mbu. *Tender* imetolewa, lakini hakuna hata kilometa moja iliyotengenezwa. Mwaka ujao wa fedha, bajeti iliyotengwa ya Shilingi bilioni nane: Swali hapa ni kwamba, itatuchukua miaka mingapi kutengenezwa barabara yenye kilometa 400?

Mheshimiwa Spika, hapa kuna tatizo linahitaji kutazamwa, hapa hakuna anayekomolewa ila CCM!

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naanza na kuipongeza hotuba hii ya Waziri Mkuu na ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la udini ambalo ni hatari sana ambalo linaweza kututumbukiza pabaya sana kwa Taifa letu, naishauri Serikali ichukuwe hatua kali kwa wale wote watakaobainika na uchochezi huu ili kuokoa kulitumbukiza Taifa katika mgogoro wa kidini.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu migogoro kati ya wafugaji na wakulima, tatizo ambalo linazidi kujitokeza nchini sehemu mbalimbali. Naishauri Serikali ichukue maamuzi ya haraka kulitafutia ufumbuzi kwa wafugaji kuwatengea maeneo rasmi ya kufugia na mashamba ya kulishia mifugo yao na kuepusha pia uharibifu wa mazingira. Suala la migongano na wakulima, hili pia litampa utulivu mfugaji na kutomfanya asihame na kumfanya apange mipango endelevu kama kusomesha watoto shuleni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu janga la madawa ya kulevya ni tatizo kubwa ambalo linazidi kukua kwa kasi sana na kuwadhuru watumiaji hasa vijana.

Ushauri wangu kwa Serikali, naiomba Serikali iwashirikishe wananchi wote kuwahamasisha kwa kutoa semia na vyombo vya habari, nyumba za ibada, na kutoa motisha kwa wale wote watakaofanikisha kwa kukamatwa kwa madawa hayo na kumlipa angalau asilimia 50 ya thamani ya mzigo. Hili litaleta hamasa sana kwa watoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu janga kubwa la uharibifu wa mazingira, naishauri Serikali ichukue hatua kali zaidi kwa wote ambao wanakata miti ovyo na kuharibu vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kulima maeneo ya vyanzo vya maji.

Pia naishauri Serikali iwaangize wananchi wote wapande miti, miche 50 kila kaya, maeneo ya makazi na mashambani pia. Miti ni mali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila Taifa lazima liwe na wazee: Je, wazee wa Taifa hili wamewekewa mipango gani kuhusu hatima yao ili nao wafaidike na Taifa au Serikali yao? Wazee hao hasa waishio vijijini, hali zao ni mbaya sana na kukata tamaa ya kuishi duniani na wengine kufikia kujiua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushuka kwa elimu, naishauri Serikali iweke msukumo mkubwa kwa Walimu; pia kutoa elimu kwa wazazi kutambua umuhimu wa elimu ikiwa pia kuwahamasisha watoto wao kutii sheria za nchi na shuleni kwao. Pia wazazi kuchangia kwa michango yote kwa wakati, kwa kujitolea kwa ujenzi wa madarasa, nyumba za waalimu na madawati; na mahusiano mazuri kati ya wazazi na Waalimu. Haya yakifanywa, ni imani yangu kuwa elimu itapanda zaidi.

Mheshimiwa Spika, upungufu ni mwingi sana katika Vituo vya Afya na Zahanati zote katika Jimbo la Nyang'hwale. Upungufu uliopo ni kama madawa, madakitari, Wauguzi na vifaa tiba. Upungufu huu umekithiri hasa Kituo cha Afya cha Khalumwa. Kituo ambacho kinapokea wagonjwa wengi sana.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nyang'hwale lina matatizo makubwa sana ya maji safi na salama. Nimewahi kuuliza swali hili na kujibiwa kuwa tayari pesa imetolewa kiasi cha Sh. 20,000,000/= kwa ajili ya upembuzi yakinifu, kutoa maji Ziwani Nyamtukuza, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea. Swali, ni lini sasa Serikali itamaliza tatizo la maji Wilaya mpya ya Nyang'hwale?

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa kwa wakulima wa Jimbo la Nyang'hwale ni pembejeo kutolewa kwa wakati na kuletwa kwa mbegu ambazo hazina ubora. Wakulima wanahoji: Je, Serikali haifahamu hili? Naiomba Serikali ifuatilie hili ili wakulima wawe na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali kwa baadhi ya barabara kufanyiwa matengenezo madogo madogo kama barabara ya kutoka Geita – Nyang'hwale na kutoka Busisi - Nyang'holongo. Napenda kuuliza swali. Mheshimiwa Rais alipokuja

Jimbo la Nyang'hwale mwaka 2010 kwenye Mkutano wa Kampeni pale Khalumwa, aliwaahidi wananchi wa Nyang'hwale barabara za kutoka – Busisi, Busowa – Nyijundu – Kharumwa – Bukwimba hadi Nyang'holongo – Kahama, na kutoka Geita - Nyang'ghwale – Kharamwa. Zitajengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la nishati ya Umeme, naishukuru sana Serikali kwa kuanza kutekeleza hili Jimboni Nyang'hwale kwa kusimika nguzo na kutandaza nyaya katika Kata ya Nyang'hwale – Nyijundu, Kalumwa. Leo ni zaidi ya miezi sita, kazi imekamilika. Je, baada ya kukamilika kwa kazi hiyo, ni lini umeme huo utawaka?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano ya simu, naiomba Serikali ifanye hima kuwashauri wenye Kampuni za Simu za Mkononi kuja Wilaya ya Nyag'hwale kuja kufunga minara Kata ambazo hazina minara kama Bukwimba, Kafita, Izunya, Nyugwa, Kakora, Nyijundu, Busolwa, Nyang'hwale, Shabaka, Nyabulanda na Mwingiro ili Wilaya hiyo mpya ipige hatua ya maendeleo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Mahakama katika Wilaya mpya ya Nyang'hwale majengo ya Mahakama na Mahabusu ni mabovu sana. Pia Vituo vya Polisi ni vibovu sana. Naishauri Serikali ikarabati majengo hayo na kujenga mapya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kazi nzuri ya kujaribu kutatua msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam, lakini katika utatuzi huu, daraja la salender, daraja la reli pale Gerezani yameachwa. Kwa hiyo, kilichofanyika/kinachofanyika ni kukusanya magari kwa wingi kutoka pande mbalimbali za Wilaya ya Kindondoni na makutano, ni katika daraja la *Salender*. Halikadhalika, magari yanatoka njia nyingi zilizofunguliwa kutoka Wilaya ya Temeke – Kurasini na

kukusanyika katika Daraja la Reli *Gerezani/Port*. Vile vile hali hii ipo kwenye njia panda ya Tazara, Ubungo, Veta Chang'ombe, Ilala Boma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali hii inafanya kazi nzuri ya Serikali kutokuzaa matunda yaliyotarajiwa. Ni kama vile kila Wilaya ilifanyiwa kazi peke yake bila kuangalia miundombinu na mpango wa Ofisi zetu kwamba zote zipo kati, yaani Wilaya ya Ilala na kufanya kila mtu lazima aje Wilaya ya Ilala. Reli ya Dar es Salaam inahitaji kuimarishwa ifanye kazi sawasawa.

Mheshimiwa Spika, msongamano huu hauishii kwenye barabara tu, lakini hata maofisini Dar es Salaam ambayo ina wakazi takribani milion 4.7 na inayotegemewa kwa asilimia zaidi ya 80 ya mapato ya Serikali ina Wilaya tatu tu. Ndiyo maana hata Taasisi nyingine zimeona ni vigumu kutoa huduma kwenye Taasisi zao na kulazimika kuunda Mikoa Maalum. Taasisi hizo ni Polisi, *TANESCO*, *TRA* na kadhalika. Hii siyo tu kwa Taasisi hiyo, lakini ni adha karibu kwa Ofisi nyingi ikiwa ni pamoja na Ofisi za Manispaa zote.

Mheshimiwa Spika, ukichukua idadi ya watu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni takribani asilimia 10 ya Watanzania kufuatana na sensa ya mwaka 2012 na idadi ya Wilaya za nchi yetu ni takribani 162. Ungedhani basi Dar es Salaam ingekuwa na Wilaya 16 ili iweze kukidhi kuhudumia wananchi wa Mkoa huo ipasavyo. Sasa hivi mwanachi wa Pemba Mnazi, Kimbiji inamchukua siyo chini ya masaa mawili mpaka matatu kwa gari kwenda Wilayani Temeke kwa gari binafsi na kama ni kupanda, basi itachukua masaa zaidi na nauli siyo chini ya Sh. 3,000/=. Hivyo hivyo kwa wakazi wa Mbotele, Msongola kwenda Ilala na halikadhalika wakazi wa Bunju Goba, Malambamawili kwenda Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Dar es Salaam basi aidha iletwe Mikoa mitatu yenye Wilaya tatu kila Mkoa? Au basi kwa kuanzia, tuwe angalau na Wilaya tisa. Hii siyo tu itasaidia kusogeza huduma kwa wananchi na ni huduma zote, lakini pia itaongeza ufanisi na hivyo kuongeza mapato ya Taifa. Sasa hivi kuna mapato mengi sana yanapotea ikiwa ni pamoja na kodi za majengo, mahoteli na biashara nyingi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ni kwa manufaa ya Taifa zima, kwani wananchi karibu wote wanahitaji huduma ya Dar es Salaam. Naomba nitie mkazo wa utatuzi wa mkakati madhubuti na mahsusi wa msongamano wa magari na huduma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inao uwezo wa kutatua ajira kwa vijana kwa mamilioni ya fursa kwa kutumia kilimo, lakini huwezi kusema uwape mkopo vijana wakafanye, ni lazima wapate kilimo chenye tija. Ni kwa nini Serikali isiandae maeneo yenye rutuba na maji, ikaandaa mashamba makubwa kwa kulima kwa trekta, ikawapa mbegu bora, mbolea, dawa na magunia, lakini pia wasaidiwe chakula kwa kipindi cha mpito? Hii itahamasisha vijana wengi kujiunga na mpango huu. Kuwaambia vijana nendeni bila kuwahakikishia kilimo kisicho na tija hakuna atakayekwenda huko.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, naanza na kuunga mkono hoja. Waziri Mkuu katika hotuba yake amegusa maeneo mengi ambayo Serikali imefanya kazi kwa manufaa ya Watanzania. Kuna changamoto ambazo napenda kuishauri Serikali iweze kufanyia kazi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Wananchi wanatumia muda mwingi

katika kutafuta maji kwa kutembea kilometa wakitafuta maji.

Naomba Serikali ichukue hatua kubwa katika kutekeleza tatizo la maji katika maeneo yote ambayo yana tatizo kubwa la maji. Katika Jimbo la Mufindi Kusini tuna matanki ya maji 10 ambayo yamejengwa na Serikali kwa kushirikiana na wananchi, lakini sasa hivi yote hayatumiki kwa sababu miundombinu imeharibika.

Tunaomba Serikali kufufua au kukarabati matanki hayo, nayo ni Tanki la Kijiji cha Sawa, Kibao, Igowole, Nyololo, Maduma, Ndumuka, Nyigo, Idunda, Njojo na Mgololo. Vyanzo vyake vipo, lakini ni miundombinu yake, imeharibika. Gharama yake haizidi Shilingi bilioni mbili tu. Naomba sana Waziri Mkuu, Serikali isaidie Jimbo hili la Mufindi Kusini, wananchi hawana maji.

Mheshimiwa Spika, umeme katika kuinua uchumi wa wananchi wetu ni muhimu sana. Vijiji vingi sana katika Jimbo la Mufindi Kusini havina umeme.

Vijana wanapenda kujiajiri kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo katika vijiji vya Idetero, Mbalamaziwa, Malangali, Ihowanza, Iramba, Nyigo, Mtambula, Idumka, Kilolo na Ihomasa; kuna Vituo vya Afya lakini havina umeme kama vile Kituo cha Afya kijiji cha Nyololo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuongelea kuhusu migogoro ya dini. Chokochoko zinazojitokeza si salama kwa mustakabali wa nchi yetu. Serikali kuwaachia viongozi wa madhehebu ya dini kuwaelimisha waumini wao si sahihi. Serikali iwachukulie hatua wale wote watakaobainika

kukomesha tabia ya kuuana na kuchoma Makanisa, Misikiti na kuingiliana katika dini zetu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tabia ya ubaguzi wa kidini hasa viongozi kubagua watu wa dini fulani katika ajira mfano *UDOM*. Kufeli kwa mwanataaluma Chuoni ni kigezo cha kumfukuza kazi au kuwa *re-categorized* kama *administrative staff*. Cha ajabu kuna Waislam wanafeli na wanapewa nafasi ya kusoma upya badala ya kufukuzwa na wakati huohuo Wakristo wanafukuzwa. Hayo ni malalamiko ya wafanyakazi wa *UDOM*. Mfano, Mwislam Khamis Mkanachi alikuwa anasoma Master *UDSM* na akafeli, yeye akapewa nafasi upya *UDOM* na anaendelea. Mkristo Masebo alikuwa anachukua Master *UDOM,* akafeli yeye akafukuzwa. Je, hamuoni pia hilo ni tatizo kwa wanaofanyiwa hivyo au kuona ni Udini?

Mheshimiwa Spika, pili ni kilimo. Kilimo kwanza ni kauli mbiu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini utekelezaji wake una udhaifu mwingi ambao unakwamisha kilimo. Naishauri Serikali, nia njema ya kutenga hizo shilingi bilioni 75 kwa ajili ya vocha za pembejeo, ni vema kuzipeleka fedha hizo Idara ya Umwagiliaji ili kuondoa adha ya ukame na umaskini. Fedha za vocha za pembejeo hutumika vibaya, kuchelewa kutolewa, makampuni na mawakala wasiofaa, matumizi ya vocha za ruzuku ya pembejeo kuwa chini ya viwango, wizi na uharibifu wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 141 cha Sheria Na. 7 mwaka 1982, Mkutano Mkuu ndio mamlaka yenye madaraka ya juu kabisa kuhusu maamuzi yote ya sera na maendeleo kijijini na ndiyo wenye wajibu wa kuchangia na kuwaondoa madarakani wajumbe wa Halmashauri ya kijiji lakini kwa

masikitiko makubwa watendaji wa Serikali, Mkurugezi Mkuu wa Wilaya, *OCD,* Mkuu wa Mkoa, badala ya kuheshimu maamuzi yanayofanywa na wananchi, wamekuwa wanawatisha na kuwakamata na kuwekwa mahabusu. Matokeo yake kuwaachia bila kuwapeleka Mahakamani ili wapate haki zao. Huu si utawala bora bali kulinda maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Jimbo *(CDCF),* kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo ya mwaka 2009 inasema orodha ya miradi inayoweza kutekelezwa na Mfuko inatakiwa kuibuliwa na wananchi ambao wanaishi katika Jimbo husika. Pia kifungu cha 10(4) kinataka kila Kata kuja na miradi inayopewa kipaumbele na kuiwasillisha kwenye Kamati ya Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kuidhinisha miradi hiyo.

Je, ni kwa nini hakuna uwazi katika usimamizi na uwajibikaji wa Mfuko wa Jimbo na hasa kutumika kwa nia ya kisiasa? Fedha za Mfuko wa Jimbo Hanang zinagawanywa zaidi wakati wa uchaguzi mfano zaidi wakati wa uchaguzi mfano wakati wa uchaguzi wa CCM NEC.

Aidha, kutofuatwa uibuaji wa wananchi kwenye vijiji bali ni kutekeleza ahadi za Mbunge, kugawa na kuwapa vikundi vya Saccos na kadhalika, kuwapatia viongozi wa CCM badala ya wavijiji. Inatakiwa huu Mfuko uwe wazi na watakaobainika wasipewe fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Viti Maalum pia ni wawakilishi Mikoani na hufanya au kutekeleza miradi ya maendeleo. Ni vema na Wabunge wa Viti Maalum kutengewa fedha za *CDCF* ili kusaidia miradi hiyo. Wabunge wa Viti Maalum wawe pia katika Kamati ya Mfuko wa Jimbo *CDCF*. Wabunge wa Viti Maalum

wawe kwenye Kamati za Uchumi na Fedha katika Halmashauri yao.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, miezi kadha imepita tokea Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kukamilisha zoezi hilo kwa kupita kila sehemu ya nchi ili wananchi na viongozi mbalimbali waweze kutoa maoni yao juu ya Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kufanya majumuisho, anipe ufafanuzi wa masuala yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 18(1) inasema kwamba kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake bila kuathiri sheria za nchi na kwa kuwa Waziri ni katika watu ambao kwa mujibu wa Ibara na kifungu cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano nilichokitaja yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake bila ya kuathiri sheria na nchi, Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa kauli gani juu ya Chama cha Siasa nchini kinachozuia watu wake kutoa maoni yoyote yakiwemo yanayohusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar?

(b) Kwa kuwa uamuzi uliochukuliwa dhidi ya aliyekuwa Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, Mheshimiwa Mansoor Yussuf Himid wa kuondolewa kwenye Baraza la Mawaziri ulitafsiriwa kuwa ulitokana na msimamo wake aliouonyesha wa kutoa maoni ya kuuokosoa muundo na mfumo wa Muungano, je, Mheshimiwa Waziri Mkuu uamuzi huo dhidi ya Mheshimiwa Mansoor Yussuf Himid uliheshimu uhuru wake wa kutoa maoni yoyote kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyosema?

Mheshimiwa Spika, watu wa Zanzibar walifuatilia kwa karibu sana matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Kenya. Kutokana na mazungumzo yao, inaonekana wamejifunza mengi lakini haijulikani kwa wale ambao hawataki kujifunza kwamba na wao watakuwa tayari kubadilika.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi yaliyosababisha watu wa Visiwani kufanya hivyo. Mojawapo ni ujirani na uhusiano wa karibu walionao na watu wa Mombasa, eneo ambalo zamani lilikuwa sehemu ya Zanzibar chini ya himaya ya Serikali ya Uingereza.

Kubwa zaidi ni kwa sababu Kenya kama Zanzibar ilipata mtihani mkubwa tokea kuachana na siasa za chama kimoja na kuja na mfumo wa vyama vingi vya siasa miongo miwili sasa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa baadhi ya viongozi wa Kenya wamefunguliwa mashtaka ya uchochezi na mauaji yaliyotokea wakati na baada ya uchaguzi mwaka 2007, ambapo baada mvutano, yalisababisha kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tumwombe Mungu viongozi wetu na waandishi wa habari wasijisahau kulazimisha Jumuiya za Kimataifa kuwawajibisha kisheria. Nayo Zanzibar labda kwa kujifunza kutokana na balaa za uchaguzi walizokumbana nazo na yaliyotokea Kenya ilipata muafaka uliosababisha kufanyika uchaguzi wa amani mwaka 2010 na baadaye kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana inaonekana wapo ambao hawakufurahia hili na tayari panasikika na kuonekana chokochoko za kuleta balaa. Badala yake ni Viongozi wa Uamsho tu ndio unasikia

wanachunguzwa na Polisi lakini hatuelezwi kinachoendelea juu ya vikaratasi vya uchochezi na matusi yanayoporomoshwa kwa marais wastaafu, Benjamin Mkapa na Amani Karume. Sijui viongozi waliopo madarakani hivi sasa Bara na Visiwani watajihisi vipi na wao wakijakukashifiwa katika vikaratasi watakapoachia ngazi za uongozi.

Mheshimiwa Spika, sasa Kenya baada ya kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa imefanya uchaguzi ambao nao umeleta shaka kutokana na kuwepo madai ya mizengwe wakati wa kuhesabu kura.

Hata hivyo, watu wake wamekataa uchaguzi kuwarudisha kwenye vurugu za kutoana roho badala yake malalamiko ya uchaguzi yamepelekwa Mahakamani kwa sababu Sheria ya Uchaguzi inatoa fursa hiyo tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo uamuzi wa Tume ni wa mwisho na hauwezi kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, hili ni eneo ambalo Tanzania na hasa Zanzibar inafaa kuliona kama ni somo kwa vile kutotoa nafasi kwa uamuzi wa Tume ya Uchaguzi kuhojiwa si demokrasi ni udikteta.zuri zaidi ni kuwa kesi za uchaguzi hasa ya kupinga matokeo ya Urais zitasikilizwa katika kipindi cha sio zaidi ya wiki mbili tokea matokeo kutolewa. Vilevile kesi zote zinazohusu uchaguzi zitasikilizwa hata siku za mapumziko na hadi usiku.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi uliopita wa Kenya ulikumbana na matatizo ya kiufundi ya teknolojia lakini palikuwepo na uwazi wa kiasi fulani na wananchi kuelewa kilichokuwa kikiendelea tofauti na Zanzibar ambapo ukimya hutanda na kusababisha kuwepo kila aina ya uvumi.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba Kenya imefanya marekebisho makubwa katika kuendesha uchaguzi ijapokuwa bado inayo safari ndefu. Hapakuwa na malalamiko ya watu wengi kunyimwa haki yao ya kupiga kura kama inavyoendelea kuonekana Zanzibar na wala hazikusikika habari za wapiga kura mamluki kupelekwa vituoni.

Mheshimiwa Spika, Kenya ilikwenda hatua moja mbele zaidi ya hata kuwa wa Jimbo la Uchaguzi wa Rais kwa raia zake wanaoishi katika nchi za Afrika Mashariki. Hii ni tofauti na Zanzibar ambapo watu zaidi ya 40,000 walinyimwa haki hiyo licha ya sio tu kuzaliwa Zanzibar bali wengine wakiwa hawajawahi hata kusafiri nje ya Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi wa Kenya, Maafisa wa Uchaguzi ndio waliokuwa wakifanya uamuzi katika vituo vya kupiga kura tofauti na Zanzibar ambapo Masheha ndio wenye uamuzi wa nani awe na haki ya kupiga kura. Masheha hawa walilalamikiwa sana na wachunguzi wa uchaguzi wa ndani na nje kuwa ndio chanzo cha vurugu. Baadhi ya Masheha hao bila ya aibu wamekuwa wakidai hawawajui watu wanaoishi mitaani kwao na vijana waliowaozesha binti zao. Ni watu wanafiki sana kiwango ambacho hakieleweki.

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha zaidi, hakuna hata Sheha mmoja aliyechukuliwa hatua wala hakuna taarifa yoyote ya uchunguzi iliyosema baadhi ya Masheha walitoa taarifa za uongo kwa Maafisa wa Uchaguzi. Badala yake huonekana mamia ya watu wakifunguliwa kesi bandia ikiwa hata Vizee kudaiwa kuwanyang’anya silaha Polisi.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Kenya walionekana kila pembe lakini walikuwa hawaingilii shughuli za

uchaguzi au kutisha wananchi. Katika chaguzi za Zanzibar, Askari wa SMZ huwa ndani ya vyumba vya kupigia kura kama wao ni Makarani wa Tume ya Uchanguzi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Zanzibar inafaa kujifunza ni kwamba uchaguzi wa Kenya ulikuwa wa watu wazima wale waliofikia miaka 18 na kuendelea wakati Zanzibar watoto ambao umri wao hauruhusu kuwa wapiga kura wanashiriki.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi hasa Mfuko wa Vijana. Fedha zinazotolewa na Serikali kuwezesha vijana kiuchumi hazitoshi ikilinganishwa na idadi ya vijana ambao ni 68% ya idadi ya Watanzania, vijana ambao ni nguvu kazi ya nchi lakini hawana mitaji ya kutosha ya kujiajiri.

Mfano kila mwaka zaidi ya wahitimu kutoka vyuo vikuu 500,000 huingia uraiani lakini hawana ajira za kudumu. Wapo walioanzisha makampuni ya kibiashara na ujasiriamali lakini vijana hawa wanashindwa kupambana na soko kwani mitaji yao ni midogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuja na mpango wa kuwezesha kaya maskini ambapo shilingi bilioni 440 zimetengwa kuzigawia fedha kaya maskini na kuzipatia chakula. Mpango wa kuwezesha vijana kiuchumi uko wapi?

Mheshimiwa Spika, 68% ya Watanzania ni vijana lakini vijana hawa wanakufa kwa maradhi na umaskini. Ripoti ya maambukizi ya HIV/AIDS, waathirika wakubwa ni vijana kuanzia umri wa miaka 15-45 ambao ni nguvu

kazi ya nchi. Ripoti ya athari za madawa ya kulevya (2012) vijana 20,426 wameathirika, idadi ambayo ni sawa na Majimbo manne ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti, zaidi ya shilingi bilioni 17 za mapambano dhidi ya UKIMWI ni fedha za nje. Naiomba Serikali iharakishe uwepo wa Mfuko wa Ukimwi tuache kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Wanawake. Bunge lilipitisha Azimio la Mfuko wa Wanawake mwaka 1993 ambapo Halmashauri zilikuwa zinachangia 5% ya bajeti zao. Mifuko hii haina kitu, wanawake wanapata taabu, Wabunge wao tumewahamasisha wajiunge na vikundi vya ujasiriamali na *SACCOS* lakini hakuna uwezeshaji wa moja kwa moja kutoka kwenye mfuko wao.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake inapata pesa kupitia *vote* ya Mfuko wa Wanawake. Je, Mfuko wa Wanawake umekufa? Nani ametengua Azimio la Bunge la mwaka 1993?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nasema naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, maombi maalum. Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu haina hospitali ya Wilaya. Katika juhudi zake za kukipandisha hadhi kituo cha Afya cha Mangaka kuwa hospitali ya Wilaya, iliomba shilingi milioni 300 kwenye bajeti yake lakini ombi hili llimefutwa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atuonee huruma fedha hii tupatiwe.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu iliomba shilingi 300 milioni ili iweze kujenga nyumba saba tu za watumishi. Hii ilikuwa na lengo la

kuwapa motisha watumishi wanaohamia Nanyumbu wapate makazi ya kuishi kwani Makao Makuu yalikuwa ni kijiji tu. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu utupatie fedha hii ambayo imekatwa kwenye bajeti ya Halmashauri tuweze kujenga nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa maombi haya mawili, tunaomba Mheshimiwa Waziri atuonee huruma na anapojumuisha basi atoe ahadi ya Nanyumbu kupatiwa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, ninatanguliza shukrani zangu za dhati kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Madaba, Songea Vijijini itakuwa Mji Mdogo?

Mheshimiwa Spika, ni lini sheria ya kuruhusu Halmashauri za Wilaya kupewa mamlaka ya kuajiri watumishi wa kada za chini italetwa Bungeni ili kuruhusu mabadiliko kutoka katika hali ya katazo lilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, TAMISEMI pamoja na wataalamu wote wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu, Jumanne Sagini, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya Bajeti finyu na nchi kubwa kieneo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu na hasa TAMISEMI ambayo inasimamia Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa ndiyo Serikali yenyewe katika utekelezaji wa sera tunazojiwekea. Haya ni majukumu makubwa sana yanayohitaji uongozi madhubuti kwenye ngazi zote *(very strong and highly committed Management and Leadership).* Nchi yetu bado ina matatizo makubwa ya kimaendeleo – wale maadui watatu wa tangu Uhuru (1961) – Umaskini, Ujinga na Maradhi bado ni sugu. Kipato cha wastani cha Mtanzania kwa mwaka *(GDP per capital)* bado ni kidogo sana shilingi 800,000 kwa mwaka, Ngara kipato cha mwaka ni kati ya Tshs 170,000 – 240,000.

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka 12 yaani ifikapo mwaka 2025 nchi yetu inatakiwa iwe nchi yenye uchumi wa kati *(medium income country)* – yenye *GDP per capital* zaidi ya *US$3000.* Hii ni changamoto kubwa sana kwa Serikali na hasa ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inasimamia maendeleo huko vijijini – lazima tupige vita umaskini, ujinga na maradhi ambayo vimekithiri huko vijijini. TAMISEMI inasimamia Elimu na Afya – ambavyo ni vipaumbele namba moja.

Ofisi ya Waziri Mkuu sharti iwe na mikakati madhubuti ya kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii ili tufikie ndoto yetu ya *Medium Income Economy*. Ni wajibu wa ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha watendaji wake wanawajibika ipasavyo. Wanawatumikia wananchi kwa uaminifu mkubwa sana ili waondoke kwenye dimbwi la umasikini.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kushauri viongozi mbalimbali wawekewe mikataba ya utendaji – Wakuu wa Mikoa, Ma-DCs, Wakurugenzi wa Halmashauri na hata Wakuu wa Idara. Mikataba hii ingesaidia sana kuimarisha uwajibikaji. Bado ubadhirifu wa mali ya umma ni mkubwa sana kwenye Halmashauri. Wakuu wa Idara ni wabadhirifu. Waheshimiwa Madiwani

hawana ubavu wa kuwakemea. Madiwani wanawekwa mfukoni kwa kupewa vihela vidogo na Wakuu wa Idara. TAMISEMI ibuni mkakati wa kuwadhibiti watendaji wabadhirifu.

Mheshimiwa Spika, Watendaji wa kata na vijiji ni dhaifu sana kielimu. Kwetu Ngara – watendaji hao elimu yao ni ya msingi, hawana upeo. Kwa kuwa kiutumishi inakuwa vigumu kuwa-*phase out* – kuwaondoa kazini – basi tutathmini chuo chetu cha Hombolo kuwaongezea uwezo watendaji hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha elimu, narudia ushauri wangu kwamba ni muhimu kwa TAMISEMI kujiimarisha kwa kuchukua baadhi ya wataalam wa elimu kutoka Wizara ya Elimu ili kuimarisha TAMISEMI yenyewe na Halmashauri zake.

Mheshimiwa Spika, fedha za uwezeshaji zipelekwe sehemu mbalimbali na hasa sehemu zenye umaskini sana. Wilaya ya Ngara haijapata fursa ya kuziona fedha za uwezeshaji.

Ofisi ya Waziri Mkuu inatakiwa isimamie maendeleo ya nchi nzima. Kusiwepo na upendeleo wa baadhi ya maeneo katika kutoa huduma za maji, barabara na kadhalika.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha ya ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi kubwa inayofanywa na Serikali katika kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi naomba kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji limeendelea kuwa kero kubwa hasa vijijini na kuleta mzigo mkubwa kwa wanawake na watoto hasa wa kike. Ukosefu wa maji safi na salama unachangia kwa kiasi kikubwa kuibuka magonjwa yakiwemo ya mlipuko.

Mheheshimiwa Spika, tatizo la maji ni kubwa kata ya Nduli, Iringa Mjini. Je, ni lini watapatiwa maji ya uhakika? Pia baadhi ya vijiji vya Tarafa ya Ismani na Shule zote zinatakiwa kuwa na maji salama. Hivyo, nashauri visima vichimbwe pale ambapo maji hakuna ili kuwapa watoto maji.

Mheshimiwa Spika, barabara za vijijini ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi kwa ujumla. Naomba nizungumzie barabara ya Musoma – Majita. Barabara hii ni kiungo cha Wilaya tatu yaani Musoma Mjini, Butiama na Wilaya ya Bunda kwa kupitia kivuko cha Busekela.

Pia wananchi wa Wilaya ya Ukerewe wanatumia barabara hii wakati wakienda kutembelea visiwa vya Ilugwa kupitia Bukima. Napenda kujua ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuwaondolea wananchi adha kubwa wanayoipata ukitilia maanani kwamba biashara ya samaki inategemea barabara hii muhimu ya kihistoria ya toka Uhuru.

Mheshimiwa Spika, suala la lishe. Napongeza Serikali kwa kuzindua mpango mkakati wa kitaifa wa lishe, mpango ambao umeanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kuajiri Maafisa Lishe ngazi ya Mkoa na Wilaya. Naomba Maafisa hawa waajiriwe kwa kufuata taaluma zao badala ya kujaza nafasi tu. Kuna wahitimu

wengi kutoka *SUA* pia wapewe vitendea kazi na wawe Idara ya Mipango, Halmashauri ya Wilaya badala ya Idara ya Afya. Elimu ya lishe itolewe kwa wananchi wote vijijini kwa kuanzia na Serikali za Vijiji ili waweke mikakati ya kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za Serikali za kuweka virutubisho katika vyakula ikiwemo unga wa mahindi, unga wa ngano na mafuta ya kupikia pamoja na chumvi.

Mheshimiwa Spika, naomba suala la viwanda vidogo vidogo vya chumvi vitizamwe ili kuhakikisha kwamba wazalishaji wote wa chumvi wanapewa elimu hasa Mkoa wa Pwani, Lindi, kuweza kuona umuhimu wa kutumia chumvi iliyowekwa madini joto. Taasisi ya *TFNC* iimarishwe kwa kupatiwa watumishi, vitendea kazi na Bodi, Mwenyekiti wake ateuliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea suala la madawa ya kulevya. Pombe ikizidi inaathari kubwa. Sasa hivi vijana wetu pamoja na kutumia madawa ya kulevya, ulevi pia umekuwa tishio. Pombe iliyowekwa kwenye paketi kwa jina maarufu Viroba inanywewa ovyo hata asubuhi wakiwemo madereva wa magari makubwa na pia huongeza ajali barabarani. Nchi ya Kenya na Uganda zimepiga marufuku pombe hizi na matokeo yake sasa zinamwagwa hapa nchini. Nashauri Serikali ipige marufuku unywaji wa Viroba kwani hata vijana wakiwemo wa vyuo wanakunywa hata asubuhi. Hii ni hatari kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mikoa ya Iringa na Njombe ina hali nzuri ya mvua na kuzalisha mazao mbalimbali yakiwemo mboga na matunda. Vikundi vya vijana na wanawake vipewe mafunzo ya uzalishaji wa mboga na matunda na wapewe mitaji kupitia Benki ya

Wanawake, Benki ya Maendeleo na pia Benki ya Vijana inayotegemewa kuanzishwa pia Mifuko mingine katika Halmashauri ili waweze kunufaika na uwepo wa kiwanja cha Ndege Mbeya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL AZIZ ABOOD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye elimu, kilimo na afya. Kilimo ni ajira na ni njia mojawapo rahisi ya kuondokana na umaskini kwa mwananchi. Kwenye Jimbo langu la Morogoro Mjini hatuna ardhi kwa ajili ya kilimo lakini Serikali katika miaka ya 1970 ilitoa ardhi kwa ajili ya kilimo kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro katika maeneo ya Wilaya Mvomero, eneo la Mgongola lakini cha kushangaza wananchi hao wanalipia mpunga katika bonde hilo la Mgongola, wanafukuzwa na wafugaji na kuonesha hati miliki waliopewa miaka hii ya 2000. Sasa wananchi ambao wamepewa ardhi miaka ya 1970 hawajapewa Hati Miliki, hao wafugaji wamepewa, kwa kweli hili linarudisha nyuma maendeleo ya kilimo kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro, nashauri Serikali iingilie kati suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kwenye elimu, shule nyingi za sekondari na msingi hazina nyumba za Walimu, madawati na maktaba kwa ajili ya kujiongezea elimu wanafunzi. Kwa upande wa sekondari maabara imekuwa ni tatizo kubwa sana, kiasi kwamba wanafunzi wanashindwa kupata fursa ya kuelimika katika kusoma

sayansi kwa vitendo badala yake wanakuwa na sayansi ya nadharia tu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, Kata zetu nyingi hazina Zahanati au Vituo vya Afya. Nashauri Serikali iongezee nguvu kwenye hizi Zahanati na Vituo vya Afya ili viweze kuhudumia kwenye Kata zao na kupunguza msongamano kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Pia nashauri Hospitali ya Wilaya iboreshwe zaidi ili iweze kupokea wagonjwa na kina mama wanaotaka kujifungua wapate huduma bora na kuweza kufanyiwa hata upasuaji katika Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu kurejeshwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Lazima Taifa likiri kwamba tulifanya makosa makubwa sana kukubaliana na ushauri wa Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* na kufuta (kusitisha) JKT. Miaka 19 bila ya kuwapo kwa JKT imekuwa miaka ambayo Taifa limeshuhudia mporomoko mkubwa sana wa uadilifu na hata Umoja wa Kitaifa kuwa shakani. JKT ni jando la Taifa na hivyo ni makosa kuona matumizi ya JKT kwa jicho la kiuchumi, JKT lazima iangaliwe kwa jicho la kijamii na uimara wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo haisaidii kuwa na JKT ambapo vijana wanafundishwa utii, uhodari na uaminifu bila ujuzi wowote wa stadi za maisha yao *(Skills)*. Vijana wanafundishwa miaka miwili kutumia silaha, utimamu wa mwili na utimamu wa akili lakini wakimaliza wanakuwa hawana kazi wanakaa wanazurura mitaani. Hii inakuwa hatari zaidi maana ni rahisi sana kupata ushawishi wa ujambazi na kadhalika hivyo ninapendekeza ifuatavyo:-

(1) Kuanzia mwaka huu wa fedha tuweke utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila kambi ya JKT inakuwa na chuo cha *VETA* ili kuhakikisha kuwa vijana wanaoingia Jeshini hasa wale wa kujitolea wanatoka na ujuzi fulani wa kazi. Ni muhimu pia kuhakikisha kuwa zile fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya Mifuko ya Vijana na kadhalika zinaelekezwa katika juhudi hizi za *VETA* katika kambi za JKT. Vijana hawa wanapomaliza wapewe vifaa vya kazi kama mikopo ya gharama nafuu. Hatua hii itaongeza nguvu kazi kubwa katika nchi yetu.

(2) Serikali ihakikishe kuwa ajira zote za Idara za Serikali na Mashirika ya Umma zinazotokana na masuala ya kiuaskari lazima zipite JKT. Iwe ni marufuku mtu kuajiriwa Jeshi la Polisi nje ya JKT. Lazima kuondokana na tabia za kupendelea watoto na ndugu wa vigogo katika ajira na kuacha vijana waliopita JKT wakihangaika bila kazi.

(3) Kuanzia mwaka ujao wa fedha, watumishi wote wa Umma ambao hawakupita JKT wawekewe utaratibu wa kupita JKT japo kwa miezi miwili yaani wiki nane tu. Walimu na watumishi wa Idara mbalimbali za Serikali lazima wapite JKT na huko mbeleni sharti la ajira lazima liwe ni kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la udini tunalichezea sana, litaigawa Tanzania kwa kiwango ambacho tutalia na kusaga meno. Ni lazima sasa kufanya uchunguzi wa Kibunge kuhusu *religious tension* nchini kwa kupita nchi nzima na kuongea na wananchi kuhusu masuala ya udini na kuja na mapendekezo ya namna bora ya kuimarisha Umoja wa Taifa letu. *Parliamentary Inquiry on Religious Tension in Tanzania* ndio naona kama suluhisho la kudumu la kupata ufumbuzi wa migogoro ya kidini nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, *CAG* ameonyesha kuwa katika deni la Taifa hivi sasa kuna zaidi ya shilingi 620 bilioni hazina maelezo. Hii inawezekana ni deni la uwongo ambalo limewekwa ili kulipa watu fulani fulani.

Napendekeza kuwa deni zima la Taifa lifanyiwe Ukaguzi Maalumu. Utoroshaji wa fedha kwenda nje ya nchi unaofanywa na watu fulani katika nchi yetu sehemu kubwa ni malipo ya deni la Taifa, malipo ya deni hewa na wadai hewa. Suala hili ni lazima Serikali ilichukulie kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya Serikali kuhusu mradi wa Umeme wa Mto Malagarasi wa 44.3MW. Mradi huu umefikia wapi?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nachangia jambo moja tu. Kwenye Wilaya jirani ya Kiteto, kuna eneo linaloitwa Emborey Flurtangos ambalo vijiji kadhaa vimeamua liwe ni hifadhi. Jambo hilo ni jema na ni la kuungwa mkono. Hata hivyo, utekelezaji wa jambo hilo umekuwa na athari kubwa zifuatazo:-

Kwanza, Kongwa tumezika na kuzika watu waliouawa na wafugaji kinyama kwa sababu inaelekea lengo la hifadhi hiyo ni ubaguzi wa kikabila tu.

Pili, hifadhi haiwezi kuruhusu kilimo au ufugaji, nchi hii ni Ngorongoro peke yake tena kwa majaribio ndio yenye uhalali huo.

Kwa hiyo, endapo eneo hilo ni uhifadhi basi wakulima watoke, wafugaji watoke kwa vile wote wanaharibu mazingira.

Tatu, ziko habari za kuaminika kuna kikundi cha viongozi wa Kiteto/Manyara kugeuza eneo hilo siku zijazo kuwa ranchi zao binafsi.

Nne, ubaguzi wa kikabila ni mkubwa sana hadi Halmashauri ya Wilaya inachangisha fedha zaidi ya shilingi milioni 150 kwa viongozi wa kabila moja dhidi ya kabila lingine. Natahadharisha, yanayoweza kutokea huko miaka ijayo ni maafa makubwa.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu na mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi hasa zile zinazoenda mwambao mwa Ziwa Tanganyika ni barabara muhimu sana lakini zimeshindikana kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi nazo ni Nkana – Kala Km.67, Kitosi – Wampembe Km.68 na Namanyere – Ninde, Km.47.

Mheshimiwa Spika, barabara zote ziko kwenye ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za mwaka 2010 kuwa zitaboreshwa. Mimi kama Mbunge wa eneo hilo, nimejitahidi kuzisemea sana barabara hizi na kupata ahadi lakini hazijazaa matunda. Mkoa kupitia Bodi ya Barabara katika vikao vyake na *RCC* imeomba Serikali kukubali maombi ya kuzichukua barabara hizi na zishughulikiwe na Wakala wa Barabara Mkoa badala ya Halmashauri ya Wilaya lakini mpaka sasa hatujasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu anazifahamu barabara zote ziendazo mwambao mwa Ziwa Tanganyika zilivyo ngumu sana kuweza kushughulikiwa na Halmashauri ya Wilaya. Mimi Mbunge wa eneo hili

nimemwona na pia nimemwandikia barua kuwasilisha maombi ya kuomba barabara hizi fedha ya kuzishughulikia lakini mpaka sasa sijafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, najua jinsi alivyo na majukumu mengi sana lakini wananchi wa Kata ya Wampembe wanaona Waziri Mkuu ndio msaada na mafanikio yao. Pia aliwaahidi kuwatembelea naomba atimize ahadi hiyo maana itakuwa ni neema za uongozi wa kitaifa. Vilevile itakuwa njia nyingine ya kuelewa eneo hili na sio tu kusikia kutoka kwa wasaidizi wake wanaokwamisha kutekelezwa kwa ahadi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa simu. Eneo zinapokwenda barabara hizi tatu hakuna kabisa mawasiliano ya simu mfano Kata ya Kala, Kata ya Wampembe na Kata ya Ninde. Kata zote hizi hazijapata mawasiliano wala barabara za uhakika.

Naomba Serikali kulivalia njuga suala la mawasiliano ya simu za mkononi katika eneo hili ambalo lina changamoto mbalimbali ikiwemo tishio la kiusalama. Natambua jitihada za Wizara inayohusika lakini nina wasiwasi kuwaachia wawekezaji pekee bila Serikali yenyewe kuona namna ya kuwafikishia wananchi mawasiliano tunaweza kukwama kufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, maji. Katika Jimbo la Nkasi Kusini kuna tatizo la maji. Miradi ya Benki ya Dunia imekwamia wapi? Maeneo yafuatayo yanatekeleza miradi hiyo lakini hatuoni matunda mfano mradi wa maji Chala Mji Mdogo na mradi wa maji Kisura kijijini. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilie miradi hii maana Serikali inaonekana kuwaahidi wananchi ahadi hewa.

Mheshimiwa Spika, kilimo. Nkasi ni mzalishaji mzuri wa nafaka ya mahindi ikishika nafasi ya kwanza. Mwaka 2011/2012 tulipata mbolea vizuri na mavuno yaliongezeka lakini mwaka 2012/2013 hali ya kusambaza pembejeo ilikuwa mbaya sana na kwamba Wilaya ilipata kwa asilimia 30% tu ya mahitaji. Sasa kwa utaratibu wa kuleta pembejeo 30% ya mahitaji, tutasonga mbele kweli? Mwaka huu naomba dosari hiyo isitokee tena.

Mheshimiwa Spika, umeme. Tumepata umeme mjini Namanyere lakini changamoto iliyopo ni usambazaji wake mjini Namanyere na vijijini. Naomba *REA* wapewe fedha waweze kutekeleza mipango yao mizuri na naomba wapeleke umeme katika vijiji vya Kilangala, Myula, Kalundi, Katani, Chonga, Ntalamila hadi Makao Makuu ya Jimbo - Kate.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Januari Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Majaliwa na Mheshimiwa Mwanri atafuata.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa na mimi kuchangia hoja hii na kutoa nafasi vilevile ya kutoa baadhi ya majibu ya Serikali kwa baadhi hoja ambazo zimechangiwa.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye hotuba iliyotolewa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Freeman Mbowe.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba mwaka 1991 Watanzania waliulizwa kwamba nchi yetu aidha iingie kwenye Mfumo wa Vyama Vingi au

tuendelee na Mfumo wa Chama Kimoja? Asilimia 80 wakasema tunataka tuendelee na Mfumo wa Chama Kimoja, asilimia 20 wakasema tuingie kwenye Mfumo wa Vyama Vingi. Sasa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM iliyokaa kuanzia tarehe 17 - 20 Januari, 1992 ikapitisha uamuzi na kuiagiza Serikali ilete marekebisho ya Katiba ili nchi yetu iingie kwenye Mfumo wa Vyama Vingi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, cha kukumbuka tu ni kwamba uamuzi wa kuingia kwenye ushindani wa kisiasa na uamuzi ambao umepelekea hata hawa ndugu zetu wawepo humu, umefanywa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msingi wa uamuzi ule ni kwamba nchi yetu itanufaika kwa kupata fikra na mawazo mbadala na michango mbalimbali kuhusu maendeleo ya Taifa letu. Ndiyo ilikuwa fikra kwa wakati ule. Mahali kwa kupata fikra hizo, mchango huo na sera hizo baada ya uchaguzi, ni Bungeni. Hapa Bungeni njia ni kupitia kwenye hotuba zinazotolewa na hawa wenzetu.

Sasa tumesikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo imesheheni mambo ya msingi yanayohusu maendeleo ya Taifa letu; elimu, afya, maji, barabara, umeme, maafa, mazingira na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi wakati Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anaanza kuzungumza niliamua kubaki ili nisikilize fikra mbadala kuhusu afya, elimu, maji, barabara, mazingira maafa na kilimo. Ukiitazama hii hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo inajibu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakuna mahali hata pamoja kilimo kimetajwa, hakuna maji, hakuna umeme, hakuna barabara, hakuna ajira, hakuna mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunapata shida kama kweli dhana ile ya kuingia kwenye Mfumo wa Vyama Vingi kupata fikra, falsafa na sera mbadala inatimia kwa hotuba za namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere mwaka 1963 aliandika makala wakati nchi yetu sasa inaamua kuingia kwenye chama kimoja alisema pale ambapo mna Vyama Vingi lakini hakuna tofauti za msingi za kisera na kiitikadi, ushindani wa kisiasa unakuwa ni sawasawa na mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, yote tunayoyaona hapa yanayoendelea kutokana na wenzetu kushindwa kujipambanua kwa utofauti wa dira na tofauti ya sera, tunachoona hapa kinachoendelea ni sawasawa na mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, dhana ya upinzani wa Vyama siyo kulalama, siyo kutema cheche, siyo kukebehi na siyo kukejeli. Ni kutoa dira tofauti. Sasa kwenye hili wenzetu limewashinda.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kwamba ili watusaidie na waisaidie nchi yetu, basi wajikite katika michango yao Bungeni hapa kuwaeleza Watanzania kwamba vile watakavyofanya tofauti na sisi ni nini? Haitoshi peke yake kusema kipi unapinga. Cha msingi kama unataka uongozi wa nchi, vilevile useme ni kipi unasimamia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umoja wa kitaifa. Kwenye hotuba hii wamesema kwamba CCM ndiyo waasisi wa siasa za udini na CCM ndiyo waasisi wa hii habari ya kuchinja. Hakuna tusi kubwa la kuitukana CCM na Watanzania kama kusema kwamba CCM ndiyo waasisi wa siasa za dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Umoja wa kitaifa wa nchi hii umeasisiwa na Chama cha Mapinduzi. Taifa hili limeasisiwa na waasisi wa Chama cha Mapinduzi na limeasisiwa katika misingi ya umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi viongozi wa Taifa hili waliasisi Chama cha Mapinduzi walitaifisha shule za dini ili kutuunganisha, waliondoa uchifu ili kutuunganisha, walipigania Kiswahili ili kutuunganisha, walipigania Umoja wa Afrika, waliunda Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wakati huo Jeshi hili lilikuwa ni sehemu ya Chama cha Mapinduzi. Kulikuwa na Katibu wa Chama wa Jeshi, kulikuwa na Wajumbe wa *NEC* wa Jeshi, kulikuwa na Makamisaa na kwenye nembo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuna neno moja tu inaitwa Umoja. Tukaunda jeshi lile tukiwa na dhamira ya kujenga umoja wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna chama kinachoweza kushinda kwa kutumia dini moja. Tutazame huku tuliko kwenye Chama cha Mapinduzi, wako watu wa dini zote, wako watu wa kabila zote na watu wako wa rika zote.

**MJUMBE FULANI:** Na wa rangi zote.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Na watu wa rangi zote. Hatuwezi kuwa waasisi wa siasa za dini na tukawa hivi. Ukimwuliza Mbunge wa CCM yeyote kwamba kwenye Wabunge wa CCM kuna Wakristo wangapi na Waislam wangapi, hakuna anayejua. Kwa sababu ni mambo ambayo hatujihangaishi nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawashauri wenzetu kwamba kweli ni chama kichanga lakini katika kauli zao wajielekeze kwenye kutusaidia kujenga umoja

wa kitaifa kwa sababu sisi mchango wetu ni mkubwa na tunaamini kwamba wanao watu ambao vilevile wanaweza na wenyewe kusaidia kutoa mchango katika kujenga umoja wa Taifa na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza viongozi wa dini, Maaskofu, Mashehe na Wachungaji kwa kuhubiri amani, uvumilivu na utulivu na sisi kama Serikali tutaendelea kufanya wajibu wetu katika kuhakikisha hayo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nilipenda kuongelea suala la Katiba. Tumesikia kwenye hotuba yao walisema kwamba wamejitoa katika mchakato wa Katiba.

Nashangaa sana, tulipitisha Sheria hapa mara ya kwanza wakaipinga na wakatoka nje. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais akawasikiliza na Serikali ikaleta mabadiliko ya Sheria hiyo hapa. Katika kuchangia hayo mabadiliko na Sheria ambayo tunaitumia mpaka sasa, katika kuchangia mjadala wa yale mabadiliko waliyowasilisha, naomba nisome wasilisho la Kambi hiyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**WABUNGE FULANI:** Kha!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kama inawezekana kwa sababu tuna utaratibu wa kuazima dakika, kama Waziri mwenzangu anaweza kuniazima dakika mbili au tatu nimalizie.

**SPIKA:** Hakuna. Sijui wenyewe. Anachukua dakika tano za Waziri wa TAMISEMI. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni wasilisho la Kambi ya Upinzani kuhusu Katiba. *"Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni siyo tu inaunga mkono Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Katiba ya 2011, bali pia inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali the narrowness of our political affiliations, tuungane na Mheshimiwa Rais katika kulipatia Taifa letu kutengeneza Katiba mpya yenye muafaka wa Kitaifa.* Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza naunga mkono hoja hii."

Mheshimiwa Spika, haya ni maneno ya Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwa hiyo, Sheria ambayo tunaitumia sasa ni Sheria hii ambayo waliiunga mkono, hakuna kilichobadilika. *(Makofi)*

Sababu ya kujitoa, haipo, labda ni kutafuta mgogoro upya. Kule kwa watani zangu Wapare, kwa Mheshimiwa Mama Anna Kilango tuna chakula chetu kinaitwa pure yaani makande, yanatumia muda mrefu sana kuiva, ni masaa manne, matano mpaka sita. Sisi tunajenga nyumba pamoja ambayo ni Katiba na wenzetu hawa. Sasa tumetenga pale sufuria la pure ambayo ni makande yanaiva baada ya masaa sita, tunajenga nyumba hii Katiba na wenzetu wanasema tunataka pure ziive baada ya dakika 10 na zisipoiva baada ya dakika 10 tunajitoa. Ni jambo ambalo haliwezekani. Tuwatendee haki Watanzania ili tupate Katiba mpya na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni mahusiano yetu humu ndani. Unafahamu kwamba sisi Wabunge humu ndani tunapendana, tunazikana, tunachangiana na hata kadi za michango ya harusi zinatembea kote huku.

Lakini cha ajabu tunapokuwa hapa tunazungumza, wakati kamera zimewaka tunatukanana, tunashutumiana, lakini tukikutana katika Kamati tunafanya kazi vizuri. Hata kantini kule. Sasa aidha ni wanafiki wakati *TV* zimewaka au ni wanafiki wakati ule. *(Makofi)*

Maheshimiwa Spika, mahusiano yetu na jinsi tunavyo husiana humu ndani tunapeleka taswira kwa watu. Sisi ni viongozi, na wanaotuunga mkono wanapambana huko kwasababu wanatuona sisi tunapambana.

Kwa hiyo, tunajenga utamaduni wa siasa ambao siyo mzuri. Kwa hiyo, ningependa yale mahusiano mazuri, mimi nina marafiki zangu wengi humu na wale wana marafiki wengi humu, ningependa yale mahusiano mazuri tuliyonayo wakati kamera zimezimwa yawepo pia wakati kamera zimewaka ili tujenge utamaduni mzuri wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo masuala ya minara ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza, naomba tu nitoe rai kwamba tunarekebisha taratibu pale Wizarani ili tufanye kazi hii kwa haraka zaidi. Tumesikia na sisi tuko *frustrated* sana kuhusu utaratibu ule wa *World Bank* uliopo.

Kwenye matatizo yale yale mnayoyaona kwenye maji, ya ucheleweshaji, kwa sababu fedha zile ni za Benki ya Dunia ndiyo matatizo hayo hayo tunayoyapata kwenye masuala ya minara. Tunaamua sasa kuweka utaratibu mpya na ikiwezekana sasa mtusaidie tupate fedha nyingi zaidi sisi wenyewe za kwetu *(own source)* ili tuweze kulifanya jambo hili kwa haraka na kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwahakikishia kuwa ahadi tuliyoitoa kuwa itakapofika 2015, kila mahali ambako hakuna mnara kutakuwa na mawasiliano. Wapo ambao watapata mwaka huu, na wapo ambao watapata 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Majaliwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, niko hapa kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizokuwa zinachangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye Sekta ya Elimu chini ya TAMISEMI. Najua maeneo yalikuwa mengi, lakini kwa muda, tumelazimika kuchukua maeneo haya ili kuweza kutoa ufafanuzi.

Moja ya maeneo muhimu yaliyoweza kuzungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni namna ambavyo TAMISEMI au Serikali inavyoshughulikia stahili za Walimu. Stahili za Walimu zimegawanyika katika maeneo mengi ikiwemo mishahara. Hili la mishahara litapata nafasi na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi) atakapokuja kuonyesha na kwa namna gani Serikali imeweza kufanya mapitio kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wote wakiwemo Walimu.

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo la mishahara hapa, tatizo tulilonalo sasa ni eneo la malimbikizo ya Walimu yanatokana na kupanda kwa madaraja na mishahara yao, jambo ambalo linaendelea kuratibiwa na Tume ya Utumishi wa Umma *(TSD)* pamoja na Halmashauri zetu. Tunakiri kwamba tuna tatizo eneo hili, lakini uko utaratibu ambao sasa tunataka tuboreshe *TSD,* na kwenye bajeti ya msimu huu

itaonyesha namna ambavyo *TSD* itakavyokuwa inawezeshwa ili iweze kufanya kazi yake vizuri pamoja na Bodi ya Mishahara na Motisha ambayo sasa itafuta utaratibu mzuri ambao hautaletea Mtumishi kupanda daraja akachukua muda mrefu kulipwa mshahara wake mpya ili tuwe na malimbikizo kwa muda mfupi.

Eneo lingine ni malipo yasiyokuwa ya mishahara kama kwenye maeneo ya likizo, uhamisho, matibabu pamoja na posho za kujikimu, haya yote tumepeleka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na sisi TAMISEMI tunapeleka ruzuku. Tunaamini kuwa hazitoshi kwasababu tuna idadi kubwa ya Walimu. Lakini pia Halmashauri zenyewe zikiweka bajeti zake na sisi tukiweka ile kama *top up* zimesaidia sana sasa kupunguza madai haya ya maeneo ya likizo, matibabu, uhamisho na masomo na sasa kusababisha kupungua kwa migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, hali hii tunaendelea kwa kuboresha bajeti yetu na lengo kubwa, tunataka tuondoe kwa kiasi kikubwa matatizo yaliyoko kwenye maeneo haya. Lakini pia liko tatizo ambalo lilikuwa linajitokeza wakati huo kwa Watumishi wanaoendelea na Utumishi kukatika kwa mishahara katikati ya Utumishi. Jambo hili lilijitokeza lakini baada ya kuweka mfumo mpya wa kulipa mishahara wa LAWSON 8.5 sasa hivi hali hiyo tumeweza kuimaliza kwa kiasi kikubwa kwasababu kila Halmashauri tumefundisha Watumishi wawili kuhakikisha kuwa wanaweza kuingiza *data* za Mtumishi anayeondokewa na Mshahara katika ya Utumishi, na hii siyo kwa walimu tu bali kwa ni kwa Watumishi wote ndani ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, tatizo kwenye eneo lile lingine ni mishahara kwa Walimu wapya. Sasa hivi tumefika wakati mzuri na kama yako malalamiko sasa, basi

Mwalimu yule atakuwa amechelewa kuripoti au ana nyaraka tofauti na ambazo haziendani na jina lake, lakini pia tunaendelea kuimarisha mitandao yetu iweze kufanya kazi wakati wote na ili Mtumishi anapoingia tu takwimu zikiingia na mshahara utoke mwishoni mwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii sasa kama mnavyoshudia hatuna malalamiko ya Mwalimu mpya anayeripoti na mshahara wake akashindwa kupata ndani ya miezi miwili.

Lakini pia tuna eneo la malipo ya Walimu wapya, nauli na posho zao, eneo hili nalo tumeliimarisha, na mwaka huu wa fedha tumetuma Shilingi bilioni 8.1 ambazo sasa tunaona maeneo yote Walimu wameripoti, ukimya unaendelea na Walimu hao wanaendelea na utumishi wao. Kama yapo ni maeneo machache sana itakuwa au ni kwasababu ya mtandao ambao tumewashauri kwenye Halmashauri waende Halmashauri nyingine kwasababu mitandao ipo katika Halmashauri zote nchini.

Eneo la pili ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge katika lugha tofauti ni upungufu wa Walimu ambao umejitokeza. Lakini ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba upungufu wa Walimu unaotamkwa hapa siyo kama ulivyo, kwasababu kwa sasa hivi Walimu wa Shule za Msingi mahitaji ya nchi nzima ni Walimu 2,494,000 na tulionao ni 171,986. Tuna upungufu wa Walimu 28,508, na upande wa Sekondari mahitaji yetu sisi ni Walimu 80,138 na tulionao ni 51,000 na mapungufu ni Walimu 28 na hii ni mpaka Desemba, 2012. Tumeajiri tena mwaka huu Walimu 26,537 tumewapeleka. Kwa hiyo, tumepunguza idadi hiyo.

Tunahitaji ajira mbili tu ili tuweze kupunguza tatizo la upungufu wa Walimu.

Tatizo tulilonalo tunalifanyia kazi ni kwamba Walimu wengi wamelundikwa maeneo ya Miji na kando kando ya barabara. Tumewaagiza Wakurugenzi wote na Maafisa Elimu waende wakapitie ikama zao waondoe Walimu maeneo yenye mlundikano wawapeleke maeneo ambayo yana upungufu wa Walimu. Jambo hili pia tumewataka Makatibu Tawala wa Mikoa waweze kulisimamia ili tuondokane na tatizo hili.

Waheshimiwa kwenye eneo hili ambalo pia limezungumzwa ni changamoto ya Walimu wa Sayansi. Ni kweli kuwa tuna upungufu mkubwa wa Walimu wa Sayansi. Mwaka huu katika ya walimu 2,101 na 2011 tuna Walimu 1,092 tu ambao wamechukua masomo ya sayansi *Chemistry, Biology* na *Physics* na *Mathematics.*

Pia tunao mkakati ambao tunaofanya, moja ni kwamba tunajenga maabara ambazo tunaendelea kuzijenga, lakini mbili tunanunua *mobile laboratory* ili baadaye wanafunzi wetu kule Sekondari waweze kusoma masomo ya sayansi. Ili baadaye waweze kusoma.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeboresha sasa kutoa mikopo kwa wanaodahiliwa kwenda kusomea Ualimu kwenye ngazi ya Vyuo Vikuu. Tunaamini idadi hii ikiendelea kuwa ya kutosha tutapata Walimu wengi wa Sayansi, lakini pia sasa na huku tutatafuta utaratibu mzuri wa kutoa motisha ya Walimu hawa wa masomo ya Sayansi ili kulifanya somo hili liweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lilijitokeza ni upungufu wa miundombinu kwenye maeneo ya madarasa, nyumba, madawati na vyoo.

Tumeweza sasa kuongeza kiasi cha fedha, kwenye madarasa mwaka uliopita tulituma Shilingi bilioni 1.5, kwenye nyumba tuliongeza Shilingi bilioni 3.5 ili kuweza kujenga miundombinu hii kwenye maeneo haya.

Tunachofanya sasa ni kwamba tunaendelea na mkakati wetu ule wa kuzifanya shule kuwa *functional schools* zile 264 ambazo tayari ujenzi umeshaanza katika kila Halmashauri nchini na Waheshimiwa Wabunge mkienda kufuatilia mtakuta kazi imeshaanza.

Tumesisitiza pia ujenzi wa shule hizi mpya, sasa hivi tumesitisha ujenzi wa shule mpya mpaka zile za zamani ziwe *improved* kwanza ili tuweze kuendelea badala ya kuwa na shule nyingine mpya ambazo hazitakuwa na uwezo wa namna hii.

Kwenye maeneo ya madawati na vitabu mnatambua kabisa Waheshimiwa Wabunge kuwa tuna fedha ile ya rada ambayo sasa tulitenga zaidi ya Shilingi bilioni 55.2 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na Shilingi bilioni 18.4 kwa ajili ya madawati ambayo fedha hizi tutazituma kwenye Halmashauri zote. Kwa hiyo, tunaamini zikichangia kwenye jitihada za Halmashauri zenyewe hatutakuwa na upungufu mkubwa wa madawati.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Halmashauri kwa kuwa mnayo misitu na mnaye pia Mwenyekiti wa Kamati ya uvunaji ambaye ni Mkuu wa Wilaya, andaeni mipango ya kupata madawati kupitia misitu tuliyonayo, badala ya kukaa na tuna upungufu lakini tuna nafasi ya kuimarisha kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na eneo ambalo Waheshimiwa Wabunge walizungumzia shule zile

ambazo tulizipa hadhi ya Kidato cha Tano tukaondoa *O' Level,* Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) tumewaandikia Makatibu Tawala barua kuwa shule zile wazifanyie mapitio na wapeleke sasa *O' Level* ili miundombinu iliyobaki ambayo haifanyi kazi iweze kufanya kazi.

Tunaamini sasa uteuzi wa mwaka 2014, shule hizo zitakuwa na watu tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la uvamizi wa maeneo ya shule, msimamo wetu bado uko pale pale kwamba shule zote maeneo yake yaimarishwe na haturuhusu kuwa na maduka wala vibanda au nyumba za wageni na vitu vingine. Yabaki kuwa ni maeneo ya taaluma.

Naomba tusimamie kuwa maeneo yote ya shule yote yabaki kuwa ni ya taaluma ili pia elimu itolewe na kwa hiyo, hatutegemei tena kama kutakuwa na uvamizi wa maeneo haya.

Kulikuwa na watoto wanaozurura Mitaani na kuwa Serikali imejipangaje. Ni kweli kabisa kuwa tuna idadi ya vijana ambao wamemaliza Darasa la Saba, ni wachache wanaokwenda Sekondari na wale wengine wanaobaki tumeaandaa utaratibu wa kuwapeleka kwenye Shule za Ufundi ambazo tunazo.

Zipo Halmashauri ambazo zimefanya jitihada zake kuwa na Shule zake za Ufundi. Lakini pia tuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii chini ya Wizara ya Maendeleo, Jinsia na Watoto ambayo nayo ina Vyuo. Sehemu hizo zote tunapeleka vijana wetu. Lakini Wizara ya Elimu pia imeboresha ujenzi wa *VETA* nchini kote na sasa hivi wameshafikia ngazi ya Mkoa. Kwa hiyo, tuna *VETA* nyingi, vijana wetu ambao wanashindwa kuendelea na *Form One* kwenye Sekondari sasa tunaweza kuwapeleka pia kwenye Vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanri kwa mujibu wa Kanuni inayonipa ruhusa kuongeza dakika, nitaongeza naye amalize na dakika kumi. Mheshimiwa Mwanri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Kapteni Komba alipokuwa anazungumza hapa alim-*quote Mao Tse-tung* na Mimi ninataka niendeleze palepale alipokuwa anasimulia kitabu kile, alisema maneno yafuatayo:-

*"Tatua tatizo la msingi kwanza na matatizo mengine yote yanaondoka." Anasema, resolve the primary contradiction first, the secondary ones* zinaondoka *automatically. (Makofi)*

Mabepari wanajua mgongano ulikuwa ni kati ya *labour* na *capital.* Katika nchi zetu changa kama hizi tulizonazo mgongano ni kati ya nguvu kazi na kiwango cha vitendea kazi. Ukitatua tatizo la msingi katika nchi yetu la uchumi, maana yake ni kwamba unaweza kubeba majukumu yote ambayo tumeyazungumza hapa ndani. Lakini kama tatizo la uchumi hatujalitatua, na Mungu aliyeko juu Mbinguni anatusikia.

Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, moja ya matatizo ambayo imekuwa ina-*address* ni kuondokana na tatizo hili la Miundombinu ambalo watu wanashindwa kupita, watu wanashindwa kusafirisha mazao.

Hili jambo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumemwona akipanda na kuteremka kuhakikisha kwamba barabara zetu zinapitika,

kuhakikisha kwamba sasa bandari zetu zinafanya kazi na hili jambo wanaweza wakabisha jambo lolote lakini jitihada zinazofanyika pale, hakuna anayeweza kujibu. *(Makofi)*

Max alimalizia kwa kusema hivi *"always the economic base determine the super structure."* Yote tunayosema hapa juu, kama hatujajenga uwezo wa kiuchumi hapa chini, patakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, yamesemwa hapa habari ya mapato ya Halmashauri. Mheshimiwa Waziri wangu wa nchi atakapokuja hapa ataeleza kwa zaidi na kwa undani. Lakini moja ya jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisemea kwa nguvu kubwa, kwanza ni taarifa ya mapato na matumizi katika Halmashauri zetu na katika Vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, tunasimama hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunasema tena, ni kinyume cha utaratibu na ni kinyume cha Sheria, Mwenyekiti pamoja na Mtendaji wake wa Kijiji kukataa kutoa Taarifa ya Mapato na Matumizi katika kijiji kinachohusika. Hilo la kwanza. Yaani pale miezi mitatu ikipita ni lazima aweke pale katika Mkutano Mkuu. Sasa ni jukumu letu Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba Mkutano huu unapoitishwa nao unatakiwa uwe na 2/3 ya wanakijiji walioko pale.

Pili, imezungumzwa hapa habari ya Wakurugenzi Watendaji ambao wanapokea hela wananyamaza kimya. Hela za *Local Government Capital Development Grant,* hawasemi kwamba wamepokea Shilingi ngapi? Utaratibu unamtaka Mkurugenzi Mtendaji a-*pin on the board,* aweke pale ukutani na watu wote wajue kwamba hela zilizokuja kwa ajili ya elimu ni kiasi kadhaa,

hela zilizokuja kwa ajili ya maji ni kiasi kadhaa. Hii itasaidia katika *transparency.*

Tatu, Waheshimiwa Wabunge, mkiingia katika vikao vya Halmashauri, kila baada ya miezi mitatu Mkaguzi wa Ndani anatoa taarifa na Mkaguzi huyu *CAG Controller and Auditor General,* anapokuja katika Halmashauri cha kwanza anachodai ni Taarifa ya Mkaguzi ya Ndani ndipo anapoanzia. Kwa hiyo, mwende nayo, hiyo mwijue kabisa, hiyo ndiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani inakusaidia kuangalia mwenendo mzima wa mapato na matumizi ya Halmashauri. Ile ya *CAG* inafanya *postmoterm* kama hela zimeliwa, zimeshaondoka. Hii ya Mkaguzi wa Ndani ambayo tumeimarisha sasa hivi na sasa hivi Mkaguzi wa Ndani, wala yule wa pale Halmashauri hawajibiki kwa Mkurugenzi Mtendaji, anawajibika moja kwa moja kwa Mkaguzi yule wa Taifa. Kwa hiyo, ana nafasi nzuri ya kumchongea huyu Mkurugenzi wake hapa. Huu utaratibu tukiutimia vizuri, utatusaidia.

Pili, namna ya kuondoa viongozi katika madaraka. Mwenyekiti wa Kijiji, wanakuja watu hapa wanasema sisi Mwenyekiti huyu hatumtaki. Sharti fupi tu linalosemwa pale, mwite Mkuu wa Wilaya awepo kwenye Kikao hicho.

Katika mazingira haya tuliyonayo ya sasa ya siasa, mmemwingiza Mwenyekiti pale, wengine wanaweza kutoka upande wa pili wakatengeneza mazingira pale wakamchomoa. Lakini mtu pekee ambaye anaweza kusimamia na kudhibiti pale na kuona Sheria na Taratibu zimefuatwa, ni Mkuu wa Wilaya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Endelea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, tuhuma zote ni lazima zijitokeze pale. Wakizungumza pale, ni lazima waseme wewe tunakutuhumu kwa hiki, uliiba hela za Kijiji, umechukua hela za korosho, umechukua nini, unaeleza yote, unaorodhesha.

Hamtoki tu pale mkasema ondoka, halafu asubuhi mnasema, tunakata, haki zetu, tunaonewa! Ondoka! Haiwezekani hivyo! Hiyo unaweza kuifanya huko kwenye Kijiwe, lakini ikishakuja kwenye utaratibu hapa inakuwa ni ngumu kidogo. Kwa hiyo, utaratibu ni huo.

Mheshimiwa Spika, sasa kama una matatizo, basi tuseme wote hapa kwamba utaratibu huo unaonekana nao una matatizo. Pili, wale wanaokwenda kukaa lazima iwe ni theluthi mbili. Wakienda wachache pale, wakamtoa kikundi cha watu hivi, halafu wakasema kwamba tumemwondoa, bado hiyo nayo itakuwa ni batili.

La tatu, ni kuhusu ajira. Tulichosema hapa, utaratibu huu wa Sekretarieti ya Ajira iliyoko katika Ofisi ya Rais hauwaondolei Halmashauri haki yao ile ya kuajiri isipokuwa yafuatayo yanatekelezwa:-

Kwanza, huwezi kuajiri tu hivi hivi, maana ukiajiri tu hivi hivi itafumka kule kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, anayetangaza kwamba kuna ajira, tunamtaka Fundi

Mchundo, tunamtaka Daktari, tunamtaka mtu fulani ni hiyo Sekretarieti ya Ajira.

Anayefanya *interview* kwasababu hata *capacity* ya Halmashauri ukitaka watu wa Halmashauri, ile Tume yao ya Ajira pale ikutafutie Daktari Mkuu, Mganga Mkuu unataka kumpata pale Siha, unawaambia kaeni mtafute, hawana hiyo *mechanism.* Lazima itoke kule! Lakini akishatoka pale akapita kwenye *interview*, atakayetoa barua ya ajira, ataleta Mama Kombani mpaka pale kwenye Halmashauri, Halmashauri ndiyo itatoa hiyo barua kusema kwamba huyu ameajiriwa.

La mwisho, kuna hawa ambao wanazungumza habari ya kada ya chini; walinzi, wapishi, Watendaji wetu wa Kata na Vijiji kule.

Mheshimiwa Spika, ililetwa hapa *under Miscellenious Arrangement* tukaambiwa kuwa halikufuata taratibu likarudishwa. Liko hapa Mkuu wangu unafahamu kabisa, jambo hilo sisi tulishamaliza, kwasababu hii hoja tumeshaipokea. Lilipokuja hapa likaambiwa kuwa halikufuata taratibu ndiyo tukakwama.

Mimi ninachojua, tulipokwenda katika katika *Councils* zilivyokutana, *Association of Local Authorities of* Tanzania Dar es Salaam, alikuja Makamu wa Rais kwa niaba ya Rais kusema kwamba Serikali imekubali jambo hili. Sasa waliondoka kwa Sheria, hawawezi wakaacha kurudishwa kwa Sheria. Kwa hiyo, kinacholeta tatizo hapa nina uhakika kwamba kitawekwa katika mpango na tutakuwa tumeondokana nalo.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Tumbi. Hospitali ya Tumbi ni muhimu na sisi sote tunafahamu. *Accident*

zote zinazotokea katika Taifa hili ni pale Tumbi ndipo tulipoponea. Pale Tumbi! Tumbi ile Sheria yake haijabadilika, tumei-*consider* kwamba ni Hospitali Teule.

Katika bajeti zetu zote tumekuwa tukipeleka fedha pale. Imezungumzwa habari ya Mochwari pale na zile nyingine.

Katika Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI zimetengwa Shilingi milioni 300 na katika bajeti hii mkiangalia kitabu cha maendeleo zimetengwa Shilingi milioni 500, ninajua ni kidogo, lakini kuna kazi ambayo imefanyika pale, bado tunaendelea kufanya kazi hiyo kuhakikisha kuwa hela nyingi zinakwenda pale kwa ajili ya kuisadia Tumbi.

Mfuko wa Vijana 5%, maneno yanayosemwa katika Halmashauri tumeyakataa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Tumesema 5% ya *own source, no matter how small the amount is,* kwa hiyo, tukienda kwenye Halmashauri na sasa hivi nikipita wakati ninapotumwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikienda katika Halmashauri nikakuta hawakutenga hela hizo, hata wenzetu wa hapa Bungeni, wakienda pale anapigwa tozo yule Mkurugenzi Mtendaji. Tunampiga tozo, kwa nini hukutenga 5% kwa ajili ya akina Mama na 5% kwa ajili ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sauti ikipanda hii mama yangu niwie radhi, ni msisitizo tu hapa, wala siyo kwamba nataka kufanya fujo. Ndiyo! *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hatutasikiliza tena ngonjera hapa tunaambiwa kwamba unajua tena hela zilikuwa ni kidogo, 5% ya hizo kidogo yaani hizo kidogo ulizopata

hapo. Tumesema tutakuwa wakali kweli, na Wabunge mtusaidie kuwa wakali. Hakuna cha kusema hela ni kidogo, 5% haikupatikana.

Pia kuna hela zinazotoka Maendeleo ya Jamii, wako hapa na Waziri anisikia hapa. Tatizo tulilolipata kule ni kwamba hela zile kishakwenda kule zinatakiwa kuwa katika *revolving fund,* kwa hiyo, unatakiwa uhakikishe zile hela zinazunguka mzunguko. Hazirudishwi! Zikienda kule zimekwenda moja kwa moja. Nazo tumesema tutawachukulia hatua wale wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa habari ya posho ya Wenyeviti wa Vijiji wame-*quote* na hotuba ambazo ametoa Mkuu kwa maana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli! Mimi nataka nikukubalie kwamba ni kweli. Lakini hela hizi tulisema kwamba hazikutengwa kwa maana hii tunayozungumza. Tukasema hela hapa kuna kitu kinachoitwa *compensation*.

Mheshimiwa Spika, hela zile ambazo tulisema zuia vitumbua visiokotwe, samaki wasiokotwe; hakikisha akina mama, maandazi yale ya kukaanga na nini msitoze. Halmashauri zote zilizoko hapa tunawapelekea kitu kinachoitwa fidia. 20% tumesema rudisha kule kwa ajili ya kujenga uwezo.

Ile hela ambayo inarudi kule kwenye kijiji na kwenye Mtaa 20% kwa ajili ya vifaa na kuendesha Ofisi ni pamoja na posho ya Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, najua **kosoa** itakayoletwa hapa ni kidogo mno, ndiyo maana kwenye hotuba tunasema kwamba nalo hili tujaribu kuliangalia.

Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge mnapokwenda katika Halmashauri, mtusaidie kufuatilia hizi hela, hazijitokezi kama zile zinazojitokeza hela zilizokwenda kwa Madiwani. Hapa kuna hela zinazoitwa *General Purpose Grant* zilikuwa hazitoki.

Mwaka huu zipo hizi zote ndizo zinazosaidia kwenda ku-*caution* up katika haya maeneo. Kwa hiyo, tunawaomba Wabunge mtusaidie twende mbele.

Mwisho, mimi ni Mtanzania na hawa wote walioko hapa ni Watanzania wenzangu. Mfalme aliwahi kuandaa chakula, akasema mle na kila mtu alikuja na kijiko lakini kirefu kama hii kawa iliyoko hapa. Watu wakaambiwa anzeni kula, wakala wakashindwa kwasababu kijiko *principle* siyo ushike mbele lazima ushike huku nyuma. Wakajaribu kula ikashindikana kwa kuwa kijiko ni kirefu hakifiki. Baadaye akawaambia vipi mbona vyakula vimeandaliwa? Hapa watu wanaita hii ni sungura.

Hii siyo sungura, ni ng'ombe. Shilingi trilioni nne na *point* zimeletwa hapa.

Mheshimiwa Spika, akaja mjanja mmoja akawaambia sikilizeni mkitaka kula hicho chakula, kila mmoja amnyooshee mwenzake alimshe mwenzake. Ndani humu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama hatutashirikiana, Wabunge wenzangu kama tutaondoa misingi ya Kitaifa ya upendo na mshikamano tuliojenga katika Taifa letu, hii kazi tunayofanya hapa itakuwa ni bure.

Mheshimiwa Spika, zitajengwa barabara hapa watu watakwenda kuzivunja, zitajengwa reli hapa watu watakwenda kuvunja; Shule za Sekondari zitajengwa hapa watu watakwenda kuvunja.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu katika Taifa letu ni kitu cha msingi. Lolote tunalolisema humu ndani ni lazima libebe wajibu kwa wananchi wa Tanzania na nchi yetu ya Tanzania na Afrika kwa ujumla. Ninashukuru. *(Makofi)*

## MWONGOZO

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mwongozo kuhusu nini? Kuhusu hotuba hii? Utanimbia baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuliza Bunge mpaka hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge liliaahirishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kusitisha shughuli za Bunge asubuhi tulikuwa tumeanza kuwaita Manaibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kujaribu kujibu baadhi ya hoja. Sasa utaratibu tutakaoutumia ni kwamba, mtoa hoja tutampa dakika 50 ambaye ni Waziri Mkuu; Mawaziri hasa Waziri wa TAMISEMI, kwa sababu alitoa hotuba mwenyewe, tunampa dakika 20; Mawaziri wawili wengine; Uwekezaji dakika 10 na Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge dakika 10.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tutaanza na Waziri wa TAMISEMI ili kusudi aungane na Naibu Waziri aliyezungumza. Waziri wa Nchi, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru na mimi kupata fursa ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi ni kwamba, wananchi wasiadhibiwe kutokana na uzembe wa Watendaji hasa katika Halmashauri ambazo zinapata hati chafu.

Mheshimiwa Spika, siyo nia ya Serikali kuwaadhibu wananchi kutokana na upungufu wa kiutendaji kwenye Halmashauri. Vigezo vya kupata ruzuku vinazingatia ushiriki wa wananchi katika kusimamia shughuli za maendeleo yao kupitia wawakilishi wao. Ni jukumu la Halmashauri ikiwa na maana pamoja na Baraza la Madiwani kuwachukulia hatua Watumishi wanaothibitika kuwa wazembe au wabadhirifu. Kwa hiyo, tunafanya hivyo kwa nia nzuri na matunda yameonekana baada ya kuupitisha utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, hati chafu zimepungua na taarifa ya mwisho ambayo *CAG* ameitoa, hakuna Halmashauri

iliyopata Hati Chafu ukiacha Mbarali ambayo *CAG* ameshindwa kutoa maoni yake kutokana na kutokupata ushirikiano wa kutosha kutoka Mbarali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, upo ushahidi ambao unaonesha kwa namna moja au nyingine katika maeneo mengine watendaji wanashirikiana na Waheshimiwa Madiwani katika kuharibu au katika matumizi mabaya ya Halmashauri. Maeneo mengine baadhi ya Waheshimiwa Madiwani wenyewe ni Wakandarasi ambao wanatekeleza miradi iliyo chini ya kiwango. Kwa hiyo, inakuwa ni vigumu mtendaji kumsimamia mwajiri wake pale ambapo na yeye anajiingiza katika kupata tenda za Halmashauri. Kwa hiyo, Serikali imefanya hivyo kwa nia nzuri.

Mheshimiwa Spika, ukichukulia suala mfano la Mbarali, tayari hatua kwa Watendaji zimechukuliwa, Mweka Hazina amefukuzwa kazi, Afisa Mipango amepewa onyo, Mkurugenzi ambaye amestaafu tayari suala lake lipo TAKUKURU na hatua zinachukuliwa kuhakikisha kwamba anafikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, pia imegundulika kuwa kuna Watumishi wengine ambao walihusika na hawakubainika pale awali lakini mchakato wa kinidhamu sasa hivi unaendelea na Watumishi wengine ambao baada ya kwenda kiundani zaidi, kuzamia na kufuatilia, Mkaguzi wa Ndani wa Mbarari naye pia amesimamishwa kazi, Watendaji wa Kata watatu, nao mchakato wao wa nidhamu pamoja na Mtakwimu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Mbarali imegundulika kuhusika kwa Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Ubaruku ambaye pia suala lake limefikishwa Polisi kwa uchunguzi. Kwa hiyo, tunafanya hivyo kwa nia nzuri, tukiamini kwamba, Waheshimiwa Madiwani wamechaguliwa na wananchi ili wawasaidie kusimamia mali zao pale Halmashauri. Sasa Waheshimiwa Madiwani nao wanapojiingiza, wanasababisha ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuonei, wananchi wanawajibika, Madiwani wanawajibika ikiwa ni pamoja na sisi Wabunge ambao pia ni Madiwani, tunapaswa kusimamia Halmashauri na pale Mtendaji anapohusika tumchukulie hatua kwa sababu ukiacha Mkurugenzi wengine wote pale Baraza la Madiwani linao uwezo wa kuwafukuza kazi, kuwapa onyo na hata kuwasimamisha kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa sana hapa ni suala la Mkoa wa Dar es Salaam kwamba, una idadi kubwa sana lakini Wilaya ni tatu tu na hivyo kuomba kwamba ikiwezekana Mkoa ugawanywe au Wilaya ziongezeke.

Mheshimiwa Spika, pia lipo suala la Mbunge wa Kilwa ambaye amelalamika kwamba, Wilaya yake imeanza muda mrefu kuliko hata Wilaya zingine ambazo zimegawanywa.

Mheshimiwa Spika, suala la kugawanywa iwe Kijiji, Kata, Wilaya hata Mkoa ni lazima lianzie kwa wananchi wenyewe. Kwa hiyo, tunawaomba wenzetu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Kilwa waanzishe mchakato wa kugawanya, pamoja na kukidhi vigezo, lakini pia ridhaa ya wananchi inahitajika na tunaipata pale tunapopata taarifa za vikao halali ambavyo vimeomba kugawanywa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejadiliwa, ni upungufu wa Watumishi katika Halmashauri pamoja na taasisi zingine ambao unasababisha kuwepo na kukaimu. Suala la kupeleka Watumishi katika Halmashauri zetu hasa Afya na Elimu, kwa kweli tunalitilia mkazo. Watumishi wa Kada za Afya na Elimu wanapomaliza tu wanapangiwa kazi bila hata kufanyiwa usaili na pale kibali kinapotoka, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, basi Sekretariati ya Ajira na yenyewe inafanya mchakato na kujaza nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanaokaimu Idara si suala la Ofisi ya Rais, Utumishi wala siyo suala la Sekretariati ya Ajira, tuziombe tu taasisi ambazo Watumishi wake wana

sifa na wanakaimu basi watuletee, wenyewe kwanza wateue na wafuate utaratibu ili kuhakikisha kwamba wanathibitishwa.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wa kuwawajibisha Watendaji wanaofuja fedha za Halmashauri, nadhani kwenye hotuba nimeelezea hatua tunazozichukua kwa Watumishi ambao si waaminifu. Pale inapobainika kwamba, tumemhamisha Mtumishi ambaye kwa kweli alifanya makosa katika eneo lake na ikithibitika ama ikionekana kwamba hawezi kuchukuliwa hatua lazima arejeshwe, huwa tunafanya hivyo mara moja.

Mheshimiwa Spika, lipo suala ambalo lilipendekezwa na Kamati ya TAMISEMI kwamba, iundwe *task force* itakayoshughulikia ajira katika sekta ya afya pamoja na kuwajengea mazingira mazuri ya kazi. Suala hili linashughulikiwa kupitia mpango wa MMAM. Lakini pia tunao utaratibu wa Wizara ya Afya, TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais, Utumishi kukutana na kutatua matatizo ambayo yanajitokeza katika sekta zetu ambayo yanatuhitaji kwa pamoja tuweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pia lipo suala ambalo limezungumzwa sana hasa upande wa pili, kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hakuna sababu yeyote ya kuwepo katika mfumo au muundo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeona umuhimu mkubwa sana wa kuwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na huo ndiyo utaratibu wa kugatua madaraka. Rais kwa madaraka aliyonayo amegatua mengine kwa Waziri Mkuu, kwa Makamu wa Rais, kwa Mawaziri na mengine yamegatuliwa kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Sasa kwa kuwa sisi ndiyo tunaotawala, basi sisi ndiyo wenye kuchagua ni muundo upi tunaoutaka ili tuende nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wenzetu kama itatokea Mwenyezi Mungu akiwajalia, basi hayo mapendekezo yenu

nadhani mtayatekeleza, lakini kwa sisi huu ndiyo muundo ambao tunauona unafaa na unasaidia, kwa sababu Rais hawezi kuwa katika kila Kijiji, kila Mkoa na kila Wilaya. Kwa hiyo, anakuwepo kupitia Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na wengine waliopo katika hizo ngazi za huko chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia lipo suala limezungumzwa kwamba, sera ya ugatuaji wa madaraka imeshindwa kutokana na Serikali Kuu kuingilia Serikali za Mitaa, ajira hufanywa na Serikali Kuu, hivyo Serikali za Mitaa hushindwa kuchukua hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, Sekretariati ya Ajira inachofanya ni mchakato tu wa ajira, lakini mchakato ule ukishakwisha mamlaka ya ajira kwa maana ya nidhamu, upandishwaji wa Vyeo na mengine yote yanakwenda kwa Mwajiri husika na tumefanya hivyo kwa manufaa, kwa sababu zipo Wizara watu walikuwa wanatengeneza *succession plan* za makabila na tunazijua. Tumefanya hivyo kuondokana na utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia yapo maeneo ambayo hayawavutii Watumishi, ilikuwa siyo rahisi ukishindanisha na maeneo mengine kuwapata watumishi katika maeneo hayo, lakini kwa masuala ya kada za chini ilishazungumzwa kwamba sheria ikirekebishwa tu hapa, kada zile za chini Halmashauri zitaachiwa, lakini kada zile za juu kwa kweli bado utaratibu uliopo ni mzuri na tunaona unafaa kwa ajili ya kuwa na utumishi wa Kitaifa na siyo ule wa kikoo, kikabila au wa kidini katika baadhi ya sekta.

Mheshimiwa Spika, pia limezungumzwa suala la ukosefu wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri unaosababisha udanganyifu. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Hazina na wadau wengine wanafanya tathmini ya kuhakikisha kwamba kwanza mifumo ipo, lakini pia tunafanya tathmini ya kuhakikisha kwamba tunaiboresha zaidi mifumo iliyopo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kupitia mradi wa *TSCP,*

*ULGSP, GIZ-SULGO* zote zinafanya uchunguzi wa kina kwa kuhakikisha kila Halmashauri tunafahamu vyanzo vilivyopo na kuweka mfumo ambao utasaidia kukusanya mapato na kufunga mifumo ukiwemo pamoja na *e-Tax* kuhakikisha kwamba kodi zote zinazopaswa kukusanywa, zinafika katika Mifuko ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeshauriwa itoe Waraka kwa Halmashauri zote nchini juu ya ukusanyaji wa mapato kutokana na ushuru wa huduma kwa mujibu wa sheria. Ushauri huo umezingatia na Waraka utaandikwa.

Mheshimiwa Spika, pia imezungumzwa kwamba, Serikali iandae mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mikoa na Halmashauri. Mifumo tunayo, upo mfumo wa *PLAN REP, LGMD, EPICOR* na sasa hivi kimeanzishwa chombo cha *Presidency Performance Bureau,* chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu. Pia sanjali na hilo Ofisi ya Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara za kisekta pamoja na Mikoa imejipanga kuhakikisha kwamba tunafanya ufuatiliaji wa miradi katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na CAG, tunao pia Wakaguzi wa Ndani na sasa hivi eneo lolote ambalo Halmashauri itabainika kuwa na ubadhirifu mkubwa, mtuhumiwa wetu wa kwanza katika Halmashauri ile ni Mkaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Mbarali tumeanza utekelezaji huo. Kwa sababu yeye tunamtegemea pale ndiye awe mfuatiliaji wa siku hadi siku. Kwa hiyo, hakuwezi kukatokea ubadhirifu wowote wa kutisha na yeye akawa salama. Kwa hiyo, Wakaguzi wa Ndani na wenyewe kila inapotokea ubadhirifu, yeye ndiye *suspect* namba moja.

Mheshimiwa Spika, ipo pia hoja kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ibadili mfumo wa Bajeti ya Maendeleo utakaozingatia fedha za ndani badala ya utegemezi wa ufadhili kutoka nje. Tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunatenga fedha za ndani nyingi pale hali inaporuhusu na miradi ya wafadhili pia tunapokuwa na uhakika kwamba watatusaidia basi tutaweka.

Mheshimiwa Spika, pia tulishauriwa kwamba, pesa nyingi sasa tuziweke katika maendeleo kuliko matumizi ya kawaida. Ushauri huu unachukuliwa na utazingatiwa katika bajeti zijazo.

Mheshimiwa Spika, suala la mfumo wa *EPICOR* kwamba uunganishwe kwenye mkongo wa Taifa ili kupunguza gharama za uendeshaji katika Halmashauri. Suala hili ni kwamba mfumo wa *EPICOR* unaotumiwa katika Halmashauri 133 Tanzania Bara umeunganishwa kwenye mkongo wa Taifa kupitia kituo cha kompyuta kuu kilichopo Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma. Gharama za kuendesha mkongo huu ni za Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI na siyo Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, *Bylaws* zinachelewa zikipelekewa kwa Waziri Mkuu. Kwa kweli kwa wale wanaoleta sheria ndogo ambazo zimekidhi vigezo tunazipeleka kwa Waziri Mkuu na nyingi zinarudishwa kwa wakati, mara nyingi zinazochelewa ni zile ambazo tunarudisha ili kufanya marekebisho ya hapa na pale. Lakini pia wapo wengine wanapeleka moja kwa moja kwa Waziri Mkuu bila kupitishia TAMISEMI, kwa hiyo inakuwa ngumu kwa Waziri Mkuu kuzifanyia kazi bila kupata ushauri wa TAMISEMI, lakini ushauri tunautoa na hatuna sheria nyingi ambazo zimekaa kwenye ofisi yetu bila kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, pia lipo suala ambalo limeelezwa kwamba, baada ya maboresho ya Serikali za Mitaa, Serikali itoe tamko ni kwa nini, hili nilishalijibu la Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, pia lipo suala lilizungumzwa kwamba Mkoa wa Lindi na Mtwara iliombwa igawanywe ili kuweza kusogeza huduma kwa wananchi na hivyo kuwa na Mkoa wa Kusini unaojumuisha Wilaya za Nanyumbu, Masasi na Nachingwea. Bado majibu yanabaki yake yale, hatukupata ridhaa ya kutoka Mikoa hiyo, kwa hiyo tunaomba mikoa husika ikae kupitia *RCC* zao, walete ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Tunduru, tunaomba *RCC* zao zao walete mapendekezo hayo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hatuoni

kwa nini Serikali isiridhie mapendekezo ya wananchi, lakini mpaka sasa hivi ofisi yetu hatujapokea maoni ya kutoka katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lipo suala limezungumzwa kwamba, sheria ndogo zikiidhinishwa na Baraza la Madiwani haziwezi kutumika hadi pale zitakapoidhinishwa na Waziri mwenye dhamana na kwamba walikuwa wanaomba Mikoa ifanye kazi hiyo. Suala hilo linatekelezwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 64 ya Katiba ya mwaka 1977, ambayo yenyewe inataka utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, zile sheria ndogo za Vijiji na Mitaa, Mkoa unamaliza, lakini inapokuwa ni sheria ya Halmashauri ni lazima iletwe kwa Waziri Mkuu. Lengo ni kuhakikisha kwamba sheria hizo ndogo zisikinzane na sheria mama. Tunaamini kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inao watalaam Wanasheria wengi sana ambao wanaweza wakamshauri Waziri Mkuu vizuri zaidi kuliko katika Mikoa yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezeshaji na Uwekezaji, dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba majibu yangu yote tutayaweka kwenye Hansard kama sitayakamilisha.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge, waliochangia Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu zila zinazohusua eneo langu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mabadiliko ya Sera ya Uchumi tangu miaka ya 90, Serikali imebaki na majukumu ya msingi ya kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi

kuchukua nafasi yake kikamilifu ya kuwa mhimili wa ukuaji wa uchumi. Sekta binafsi ikitekeleza majukumu yake kwa ufanisi, itatoa mchango mkubwa katika jitihada za kujenga uchumi imara na wa kisasa utakaohimili ushindani wa Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wamehoji matokeo ya ukuaji uchumi, hayajaleta maisha bora kwa Watanzania walio wengi. Hii imetokana na msukumo wa uchumi wa soko ambapo ongezeko la uwekezaji limekuwa zaidi katika sekta za madini au utalii na mawasiliano, ambazo hazina uhusiano wa moja kwa moja katika kuleta maisha bora. Serikali, itaelekeza mapato yanayotokana na sekta hizi katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia sekta zenye uwezo wa kuajiri kwa wingi kama kilimo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa ndani na nje, ni muhimu katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa Taifa lolote duniani na ndio utakaoleta maisha bora. Ushindani wa kiuchumi miongoni mwa nchi mbalimbali duniani, unategemea uwezo wa nchi hizo katika kuzitumia kwa ufanisi maliasili zake. Uwepo wa rasilimali asili nchini, hautoshi peke yake kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii yatakayoleta maisha bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji una mchango mkubwa katika kuzibadilisha rasilimali kuwa bidhaa na huduma, hivyo kuliwezesha Taifa kukuza uchumi na kuleta maisha bora na kuondoa umaskini. Manufaa yatokana na ongezeko la uwekezaji ni mengi, lakini ni pamoja na ongezeko la mitaji, teknolojia na ujuzi pamoja na ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wameitaka Serikali iondoe vikwazo vinavyoathiri utendaji wa kituo cha utoaji huduma kwa pamoja katika Bandari ya Dar-es-Salaam. Uanzishwaji wa kituo hicho ni hatua ya awali ya kuboresha huduma zinazotolewa na bandari yetu katika kuondoa urasimu. Hivi sasa Serikali, imeandaa Mwongozo kuhusu utaratibu unaotumika na utakaofuatwa na wateja

wakati wa kutoa mizigo Bandarini; lengo kuu litafikiwa kikamilifu baada ya Serikali kufanya marekebisho ya Sheria zilizounda taasisi hizo zilizounganishwa chini ya mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge vile vile wametoa hoja kwamba, Serikali, itoe elimu ya kutosha kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, maarufu kama *PPP.* Sera ya Sheria ya *PPP* ina lengo la kuweka mfumo wa Kisheria utakaorahisisha ushiriki wa sekta binafsi katika kujenga uchumi na kutoa huduma bora. Serikali kwa kutambua kwamba, dhana ya *PPP* ni mpya hapa nchini, imeendelea kutoa mafunzo kwa wadau wote wakiwemo wa Serikali na wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wameishauri Serikali, kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya kilimo na hili ni muhimu sana na tunafanya hivyo, kupitia taasisi ya sekta binafsi Tanzania na kwa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, kupitia Baraza la Taifa la Biashara, Mabaraza ya Mikoa na Wilaya, imehamasisha kuwekeza kwenye miradi ya kilimo. Kutokana na uhamasishaji huo idadi kubwa ya wawekezaji wa kwenye ukanda wa kilimo wa Kusini mwa Tanzania na nina hakika itakuwa hivyo katika Kanda zingine.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ufafanuzi wa hoja kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali, dhidi ya mwekezaji aliyepewa eneo la hekta 10,529 Mkoani Kigoma. Mwekezaji aliomba kuwekeza Mkoani Kigoma kwenye sekta ya kilimo mwaka 2010, ardhi aliyoomba iko kwenye eneo la shamba Namba 206, lililokuwa Ranchi ya mifugo, likimilikiwa na Serikali, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, Ranchi hiyo yenye ukubwa wa hekta 15,000 ilitumiwa na Serikali, kama Kambi ya Wakimbizi ya Rugufu, kutoka Burundi.

Mheshimiwa Spika, kati ya hekta hizo, mwekezaji alipewa hekta 10,529 na zilizobaki zimepangwa kutumika kwa ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, kwa hivyo, Halmashauri haijanyimwa fursa hiyo. Baada ya kufuata taratibu zote za Kisheria za kumilikishwa ardhi kupitia

Hati isiyo Asili, kupitia *TIC,* tarehe 23 Februari, 2012, Mwekezaji amepewa umiliki huo wa kuweza kuwekeza kwenye shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na dhana potofu inayoenezwa na baadhi ya watu kwamba, wawekezaji wa nje wanapokonya ardhi ya wananchi. Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Mwekezaji kutoka nje haruhusiwi kumiliki ardhi nje ya utaratibu nilioueleza. Ni juu yetu wananchi na Serikali yetu, kuona kwamba, wawekezaji wa nje hawaitumii fursa hii vibaya. Kuna umuhimu mkubwa kwa nchi yetu kuendeleza jitihada za kuwa na Sera za uwekezaji zinazotabirika kuweka vivutio ili wawekezaji wanaoshindaniwa duniani, waweze kuja huko.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni zile zinazohusu masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza jukumu hili kwa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Sheria ya Uwezeshaji Wananchi ya Mwaka 2004. Uwezeshaji wananchi kiuchumi unalenga kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika kumiliki, kusimamia, kuendesha na kujenga uchumi wa nchi yetu. Serikali, kupitia usimamizi wa Mifuko ya Uwezeshaji imeongeza mitaji kwenye Mifuko mbalimbali; lakini ningependa kuliongelea hilo kuhusiana na vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, wanawake na vijana ni sehemu muhimu ya jamii hivyo, Serikali, imewapa nafasi ya kipekee ndio maana wameundiwa mifuko mbalimbali. Vijana ni zaidi ya 60%, ni nguvu kazi ya Taifa ni Taifa la leo na la kesho. Ni tegemeo la wazazi, jamii na Taifa, lakini wengi wao hawana ajira ya kudumu, mitaji ya kuanzisha na kuendeleza miradi na ujuzi wa kutafuta masoko na kuhimili ushindani. Wanawake ambao ni mama zao, ni masikini na ndio wanaobeba umasikini wa familia, jamii na Taifa. Mifuko waliyoundiwa vijana na wanawake ina fedha kidogo, Serikali, inatambua hilo na italipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, naahidi Bunge lako Tukufu kwamba, changamoto zilizojitokeza na nyingine zilizolalamikiwa vikali na Waheshimiwa Wabunge, zitafanyiwa kazi. Napenda kutoa rai kwa wananchi, hususan vijana na wanawake, kujiunga kwenye *VICOBA*, ili Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Benki Kuu waweze kuratibu na kusajili na kuweka Sheria, ili hatimaye wenye *VICOBA* watambuliwe na mabenki na wakopeshe.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, pia wameshauri kwamba, Baraza la Uwezeshaji wananchi kiuchumi liongeze juhudi za kupanua wigo kwa kuwawezesha wananchi kwenye maeneo mengi zaidi; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi, litazingatia hivyo.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niseme vile vile kwamba, amani na utulivu ni mazingira wezeshi kwa wawekezaji. Amani na utulivu ndio itakayovutia wawekezaji wa ndani na wa nje. Naomba sana amani na utulivu uzingatiwe. Kutukanana humu ndani, uzushi unaotokea humu ndani, unaashiria kwamba, kuna uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge, wawe wa kwanza kutoa taswira hiyo ili wawekezaji wa ndani wawe na uhakika, wasiwe na hofu na wale wa nje vile vile wavutiwe na hawa wa ndani kuwekeza ndani ya nchi hii ambapo vijana wanataka ajira, wananchi wanataka maisha bora na Taifa, linataka uchumi ulio imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kabla kengele haijalia, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge, kwa dakika kumi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichangie kidogo hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa

kueleza machache katika maeneo yatakayowezekana kwa dakika kumi. Nianze na Menejimenti ya Maafa.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaarifu tu Wabunge, kwamba, tumeanza mapitio ya Sheria Namba 9 ya mwaka 1990, ambayo imelenga zaidi katika kukabili maafa badala ya hatua ya kuzuwia na kupunguza athari zinazotokana na maafa, ili iendane na wakati. Kwa hiyo, changamoto zote tulizozisikia tutazizingatia katika marekebisho ya Sheria hii. Lakini pia Serikali imezindua Mpango wa Kujiandaa Kukabili Dharura za Maafa Nchini.

Mheshimiwa Spika, Mpango huo umeanza kutekelezwa kwa kufanya tathmini ya maafa yanayoweza kutokea na uwezo wa kuyakabili katika Halmashauri; tumeanza Chamwino, Kondoa na Mpwapwa na zoezi hili linaendelea katika Halmashauri za Maswa, Kwimba, Bunda, Nzega na Kilosa, Mwanga na Same. Nia ni kuwa na utayari wa kukabili maafa katika Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka huu wa fedha Serikali, imetenga shilingi bilioni moja, kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kuratibu dharura za maafa. Vile vile Serikali, imesogeza huduma za misaada ya dharura za maafa karibu zaidi kwa wananchi, ili yakitokea maafa tuweze kuhudumia kwa ukaribu. Kanda ya Kusini, Kituo tumeweka Mtwara; Mashariki, Dar-es-Salaam; Magharibi, Shinyanga; Kaskazini Moshi na Kanda ya Kati, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo, Serikali, imehudumia mwaka huu 2012/2013, Serikali imetoa zaidi ya tani 609,452 za chakula chenye thamani ya shilingi bilioni 26 na pia imetoa zaidi ya shilingi bilioni 4.6 kwa maafa mbalimbali yaliyojitokeza. Nataka kumkumbusha Mheshimiwa ndugu yangu wa Kishapu kwamba, mwezi Disemba tulitoa tani 1,800 Kishapu na mwezi Februari tumetoa tani 1,200 na jana tumepokea maombi mapya ambayo leo ameyasema Bungeni, tunayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa dawa za kulevya.

Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya Tume, mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka 2013/2014, Tume imetengewa shilingi bilioni tano ukilinganisha na shilingi bilioni 2.5 zilizotengwa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kuratibu Madawa ya Kulevya na yenyewe Sheria yake tunaifanyia marekebisho ili angalau ifanane na wakati uliopo, mianya mingi iweze kuzibwa iliyokuwemo katika Sheria iliyopita.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, pamoja na wafanyabiashara wa dawa za kulevya kutumia mbinu mbalimbali, Serikali kwa kutumia Kikosa Maalum cha Kudhibiti Biashara hiyo Haramu, imeendelea kuwasaka, kuwakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka 2010 mpaka 2012 kiasi cha kilo 714.4 za *heroine* na 344 za *cocaine* zilikamatwa na watuhumiwa 162 walikamatwa kwa kuhusishwa na biashara hiyo. Aidha, baadhi ya washtakiwa wamehukumiwa vifungo vya kuanzia miaka 20 na wengine vifungo vya maisha na kesi zinaendelea. Hivyo, nataka kuwahakikishia hakuna watu wanaojihusisha na dawa za kulevya ambao vyombo vya dola vinawafumbia macho kama baadhi ya Wabunge, walivyofikiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Uchaguzi; Serikali imeanzisha maandalizi ya kuiwezesha Tume ya Uchaguzi kuwa na jengo lake kwa kutenga kiwanja, kuandaa michoro pamoja na kufanya upembuzi yakinifu. Serikali, inalifanyia kazi suala la Tume kuwa na watumishi wake hadi kwenye ngazi ya Wilaya. Hata hivyo, kutokana na uzoefu wa nchi nyingine na hali halisi ya utekelezaji wa majukumu yake, Tume bado italazimika kutumia wafanyakazi wa muda, hususan nyakati za Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, fedha kwa ajili ya uboreshaji wa daftari ziko Hazina. Mwaka huu wa fedha kuna fedha kidogo watapewa za kuanzia, lakini mwaka ujao unaoanza mwezi

Julai, fedha zimetengwa Hazina na marekebisho ya Daftari lile la Kupiga Kura, yatafanyika mara mbili kabla ya Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, eneo la Bunge, nataka niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, tulipata *briefing* juzi, Viongozi wetu wa Bunge, wataendelea kutoa *briefing* kwa yale yanayotuhusu ambayo yameulizwa juu ya Ofisi na samani na kila kitu. Juzi tumepata *briefing,* kwa hiyo, nisingependa kurudia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maadhimisho ya Taifa; limezungumzwa suala la eneo la kuzika Viongozi, ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba Moja (1) ya Mwaka 2006, inayohusu Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa. Sehemu ya IV ya Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo kimetamka kuanzisha kwa makaburi ya Viongozi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali, katika kutekeleza Sheria hiyo, imetenga hekta 129 katika eneo la Iyumbu, Manispaa hii ya Dodoma katika bajeti ya mwaka huu na Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kulipa fidia eneo hilo ambalo linatayarishwa, ili kutekeleza Sheria hii. Hailazimishi Sheria hii kila mtu azikwe hapo, wala msiwe na wasiwasi, Sheria hii imeelekeza nani anayestahili kuzikwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni ustawishaji wa Makao Makuu. La kwanza linaloashiria kwamba, tuko *serious* kuhamia Dodoma, Serikali, imeandaa na imekamilisha mapitio ya mpango kabambe ya Mji wa Dodoma, ili uendane na kasi ya ukuaji wa mji wa Dodoma na ongezeko la watu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu na huduma za jamii hapa Dodoma, ili kukidhi mahitaji ya sasa. Mwaka 2012/2013, peke yake Serikali, imejenga barabara za kilomita 20.6 za lami na imekarabati mtandao wa maji wenye urefu wa kilomita 15.5 na kusambaza umeme wa msongo mkubwa kilomita 13.5.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, inaunganisha Miji ya Dodoma/Iringa kupitia Mtera na Arusha kupitia Kondoa na Babati. Ili kufanya suala la kuhamia Dodoma kuwa la Kisheria, tunafanya lile alilosema Mheshimiwa Juma Nkamia la kuleta Sheria hapa Bungeni na kupitia miradi yetu ya *Tanzania Strategic Cities,* Dodoma imepewa Dola milioni 32 kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya hapa mjini kwa kushirikiana na Manispaa. Ni Manispaa pekee iliyopewa fedha nyingi kuliko Manispaa zote katika mradi huu, hii ni kutambua tu kwamba, mahitaji ya nchi yatakuwa hapa na inahitaji miundombinu iliyokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuwahakikishia wote pamoja na Mheshimiwa Juma Nkamia, nia ya Serikali ya kuhamia Dodoma iko pale pale na Mwenyekiti wa Bodi ni mimi ndio, kama ulivyosema na Serikali, ilifanya makusudi kuweka Waziri, ili kuipa uzito Bodi yenyewe. Mwenyekiti wa Tume ya Ustawishaji wa Makao Makuu ni Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, suala la UKIMWI limeingizwa kwenye Mitaala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na linafundishwa katika shule kama yalivyo masomo mengine. Ili kuhakikisha mapambano ya UKIMWI yanaendeshwa Serikali ya Marekani inaandaa utaratibu wa kuisaidia Serikali ya Tanzania kwa kipindi cha miaka mingine mitano kuanzia Oktoba mwaka huu, msaada wa UKIMWI, ambao unakadiriwa utakuwa shilingi bilioni 400 kwa mwaka. Serikali, imeandaa utaratibu mbadala wa kupata fedha hizi na hivi sasa tuko kwenye hatua ya mwisho ya kuanzisha *AIDS Trust Fund;* Waraka uko kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi, ambapo kila mwaka sasa nao wanachangia karibu shilingi bilioni saba. Mwezi Machi mwaka huu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alizindua Taarifa ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI kwa mwaka 2011/2012. Matokeo ya utafiti huu yametoa mwanga juu ya janga hili. Kwa ujumla maambukizi katika mwaka 2011/2012, yameonesha kushuka hadi 5.1% ukilinganisha na 5.7% mwaka 2007/2008 na 7% iliyokuwepo mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wenye kasi ndogo ya maambukizi ni Kaskazini Pemba kwa sasa, ambayo ni 0.1% wakati Mkoa wenye kasi kubwa ya maambukizi ni Mkoa wa Njombe wenye maambukizi, kwa takwimu za sasa, 14.8% na mkitaka taarifa zaidi naweza nikaitoa kama muda ukiruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Waheshimiwa Wabunge wengi, wamesemea eneo hili; nataka kuwahakikishia kwamba, Serikali inaendelea hatua kwa hatua kuongeza fedha za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, ili kununua mitambo ya kisasa itakayomwezesha kutoa kazi kwa ubora unaotakiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, natoa wito tu Taasisi za Serikali, Halmashauri na Mikoa, iendelee kumtumia Mpiga Chapa Mkuu, kwani anayo mitambo inayomwezesha kufanya kazi zote hizo. Mwaka huu peke yake, kwa mfano, tumemtengea shilingi bilioni moja ukilinganisha na shilingi milioni 500 za mwaka uliopita. Pia Serikali inakusudia kuifanya Idara ya Mpiga Chapa kuwa Wakala, ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, waliochangia maeneo mengi. Lakini kama mlivyoona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imechangiwa na hoja zinazogusa Wizara zote. Hoja hizi zimekabidhiwa kwa Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika, ndizo watakazoanza kujibu wakati wa mijadala ya hoja zao. Wenyewe wameshajua kwamba, kumbe hoja zetu mwaka huu zina upeo kiasi gain, kwa hiyo, hoja hizi nyingi ambazo zimejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, zitajibiwa na Mawaziri wa Kisekta, sisi tumejitahidi ku-*wind up* hizi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kama wenzangu walivyotoa wito, nawashukuru sana kwa mshikamano wenu, tuendelee kushikamana katika kutatua kero zetu za Kitaifa. Yaliyopita si ndwele, tuliyoyasikia jana na leo, lakini nadhani wote tumejifunza vijana na wazee kwamba, tutumie Bunge hili kwa busara ili kujenga mustakabali mzuri wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Makamba, kwa Hotuba yake ya asubuhi, ambayo nataka kuwahakikishieni Mheshimiwa Makamba, tulimpanga makusudi ili atoe mfano, ili awe kama shamba darasa kwa hotuba nzuri za vijana, wanazopaswa kutoa ndani ya Bunge hili. Lazima aweke tofauti, tulitaka kuweka mfano ulio tofauti na ulio wa wazi. Bila shaka watu wote wamefurahia kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Makamba. Nampongeza sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mhshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa mtoa hoja!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kukutana leo ili kukamilisha kazi ambayo tumeifanya kwa karibu siku tano hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu Waheshimiwa Wabunge 217 walichangia; Wabunge 119 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na wengine 98 wamechangia kwa njia ya maandishi. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba idadi ni kubwa sidhani kama mimi na Mawaziri wangu kwa kipindi hiki tutaweza kutumia muda uliopo kuweza kujibu kila kitu. Lakini kama walivyosema tumeziagiza Wizara nyingine zote na zenyewe zichukue masuala haya ili na wao waweze kujibu wakati watakapokuwa wanawasilisha *paper* zao.

Mheshimiwa Spika, niko hapa kwa kutumia Kanuni ya Kudumu ya Bunge 99(9) ambayo ndiyo hasa inaniongoza. Naomba pengine nianze na hotuba ya Ndugu yangu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe, ilikuwa ndefu lakini tutajitahidi na sisi kupitia baadhi ya maeneo kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijasema hivyo, nataka niwashukuru Wabunge wote kwa ujumla kwa michango

mizuri. Kwa namna ya pekee kabisa niwashukuru sana Wabunge Mheshimiwa Lugola na Mheshimiwa Filikunjombe ambao wao waliamua kutokubali hotuba au bajeti ya Waziri Mkuu. Nadhani wanazo sababu za kutosha, Bunge lingekubali lote kwamba sawa maana yake hata Bunge lenyewe tungekosa pesa, kwa hiyo sijui tungefanyaje, Serikali zetu za Mitaa zote zingekosa pesa. Kwa hiyo, nadhani Serikali yote sasa itafika mahali isifanye shughuli zake, lakini naheshimu sana mawazo yao tutayazingatia katika utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini moja ambalo nimepata tabu nalo ni lile la Mheshimiwa Filikunjombe, alilojaribu kunishawishi mimi na Serikali yetu, tufike mahali tuwe tunakubaliana na mawazo yanayotoka Upinzani. Hili limenisumbua kidogo, limenisumbua si kwa sababu yoyote ile, lakini kwa sababu sijawahi hata siku moja kusikia Mbunge wa CHADEMA anaunga mkono hoja yoyote ile ya Serikali. Najua wengine wanatikisa kichwa ninaposema hivi nazungumza hoja za msingi, sana sana nilichokipata ni watu kutoka nje kwa sababu bajeti hawaitaki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa mambo haya ni pande zote mbili, tuheshimiane, sisi tutapokea maoni yenu lakini tunaombeni na nyinyi basi mchukue haya ambayo Serikali inayafanyia kazi tena wakati mwingine kwa pamoja, lakini mnavyofika kwenye hatua ya kupiga kura au kujaribu kuunga mkono kila mmoja anasema siungi mkono hoja, siungi mkono hoja, lakini bajeti ikipita tuko pamoja katika mambo yanayoendelea, sasa unajua na yenyewe haina maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Mbowe ananiambia kwamba, tatizo kubwa la Serikali inayoongozwa na CCM ni kukosa weledi wa kutekeleza kikamilifu vipaumbele vyake pamoja na kuviainisha kupitia Mpango wake wa miaka mitano, bajeti na *program*. *To be frank,* nimeshtuka sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii tuliamua kwa makusudi

kuandaa mpango wa miaka 15, mpango ambao umegawanywa katika miaka mitano, mitano, tukaomba Wabunge, tukakaa pamoja, tukauzungumza, mkatoa maoni na sisi tukaahidi kwamba tutayasimamia kwa kadiri itakavyowezekana. Kikubwa katika mpango ule tumesema ni kweli tuna mambo mengi tunataka tuyasukume lakini kwa uchumi wetu na uwezo wetu ulivyo kiuchumi, haitawezekana kwenda na mambo yote. Kwa hiyo, tuchague machache yale ambayo yatakuwa na msukumo katika uchumi na kupunguza umaskini wa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, tukachagua maeneo machache yafuatayo:-

Kwanza ni miundombinu, kwa hiyo katika miundombinu tumechukua nishati, tukachukua usafirishaji, tumechukua TEHAMA, maji safi, maji taka na umwagiliaji, ndiyo eneo tuliloona tulipe nafasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, pili, tukasema kilimo kwa maana ya kilimo mazao, mifugo, uvuvi, misitu na ufugaji nyuki.

Mheshimiwa Spika, tatu, maendeleo ya viwanda, tukasema nalo hili tulipe nafasi kubwa na hasa viwanda vile ambavyo vitatumia rasilimali za ndani au *raw material* za ndani. Kwa hiyo, tukasema hiki kikifanyika, tunaamini kabisa uchumi wetu utakuwa haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini nne, tukasema ni maendeleo ya rasilimali watu; ujuzi, maarifa kwenye sekta za Afya, maji na elimu. Kwa hiyo, sisi tuliamua vipaumbele vikubwa vinne kwa makusudi kabisa, tukiamini kwamba tukijipanga vizuri, hivi vitakuwa na nguvu sana ya kuleta mabadiliko katika uchumi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, sasa tumepanga hivyo, lakini tukaambiwa hatuna weledi na wala hatujui kupanga, tena tulipanga pamoja, tukakubaliana, sasa tatizo hapa linatoka wapi? Kwa nini mimi na timu yangu ndiyo tuonekane hatuna weledi? Basi kama ndiyo vipaumbele hivi vinatuongoza, wote

hatuna weledi, maana wote tulipanga pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, hivi kweli hatuna weledi? Kwenye eneo la uchumi, nchi yetu tumesifika karibu duniani kote kwamba ni miongoni mwa nchi tunaofanya vizuri sana katika uchumi. *GDP* yetu 6.9, bajeti ya Serikali tumeiongeza kutoka trilioni 4.2, 2005/2006 leo tunazungumza trilioni 16.7, 2013/2014. Makusanyo ya kodi 2005/2006, zilikuwa bilioni 117, leo tunazungumza bilioni 680 kwa mwezi. Sasa tusingekuwa na weledi jamani haya tungeyaweza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukasema tuzamie kwenye barabara. Mwaka 2000 barabara kuu za lami zenye urefu wa kilomita 3909, ndizo tulizokuwa nazo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu ikaanzisha miradi 14 ya barabara zenye urefu wa kilomita 1226, akajitahidi baba wa watu akapiga miradi saba kilomita 403 zikakamilika. Alipoingia Jakaya Mrisho Kikwete tukachukua miradi yote iliyobaki, tukaikamilisha yote kilomita 823, akaanzisha miradi 26 mipya yenye urefu kilomita 1759.6. Kati ya hizo jumla ya kilomita 1270.8, sawa na asilimia 72 zimekamilika kwa kiwango cha lami, tumebakisha kilomita 488.8.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Nne, imejenga barabara kuu mpya zenye urefu wa kilomita 2093.8, katika kipindi hiki cha miaka saba tu. Sasa tumefanya ukarabati kwenye barabara za lami kilomita 841.2, kilomita650 sawa na 77% zimekamilika, 191.2 tunaendelea nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awamu hii imeibua miradi mingine 43, kilomita 5739. Kati ya miradi hiyo 16 yenye urefu wa kilomita 3817, ipo katika hatua mbalimbali za kukamilisha usanifu, 27 ndiyo inaendelea kufanyiwa usanifu. Tumefanya hivi makusudi kwa kujua na barabara muhimu zenye uwezo wa kubeba mizigo kukuza uchumi ni tatizo, tatizo letu kubwa ni uchumi, barabara ni uchumi mkubwa, ndiyo maana tukapanga kwamba kwenye miundombinu hili jambo tulipe kipaumbele kikubwa.

Mheshimiwa Spika, tukaanzisha Mfuko wa Barabara, tulianza na shilingi bilioni 85.74, kufikia 2007/2008 tulikuwa na bilioni 218.47 na hii tuliifanya makusudi ili tuongeze uwezo wetu wa matengenezo ya barabara. Sasa hivi ni wastani wa bilioni 220 hivi karibu kila mwezi tunakusanya, tunaweka kwenye barabara. Yote hii ni kulenga kuleta matokeo ya haraka katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madaraja; jamani eeh unaweza ukajenga barabara hizi, lakini kama huna madaraja tabu tupu, tumejitahidi kweli. Sasa hivi tumejenga daraja la Umoja, madaraja ya Nangoo na Nanganga, Mtwara; daraja la Ruvu lile; daraja la Mwatisi, Morogoro; Luwekei pale Ruvuma; daraja la Sibiti, daraja la Mbutu, daraja la Mto Malagarasi, juzi wote mmeliona pale.

Mheshimiwa Spika, sasa tunakwenda na daraja la Kigamboni na lile la Kilombero pamoja na Sumo Kagera. Sasa jamani mnataka tufanyeje, sisi tunajitahidi sana kwenye eneo hili. Tuna malengo mazuri ambayo yakifanikiwa, tuna hakika kabisa uchumi wa nchi hii utakuwa kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumejenga vivuko kwenye Awamu hii Nne peke yake na vivuko ambavyo vina uwezo wa kubeba mizigo mikubwa, kwenye maziwa, kwenye bahari kote kote tumejitahidi. Vivuko hivyo ni *MV.* Kilombero, *MV.* Luhuhu, *MV.* Misungwi, *MV.* Magogoni , *MV.* Kome, *MV* Pangani, *MV.* Utete, *MV.* Ruvuvu, *MV.* Ujenzi, *MV.* Kalambo kule Mtwara.

**MBUNGE FULANI:** Kilambo!

**WAZIRI MKUU:** *MV* Kilambo, kule Mtwara. Yote hii ni katika jitihada za kujaribu kuwasaidia watu waweze kwenda kwa haraka, wafanye shughuli zao ili kujiletea maendeleo. Haya mnasema hatuna weledi, weledi gani mnaoutafuta jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunahangaika na usafiri wa reli, tunafanya jitihada kubwa tu kwa sababu tunatambua

ni jambo la msingi sana. Tulikuwa tuna Kampuni ya *RITE* tukaiondoa, tukasema acha tujidhatiti upya, kwa hiyo, tunakwenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunachojaribu kufanya, kwanza ni kukarabati reli katika maeneo yale ambayo tunajua yana shida kubwa hasa maeneo ya Kilosa pale Gurwe. Pale tuliweka bilioni 26.36 mwaka 2009-2012, lakini vile vile Serikali ya Marekani nao wametusaidia dola milioni 33 kwa ajili ya kununua vyuma vya reli vile, *slippers* au mataluma na sasa jitihada hizi tumesema hazitoshi, tunataka tuendelee sasa kuboresha reli ya kati ili iweze kubeba mizigo mizito zaidi kuliko ilivyo sasa, ndiyo maana tumeibua mradi mkubwa ambao tunataka sasa uweze kuhudumia kilomita 1661 kutoka Dar es Salaam, Isaka, Keza, Kigali mpaka Msonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu wa mradi huo umekwishakamilika, usanifu wa kina wa mradi huu umeshaanza, kwa hiyo matarajio yetu ni kwamba tukimaliza tunaingia katika *process* sasa ya kuweka fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, *TAZARA* hatukuisahau, tumepata dola pale 39.9 milioni. Lengo letu sisi ni kuboresha ile reli na yenyewe iweze kufikia mahali pazuri. Tunataka tuanze ujenzi wa reli mpya ya Tanga, Arusha, Musoma mpaka Kampala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuboresha reli hiyo mpaka Arusha tumeuanza mwaka jana na lengo ni kukamilisha jambo hilo mapema iwezekanavyo ili sasa tuunganishe nguvu za pamoja za nchi hizo ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa reli ya ukanda wa Mtwara; nalo hatukulisahau kwa sababu tumepata chuma, tumepata na makaa ya mawe pale Mchuchuma na Liganga. Kwa hiyo, sasa tumefanya upembuzi yakinifu. Tumepata fedha kutoka Japan kupitia *JICA* ili tuweze sasa kukamilisha ile reli ambayo tunajua itakuwa na manufaa

makubwa sana. Reli hii tunataka ituunganishie Bandari ya Mtwara mpaka Mchuchuma na Liganga ili tuweze kuwa na uwezo mkubwa wa kubeba ile mizigo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeibua Bandari mpya ya Bagamoyo makusudi kwa kutambua kwamba Bandari ya Dar es Salaam peke yake haitaweza sasa kukidhi fikra tulizonazo za namna sasa ya kuunganisha Tanzania na nchi zinazotuzunguka kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, pale Bagamoyo tumepata hekta 2518 na jitihada hizi tunadhani zitazaa matunda mazuri chini ya utaratibu wa *PPP*. Mtwara pale tumetenga hekta 2647 kwa ajili ya kupanua ile Bandari ili sasa tuweze kuingia katika ujenzi kwa njia ya *PPP* na njia zingine zozote ili kuwezesha meli kubwa ziweze kufanya kazi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwenye mawasiliano hapa nchini tumejitahidi, tumeanzisha mradi mkubwa mkongo wa Taifa ule na leo tunavyozungumza tumeshakamilisha kilomita 7560. Hii yote ni katika kuleta chachu kwenye uchumi na sasa hivi watu wameshaanza kuona, kwa taarifa tulizonazo hata bei sasa za simu kwa maana ya matumizi yetu inaanza kushuka, zile *tariff,* kwa sababu ya matumizi haya mazuri ya mkongo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeunganisha mkongo huu na Zanzibar na tunadhani nayo itatusaidia upande wa Zanzibar, lakini si hiyo tu, tunafanya jitihada kubwa sana ili tuunganishe nchi zote za jirani na mkongo huu wa Taifa kwa sababu una uwezo mkubwa na tutaweza vile vile kuwa ni chanzo cha mapato kwa upande mwingine. Kwa hiyo, jitihada zote hizi ni za makusudi katika jitihada za kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoweza kusema ni nini? Matokeo kwa mfano ya jitihada hizi mpya kwenye mkongo wa Taifa, ni ongezeko sasa la matumizi makubwa ya simu za mkononi na hizi zina faida kubwa. Sasa hivi jitihada hizi zimeongeza sasa watumiaji kutoka milioni 3,118,157 mpaka

milioni 27, 395,650, sawa na 61. Hii imetusaidia sasa kwa mambo ya *M-pesa*, kutuma kwa njia ya *tigo* na wananchi vijijini sasa wanaweza kupata huduma hii ya fedha kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa intaneti hatukusahau hata kidogo na yenyewe imetusaidia sana kuongeza watumiaji kwa sababu TEHAMA ni muhimu sana katika maendeleo ya uchumi. Watumiaji walikuwa 1,681,012 leo tuna watumiaji 7,519,078 ni jitihada nzuri, ni kazi nzuri tumeifanya, katika nchi yetu tunafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi 2013 uwezo wa kuzalisha umeme ni megawati 1438. Tumeweka lengo kwenye mpango huu tuende mpaka megawati 2780 hadi 3000 itakapofika 2015, ipo kwenye mpango na jitihada zote Waheshimiwa Wabunge wanajua nini tunajaribu kufanya.

Mheshimiwa Spika, Miradi mingine ambayo tumeibua ni pamoja na mradi wa Somangafungu ambao unatekelezwa na kampuni ya Kilwa *Energy,* utazalisha megawati 320.

Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine ni ule wa kufua umeme wa Mchuchuma wa kuzalisha megawati 600 na mradi wa makaa ya mawe wa Ngaka unaozalisha megawati 40. Sasa jitihada hizi kama ninavyosema ni kwa nia njema. Sasa hivi katika Wilaya 133, Wilaya 117 tayari zina umeme, tumebakiza kidogo, tutazikamilisha baada ya muda si mrefu na nyinyi mnajua manufaa ya umeme kwa maana ya Wilaya zetu ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kilimo tumejitahidi, wengi wanaona kama vile hakijazaa matunda mazuri; lakini siyo kweli, mimi natembea sana nchi hii, nimeona jitihada za kuongeza tija. Katika uzalishaji, nimeona sasa wananchi walivyochangamkia matumizi ya mbegu bora na matumizi ya pembejeo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinatia moyo

kwamba, huko tunakokwenda ni kuzuri na tunaweza tukafika mahali tukaondokana na njaa na tukamaliza mambo mengine yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata ule ukanda wa Kusini tulio uanzisha *SAGCOT,* lengo lake ni hilo. Walengwa wakubwa ni wakulima wadogo wadogo, lakini tunataka tuwaunganishe pamoja na wale wakubwa. Kwa hiyo, sasa hivi jitihada hizo tunakwenda nazo.

Mheshimiwa Spika, Benki ya kilimo tumeisema, lakini nataka niseme kwamba, benki hiyo tayari imesajiliwa na Serikali, tumeshateua Wakurugenzi wa Bodi wa muda na Mtendaji Mkuu wa muda ambao ni mwelekeo mzuri, tunafikiri tutakwenda vizuri pale tunapotaka. Tulichofanya sasa, tumetangaza nafasi za kazi za Watendaji Wakuu wa Benki hiyo, mtu yeyote mwenye uwezo atajitokeza ili aweze kushiriki katika zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi sana kusukuma suala la matumizi ya zana bora za kilimo, tulianza na matrekta madogo, nimehimiza sana maksai, baadaye tumepanda tumekuja kwenye matrekta makubwa na sasa hivi kilio ni kikubwa zaidi, maana sasa hivi matrekta makubwa na madogo hapa nchini, bado hatujafika tunapopataka.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaamini kabisa tutafika huko kadri muda unavyokwenda; maana jumla sasa hivi ni matrekta makubwa 8466 na madogo 4571. Kwa hiyo, ni jitihada ambazo zimetokana na msukumo mkubwa kwenye eneo hili. Kilimo cha umwagiliaji tumeongeza kidogo maeneo, lakini bado tunajua hatujafikia pale tunapohitaji.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vinaendelea kuongeza tija katika uzalishaji na hasa vile vikubwa tulivyovizoea Saruji, Bia, Karatasi, Sigara, vina mchango mkubwa sana. Sasa tunataka tujielekeze zaidi katika viwanda ambavyo vitatumia rasilimali ya ndani, hasa pamba kwa upande mmoja, lakini hata korosho hizi tungependa sasa zianze kubanguliwa hapa nchini. Kwa hiyo, jitihada hizi zote, zinaonesha kwamba,

Serikali hii, pamoja na mengine yote mnayoyasema, lakini tumejitahidi. Serikali makini, mahiri, ndiyo maana haya mambo mnayaona yanakwenda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kidogo juu ya hili la elimu, kwa sababu wakati mwingine tunafika mahali tunaona kama vile katika elimu yote sasa ni hakuna kitu, ni upuuzi, jamani upuuzi unatoka wapi na sijui mlitaka tufanye nini? Wananchi wanaongezeka, maana mwingine anasema bora hata tusingeongeza shule, tungebaki hivyo hivyo. Mimi sikubaliani naye, kwa sababu sidhani kama ni sahihi. Kikubwa ni kutazama changamoto zinazotokana na ongezekeo hilo, tuweze kuzijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi jamani, zimeongezeka kutoka shule 14,400 mwaka 2006 mpaka 16331 mwaka 2012. Wanafunzi wameongezeka kutoka milioni 7.9, mwaka 2006 mpaka wanafunzi milioni 8.3 mwaka 2012. Sasa ongezeko hili siyo dogo kwenye ngazi ya shule za msingi, ni wazi litakwenda *strain* kwenye mambo mengi, kwenye huduma za msingi, hakuna mashaka katika hili.

Mheshimiwa Spika, lakini tumefanya jitihada vile vile wakati huo huo. Mwaka 2005 tulikuwa na Walimu laki moja thelathini na tano na kumi na tatu(135,013), leo tuna Walimu laki moja themanini elfu mia tisa themanini na saba(180,987) mwaka 2012. Uwiano wa Walimu na wanafunzi ulikuwa Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 51 angalau tumefika mwalimu mmoja (1) kwa wanafunzi 46, tunataka tufike mpaka 40. Jitihada hizi zote ni nia njema kwenye ngazi za shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye sekondari tulikuwa na shule 1845 mwaka 2006, leo tuna shule 4528 mwaka 2011/ 2012, ongezeko ni kubwa tunakubali. Lakini ndugu zangu Wabunge, mlitaka tufanye nini hapa? Tubaki na shule 1845 za mwaka 2006 hizo hizo eti kwa sababu mkiongeza mtazaa matatizo ya elimu, hata kidogo, hatuwezi kwenda hivyo. Lazima Serikali muonekane mna nia njema ya kujaribu kusaidia wanafunzi hawa, wakati huo huo mfanye jitihada

za kweli kujaribu kupunguza matatizo yake, ndiyo kitu ambacho tumejaribu kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua idadi ya Kidato cha kwanza imeongezeka. Mwaka 2006 walikuwa laki moja na tisini na sita elfu mia tatu tisini na moja (196,391). leo tuna wanafunzi 517,993. Nani asiyejua kwamba, lazima kutakuwa na mzigo mkubwa. Inajulikana, lakini hatuwezi kusema tuache.

Mheshimiwa Spika, Walimu wakati huo na sisi tumejaribu kuongeza, walikuwa (23,805), leo tuna Walimu (65,586) mpaka mwaka 2012. Jitihada nyingine wenzangu wamesema, nini tunataka tufanye mwaka huu kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Elimu ya Juu. Jamani, mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada yanatolewa sasa katika Vyuo 34 vya Serikali na Vyuo 82 visivyo vya Serikali vyenye uwezo wa kudahili wanachuo 47,898 kwa wakati mmoja. Uandikishaji wa mwaka kwa mwaka kwa vyuo hivyo ni takribani wanachuo 43,258. Kwa hiyo, tunakwenda, ingawa inaweza ikaonekana kasi ya ongezeko la wanafunzi ni kubwa, lakini hatujapuuza jambo hili, hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vilikuwa 26 mwaka 2005, leo tuna Vyuo hivyo 46, yote hii ni katika kujibu tatizo ambalo ni la msingi, Serikali inalijua, kama mnavyolijua ninyi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, Rais alipoagiza tujenge Chuo Kikuu cha *UDOM* hapa Dodoma, ilionekana kama ndoto, alisema nataka wanafunzi 40,000. Tukasema eeh Mzee tutaweza? Akasema acha tujitahidi. Kwa hiyo, kazi inayofanyika pale ni kuongeza udahili mwaka hadi mwaka. Sasa matokeo ya hii ni nini?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005, wanafunzi wa Vyuo Vikuu walikuwa 40,719, leo laki moja sitini na sita elfu, mia nne themanini na nne (166,484) mpaka mwaka jana. Sasa

tunakubali kwamba wapo wanaobaki, lakini mkubali vile vile kwamba, tumeongeza wasomi, kutokana na jitihada hizi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tusingefanya hili nalo lisingetusaidia sana. Fedha za mikopo tumeongeza sana, mwaka 2005 tulikuwa na bilioni 56, mwaka huu tuna bilioni 326, yote hiyo ni katika kusaidia kuongeza idadi ya wanafunzi. Wanafunzi wanaopata mikopo nao wameongezeka, mwaka 2006 walikuwa 55,000, leo tunazungumza wanafunzi 98,772 mpaka mwaka jana wanaopata mikopo ya Serikali, yote hiyo ni kusaidia kukuza elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naweza nikasema mengi, lakini nia yangu hapa ilikuwa ni kutaka tu Waheshimiwa wajue kwamba, tulipoamua kutoa kipaumbele kwenye maeneo haya tulikuwa na sababu za msingi. Tulijua ndiyo maeneo yatakayotusaidia sana kuleta chachu ya maendeleo, ndiyo maana hata kwenye sekta ya afya hatukuacha. Ndiyo maana mnaona leo wanasema idadi ya vifo vya watoto wachanga na wale wa chini ya miaka mitano vimepungua sana.

Mheshimiwa Spika, hii imetuongezea vile vile fursa ya kuwa na watoto wengi. Idadi ya vifo vya akina mama na yenyewe inakwenda inapungua na yenyewe inatusaidia kuwa na watoto wenye afya njema kuliko ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, Maleria imepungua sana nchi hii kutokana na jitihada zilizokuwepo. Kwa hiyo, yote haya yana nia njema. Mheshimiwa Mbowe kauli yako ile ya kwamba, sisi huku hatuna weledi, hakuna nini na nini, kidogo ilinisumbua. Ndiyo maana Waswahili wanasema, mnyonge mnyongeni, lakini mpeni haki yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo kuhusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Mchakato. Nimejaribu kumsikiliza sana Mheshimiwa Mbowe na pengine hapa ndipo niseme kwa sababu kwenye hotuba yeke alipokuwa ameamua kukejeli vipaumbele vya Serikali na kutufanya sisi

hatuna weledi, akaamua kuja na vipaumbele vyake, kwa niaba ya Upinzani. Kwa hiyo, kipaumbele chake cha kwanza ambacho anasema tulitakiwa sisi Serikali tukifikirie ni Tume ya Mabadiliko ya Katiba na mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nikajiuliza, mimi nataka tuhangaike na uchumi, tusaidie watu waweze kupata uwezo mkubwa zaidi. Kwa hiyo, tujikite katika vipaumbele hivi kwanza. Akasema hapana, kipaumbele ambacho tulitakiwa tuje nacho hapa, ni Tume ya Mabadiliko ya Katiba na mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi ni sawa, naelewa hoja hii ni ya msingi, lakini nije hapa Bungeni nitumie muda wangu hapa, nazungumza juu ya jambo hili jambo ambalo tunaendelea nalo, tunalijua, matatizo yako wapi tunajua na tunaendelea, nikasema hapana. Nadhani Mheshimiwa Mbowe hapa pengine aliteleza tu, hakiwezi kuwa ndiyo kipaumbele ambacho kitatusaidia kukuza uchumi hapa nchini, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake amesema hivi, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imethibitisha haina weledi wa kusimamia mchakato huru usiofungamana na upande wowote. Tume ambayo imechaguliwa kwa utaratibu ambao wote tunaujua anasema haina weledi hata kidogo. Sasa nikawa najiuliza, jitihada zote tulizofanya zile, tumeweka mpaka Maprofesa, tena Profesa mmoja Baregu wa CHADEMA! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi kweli wote hawa hawana weledi wa kuweza kusimamia jukumu hili vizuri? Nikasema *okay* bwana, maana mtu ukipewa nafasi ya kusema sawa, lakini naomba tu niseme kwamba, kwa mujibu wa sheria ile iliyopitishwa ndani ya Bunge, tulifanya jitihada nzuri sana. Kujaribu kuona Tume ile iundwe na wajumbe wa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Siasa vilitoa majina

waliyoyaona yatafaa, Jumuia za Kidini zikatoa, Asasi za Kiraia zikatoa, Taasisi nyingine Zisizo za Serikali, wakatoa. Ndani ya hilo ndiyo tukapata lile kundi ambalo nasema ni kundi nzuri, la heshima na ambalo kwa kweli linastahili kupongezwa na wala siyo kubezwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulijitahidi sana, tukasema ndani ya kundi hili la wajumbe wa Tume tuchukue na Wazee na vijana kutoka Zanzibar, kwa makusudi tu kwa sababu huu ni Muungano. Lakini inaonekana kidogo tabu, hawa wote hawana weledi, mbumbumbu wale eeh, jamani! Hivi kweli Timu hii, akina Mzee Warioba, akina Salim, akina Beregu, ijui akina nani! Hivi kweli hawa wazee ni mbumbumbu kiasi hicho! Hapana. Mimi nafikiri tuwatendee haki wazee hawa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili anasema, Tume kutokuwa na nia na dhamira ya kusimamia Mchakato huru wa Katiba. Anailaumu kwa kutokuwa na dhamira ya kusimamia mchakato huru wa Katiba. Labda! Lakini sheria hii tumeitunga, Wazee wale wanajitahidi kufuata sheria ile mliyoitunga kwa kadri mlivyokuwa mmeelekeza, hakuna jipya pale walililoliongeza hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kama ni hadidu, ziko kwenye sheria. Hata mfumo wa namna ya kutenda upo kwenye sheria. Sasa ili mradi sheria ile ilitungwa na Bunge hili; tusihamishe lawama hii kupeleka kwenye Tume ambayo kazi yake ni kutekeleza matakwa ya sheria ya Bunge hili, hapana. (M*akofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaposema hawana dhamira ya kweli, kwa kweli tunawavunja moyo na sana tunawakatisha tamaa. Watu ambao wamejitahidi sana kuzunguka nchi nzima, kwa nia njema ya kujaribu kuleta kitu, ambacho tunadhani kitaweza kuwasaidia Watanzania huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kwamba, Wazee hawatakatishwa tamaa na kauli ya Kiongozi wa Kambi wa Upinzani. Kama kauli ile ni kwa niaba ya wenzake, wala msikatishwe tamaa na wenzake na Mheshimiwa ambaye ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, badala yake, tendeni kazi yenu, timizeni wajibu wenu. Naamini wapo Watanzania wengi nyuma yao, ambao wanaona kazi ile inakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbowe anasema, Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba yaliyokusudiwa yanaelekea kuilinda CCM na Serikali yake na kuendeleza baraka za *Status quo*. Nikasema wapi na wapi! Hivi kwa mjumuiko ule wa Wazee waliomo kwenye ile Tume, unasemaje hili? Yaani zile Asasi zilizomo mle za Kiraia, wale Wazee wa Madhehebu ya Dini, wale Viongozi wa Vyama mliotuletea pale ndani, wale wote *is nothing*. Wale wote sasa ni CCM, aaa wapi! Wapi na wapi! Siyo kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani hili jambo jamani hebu tulitendee haki, tusianze kuwafanya Watanzania, waanze kukata tamaa, waone kwamba kweli jambo hili pengine halina maana, hata kidogo! Nadhani tuwatendee haki Watanzania, jambo hili ni jema, tuendelee nalo kwa nguvu zetu zote, tuhakikishe linakwenda mpaka tufikie mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema ndugu zangu, mchakato mzima huu ni mrefu, bado mtakuwa na Bunge hili la Katiba. Humu ndani Wabunge wote hapa ni wajumbe, toka Zanzibar tuna Baraza la Wawakilishi. Hivi tunaanza kusema haya kwa msingi gani? Ama ni hofu tu, sasa kama mmeingiwa na hofu hilo ni jambo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu niliposoma *speech* yote ya Mheshimiwa Mbowe, unaona kabisa akili zake zote

ni Uchaguzi wa mwaka 2015, ndiyo tatizo kubwa liko pale, mwaka 2015, ndiyo! Kwamba pengine tukisema hili itatusaidia, tukijaribu hivi litatusaidia, hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbowe anasema, eti Tume haikuwa na utaratibu madhubuti wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala yote yanayohusu Katiba Mpya na kwamba haikutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuandaa kuchangia maoni yao kwa Tume ya Katiba. Nikasema sawa, lakini wamesoma ile sheria, wakajaribu kuitafsiri, ndiyo maana wakaja na kila mbinu, wametumia vyombo vya habari, redio, runinga, magazeti, wametoa machapisho, wamejaribu kuchapisha hata Katiba ile, ile sheria wameitafsiri kwa Kiswahili na Kiingereza, wakaisambaza, hadidu za rejea wamezisambaza. Wamejaribu kuonesha majukumu ya Tume yenyewe ni yapi na mambo mengine chungu nzima.

Mheshimiwa Spika, yote yale ilikuwa ni kusaidia umma kwa upana wake waweze kupata kile ambacho Tume inataka wajue na namna watakavyoweza kuifanya hiyo kazi vizuri zaidi. Siyo hivyo tu, usambazaji wala haukuwa Bara tu, tumekwenda mpaka Visiwani, tumefanya hiyo kazi. Tumepeleka Makabrasha haya yote, tumieni redio kadri mtakavyoweza.

Mheshimiwa Spika, sasa aliponikuna zaidi Mheshimiwa Mbowe ni pale aliposema, eti mfumo ule wa Kenya ni mfano mzuri kwetu. Nikasema hata kidogo, haiwezekani! Kwa sababu wale mchakato wao ulikuwa na hatua kubwa mbili; kutoa elimu ya Katiba na pili kwenda kwa wananchi kukusanya maoni.

Mheshimiwa Spika, sisi kwenye Sheria ile tuliyotunga hapa ina hatua karibu nne; Elimu, ilikuwa kwenda kwa wananchi kukusanya maoni, iko kurudi, liko Bunge, bado mwishoni kule mtakuwa na kauli, kwenda kwa wananchi tena

mnapiga kura kama ni ndiyo au hapana, vitu ambavyo sehemu nyingine hawakuwahi kufanya.

Mheshimiwa Spika, sasa nikasema pamoja na mengine yote ambayo tunajaribu kukosoa, lakini nadhani katika hili hapana; lazima tujione kwamba na sisi ubunifu wetu kwa mujibu wa Sheria hii haukuwa mbaya kiasi ambacho tunataka tuwafanye wananchi waone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alifika mahali sasa akatoa tishio la kuitisha maandamano nchi nzima ya kuwataka wananchi wagomee huu mchakato au hii Katiba, nikaogopa kweli! Nikasema, kweli tulikuja hapa kwa nia njema, tukakubaliana kwamba tutaungana mkono katika jambo hili jema, tuhakikishe tunafika mpaka mwisho. Hivi katika hatua tuliyonayo hapa, mnataka kwenda kuwataka wananchi waandamane kwa lipi hasa? Wakati bado fursa za kutaka kurekebisha na kufanya yale yote yanayotakiwa kufanyika ipo kubwa tu.

Mheshimiwa Spika, sioni ndani ya Bunge hili ni namna gani tutakuja kukaa hapa, CHADEMA mkubaliane na yale mnayoyaita ya CCM bila ubishi hapa, sioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani bado tunayo nafasi kubwa ya kujaribu kuona kila linatakalowezekana ili tuweze kufanya inavyotakiwa. Sasa nataka niwasihi Watanzania wenzangu, haya mambo ya kuja kuambia sijui mkaandamane, hapana, kataeni ninyi wenyewe, msikubali; ndiyo akili za kuambiwa, lakini changanya na zako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbowe anasema Tume kutokuwa huru au kutafsiri uhuru vibaya na kutoa taarifa zake kwa Mheshimiwa Rais, haaa! Nikasema jamani! Mambo mengine haya tujaribu kidogo kuwa na stahimili. Mwezi Desemba mwaka jana, Mwenyekiti wa Tume hii ya Mabadiliko ya Katiba aliongea na vyombo vya habari, katika kuongea alijaribu kueleza na akatoa hata ratiba ya mpangilio wa mambo yalivyo, wala ratiba ile si siri hata kidogo, ukisoma kwenye Sheria ile utaiona ratiba inajiseti yenyewe. Rais mwisho wa mwezi alichokuja kufanya kwa kuamini kwamba umma mkubwa unamsikiliza kila mwezi, akaamua kurudia ile ratiba ili Watanzania wote waone kitu gani kinakuja. Mheshimiwa Mbowe anasema hapana, hizo ni njama, za Serikali hii na Tume, mimi nikasema njama gani hapa! Hakuna njama yoyote, alichokuwa anakifanya ni kitu cha kawaida kusaidia wananchi wajue, Tume ile itafanyaje kazi, si siri, kwa hiyo, ni vizuri wakajua ni nini kinakuja mbele yao. Sasa kumshtaki Rais kwamba yeye katika kufanya hivyo basi kuna Agenda ya sirisiri na Tume, mimi nikasema hapana, mimi nadhani hatukumtendea haki hata kidogo. Kusema kwamba Tume inatoa taarifa zake za utendaji kwa Rais na Serikali tu, siyo sahihi, bali taarifa inatolewa kwa umma wote, ndiyo maana Rais alifanya hivyo. Kwa hiyo, mimi nataka nimwombe sana Mheshimiwa Mbowe kwa hili nadhani tuwatendee haki Tume pamoja na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu alikisema, mimi nitakisema kwa kifupi sana, alisema Tume ya Mabadiliko ya Katiba kutowajibika kwa Bunge. Nilijaribu kuelewa alichokuwa anajaribu kusema ni nini, lakini nikasema hapana, mimi nadhani kwa upande wa Serikali tunadhani halikuwa jambo baya kwa Tume kusema hapana maana ndiyo kwanza tuko kwenye mchakato, unataka kuipeleka mbele ya Kamati katikati ya mambo wakati bado yanaendelea, tukadhani hili pengine isije ikaonekana tena kama vile Bunge mnataka kuanza ku-*detect* mambo ya Tume na nini na nini! Kwa hiyo, nikafikiri pengine ilikuwa ni busara nzuri tu, sidhani kama ni jambo la kuliwajibisha sana, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini stahili iliyotakiwa ilikuwa ni Waziri wa Sheria mwenyewe kumwita, kama kulikuwa na jambo lolote ajibu kwa niaba ya Tume pale waziwazi, kuliko Tume yenyewe. Ingekuwa ni jambo tofauti kama Kamati ya Bunge ingesema aaa, Mzee Warioba tunaomba tuje tukutembelee hapo kidogo tupate *briefing* na nini na nini, lakini mnapokuja kwenye Tume katika jukumu lake la kikazi, ni tofauti kabisa na hilo lingine. Kwa hiyo, inaweza ikaonekana kama pengine hawakutenda lakini nadhani kulikuwa na ile *element* ya unyeti kwamba mmh, sisi Waziri wetu si yupo, kwa nini asiulizwe kwanza huyo ili kupata majibu yote hata kama ikibidi kulala naye mpaka asubuhi. Kwa hiyo, nadhani jambo hili sikutaka sana tulisemee lakini ilikuwa ni kutokana na hiyo hali.

Mheshimiwa Spika, hasa limekuja hili la Mabaraza amabalo nadhani lilikuwa ndiyo tatizo kubwa lililojitokeza. Hapa ndiyo kuna mashtaka makubwa kwamba Mabaraza haya yamekaa ki-CCM, CCM hivi, lakini kama ni kosa basi ni kosa letu kama Bunge maana ndiyo tuliokubali katika hatua hiyo *Ward C* ndiyo zitumike.

**WABUNGE FULANI:** Sio kweli.

**WAZIRI MKUU:** Ndiyo, ndiyo, eee! *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Walikimbia.

**WAZIRI MKUU:** Ndivyo Sheria ilivyo sasa.

**WABUNGE FULANI:** Hapana!

**WAZIRI MKUU:** Ngoja bwana! Sasa tunabishana? Wenzangu wananiambia inawezekana siku hiyo hamkuwepo, sasa sijui. *(Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *anyway*, *point* yangu kubwa ni nini hapa? Ni ile tu kwamba katika hatua hii ya Mabaraza, tulichokuwa tunatafuta ni watu watakaoweza kwenda kujumuika katika kutazama maoni ambayo tayari Tume

imeyakusanya, baadaye yatoke pale yaende sasa kwenye Wilaya, baadaye tuje kwenye Taifa. Kwa hiyo, mfumo ulioonekana pengine ni mzuri katika hatua hii ni ule wa kupata watu katika ngazi hiyo wa kwenda mbele. Sasa rai ilikuwa ni kwamba wangeacha wote waliojitokeza, waende kwenye mkutano mmoja kwenye Kata kule, wakapige kura za moja kwa moja, sijui, pengine ni mawazo mazuri lakini kiutekelezaji, inawezekana yakawa si rahisi sana. Kwa hiyo, mfumo ule kwa sababu ndiyo tunaoutumia kwenye Serikali za Mitaa na kwenye *Ward C* ndiyo unakuta kuna Wenyeviti wote wa Serikali za Vijiji, ndiyo maana inakuwa nyepesi kuiona hivi. Sasa inawezekana kweli, kama alivyosema ndugu yangu Mbowe, kwamba Li-CCM hili lina Wenyeviti wa Vijiji wengi, ambalo ni jambo zuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hilo hatuwezi kulaumu mtu, ndivyo jamii ilivyoamua, kwa niaba ya walio wengi, hatuwezi kui-*condemn* hiyo *system* kwa sababu hiyo tu, hapana! Kwa hiyo, mimi nikafikiri jambo hili, ni kweli inawezekana ikaonekana pengine lina kasoro kasoro hivi, lakini mwisho wa yote ni ile tu kwamba bado tuna mwanya mkubwa sana mbele ya safari, namna tutakavyoweza kurekebishana ili tuweze kufika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume kukataa kubadilisha muundo wa Mabaraza ya Katiba hata baada ya kupewa maoni ya wadau. Sasa, sina hakika lakini mimi naambiwa CHADEMA haikutoa maoni yake kwenye Tume...

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI MKUU:** Ngoja ngoja, ngoja, kuhusu Mwongozo uliokuwa umetolewa. Maana walichofanya Tume, walitoa Rasimu ya Mwongozo kwanza, wakataka wapate *comments*, CHADEMA hawakufanya hivyo, badala yake ilikuja ikatoa maoni yake katika Mkutano wa hadhara baada ya Mwongozo kuchapishwa na kusambazwa. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)*

**WAZIRI MKUU:** Sasa kama hivyo ndivyo ilivyokuwa basi tusilaumiane, ni kwamba kulikuwa na *opportunity* pengine ya kuweza kufanya marekebisho, lakini pengine hatujayatumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Marekebisho ya Katiba imefanyiwa marekebisho mara moja tu kinyume na makubaliano ya CHADEMA na Mheshimiwa Rais. Tarehe 10 Februari mwaka jana, ndipo Sheria yetu ilipopitishwa na Bunge hili, tukaja tukafanya marekebisho baadaye, baadaye Mheshimiwa Rais akaridhia, baada ya marekebisho hayo, ndiyo Rais akateua ile Tume ianze kazi yake na ilianza mwezi Mei. Marekebisho yaliyofanyika wakati ule yalitokana na maoni kutoka Serikalini pamoja na wadau wakiwemo vyama vya siasa, CHADEMA walishiriki, CUF walishiriki, NCCR walishiriki, katika hatua ile ya mwanzo wote walishiriki. Katika majadiliano yaliyojitokeza, wakakubaliana na Serikali kwamba Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yafanywe kwa awamu tatu, awamu ya kwanza ilihusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba na masuala mengine yanayohusiana na nayo, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kupata Wajumbe wa Tume na kuruhusu wanasiasa kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume. Vilevile ilikubaliwa kuwa, awamu ya pili ya marekebisho, itahusu Bunge maalumu la Katiba pamoja na masuala yote yanayohusiana nayo. Halafu ile ya tatu ndiyo tuje tutazame sasa suala la kura za maoni.

Mheshimiwa Spika, hasa jambo hili tumelifanya, kilichotokea ni nini? Katika awamu hii ya pili, mwezi Januari, CHADEMA, CUF, NCCR, waliwasilisha maoni yao kwa maandishi. Kati ya tarehe 4/3/2013 na 8/3/2013, CHADEMA, CUF na NCCR Mageuzi wakakutana na Serikali, *AG* alikuwepo, Lukuvi alikuwepo, wakazungumza na ilikuwa inahusu sasa awamu hii ya pili. Wamezungumza vizuri na CHADEMA walikuwa na maeneo 16 ambayo waliwasilisha, NCCR Mageuzi maeneo 16, CUF maeneo 15 na yote yalichambuliwa vizuri kwa utulivu, wote kwa pamoja, mwisho wakakubaliana waliyokubaliana na sisi tukasema basi haya sasa tunayaingiza kwenye Muswada ambao matumaini yangu ni kwamba tukipata nafasi Bunge hili tutaingiza

angalau usomwe kwa Mara ya Kwanza. Sasa kwamba ni mara moja tu kulitokana na makubaliano yaliyojitokeza katika majadiliano ya awamu ya kwanza, sasa tumekamilisha tena kwa pamoja, tunabakiza awamu ya tatu ambayo itakuwa ni ya kura za maoni. Kwa hiyo, mimi nadhani hakuna jambo hapa ambalo hatujaweza kulitekeleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa kulikuwa na maeneo ambayo yalikuwa na maneno maneno kidogo, moja ilkuwa ni ile idadi ya watu 166 na vilevile suala la Rais kushauriana na Rais wa Zanzibar, wenzetu walikuwa wanaonyesha kwamba hakuna sababu, hapa ipo sababu kwa sababu ni Muungano na lazima hawa watu wawemo, lazima washauriane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakaja na wazo lingine kwamba hawaoni kwa nini Baraza la Wawakilishi na wenyewe waingie kwenye Baraza lile hapa, tukasema aah, aah, kwa nini? Walijaribu kutoatoa hoja, lakini baadaye wakasema aaah, unajua, Baraza la Wawakilishi likija hapa, litazidi kuongeza sasa idadi ya CCM na CUF, nikawaambia wala haina sababu hata kidogo, kwa sababu mwisho wa yote ni lazima mpate *Two-third* huku na mpate *Two-third* upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, ile ni ushirikishwaji tu kwa maana ya mfumo wetu wa Muungano ulivyo, ndiyo maana tukasema hapa hakuna kilichoharibika, tunakwenda vizuri, nadhani ni vizuri Watanzania wakaliona hilo na mimi naamini tutafika salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamesema hakuna Sheria inayompa Mheshimiwa Rais Mamlaka ya kuitisha upya Bunge Maalum la Katiba na kulielekeza kuboresha masharti ya Katiba Mpya. Tumejaribu kupitia na wenzangu pale, tukasema mmh, mbona Sheria yenyewe mliyoitunga hapa inavyo vifungu vinavyomwezesha Rais kuyafanya haya? Tatizo liko wapi? Kwa hiyo, tukasema hili nalo ni suala tu la kuangalia, kama pengine maneno hayakukaa vizuri, liangaliwe, lakini kwamba hakuna mamlaka, hapana, mamlaka yapo, isipokuwa tu labda kuboresha kama kuna haja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, haijulikani uhalali upi wa kisheria utakaoiruhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi kusimamia na kuendesha kura ya maoni. Mimi nasema wakati mwingine ni kusoma tu hizi sheria vizuri, tuzisome, mkizisoma vizuri sidhani kama liko tatizo ambalo linajaribu kuonyeshwa pale kwamba lipo, sidhani, lakini kama lipo ndiyo maana tunasema litachukuliwa sasa pengine katika Muswada tutakaouleta ule wa Kura za Maoni, ili kama kutakuwa na mahali pa kuboresha, tuweze kuboresha hivyo kwa kadri itakavyo wezekana.

Mheshimiwa Spika, niliona niyaseme haya kwa sababu kwenye hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani yapo mambo mengi lakini nimeona angalau nichukue haya machache. Kengele bado inaniruhusu?

**SPIKA:** Eee, una dakika 10.

**WAZIRI MKUU:** Bado kidogo, haya!

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo tu kuhusu hili la elimu siyo kipaumbele cha Taifa kwa CCM na Serikali yake. Haya ndiyo alisema Mheshimiwa Mbowe, ndivyo alivyosema, alisema siyo kipaumbele na hapa mtakumbuka ndipo alipotumia na ile *quotation* ya Rais mmoja wa zamani sana huko nikasema eeeh, hivi unakwenda kote huko kwa jambo lililowazi hivi! Jambo liko *clear*, jitihada zimefanyika, changamoto zake zinajulikana, kuona tunafanyaje kuzitatua. Sasa mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, katika bajeti za Serikali za nchi hii, tangu mwaka 2006 mpaka leo tunavyosema hapa, sekta ambayo imekuwa ikipewa bajeti kubwa kuliko zote, ni Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulianza na bajeti ya shilingi bilioni 669.5 mwaka 2005/2006 mpaka mwaka jana walikuwa na shilingi trilioni mbili, bilioni mia nane na tisini, wao ndiyo waliokuwa wanachukua sehemu kubwa kabisa ya bajeti. Tatizo hapa jamani, ni changamoto zilizomo ndani ya sekta yenyewe, ndiyo maana fedha zile zinaonekana kama vile hazitoshi, lakini pili, ni uchumi wenyewe ambao tunajaribu

kuhudumia kuhudumia sekta hizi zote, bado mdogo na hiki kiasi ni kikubwa, mnaona ninyi wenyewe kilio kinavyojitokeza tukija hapa, kila Kamati inasema sekta hii inahitaji fedha zaidi, sekta hii inahitaji fedha zaidi, lakini unatoa wapi? Hichi tulichofanya ni makusudi, katika kujaribu kujibu matatizo ya Sekta hii ya Elimu. Sasa, nimeshatoa takwimu za kutosha kuonyesha tulikotoka, namna tulivyofanya kazi na kwa hiyo, tukafikiri yale yanatosha.

Mheshimiwa Spika, sasa tumepata lawama kidogo Serikalini kwamba, hivi wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, uliunda ile Tume hasa kwa ajili ya nini? Matatizo mbona unayajua? Ilikuwepo Tume nyingine iliundwa, kabla hujamaliza hiyo unakuja na jipya, sawa! Ni kweli tuliunda, tuliunda Kikundi Kazi, kilitokana na Watumishi ndani ya Serikali. Hatukuwa tumepanua wigo kwenda kwa watu wengine ambao ni wadau wakubwa katika Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilikuwa ni Kikundi Kazi, kilifanya kazi nzuri, mambo waliyoyasema na tukaanza kuyafanyia kazi. Lilipotokea hili baada ya kuona jitihada hizo zote hazizai matunda, tukasema hapana, inaonekana kuna tatizo hatujalijua, lakini kilichotusukuma zaidi, ni baada ya kuona kwamba katika kushuka, tulifikiri ni shule za Serikali tu, lakini hata shule za watu binafsi, mashirika ya dini, sekta binasfi, hata zile zilizokuwa zina-*perform* vizuri sana na zenyewe vilevile zikashuka. Tukasema, hata kidogo, lazima kuna jambo lingine ambalo hatujalijua vizuri. Ndiyo maana safari hii mtaona tumeingiza kweli wataalam kutoka Serikalini, kwenye Vyuo Vikuu, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, tukaona tuingize na Madhehebu ya Dini, tumeweka Chama cha Walimu mle, tukaona tuweke na Sekta binafsi na Muungano wa Walimu tukasema na wenyewe tuwaingize mle, Wakuu wa Sekondari, ili watusaidie kuweza kubaini hasa hasa, kwa nini sasa si Serikalini tu lakini hata Sekta binafsi na Mashirika ya Dini yote sasa safari hii yameshuka. Ndiyo maana tukasema pengine busara nzuri iwe ni hiyo, tukiamini kwamba safari hii wigo umepanuka, itatusaidia zaidi kuweza kubaini mambo yalivyo. Tumemchukua *Professor* Mchome atusaidie kusimamia ile Tume, matumaini yangu ni kwamba watakuja na mambo

mengi ambayo yatatusaidia pengine kuweza sasa kulipa jambo hili umuhimu stahiki na tuone namna gani tunaweza kufanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, niliona kwa hili niseme kwa kifupi tu kwa sababu ya jambo hili lilivyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, sasa kumekuwa na rai kwamba na hili limerudiwa sana na wengi tu, kwamba, hapana, ilitakiwa kwa kweli Mawaziri na Katibu Mkuu wajiudhuru, haikutosha, mwingine akasema hata Waziri Mkuu mwenyewe na yeye vilevile ajiudhuru. Mimi nasema, kubwa hapa ni moja tu, unaweza ukamwajibisha rafiki yangu Kawambwa, lakini kama hujapata kiini cha tatizo hili hasa imehusisha maeneo yote mawili, shule za umma na za binafsi, utakuwa bado hujafanya kazi ya kutosha. Hawa watawajibika, lakini kwanza tujue kiini ni nini, kama ni uzembe, *fine,* lakini katika mazingira tuliyonayo, ni lazima kwanza tujiridhishe tuone hasahasa chimbuko lake ni kitu gani. Tukifika wakati huo mzuri tutaweza kabisa kuona nini tufanye kwa pamoja, kama kwa kuwajibishana tutawajibishana tu kwa sababu hilo si tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na rai kwamba, ushiriki wa wanafunzi wa elimu ya juu katika siasa unaonekana kuipendelea CCM. Msingi wake Mheshimwa Mbowe alipokuwa anazungumza anasema kwa nini mmeanzisha kitu kinaitwa Mkoa wa Wanafunzi? Sasa si kila chama kina mbinu jamani! Hii inawezekana ndiyo mbinu ya Chama cha Mapinduzi katika kuvuta hisia za wanafunzi kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachokataa sisi ni watu kwenda kufanya shughuli za chama chochote ndani ya vyuo vyenyewe kama ambavyo Mheshimiwa Mbowe anavyopendekeza, hilo tumesema hapana. Kwanza nani asiyejua, pale chini pale si mna ofisi ya CHADEMA ya wanafunzi pale! Hakuna anayenung'unika na sehemu nyingine nyingi tu na sisi tunazo ofisi za namna hiyo, sababu wale wanafunzi huwezi ukasema ni nje kabisa ya mfumo wa vyama hivi, hapana, wamo kwenye vyama, tunachokataa visiende kuathiri masomo yao, kwa kuendesha shughuli ndani

ya vyuo vyenyewe. Kwa hiyo, mimi nadhani hili ni jambo ambalo tulitazame kwa nia njema, lakini tusiende kuwavurugia taratibu zao pale ndani.

Mheshimiwa Spika, hili la mikopo kwa wanafunzi bahati nzuri nimelieleza pale mwanzoni, nisingependa kuyarudiarudia, lakini nataka niseme moja tu kwamba, tunafanya jitihada sasa za kuboresha utaratibu wa namna ya kukusanya fedha ambazo ziko mikononi mwa wale ambao tumewasomesha kwa mikopo hiyo. Ni kweli kumekuwa kidogo na kutokuwa na kasi ya kutosha, lakini sasa tunafikiri tutafanya vizuri zaidi na hasa baada ya kuwa tutapata hivi mnaita Vitambulisho vya Kitaifa, nina hakika itatusaidia sana kuweza kufanya vizuri zaidi. Kkwa hiyo, chondechonde tuvute subira, tutaweza kuifanya kazi hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia, niseme hili sasa la utulivu na amani, CCM sijui inahusika, jamani tusiende huko! Maana wote tunajuana hapa, nani mwaka 2010 alikuwa anatumia sana udini kutaka apate uongozi, wanajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kubwa hapa ambalo nataka wote tukubaliane, tusije tukakubali kuingiza udini kwa namna yoyote ile katika masuala haya ya kujaribu kupata viongozi kwa kudhani ukiwa wa dini fulani, itakusaidia, haitakusaidia hata kidogo, haitakusaidia hata kidogo, hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania hawa, tupo Wakristo, Waislamu na Wapagani na wote ni Watanzania. Kiongozi anayetaka kuja kuongoza nchi hii ni lazima ukubali wote hawa ni watu ambao lazima uwaongoze kwa dhamira moja. Tusikubali hata kidogo kuingia katika mtego wa kutumia udini kwa namna yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niwasihi sana Watanzania kwamba kwenye hili tusije tukafanya makosa. Huyu atakayeingia kwa kofia ya dini moja ajue dini nyingine itahakikisha hatawali hata kidogo, hata kidogo! Suluhu ya

kweli tujitahidi tujiepushe na njama ya namna yoyote ile ya kudhani udini utakusaidia kukuingiza madarakani, utakuponza, hutaweza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na suala la uuzaji wa hisa za Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA).* Niseme tu kwa kifupi kwamba Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali alifanya kazi yake vizuri akaleta taarifa Serikalini, tukaichukua taarifa ile tukampa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akaturudishia ushauri vizuri sana na alipokuwa ameturudishia akashauri kwamba kwa mujibu wa sheria ambayo anaitumia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anayo mamlaka ya moja kwa moja ya kuwezesha kuanzisha mashtaka kwa mtu yeyote ambaye ameona matendo yake ama ya kirushwarushwa au ni ya kiwiziwizi na ndicho alichofanya. Kwa hiyo, baada ya kukamilisha ushauri ule basi tukaamua sasa hatua stahiki zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, miongoni mwa watuhumiwa waliofikishwa Mahakamani ni pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la UDA, Mzee wetu Idd Simba, wajumbe wa Bodi hiyo Bwana Bakari Kingobi na Bwana Salum Mwaking'anda na aliyekuwa Meneja Mkuu wa UDA, Bwana Victor Milanzi. Hawa wote walifunguliwa mashtaka Mahakamani. Sasa kesi ile namba 137 ya mwaka 2012 inaendelea na kesi imeshaanza kutajwatajwa na sasa hivi nimearifiwa kwamba tarehe ya kusikilizwa ni tarehe 29 na 30 mwezi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamekuja na jambo hili kwamba katika mazingira tuliyonayo kwa vile lipo Mahakamani tayari na watu wameshafikishwa Mahakamani basi tufanye subira badala ya kuingiza mjadala huu humu Bunge tusubiri tuone Mahakama hiyo itakachofanya ni nini.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya wafugaji na wakulima, jambo ambalo limejitokeza sana. Ni kweli lipo tatizo kubwa katika eneo hili na ni changamoto moja kubwa sana. Tuna ongezeko kubwa sana la mifugo kama lilivyo ongezeko

la binadamu. Kwa hiyo, iko kazi kubwa sana ya namna ya kuwezesha makundi yote mawili kuweza sasa kutumia ardhi tuliyonayo, maji tuliyonayo na majani au malisho yaliyopo. Kwa hiyo, changamoto ni kubwa lakini mimi nataka nitumie nafasi hii kuwaomba sana Watanzania kwamba kwa vyovyote vile kwa kiasi kitakachowezekana kuvumiliana sana. Wafugaji hawa ni Watanzania kama sisi, ni kweli wana tatizo la kuwa na mifugo mingi lakini ipo leo mifugo hiyo na wala sidhani kama kuna mtu atakuja atasema tuichinje ndiyo tuipunguze, hata kidogo kwa sababu haitawezekana. Kwa hiyo, tunachohitaji hapa ni kukaa chini kwa pamoja ili tuone ni namna gani tutasaidia kundi la wafugaji liweze kufika mahali lione namna ya katumia rasilimali hiyo katika kupambana na kujiwezesha kiuchumi. Upande mmoja wa Serikali tutasukuma sana viwanda hasa vya ngozi na nyama kwa sababu ni njia mojawapo lakini upande wa pili ni lazima tuwe vilevile na mfumo wa kuwezesha mifugo kuuzwa hata kama ikiwa ni nje ili mradi iwawezeshe kupata uwezo wa kifedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwaombe sana vyombo vile vinavyohusika na eneo hili yaani Wizara ya Mifugo na Uvuvi mchukue jambo hili kwa uzito unaotakiwa, tuwasikilize wafugaji na tuwasikilize na wakulima tuone namna gani tutawasaidia. Nimepata faraja sana leo kwa sababu nimekutana na wawakilishi wa wafugaji Kanda ya Ziwa wanne. Walichokifanya kizuri wameamua kuanzisha Chama cha Wafugaji Kanda ya Ziwa, wameshasajili tayari. Sasa naamini tumepata chombo ambacho tunaweza tukakitumia kuzungumza kwa pamoja. Kwa hiyo, nimewaasa kwamba basi tutapata muda ili Wakuu wa Mikoa, wawakilishi wa wafugaji hao, Wabunge wanaotoka kwenye Mikoa yote ya wafugaji tukae pamoja ili tujaribu kulitazama hili jambo kwa nia njema ili kama hapana budi kama alivyosema Mheshimiwa Prof. Tibaijuka yale mashamba ambayo hayana watu au *ranch* zile tuone kama mkiwa na chombo kama hiki tungeweza polepole tukaanza kuchukua makundi haya kuyaingiza kwenye mashamba kama hayo, tuyatengenezee utaratibu mzuri ili waweze na wenyewe kubadili mfumo wao

wa ufugaji kwa kadri itakavyowezekana. Mimi nadhani jambo hili ni la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka Wakuu wa Mikoa hebu hakikisheni hata pale mnapojaribu kufanya *operation* yoyote simamieni jambo hili vizuri. Zipo taarifa za uhakika kwamba baadhi ya watumishi kule wanatumia mwanya huo kujitajirisha kwa kiasi kikubwa sana, ndiyo! Wanaomba pesa, wanapewa haziendi Serikalini bali zinakwenda mfuko, hatuwezi kwenda namna hiyo hata kama mlikuwa na nia ya kuwaondoa kwenye maeneo ya hifadhi lakini msitumie fursa hiyo kujitajirisha au kujipatia fedha kwa njia ambazo si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile *operation* iliyofanyika Biharamuro kwa sababu kuna watu pale ambapo yapo maelezo ya kuonyesha kabisa kwamba wamepokea fedha kutoka kwa wafugaji kinyume kabisa na utaratibu, nimewaambia Mkuu wa Mkoa lazima achukue hatua zinazotakiwa dhidi ya wale wote ambao wamehusika na jambo hili. Hatukuwatuma kwenda kufanya hayo, tuliwatuma wakishachukua hatua wapeleke watu wanaohusika kwenye vyombo vya sheria ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Kwa hiyo, nadhani hili tutahakikisha kwamba linafanya kazi kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Bodaboda nimelisikia na limenisononesha na mimi kwa sababu sikujua kwamba kumbe tunapokubaliana hapa vitu vingine haviendi kufanya inavyotakiwa. Nimeshamwambia Mkuu wa Mkoa atupe taarifa tuone kumetokea nini mpaka imetokea hivyo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Kahawa upande ule nadhani Mheshimiwa Rais ameshalimaliza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI MKUU:** *Time* tayari?

**SPIKA:** Ndiyo.

**WAZIRI MKUU:** *Ooh, sorry,* unajua ukinogewa hapa taabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba sasa nimalizie kwa kurejea kuwashukuru sana Washimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, tutafanya kila itakalowezekana kutekeleza yale yote mliyokuwa mmeyashauri na mimi naamini tutakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, Mwongozo!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) kuhusu jambo ambalo limetokea hivi punde.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majumuisho ya hoja hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo yasiyokuwa sahihi na yasiyokuwa ya kweli kuhusiana na suala la Mabaraza ya Katiba. Mosi, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba Bunge hili lilipitisha sheria ikieleza muundo wa Mabaraza ya Katiba kufanyika kwenye ngazi ya Kata. Ukweli ni kwamba, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba iliyopitishwa na Bunge inachotamka tu ni kwamba Tume itaunda Mabaraza ya Katiba kwenye maeneo ya kijiografia, yatakayohusisha makundi ya kijamii. Hakuna popote kwenye Sheria iliyopitishwa na Bunge hili, hakuna popote kwenye sheria iliyopitishwa na Bunge hili ambapo sheria inasema...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalize.

**SPIKA:** Naomba mumsikilize!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hakuna popote kwenye sheria kulipotoa maelekezo ya Mabaraza ya Katiba kuundwa kwenye ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo yasiyokuwa ya kweli kwamba CHADEMA haikupeleka maoni yake kuhusu Mwongozo huu wa Mabaraza. Naomba kushuhudia kwako kwamba mimi ndiye nilikuwa Kaimu Katibu Mkuu wa Chama wakati wa upelekaji wa maoni kuhusiana na Mabaraza, tulipeleka na kuna ushahidi kwamba tulipeleka na maoni haya hayakuzingatiwa na badala yake Tume ikapitisha muundo ambao wajumbe wakichaguliwa kwenye ngazi ya Vijiji wanakwenda kuchujwa kwenye ngazi ya Kata ambapo CCM inahodhi kinyume kabisa na mfumo mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako, ni hatua gani tunaweza kuchukua pale ambapo majumuisho yanayotolewa na Waziri Mkuu yanakuwa yanatoa maelezo ya uongo tukizingatia kwamba huko nyuma tuliwahi kuomba Mwongozo mwingine na haujafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, tutatoa majibu kesho, kwa sasa mimi sina majibu.

Waheshimiwa Wabunge, naamini wote mna kitabu cha Kanuni kwa sababu sasa tunakwenda kwenye Kamati ya Matumizi, kwa hiyo, kuna mambo ambayo ningependa myafahamu na yazingatiwe.

Tukiwa katika Kamati ya Matumizi, unayo ruhusa ya kuweza kupata ufafanuzi katika kifungu kimoja kimoja. Sasa ukishapata ufafanuzi kwa mujibu wa Kanuni zetu hizi unaweza kuongea dakika tano lakini huna nafasi ya kurudia, mahali utakapokuwa na nafasi ya kurudia ni pale utakapotoa hoja ya kutoa shilingi. Yule mtoa hoja wa kutoa shilingi atakuwa na dakika tano, anaweza kuungwa mkono na wenzake wowote wale yaani wanaokubali na wasiokubaliana na hoja watachangia kwa dakika tatu. Baadaye Serikali itajibu lakini *onus* ya kujibu mwisho ni yule mwenye shilingi na *in case* ile shilingi yake imekubalika kwa maana itabidi niwahoji, ikikubalika basi fungu lile litakuwa linapita lakini halina shilingi moja. Iwapo litakataliwa basi tunaendelea na mtu mwingine anaweza kuhoji sehemu nyingine. Kwa hiyo, hii naomba muangalie.

Lakini kuna mabadiliko makubwa kuhusiana na mshahara wa Waziri. Siku zote na miaka yote hata Bunge la Tisa hata Bunge hili, tumetumia muda wetu wote kwenye mshahara wa Waziri, kwa hiyo unakuta hatuitendei haki kazi ya Kamati ya Matumizi kwa sababu tunaishia kifungu cha mshahara wa Waziri basi, hatupitishi maendeleo wala kitu chochote. Kwa hiyo, hii ilionekana ni udhaifu mkubwa sana katika uendeshaji kazi zetu. Kwa hiyo, Kamati ya Kanuni ikafikia mahali ikasema kwamba mshahara wa Waziri kama tunavyoutumia sasa inakuwa kama ni njia nyingine ya kuanza mjadala upya, kwa hiyo, kifungu kinasema utauliza swali linalohusika na sera. Kwa hiyo, Kamati tumeshakubaliana kwamba dakika zitakazotumika katika mshahara wa Waziri ni 25 na muda atakaouliza swali la kisera ni dakika tano. Kwa hiyo, tunaweza sana kupata wasemaji watano, watatu kutoka Chama Tawala na wawili kutoka Kambi ya Upinzani. Hivyo ndivyo itakavyokuwa. Kwa hiyo, naomba mzingatie hilo na itabidi tuangalie lakini itatuwezesha kwenda kwenye vifungu vingine mpaka vile vya maendeleo kwa sababu tutakuwa na muda ambao unatosha.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nategemea mnazo hizi Kanuni kwanza, nategemea pia mnavyo vile vitabu kwa sababu mnaweza kuwa mmekuja na kusema tu

ndiyo, ndiyo, kumbe vitabu vyenyewe havipo. Kwa hiyo, kwa kufikia hapo.

Jambo lingine ambalo naomba Mwongozo wenu, leo tuna mafungu ya Mikoa na Mikoa ipo mingi kabisa kama na yenyewe tutakwenda kifungu kwa kifungu basi itabidi mlale hapa na muda wenyewe hauruhusu. Uzoefu tuliofanya miaka yote tunapofika kwenye Mikoa tunasema fungu moja la Mkoa halafu tunalipitisha lakini kama kuna mtu ana jambo fulani katika eneo fulani basi atatuambia wapi tuangalie kwa sababu tukisema twende kifungu kwa kifungu kwanza muda wenyewe hautoshi na itabidi twende kwa *guillotine* lakini tukienda kwa mafungu inawezekana. Naomba tuendelee!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu**

Kif. 1001 *Administration and HR Management*... ... ... ... ... ... Tshs. 6,386,889,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

**MJUMBE FULANI:** Hatusikii!

**MWENYEKITI:** Husikiki!

Kif. 1001 *Administration and HR Management* ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 19,388,739,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kif. 1001 *Administration and HR Management* ... ... ... ... ... ... ... .. Tshs. 4,430,857,000/=

**MWENYEKITI:** Ndiyo mshahara wa Waziri! Mheshimiwa, Mariam Kasembe, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Barwany na Mheshimiwa Mwijage, tuanze na Mheshimiwa Mbowe!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuzuia mshahara au kutoa shilingi ili nijadili suala moja la msingi sana la kisera kuhusu Katiba.

**MWENYEKITI:** Dakika tano tu!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili nikijua umuhimu wa Katiba kama jambo la msingi na kipaumbele cha kwanza kwa Taifa lolote kwa sababu Taifa hili linaunganishwa na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yote ambayo tunaweza kuwa nayo iwe ya kiuchumi au kijamii kama hatujaweza kutambua utaifa wetu kwa pamoja kwa msingi wa Katiba, tunaweka msingi mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu wakati nikichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kweli nilizungumza Katiba kama jambo la *priority* na ni kwamba ilikuwa ni kipaumbele chetu na bado ni kipaumbele chetu na kitaendelea kuwa kipaumbele chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukatibu majeraha mangapi kama nchi kwa kuheshimu mkataba wa kitaifa ambao ni Katiba? Nililizungumza hili kwa niaba ya wenzangu nikitambua kwamba sisi kama Taifa tunahitaji kutibu makovu ambayo tunayo, tunahitaji kutengeneza mshikamano wa kitaifa, tunahitaji kujenga uzalendo na

tunahitaji kuwa wamoja na nilijua hili ni *process* inaweza ikapatikana kwenye Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukatumia wingi wetu ndani ya Bunge tukasema chochote tunachotaka kusema, tunaweza tukatumia nguvu na mamlaka tuliyokuwa nayo tukasema lolote tunalotaka kusema, tunaweza tukabezana sana kwa sababu tuna fursa ya kusema na hatuna fursa ya kutoa majibu ya kutosha lakini tunajenga mbegu gani katika taifa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubezana hapa na vijembe kuhusiana na masuala ya Katiba haya ni masuala ya msingi ya Taifa. Nasikitika sana kwamba tunapokwenda kuingia katika kubezana kwa sababu tu pengine wengine hawana fursa ya kuzungumza sana kama ambavyo Wabunge hapa ndani wanataka kulifanya, sisi kama Chama, kama wadau na sisi tunazungumza kwa niaba ya Watanzania wengine ambao ni kundi lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema mambo mawili tu ya msingi katika hotuba yetu pamoja na mengine mengi tukiomba rejeo ya mambo mawili ya msingi na tukasema hatutakuwa na uhalali wa kuendelea kushiriki mchakato huo na tuliimaanisha hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mawili tu tuliyataka hapa. La kwanza, tulisema utaratibu mzima wa Mabaraza ya Katiba umevunjwa na kuna ushahidi ambao haupingiki. Jambo hili limewagawa wananchi wetu ngazi za chini, tunataka kulilfungia macho, tuliburuze hili kwa sababu ya wingi wakati tunajenga ufa kwa wananchi wetu kule chini. Halafu tunasema hapa leo tunajenga Taifa. Tulisema sisi huu mpango ukiendelea hivyo tuwaachia nyie ambao mnataka kuendelea muendelee, hilo la kwanza. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Oooh!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na msimamo wetu upo hapo kwamba utaratibu wa

Mabaraza ya Katiba kama ulivyo leo ni kinyume cha utawala bora na sisi kama CHADEMA hatuukubali. Mabaraza haya hatuyakubali na ninatangaza tena tutajitoa kwenye mchakato wa Katiba mwisho wa mwezi kama jambo hili litapuuzwa.

**MBUNGE FULANI:** Jitoe mara moja.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tulizungumza kuhusu sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa...

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado muda ninao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbowe muda bado unao lakini suala ni moja.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala moja tu la Katiba na Katiba ina vipengele vingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbowe, hapana. Suala la Katiba umeeleza, sasa suala la kutunga sheria haliruhusiwi na kanuni inasema hivyo.

**MBUNGE FULANI:** Dakika tano!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sasa Waziri Mkuu atakuwa tayari kutoa kauli ya Serikali kwamba Mabaraza haya yanafuatwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Kasembe.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nipo kwenye mshahara huohuo...

**MWENYEKITI:** Watauliza maswali yote halafu Mawaziri watajibu.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye mshahara Waziri na ninataka kuzungumzia suala la kisera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri hapa alizungumzia sana kuhusu suala la korosho pamoja na mazao mbalimbali lakini na sisi katika michango yetu mbalimbali tuliiomba Serikali wakati wa majumuisho iweze kutueleza hatma ya mfumo wa stakabadhi ghalani utakavyokuwa katika msingi ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa, katika majumuisho yaliyotolewa hapa, sikusikia jambo lolote linalohusu mfumo huu wa stakabadhi ghalani na hatma ya uuzaji wa korosho katika msimu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoiomba Serikali, suala hili sasa hivi limekuwa ni kero ndani ya Bunge kwa sababu kila wakati sisi Wabunge tunaotoka kwenye Mikoa inayolima korosho imekuwa sasa ni wimbo wa Taifa kila siku tunalizungumzia suala la mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoiomba Serikali itueleze leo hatma ya mfumo huu wa stakabadhi ghalani na jinsi wakulima wetu watakavyouza korosho kwa msimu ujao? Kwa sababu majibu bado hatujayapata na vinginevyo kama sitaweza kupata majibu leo, wakati wa hotuba ya Waziri wa Kilimo, humu ndani hapatatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itueleze juu ya mfumo wa stakabadhi ghalani kama umeshindikana leo tueleze na kama kuna utaratibu wowote ambao Serikali imeuweka basi mtufafanulie leo ili na sisi tunavyoondoka hapa kurudi Majimboni kwetu, tupate jibu la kuwaeleza wakulima wetu ambao hadi leo hii wengine hawajauza korosho zao, wengine hawajapata fedha zao kupitia mfumo huu wa stakabadhi ghalani. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Suala langu ni la kisera na ninasimamia mshahara huohuo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi, Wabunge wote, kila mmoja ni shuhuda, kuanzia Kaskazini mpaka Kusini kila mtu amelalamikia maji lakini si kwa hapa tu hata kule tunakotoka maji hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia katika maandiko ya Serikali, unakuta kila kulipokuwa na tatizo la maji wanaelekeza nguvu kwenye *World Bank* na wahisani wengine. Mimi busara yangu inanituma, kwa nini Serikali msitafute majawabu kwa kujaribu kutenga vyanzo vya maji vilivyo vingi kuliko kutegemea wahisani. Maji ni uhai, inakuwaje uhai wetu sasa tunamwachia *world Bank, world bank* ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninazuia mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu mpaka nipate majibu kuhusu suala la maji. Nataka maji kwa nchi hii, maji nyumbani, maji Jimboni. *(Makofi)*

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi kama wenzangu waliotangulia najielekeza zaidi katika suala la kisera katika eneo hasa la uwezeshaji na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa tumekuwa tunazungumzia suala nzima la viwanda vya korosho katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani ambapo viwanda hivyo vilijengwa zaidi ya miaka 20 iliyopita. Hii ilikuwa ni hoja ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu hakutoa ufafanuzi katika majumuisho yake lakini amejikita zaidi katika kujibu hoja za CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya korosho ambavyo vipo katika mkopo wa Benki ya Dunia ambapo kwa muda mrefu viwanda hivi vimesimama havifanyi kazi. Mzigo mzima wa ulipaji madeni hayo unategemea sekta nyingine

siyo sekta ambayo viwanda hivi vilikusudiwa kujengwa. Kwa maana hiyo, deni la Taifa limeongezeka kwa ajili ya mkopo wa deni hili la ujenzi wa viwanda vya korosho katika Mikoa hii ambayo nimeitaja. Hivyo basi Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hoja yake amezungumzia suala nzima la soko la dunia, amezungumzia korosho ghafi ambako ndiko kunakopatikana majibu ya bei ya korosho katika maeneo hayo lakini makusudio ya kujengwa viwanda vile ilikuwa ni kufanyia *processing* ya korosho zetu ili tuuze katika soko la dunia bila kuuza korosho ghafi katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kufahamu, hivi viwanda mpaka sasa vipo mikononi mwa nani? Nani anamiliki viwanda hivi na tuna taarifa kabisa kwamba viwanda hivi sasa hivi vimekopewa fedha katika taasisi za fedha na fedha zilizokopewa katika taasisi hizo za kifedha hazikwenda moja kwa moja katika uwekezaji wa viwanda hivi na bado taasisi hizo ni taasisi za wananchi na viwanda hivyo bado vilichukuliwa vikawa mikononi mwa watendaji wakuu wa Serikali. Tumekwenda *BRELA* tumeona majina ya Wakurugenzi wa viwanda hivyo. Sasa tunataka Waziri Mkuu, atoe ufafanuzi wake hapa Serikali itakavikamata lini viwanda hivi, itavirudisha lini kwa Serikali ili wapewe wawekezaji wengine kwa ajili ya kufanya *processing* ya korosho hizi ili tuachane na mpango huu wa kuuza korosho ghafi na kuuza korosho ambazo zimefanyiwa uboreshaji ili tupate soko nzuri katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sote tunavyojua juu ya dhamira njema ya Chama kinachotawala kwenye Ilani yake ya Uchaguzi, tulibainisha kwamba lengo letu kubwa ni kuwatoa Watanzania kutoka katika uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuwapeleka katika uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu japo nilikuwa Jimboni kwa shughuli

zingine za mafuriko ya Jimbo langu na nimesoma sana hotuba yake na hasa ukurasa wa 46 kuhusu suala nzima la gesi asilia. Wabunge wa Bunge hili wanajua na Watanzania wanajua kwamba nchi yetu imegundua gesi asilia kiasi cha futi za ujazo zaidi trilioni 35 ambazo zikitumika vizuri zinaweza kulitoa Taifa letu kutoka hapa tulipo na kutufikisha mahali pazuri kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bahati mbaya sana wakati tunazungumzia haya hatuna sera, hatuna sheria lakini tumewapa watu leseni za kuchimba na kutafiti gesi na mafuta katika nchi yetu yanayoweza kujitosheleza. Ningependa kupata maelezo ya Serikali na kwa sababu ninamwamini sana Waziri Mkuu na ninamwamini aliyemteua ambaye ni Rais wa nchi yetu, sina haja ya mshahara wake kwa siku ya leo lakini nataka maelezo ya kina kwamba hatuwezi kuendelea kuchimba gesi kwa mikataba, tunahitaji kuchimba gesi baada ya kuwa na sera, baada ya kuwa na sheria itakayopitishwa na Bunge hili ambayo itabainisha na kuwaongoza watakaoingia katika mikataba kwa manufaa mapana ya nchi yetu na kuhakikisha kwamba Taifa hili linanufaika na gesi badala ya hivi sasa ambapo mashaka yangu yapo kwamba gesi hiyo wanaoichimba wanaweza wakanufaika zaidi. Nataka nijue ni lini watakamilisha suala la sera na lini wataleta sheria katika Bunge hili ili gesi hii ichimbwe kwa manufaa makubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mmejipanga namna gani kujibu suala la kwanza la Katiba, Mheshimiwa Waziri wa Katiba.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mheshimiwa Freeman Mbowe nafikiri ndiye aliyezungumza kuhusu suala la Katiba na akasema kwamba utaratibu wa Mabaraza ya Katiba ni kinyume na utaratibu na wao hawaukubali. Wao hawaukubali hilo ni jambo lipo wazi lakini utaratibu huu ikumbukwe kwamba uliwekwa na Tume ambayo tuliipa

madaraka sisi wenyewe chini ya kifungu cha 18(3). Tume tumeipa madaraka ya kuweka utaratibu itaendesha vipi mambo yake. Tume ikaweka utaratibu huu, ikatoa mapendekezo kwa umma kwamba tunataka kufanya utaratibu huu, umma wakapata nafasi ya kupeleka maoni yao kwa Tume. CHADEMA niseme tu labda maoni yao hayakubaliwa na Tume, lakini hicho ni kitu cha kawaida tu. Si kila oni unalopeleka lazima likubaliwe na siyo maoni yao pekee yao yaliyokataliwa, inawezekana wapo wengi walipeleka maoni yao na yakakataliwa. Haya yaliyokubaliwa na Tume ndiyo haya yaliyozaa Mwongozo ule na ndiyo unaotumika hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume tuipa kazi hiyo lakini pia tuipe uhuru na kinga kwamba isiingiliwe. Sasa Serikali haiwezi kuingilia Tume kwamba badilisheni utaratibu wenu, hapana, ndiyo kazi tuliyoipa na tumeipa kazi hii kisheria, imefanya hivyo. Sasa kwamba utaratibu huu ni mbaya huwezi kuingiza Serikali humu. Tumetunga sheria sisi tukaiambia Tume unayo madaraka ya kuweka utaratibu utaendeshaje mambo haya. Tume ikaweka utaratibu huo, ikaupeleka kwa wananchi, wananchi wakakubaliana nayo, imetoa sasa tunatekeleza, kama sisi hatukubaliani nayo basi tujaribu labda katika hatua zijazo kama alivyopendekeza Waziri Mkuu, tujaribu huko mbele yatakapokwenda Mabaraza haya kuketi, tupeleke maoni yetu zaidi huko, watakapokwenda kwenye Bunge la Katiba tupeleke maoni huko. Labda pia tutakapokuwa hatukubaliani na mengine yatakayopitishwa na Bunge la Katiba tupeleke maoni yetu kwenye *referendarum,* bado nafasi za kutoa maoni zipo na mnakaribishwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba hamkubaliani kwa hiyo mnajitoa, *well* kujitoa ni uamuzi na kama mmeufanya basi mmeufanya lakini mnaufanya uamuzi huo mkiwa mnazingatia kwamba tulipitisha sheria hii sisi wenyewe ndani ya Bunge, tukaipa madaraka Tume hii, Tume hii imefanya kazi yake kwa kuzingatia sheria ile na imekwenda zaidi, imekuja hata kuomba ushauri. Tulidhani ni jambo nzuri, Tume hii mnaijua, ina watu wengi, ina watu wenye heshima

zao, wamefanya kitu hiki kizuri. Mimi ningewashauri tu wakae tena waangalie upya waone nafasi yao katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na hoja ya pili ya korosho. Naomba wanaojibu wawe *brief* la sivyo tunalala hapahapa. Hoja ya korosho ni pamoja na soko na viwanda.

**WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja mbili za Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Barwany kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mfumo wa stakabadhi ghalani wote tunajua ulipoanza miaka miwili ya kwanza ulifanya vizuri sana. Baadaye ukaghubikwa na matatizo...

**MWENYEKITI:** Nyanyua *microphone* yako kidogo haisikiki.

**WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema wote tunajua mfumo huu wa stakabadhi ghalani ulipoanza ulianza vizuri mwaka wa kwanza na wa pili, ulikwenda vizuri wakulima walipata malipo yao kwanza, ya pili na hata majaliwa. Mpaka ulipoingiliwa na wale ambao waliona maslahi yao yameingiliwa wakaanza kuuchakachua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo hakuna kitu kizuri ambacho kinakwenda moja kwa moja hata *model* za kisayansi unapoziweka unazi-*test* kwanza, unaangalia zinavyo-*perform*. Sasa mfumo huu wa stakabadhi ghalani kama ilivyo mifumo mingine kama kilimo cha mkataba cha pamba kule, zipo changamoto ambazo zimejitokeza, zipo changamoto za kuchelewesha malipo kwa wakulima, kuchelewa kununua mazao, upotevu wa korosho, mianya ya wanunuzi na hata matatizo yanayotokana na zile sheria zenyewe za ghalani, fidia upotevu unapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, sasa tulivyojipanga ni kwamba sisi Serikali tutaleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ambao utarekebisha kasoro hizi ambazo ndizo zinazopelekea utaratibu mzima kumchelewesha mkulima. Kwa hiyo, tumejipanga kuleta Muswada huo na tunaamini kabisa kwamba wakati huo tunapoleta Muswada huo tutakuwa tumeufanyia kazi ili tuondoe kasoro zote hizi ambazo ndizo zinaonekana kumleta matatizo mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, viwanda vile vya korosho vilipobinafsishwa vyote vilibinafsishwa kwa asilimia 100. Kwa maana hiyo vinamiliki na wenyewe viwanda. Tukienda moja kwa moja tukasema tunawanyang'anya wale, Serikali itajitia katika matatizo mengine. Tulivyojipanga sisi ni kuanza kutazama upya, kuhamasisha ujenzi wa viwanda vingine na siyo Serikali inayojenga viwanda, sisi tuhamasisha sekta binafsi ijenge viwanda na kwa sababu hiyo tumeshaanza mazungumzo na wenzetu kwa mfano wa *NSSF* wamekubali kabisa kwamba kama watakuwepo watu wapo tayari kuingia kwenye viwanda wao watachangia asilimia 60 na yule anayejenga asilimia 40. Kwa hiyo, tutajitahidi sasa kuanza kuwahamasisha wote ambao wapo tayari ili tuingie kwenye mfumo wa kujenga viwanda vipya vyenye teknolojia ya kisasa siyo hivi vya kizamani ili angalau tuhakikishe kwamba korosho yote inabaguliwa badala ya kuuzwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo ambayo tumejipanga Kiserikali. *(Makofi)*

